**30 APRILI, 2025**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA TISA**

**Kikao cha Kumi na Tano – Tarehe 30 Aprili, 2025**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara Madini kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora) kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**MHE. BAHATI K. NDINGO K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Utekelezaji wa Mfuko wa Mahakama Fungu Na. 40 kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Maswali Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Parreso.

Na. 182

**Ujenzi wa Barabara za Lami katika Mji Mdogo wa Karatu**

**MHE. CECILIA D. PARESSO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa barabara za lami katika Mji Mdogo wa Karatu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na ujenzi wa barabara za lami katika Mji wa Karatu ambapo hadi sasa jumla ya kilometa 3.595 zimejengwa kwa kiwango cha lami ambapo mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali ilijenga barabara yenye urefu wa kilometa 0.610 kwa gharama ya shilingi milioni 500. Aidha, mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali ilijenga barabara yenye urefu wa kilometa 0.725 kwa gharama ya shilingi milioni 475.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Serikali vilevile, inaendelea kujenga barabara yenye urefu wa kilometa 0.710 kwa gharama ya shilingi milioni 469.5. Pia, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Serikali imeweka katika mipango yake kujenga barabara yenye urefu wa kilometa 0.9 kwa gharama ya shilingi milioni 604.2.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kutekeleza ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami katika Mji wa Karatu na miji mingine nchini kulingana na upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza nichukue fursa hii kuipongeza Serikali kwa kazi kubwa ya ujenzi wa barabara ambayo inaendelea katika Mji wa Karatu. Kwa kuwa Mji wa Karatu ni mji unaokua kwa kasi na ni mji muhimu kwa maana ya eneo la kiutalii.

Swali la kwanza; je, Serikali haioni haja sasa ya kupanua wigo wa ujenzi wa barabara katika maeneo mengine ya pembezoni katika Mji wa Karatu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kuna baadhi ya kata ambazo zinakuwa kwa kasi zikiwemo Kata ya Mang'ola, Barai, Endambashi, Mbulumbulu na Rotia. Je, Serikali haioni ni muhimu

angalau baadhi ya barabara katika maeneo hayo na yenyewe ikajengwa kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kumpa taarifa Mheshimiwa Cecilia Paresso kwamba, Serikali ya Awamu ya Sita ina dhamira ya dhati ya kuendelea kuongeza mtandao, lakini kuboresha miundombinu ya barabara zetu hizi za wilaya ambazo zinasimamiwa na *TARURA* ili ziweze kuwa katika hali nzuri ifikie mtandao mrefu zaidi na wananchi waweze kufanya shughuli zao za kiuchumi vizuri zaidi, lakini wananchi pia waweze kufikia huduma za msingi kabisa za kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niendelee kumtaarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba dhamira hiyo ya Serikali ya Awamu ya Sita utaiona hata kwenye kuongeza bajeti ya *TARURA* kwa maana ya kuhudumia barabara hizi muhimu za wilaya. Utaona wakati Serikali ya Awamu ya Sita inaingia madarakani bajeti ya *TARURA* ilikuwa ni bilioni 275 kwa mwaka, lakini tunavyozungumza wakati huu tunatarajia katika bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026 bajeti ya *TARURA* itakuwa ni trilioni 1.18, kwa hiyo, dhamira unaiona.  Katika Wilaya ya *Karatu DC,* kipindi cha miaka hii minne utaona kwamba jumla ya shilingi bilioni 7.8 zimetumika kwa ajili ya kuboresha barabara zetu hizi za wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, tunatajaria kuwa na bajeti ya bilioni 2.25 katika Wilaya hii ya Karatu *DC*. Kwa hiyo, ninaomba niendelee kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwenye maswali yako yote mawili kwamba, Serikali itaendelea kuhakikisha kila mwaka wa bajeti inatenga fedha kwa ajili ya kuja kuhudumia na kuboresha miundombinu ya barabara hizi muhimu kabisa katika Wilaya hii ya *Karatu DC* ili ziweze kuwanufaisha wananchi kiuchumi, lakini kuwawezesha kufikia huduma za muhimu kabisa za kijamii.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ahsante. Mheshimiwa Swalle

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi. Mtwango ni mji mdogo katika Jimbo la Lupembe na kuna barabara za *TARURA* pale, palikuwa na barabara ndogo ambayo ujenzi ulianza, lakini hauendelei. Ni lini ujenzi wa lami Mtwango utakamilika Mheshimiwa Naibu Waziri?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kusisitiza kwamba dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita ni kuhakikisha barabara hizi muhimu kabisa za wilaya ambazo zinasimamiwa na *TARURA* zinaendelea kuimarika na zinaweza kupitika katika kipindi cha mwaka mzima. Dhamira hii ya Serikali utaiona jinsi gani kila mwaka wa bajeti fedha zinatengwa kwa ajili ya kuhakikisha mtandao mrefu zaidi wa barabara hizi za *TARURA* unaweza kufikiwa na barabara hizi zinakuwa katika hali nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Edwin Swalle kwamba hata katika eneo hili alilolitaja eneo la Mtwango Serikali itafika italeta fedha kwa ajili ya kuhakikisha inajenga barabara hiyo, inaweka miundombinu yote muhimu kwa ajili ya kuwezesha barabara hizi muhimu kabisa kiuchumi, lakini kijamii ziweze kuwa katika hadhi nzuri na ziweze kuwanufaisha wananchi.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Kamguna.

Na. 183

**Ujenzi wa Barabara Malinyi**

**MHE. ALEKSIA A. KAMGUNA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga barabara za Wilaya ya Malinyi kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inakusudia kujenga kwa tabaka la lami barabara za Makao Makuu ya Wilaya zote hapa nchini ikiwemo Wilaya ya Malinyi. Katika mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali inaendelea na ujenzi wa Barabara ya Mnadani - Bomani inayoelekea Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Malinyi kwa tabaka la lami yenye kilometa 0.85 kwa thamani ya shilingi milioni 759. mpaka sasa ujenzi bado unaendelea na umefikia 30%.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kamguna

**MHE. ALEKSIA A. KAMGUNA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa nafasi na ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali na jitihada ambazo inachukua katika Wilaya yetu, lakini katika Mkoa wa Morogoro miundombinu mingi imeharibika hususani katika Wilaya ya Malinyi na Wilaya ya Malinyi. Sasa hivi ninavyoongea mawasiliano ya barabara hakuna ukitoka mjini kwenda halmashauri ya mji ambapo ndipo kunapatikana huduma za jamii. Sasa hivi tunapita barabara ya mchepuko ambayo inaitwa Barabara ya Mchangani na hiyo barabara ni mbovu.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; je, Serikali ipo tayari kutengeneza hiyo barabara kwa dharura ili wale watu wapite na pia itengenezwe kwa kiwango cha lami kupunguza adha wanazozipata hawa wananchi wanawake na watoto?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; katika Mkoa wa Morogoro Serikali inajitahidi sana kupeleka pesa ili kutengeneza hizo Barabara, lakini baada ya muda mfupi zile barabara zinaharibika. Je, Serikali inawachukulia hatua gani wakandarasi ambao wanatengeneza barabara hizo chini ya kiwango?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba swali la kwanza la Mheshimiwa Aleksia Kamguna kwamba barabara hii anayoizungumzia Barabara ya Mchangani ambayo kwa jina inaitwa Barabara ya Malinyi – Igawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli barabara hii ni barabara mbadala ya kuingia katika Mji wa Malinyi na usiku wa tarehe 16 Aprili, 2025, yalitokea mafuriko ambayo yanatokana na mvua za masika ambazo zinaendelea kunyesha Malinyi na barabara hii kimsingi mawsiliano yamekatika na mpaka wakati huu *TARURA* inachukua hatua za kidharura ili kuhakikisha kwamba inarudisha mawasiliano kwenye barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inafanya mpango wa kudumu wa kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami ili iweze kuwa katika mazingira mazuri na iweze kuhudumia wananchi katika kipindi cha mwaka mzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na swali lake la pili ni kwamba, Serikali inapotoa nafasi ya ujenzi wa barabara hizi kwa wakandarasi inatarajia kwamba wakandarasi waweze kuzingatia mkataba wanapokuwa wanatekeleza ujenzi wa barabara hizi za wilaya na Serikali inakuwa makini kusimamia viwango kwamba mikataba siyo tu inakwisha kwa wakati, lakini ujenzi pia uzingatie viwango.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuchukua hatua kwa wale wakandarasi ambao kwanza hawatimizi mikataba yao kwa wakati, lakini pia hawatimizi viwango ambavyo vinakusudiwa kimkataba katika ujenzi wa barabara hizi muhimu. Kwa hiyo, Serikali itaendelea kuchukua hatua hizo kuhakikisha kwamba barabara zetu zinajengwa kwa viwango na zinaweza kudumu kwa muda mrefu baada ya kuwa zimejengwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sophia.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Barabara ya Bujela, Masukulu, Matwebe ni barabara ya kimkakati na ni nzuri sana tuliiombea wakasema wataiwekea kiwango cha lami ni lini wataitekeleza ahadi hiyo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Awamu ya Sita inafanya uwekezaji mkubwa katika kuimarisha miundombinu ya barabara na hasa barabara zetu hizi za wilaya zinazosimamiwa na *TARURA* na utaiona dhamira ya Serikali hata kwenye upande wa kutenga bajeti kwa ajili ya barabara hizi za *TARURA* wakati Serikali ya Awamu ya Sita inaingia madarakani bajeti ya *TARURA* ilikuwa ni bilioni 275, lakini mpaka wakati huu tunapozungumza bajeti hiyo imeendelea kuongezeka kila mwaka na tunatarajia mwaka wa fedha 2025/2026 bajeti ya *TARURA* itakuwa ni trilioni 1.18.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo tunaona kabisa dhamira ya kuendelea kuimarisha miundombinu ya barabara hizi muhimu za wilaya. Ninaomba niendelee kumuhakikishia Mheshimiwa Sophia Mwakagenda kwamba barabara hii aliyoitaja na miundombinu ya eneo hili alilolitaja Serikali itafika na itaendelea kutenga fedha kila mwaka kwa ajili ya kuhakikisha inaimarisha miundombinu hii ili iweze kuwanufaisha wananchi kiuchumi, lakini iwawezeshe kufikia huduma za msingi kabisa za kijamii.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Monni.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya kwa Mtoro Sanzawa hadi Mpendwe yenye kilometa 54 iliharibiwa kabisa na mvua za 2023/2024 tulishaleta maombi ya fedha *TARURA*. Ninaomba kujua ni lini sasa Serikali itatoa fedha hizo ili tuweze kurekebisha barabara hii? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika,

ninaomba kuendelea kumuhakikishia Mheshimiwa Mohamed Monni kwamba kwa kweli amekuwa akifanya ufuatiliaji wa karibu sana kuhakikisha miundombinu ya barabara katika jimbo lake inaweza kupatiwa fedha na inaweza kuimarishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimhakikishie kwamba maombi tumeyapokea na tunayafayia kazi na fedha zitaletwa kwa ajili ya kuendelea kuimarisha miundombinu ya barabara hizi zinazosimamiwa na *TARURA* katika jimbo la Mheshimiwa Mbunge.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Pallangyo.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kujenga kwa kiwango cha lami kilometa tano pale Mji wa *Usa River* ambazo zilitolewa mwaka 2015 na Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kumhakikishia Mheshimiwa Dkt. Pallangyo ambaye kwa kweli amekuwa akifanya ufuatiliaji wa mara kwa mara kuhakikisha kwamba miundombinu ya barabara hizi za wilaya zinasimamiwa na *TARURA* zinaweza kujengwa na kuweza kuwanufaisha wananchi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimhakikishie kwamba Serikali italeta fedha kuhakikisha kwamba barabara hizi ulizozitaja katika eneo la *Usa River* zinajengwa kwa kiwango cha lami ili ziweze kuwanufaisha wananchi wako. Kilio chako na sauti yako na sauti ya wananchi wako imesikika na Serikali sikivu Serikali ya Awamu ya Sita itahakikisha inaleta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hizo muhimu kabisa katika jimbo lako.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kabati.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Barabara inayotoka Idete kwenda Itonya – Muhanga mpaka Uluti katika Wilaya ya Kilolo haipitiki kabisa wakati huu wa mvua na kusababisha hata pikipiki sasa kusombwa na maji badala ya kuwabeba watu na wananchi kupata shida hasa wajawazito, wagonjwa na watu wazima. Je, Mheshimiwa Waziri yupo tayari sasa kuja Kilolo aje ajionee hasa wakati huu wa mvua barabara nyingi sana hazipitiki ili aweze kusaidia wananchi wa Kilolo? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mnzava.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa sababu ya mvua zinazoendelea hali ni mbaya kwenye maeneo mengi sana na *TARURA* hawana fedha ya dharura kwa ajili ya kukabiliana na dharura hii ni nini kauli ya Serikali juu ya jambo hili? Ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Timotheo Mnzava kwamba kila mwaka wa bajeti, Serikali inatenga fedha ya dharura. Pia, ninaomba nimpe taarifa njema kwamba katika mwaka huu wa bajeti, Bunge hili Tukufu limepitisha nyongeza ya bajeti ya shilingi bilioni 50 kwa ajili ya kutengeneza barabara ambazo zimeharibika kutokana na madhara mbalimbali ikiwemo madhara ya mvua kwa dharura.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itachukua hatua ya dharura kuhakikisha kwamba inarudisha mawasiliano kwenye maeneo ambayo mawasiliano yamekatika na kuimarisha miundombinu ya barabara hizi za wilaya ili ziweze kupitika katika kipindi cha mwaka mzima na ziweze kuwanufaisha wananchi kiuchumi pamoja na kufikia huduma za msingi kabisa za kijamii. Kwa hiyo, ninaomba Mheshimiwa Mbunge afahamu kwamba

tutafika katika Jimbo lake kuhudumia maeneo ambayo mawasiliano yamekatika na tutachukua hatua za kidharura.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea, Mheshimiwa Neema uliza swali lako.

Na .184

**Mshahara kwa Madiwani**

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza kutoa mshahara kwa Madiwani ili waweze kutekeleza majukumu yao kikamilifu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua na kuthamini mchango mkubwa wa Waheshimiwa Madiwani katika kusimamia utekelezaji wa shughuli za maendeleo na huduma za jamii katika mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa, Waheshimiwa Madiwani hulipwa posho za kila mwezi kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Halmashauri na Waraka wa Serikali wa Desemba, 2014 na Waraka wa Aprili, 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia kwamba nafasi ya udiwani ni ya muda maalum wa uongozi na sio ajira ya kudumu inayohusisha utumishi wa moja kwa moja ndani ya mfumo wa Serikali, malipo ya posho yameendelea kuwa njia nzuri ya kutambua mchango wa Waheshimiwa Madiwani, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Neema.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; je, Serikali haioni kukosekana kwa mishahara na posho isiyoridhisha kwa Madiwani ni chanzo cha rushwa na kuzoroteshwa kwa miradi katika maeneo yanayosimamiwa na Madiwani?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; kwa kuwa maeneo ya usimamizi ya kiutawala ya Madiwani ni makubwa kuliko posho wanayopata; je, Serikali haioni ipo haja ya kuwapatia Madiwani usafiri kama vile ambavyo CCM imeweza kufanya kwenye kata zake? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali hii inatambua, mchango mkubwa sana wa Waheshimiwa Madiwani katika kusimamia halmashauri zetu, kusimamia miradi ya maendeleo na huduma za kijamii kwa ujumla. Pia, Serikali hii inathamini sana mchango wa Waheshimiwa Madiwani na ndiyo maana Mwaka wa Fedha 2021/2022, Serikali Kuu ilichukua jukumu la kulipa posho za Waheshimiwa Madiwani kwa 95% ya halmashauri zetu kote nchini ili kuwawezesha kwanza kuwa na uhakika kwa kupata posho zao kwa wakati, lakini pili kupata posho hizo ambazo pia ziliongezwa kiwango.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunafahamu kwamba bado kiwango cha posho za Waheshimiwa Madiwani hakitoshelezi, lakini Serikali inaendelea kujiongezea uwezo wa ukusanyaji wa mapato ili kadri uwezo unavyoongezeka tuendelee kuongeza posho za Waheshimiwa Madiwani na waweze kufanya kazi kwa ufanisi mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, tunafahamu, ni kweli wapo Waheshimiwa Madiwani ambao wana kata kubwa sana na wana changamoto ya usafiri. Serikali itaendelea kufanya tathmini na kuona uwezekano wa kupata vyombo vya usafiri kwa kadri uchumi utakavyokuwa unaruhusu ili Waheshimiwa Madiwani

waendelee kufanya kazi kwa ufanisi mkubwa zaidi. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kajege.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakubaliana na majibu ya Serikali, lakini kwa kweli posho za Madiwani ni ndogo sana. Je, ni lini Serikali itafanya mapitio ili kuboresha kipato cha Madiwani? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekwishafanya tathmini na inatambua kwamba kweli posho za Waheshimiwa Madiwani hazitoshelezi. Hata hivyo, ili kuwa na kiwango kikubwa cha posho, lazima tujenge kwanza uwezo wa mapato ya Serikali yenyewe ili iweze kumudu kulipa posho hizo za Waheshimiwa Madiwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nitumie nafasi hii kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge kote nchini kwamba Serikali inatambua sana mchango wao katika usimamizi wa shughuli mbalimbali katika halmashauri na ndiyo maana imechukua jukumu la kulipa posho katika halmashauri zaidi ya 95% badala ya siku za nyuma ambapo halmashauri zilikuwa hazina uwezo wa kuwalipa hata hizo posho za kila mwezi na kuwezesha Waheshimiwa Madiwani kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kadri Serikali itakavyoendelea kujenga uchumi na uwezo wake wa mapato ya ndani, tutaendelea kuona uwezekano wa kuongeza posho za Waheshimiwa Madiwani. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea na Mheshimiwa Mkundi.

Na. 185

**Hitaji la Watumishi wa Kike Kada ya Afya Ukerewe**

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka Watumishi wa Afya wa kutosha wa Kike - Ukerewe ili kulinda haki ya kijinsia ya Mtoto wa Kike?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe ina jumla ya watumishi wa Afya 381. Kati ya hao watumishi 197 ni watumishi wa kike na watumishi 184 ni watumishi wa kiume.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ajira ya Mwaka wa Fedha 2024/2025, Halmashauri ya Ukerewe imepokea watumishi 30 ambapo watumishi 18 ni wa kike na watumishi 12 ni wa kiume. Serikali imekuwa ikizingatia uwiano wa kijinsia wakati wa kuajiri watumishi wa afya na kuwapanga katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mkundi.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa majibu ya Serikali. Ninatambua jitihada kubwa zinazofanywa na Serikali na nitumie nafasi hii kuwapongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kwenye maeneo ya pembezoni, kwa mfano tuchukulie Zahanati ya Kulazu, Kisiwa kidogo cha Ilugwa haina mtumishi wa kike, Zahanati ya Kwelu kwenye Kisiwa kidogo cha Kwelu haina mtumishi wa kike na Zahanati ya Busumba kwenye Kisiwa kidogo cha Bwilo haina mtumishi wa kike. Jambo hili linaleta changamoto kubwa na sababu kubwa inayopelekea watumishi wa kike kukimbia maeneo haya ni kwa sababu ya mazingira magumu hasa kukosa

nyumba za watumishi. Nini sasa mkakati wa Serikali kuweka mazingira mazuri hasa ujenzi wa nyumba za watumishi ili hao watumishi wa kike waweze kukaa na kuhudumia wananchi wetu? Ninashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninaomba nianze kwa kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba katika Sekta ya Afya na katika utoaji wa huduma za afya, wataalam wa kike na wataalam wa kiume siyo kigezo cha kutoa huduma bora katika vituo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi yapo mazingira ambayo wateja au wagonjwa wa kike wangeweza kuhudumiwa zaidi na wauguzi wa kiume au madaktari wa kiume na kinyume chake. Kwa hiyo, kwanza, ninaomba niweke hii rekodi sahihi zaidi, kwamba hakuna utaratibu wa kuhakikisha kwamba kila zahanati ina mtumishi wa kike na kama haina mtumishi wa kike kwamba zahanati hiyo haina watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu ni kwamba mtumishi yeyote awe wa kike au wa kiume amekuwa *trained*, ana miiko, ana utaalam na anaweza kutoa huduma za afya kwa muktadha huo. Kwa hiyo, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba eneo hilo la jinsia si eneo muhimu sana katika Sekta ya Afya, suala ni mtaalam anayeweza kutoa huduma hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na nyumba za watumishi. Nimhakikishie Mheshimiwa Mkundi kwamba Serikali hii ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imeanza ujenzi wa nyumba za watumishi na hasa katika vituo vya pembezoni zaidi ikiwemo Halmashauri ya Ukerewe. Juzi tulikuwa pale tumeona kazi nzuri ambayo inaendelea kufanyika. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Serikali itaendelea kujenga nyumba za watumishi katika vituo vya pembezoni ili watumishi waweze kufanya kazi katika mazingira bora zaidi. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Vituo vya Afya vya Kasekese, Sibwesa na Bulamata ni miongoni mwa vituo ambavyo havina watumishi wa kutosha katika hayo maeneo. Ni lini Serikali itapeleka watumishi wa kutosha kwenye maeneo hayo? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Halmashauri ya Tanganyika na katika hivyo vituo vya afya ambavyo Mheshimiwa Mbunge amevitaja vina upungufu wa watumishi. Hata hivyo, Serikali hii ya Awamu ya Sita na ni dhamira ya dhati kabisa ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kipindi hiki cha miaka minne ya Serikali hii, jumla ya watumishi 32,750 wameajiriwa na kupelekwa katika vituo vya huduma za afya kote nchini. Katika halmashauri ya Tanganyika wamepata pia watumishi wa Sekta ya Afya na tunaendelea kuwapeleka watumishi hao kwa awamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatambua upungufu huo na kila kibali cha jira kikitokea tutahakikisha tunatoa kipaumbele katika Halmashauri ya Tanganyika na zile nyingine ambazo ziko mazingira ya pembezoni.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Mussa Omar Salim.

Na. 186

**Kuzuia Maji Chumvi Kuingia Bonde la Mpanja**

**MHE. SALIM MUSSA OMAR** aliuliza:-

Je, ni lini ahadi ya Serikali ya kuzuia maji chumvi kuingia katika Bonde la Mpanja Gando itatekelezwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kukabiliana na changamoto za athari za mabadiliko ya tabianchi zinazochangia kuongezeka kwa kina cha Bahari kunakosababisha maji ya chumvi kuingia katika Bonde la Mpanja, Gando. Hatua hizo ni pamoja na kuendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kusaidia kurejesha maeneo yalioathirika kwa kuandaa maandiko ya miradi na kuwasilishwa kwa wadau wa maendeleo ikiwemo Mfuko wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi (*Adaptation Fund*) na Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muktadha huo, shughuli za kuzuia maji chumvi katika Bonde la Mpanja Gando zitaanza kutekelezwa baada ya fedha kupatikana kupitia miradi hiyo ili wananchi wa maeneo hayo waweze kuendelea na shughuli zao. Ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Salim.

**MHE. SALIM MUSSA OMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na ninashukuru kwa majibu mazuri na yenye kutia matumaini ya Serikali, lakini nilikuwa na maswali mawili ya nyongeza ambayo ningependa kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; kwa kuwa kilimo kile ni kilimo cha matumizi ya chakula moja kwa moja kwa wananchi wa Jimbo la Gando na wewe mwenyewe pamoja na Mheshimiwa Kijaji (Waziri yule aliyepita) walikuja wakajionea mashamba haya takribani 200 yameendelea kuathirika siku hadi siku. Je, katika maandiko hayo ambayo wameandaa, wako tayari kuweza kuipa *priority* maalum Shehia hii ya Jimbo la Gando ili kusudi kuweza kuwalinda na janga la njaa wananchi hawa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa tatizo hili halipo Gando tu kwa Zanzibar, limekuwa ni tatizo kubwa na linaendelea kutuathiri sana; je, ni mpango upi mahususi wa Serikali walioupanga kwa ajili ya kuweka *constant budget* kuweza ku-*overcome challenge* hii?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana. Ninaomba nimjibu maswali mawili ya nyongeza lakini nichukue fursa hii kumpongeza sana kwa kuliona hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tumefika katika Kijiji cha Mpanja katika Jimbo la Gando mimi na Mheshimiwa Kijaji wakati ule na tuliona athari kubwa ambayo wananchi wanaathirika. Maji ya bahari yameingia kwenye vipando ambavyo havistahimili maji ya bahari lakini pia maji ya bahari yameingia kwenye makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwambie tayari tumeshaomba dola za kimarekani milioni 10, tumeshaziomba na katika hizo tayari milioni 3.5 zinakuja kushughulikia tatizo kwa upande wa Zanzibar. Nimwambie Mheshimiwa aendelee kuwa na subira, tupo tunafanya utaratibu, zitakapopatikana tutahakikisha Gando na maeneo mengine yakiwemo Nungwi na maeneo mengine ya Lindi na Mtwara tunakwenda kuondoa hii changamoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba, pia tutahakikisha Jimbo la Gando tunalipa *priority* kwa sababu ya umuhimu na changamoto ambayo tumeiona imejitokeza pale.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Chaurembo.

Na. 187

**Kukatika kwa Umeme Mara kwa Mara Kata za Jimbo la Mbagala**

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO** aliuliza:-

Je, lini tatizo la kukatika kwa umeme mara kwa mara katika Kata za Jimbo la Mbagala ikiwemo Chamazi, Mianzini, Kilungule, Charambe, Mbagala, Kiburungwa na Kijichi Mbagala Kuu Maji litaisha?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya kukatika kwa umeme mara kwa mara katika Jimbo la Mbagala katika maeneo tajwa kunatokana na kuzidiwa kwa Kituo cha Kupoza Umeme cha Mbagala. Ili kutatua changamoto hii, Serikali kupitia *TANESCO* imefunga transfoma yenye uwezo wa *MVA* 120 katika kituo hicho na inatarajia kuiwasha hivi karibuni. Aidha, Serikali inatarajia kufunga nyaya zenye uwezo mkubwa katika njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kilovoti 132 kutoka Kinyerezi hadi Mbagala kupitia Gongolamboto.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande mwingine, *TANESCO* inaendelea na usimamizi wa Mradi wa kuipatia Wilaya ya Mkuranga kituo kikubwa cha kupozea umeme chenye uwezo wa *MVA* 240 eneo la Dundani na kuacha utegemezi kwenye Kituo cha Mbagala. Kukamilika kwa miradi hii kutasaidia kumaliza tatizo la kukatika kwa umeme mara kwa mara katika Jimbo la Mbagala. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chaurembo.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; kutokana na Jimbo la Mbagala kuwa na wananchi wengi na wanaongezeka siku hadi siku; je, Serikali

haioni ipo haja ya kujenga *substation* nyingine katika eneo la Chamazi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kutokana na ubadilishaji wa nguzo unaoendelea hivi sasa, kumekuwa na tatizo la kukatika kwa umeme zaidi ya saa 18 kwa siku. Je, Serikali haioni ipo haja ya kupunguza mgao huu na kufanya saa zikawa nane?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru na nimpongeze sana Mheshimiwa Chaurembo, kwa kweli amekuwa akifuatilia kwa muda mrefu jambo la kuimarika kwa hali ya umeme katika Jimbo la Mbagala.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na kujenga *substation* (kituo cha kupooza umeme) katika eneo la Chamazi. Ni kweli Kituo cha Kupooza umeme Mbagala kinahudumia maeneo mengi sana; Mbagala, Yombo, Chamazi mpaka Mkuranga. Tulipofanya tathmini, eneo la Mkuranga lina *load* kubwa sana na ndiyo maana kipaumbele kikawepo kwamba kupitia mradi wetu wa *North East Grid* tujenge kwanza kituo cha kupooza umeme pale Mkuranga chenye uwezo wa *MVA* 40 kwa ajili ya kupunguza *laod* kubwa ambayo ipo katika Kituo cha Kupooza Umeme cha Mbagala.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, mradi huu utakapokamilika, Kituo cha Kupooza Umeme cha Mbagala kitakuwa kimeondolewa na *load* kubwa sana na hivyo kuimarika kwa hali ya umeme katika Jimbo la Mbagala. Pia, huko mbeleni tutaendelea kutafuta bajeti kwa ajili ya kuendelea kujenga vituo vya kupooza umeme kulingana na mahitaji yatakayokuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na hali ya kukatika kwa umeme. Ni kweli tulikuwa tunafanya maboresho katika *line* ambazo zinahudumia baadhi ya maeneo hususan katika eneo la Mbande. Kwa hiyo, makubaliano ilikuwa ni kwamba tunapofanya marekebisho umeme ukosekana kwa saa nane tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, nimwelekeze Meneja wa Mkoa na Meneja wa Wilaya wahakikishe makubaliano tuliyokubaliana nao ya saa nane tunapofanya matengenezo, hayo ndiyo yabaki. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aida.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mkoa wa Rukwa bado tunatumia umeme kutoka Zambia na umeme unakatika sana na kuleta kero kwa wananchi. Wizara ina mkakati gani wa haraka wa kuondoa kero hiyo kwa wananchi wa Mkoa wa Rukwa ya umeme kukatika mara kwa mara?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, jana wakati tunahitimisha bajeti nilielezea kuhusiana na mkakati wa Serikali wa kupeleka umeme wa Gridi katika Mkoa wa Rukwa. Kwa sasa tunao Mradi unaitwa *TAZA* ambao unajenga *line* kutokea Iringa, Tunduma hadi Rukwa kwa ajili ya kufikisha umeme wa Gridi katika Mkoa wa Rukwa. Ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Mkoa wa Rukwa, Serikali iko kazini. Mkandarasi ni mzuri sana na yupo *site* kuhakikisha anajenga *line* ya umeme na vituo vya kupooza umeme ili mwisho wa siku tuweze kufikisha umeme wa Gridi Mkoani Rukwa kama ambavyo Mheshimiwa Waziri Mkuu aliahidi alipofanya ziara Mkoa wa Rukwa na Mheshimiwa Rais alifanya ziara pia na aliahidi jambo hilohilo. Mkandarasi yupo *site,* kazi inaendelea.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hasunga, jiandae Mheshimiwa Kawawa.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa kuwa tatizo la kukatikatika kwa umeme

limekuwa sugu sana katika Jimbo la Vwawa, Wilaya ya Mbozi na Mkoa wa Songwe; je, zipi hatua za dharura za kuhakikisha kwamba tunanusuru tatizo hilo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Songwe yanapewa umeme kupitia *substation* ambayo iko Mbeya. Kwa hiyo, kupitia Mradi huu wa kupeleka Gridi Mkoa wa Rukwa, Kituo cha Kupooza Umeme kitajengwa pale Songwe na hivyo kusababisha baadhi ya majimbo pale likiwemo Jimbo la Mheshimiwa Mbunge wasiweze kupata umeme kwa kutumia *line* kubwa ambayo ni ndefu sana jambo linalosababisha kukatikatika kwa umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkandarasi yuko *site,* kazi imeanza na mradi ukikamilika, wananchi wa jimbo lako wataona mabadiliko hayo kwa sababu tunajenga kituo cha kupooza umeme pale kwa ajili ya kuzuia *line* ndefu wawe wanapata umeme kwa kutokea karibu ili uendelee kuimarika. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kawawa.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kumekuwa na shida ya kukatika umeme usiku mara kwa mara katika njia kuu ambayo inatoka Kata ya Luwegu, Luchili, Mkongo, Limamu, Nalisimonji, Ligela, Lusewa hadi Magazini; je, Serikali inaweza kuielekeza *TANESCO* waangalie shida ni nini kila inapofika usiku umeme huwa unakatika? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana kwa swali la Mheshimiwa Mbunge na tutalifanyia kazi kwa umahususi. Kwa niaba ya Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, ninaomba nimwelekeze Meneja wa Mkoa wa Ruvuma afanye jambo hilo kwa haraka. Wafanye *survey* kugundua tatizo ni nini, baada ya hapo tutafanya marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Wilaya ya Namtumbo, Serikali inao mkakati wa kujenga kituo cha kupooza umeme pale katika awamu ya pili ya Mradi wa Gridi Imara. Hata hivyo, kwa sababu Namtumbo ni Wilaya ya kimkakati kuna madini muhimu sana, tunaona uwezekano wa kuharakisha zoezi hilo kwa ajili ya kuimarisha hali ya umeme Namtumbo kwa ajili ya shughuli hii ya kiuchumi ya madini muhimu ambayo yapo pale.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, Mkoa wa Dar es Salaam nao unapata shida sana ya umeme kukatikakatika, Ilala, Kinondoni maeneo ni mengi sana. Ninakuomba tu, ninajua mnayo mipango mizuri, mkamilishe haraka kwa sababu Dar es Salaam ndiyo inachangia pato kubwa sana la Serikali kwenye masuala ya uchumi.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii Mheshimiwa Maboto.

Na.188

**Ujenzi wa Makao Makuu ya *TANAPA* – Bunda**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE K.n.y. MHE. ROBERT C. MABOTO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Makao Makuu ya *TANAPA* katika Halmashauri ya Mji wa Bunda?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imetenga eneo lenye ukubwa wa ekari 41.13 katika eneo la Kunzugu, Kata ya Balili, Mjini Bunda kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi za *TANAPA* Kanda ya Magharibi. Kwa sasa, Serikali imekamilisha zoezi la upembuzi yakinifu na uandaaji wa michoro kwa ajili ya ujenzi wa ofisi hiyo. Kazi ya ujenzi inatarajiwa kuanza kwenye Mwaka wa Fedhaa 2025/2026.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Bunda *TC* ilitenga eneo hilo kwa kutumia hela milioni 85 kuwalipa watu fidia na ikawapa Kanda ya Magharibi ya *TANAPA* bure wajenge, toka 2014 mpaka leo ni kama miaka mitano iliyopita. Swali la kwanza; je ni lini sasa Serikali itaamua kwa maksudi kujenga eneo hilo ambalo watu wa Bunda wanalihitaji?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Wilaya ya Bunda na Wilaya ya Butiama ili waende kwenye Hifadhi ya Serengeti inabidi waende Serengeti Wilayani au waende Lamadi. Sisi tuna geti la kutoka Kata ya Mgeta kwenda Kilawila kilometa 17. Je, ni lini Serikali au *TANAPA* itafungua geti hilo kwa watu wa Bunda? ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Getere, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu kwenye swali la msingi kazi ya ujenzi itaanza mwaka wa fedha 2025/2026. Kuhusiana na swali lake la pili la kufungua geti hilo, kwa sasa kuna mageti ambayo yanafanyiwa kazi tukimaliza kukamilisha mageti haya tutaweka kwenye mpango unaofuata kulingana na vipaumbele vya ufunguaji wa hifadhi za Taifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Saputu.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi. Ninataka kufahamu kwa kuwa wanyamapori wanawasumbia wananchi kwenye Vijiji vya Oljorobusi na Engaraoni na nilishawasilisha kwako kwa Naibu Waziri akatoa majibu kituo cha dharura kijengwe katika vijiji hivyo na hadi sasa kituo hicho cha dharura hakijajengwa. Je, nini kauli ya Serikali ili kuwanusuru wananchi ambao wanasumbuliwa na wanyama hasa tembo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali lanyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua changamoto ya wanyama wakali na waharibifu na ndiyo maana inatumia mikakati mbalimbali kuhakikisha inawadhibiti, sasa tumeingia kwenye matumizi ya teknolojia ya ndege nyuki, vilevile maeneo mengine tunatumia helkopta na tunatumia vilevile matumizi ya mabomu baridi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuhusu ujenzi wa vituo tunaendelea nalo kwa jinsi ambavyo upatikanaji wa fedha unapatikana. Nimwombe Mheshimiwa Mbunge awe na subira bado nia ya serikali ni kujenga kituo kwenye eneo lile.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Hifadhi ya Mwalimu Nyerere pamoja na pori la akiba la Selous *Game Reserve* linapakana na Liwale. Je, Serikali haioni imefika wakati sasa kujenga geti la kuingilia watalii Wilayani Liwale ili wana Liwale nao wafaidi faida za utalii kwenye nchi hii? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo mipango ya kujenga mageti kwenye maeneo mengi na kwa upande huu wa Mikoa ya Kusini tunao mkakati madhubuti wa kuifungua Mikoa hii ya Kusini kwenye suala la utalii. Ninamwomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira tumalizie kazi ambazo tunazifanya sasa hivi tukikamilisha tutahamia kwenye maeneo yake.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Kilimo Mheshimiwa Mpakate.

Na.189

**Ujenzi wa Maghala Vijijini**

**MHE. DAIMU I. MPAKATE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga maghala ya kuhifadhia mazao Vijijini?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka wa fedha 2025/2026 mpaka 2029/2030 Serikali ina mpango wa kujenga maghala na vihenge yenye uwezo wa kuhifadhi tani 3,000,000 za chakula. Katika mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali imekamilisha ujenzi wa ghala za kisasa 20 za ngazi ya kijiji zenye uwezo wa kuhifadhi tani 47,000 katika Mikoa ya Dodoma, Babati, Tabora, Kigoma, Ruvuma, Simiyu, Mtwara, Geita, Mwanza na Morogoro. ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutambua umuhimu wa maghala na vihenge katika kuimarisha usalama wa chakula nchini, kwa sasa zoezi la kufanya tathmini ya utambuzi wa ghala za umma na binafsi linaendelea. Zoezi hilo litakapokamilika litawezesha kutoa mwongozo wa namna bora ya uwekezaji wa ghala katika maeneo mbalimbali nchini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mpakate.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; kwa kuwa tatizo la maghala kwenye vyama vya msingi na vijiji vyetu katika Jimbo la Tunduru Kusini ni kubwa. Ni kwa nini sasa Serikali haioni haja ya kuwashirikisha benki za biashara na vyama vya msingi katika kujenga maghala ili kuondokana na adha ya vyama vya msingi kutumia nyumba za watu binafsi ambazo hazina ubora wa kuhifadhia mazao?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; mwaka wa fedha 2014/2015 Bodi ya Korosho ilianza kujenga ghala la kuhifadhia

mazao katika Mji wa Tunduru lenye uwezo wa kuhifadhi mazao tani 10,000, lakini ujenzi ule umesimama mpaka leo. Je, ni lini Serikali itatoa fedha kukamilisha ujenzi ule kwa kuwa bilioni moja iko pale na bado haifanyi kazi yoyote?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Mpakate kwa kazi nzuri anayoifanya katika Jimbo lake hususani kufuatilia maghala ya uhifadhi wa chakula. Ninamthibitishia tu kwamba mpango wa Serikali wa sasa tumevielekeza vyama vya ushirika na vile vyama vya msingi na vyama vikuu pamoja na sekta binafsi kuingia katika ujenzi wa maghala ambayo yatasaidia katika uhifadhi wa chakula. Kwa hiyo, jambo hili lipo katika mpango wetu na tumeendelea kulisukuma kwa sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ambalo ni la msingi kabisa ni kwamba ni kweli Bodi ya Korosho ilianza kujenga katika Mwaka wa Fedha 2014/2015 na hapo Katikati tulikwama kupata fedha, lakini ninavyozungumza sasa hivi ni kwamba tayari Bodi ya Korosho ina fedha bilioni 2.6 kwa ajili ya ujenzi wa ghala hili. Tumeshawalekeza kwamba katika msimu unaofuatia ghala lile liwe limejengwa limekamilika na lianze kutumika kwa ajili ya kuhifadhia mazao. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia Mheshimiwa Timotheo Mnzava

Na.190

**Mawasiliano ya Simu Kata za Jimbo la Korogwe Vijijini**

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka mawasiliano ya simu kwenye Kata za Mkalamo, Magila, Gereza na Kalalani – Korogwe Vijijini?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILINAO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo tarehe 13 Novemba, 2015 Serikali kupitia *UCSAF* iliingia makubaliano na kampuni ya *Honora (Yas)* kujenga mnara katika Kata ya Mkalamo. Pia, mnamo tarehe 13 Desemba 2018 *UCSAF* iliingia makubaliano na Shirika la Mawasiliano Tanzania *(TTCL)* ili kufikisha mawasiliano katika Kata hiyo ambapo ujenzi wa minara yote miwili ilikamilika kwa kujengwa katika Vijiji vya Magamba na Mpasilasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kutokana na changamoto kubwa katika Kata ya Mkalamo mtoa huduma Honora alijenga minara mingine miwili katika vijiji vya Kwaisewa na Toronto Mbugani na kuifanya Kata hii kuwa na idadi ya minara minne.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge ameuliza swali kuhusu Serikali kupeleka mawasiliano katika Kata husika, inaashiria kuwa bado kuna changamoto. Hivyo, Wizara kupitia *UCSAF* itafanya tathmini katika kata hiyo ili kubaini mahitaji halisi ya mawasiliano na endapo itabaini kuwepo kwa tatizo la mawasiliano katika kata hiyo ambapo itaingizwa katika zabuni ya miradi itakayotekelezwa katika mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Kata za Magila, Gerezani na Kalalani, Serikali kupitia *UCSAF* itazifanyia tathmini Kata hizi ili kubaini changamoto za mawasiliano zilizopo na zitajumuishwa katika zabuni zitakazotangazwa katika mwaka wa fedha 2025/2026.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mnzava.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Serikali tuna changamoto kubwa sana ya mawasiliano kwenye baadhi ya vijiji vya Kata ya Mkalamo eneo la Magila, Gereza kwa maana ya kwa Sunga ambayo ni Makao Makuu ya Halmashauri na eneo la Kigwasi mahali ambako kuna mgodi wa madini. Ninataka kujua hii tathmini ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri anasema wataifanya itafanyika lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Jimbo la Korogwe vijijini tulikuwa na ahadi ya kujengewa minara na bado kuna minara mitatu mpaka sasa hivi bado haijajengwa. Ninataka kujua ni nini kauli ya Serikali juu ya ujenzi wa hii minara mitatu ambayo haijajengwa? Ninashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILINAO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tathimini itafanyika lini Mheshimiwa Mbunge Mnzava amefuatilia sana hili, ninamwomba tuendelee kuwasiliana namna ambavyo amekuwa akifanya, lakini tutahakikisha ndani ya mwaka ujao wa fedha haya maeneo yote mawasiliano yanakwenda kuimarika na tathmini itafanyika kwa haraka sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika hii minara mitatu ambayo bado haijajengwa pia niendelee kumpongeza kwa namna ya ufuatiliaji wake wa karibu, nimeshaongea na wataalam wetu wanaendelea kufuatilia kuona minara hii iweze kujengwa mapema iwezekanavyo kadri fedha tunavyopata ndani ya mwaka huu wa fedha, lakini pia kufika mwaka ujao wa fedha tutahakikisha minara hii inakamilika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Magessa

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana. Je, ni lini mnara wa kutoka Kijiji cha Msasa Kata ya Busanda utakamilika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILINAO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Magessa, Mbunge wa Busanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kijiji hiki cha Msasa mnara huu tunautarajia ukamilike ndani ya mwaka huu wa fedha na

Mheshimiwa Waziri Jerry Silaa ameshaagiza minara hii yote ambayo imeanza ujenzi lazima ikamilike ndani ya muda. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Chaya.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Vijiji vya Simbanguru na Kapiti Manyoni havina mawasiliano ya simu. Ni upi mkakati wa Serikali wa kupeleka mawasiliano ya simu katika vijiji hivyo? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILINAO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Chaya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika vijiji hivyo alivyovitaja Wilayani Manyoni Serikali dhamira yake ni kuhakikisha maeneo yote vijijini yanapata mawasiliano ya uhakika, kama vijiji hivi havipo kwenye 758, havipo kwenye 632 nimtoe shaka katika minara ambayo itapewa *TTCL* pamoja na watoa huduma wengine tutahakikisha tunakwenda kujenga katika mwaka ujao wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mabula.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, niliuliza swali hapa kuhusiana na mawasiliano kwamba Serikali inazidi kuboresha mawasiliano na kila siku tunaongeza mawasiliano maeneo yasiyofikika, lakini pamoja na maendeleo hayo mazuri utapeli pia umezidi kuendelea kutapeli watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jina langu limekuwa likitumika mara kwa mara na leo ni mara ya tatu ninazungumza hapa. Nini kauli ya Serikali katika kusafisha majina ya watu ambayo yanazidi kuchafuliwa kwa maendeleo ya mtandao lakini bado watu wanaibiwa kwa kutumia majina ya viongozi. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILINAO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Angeline Mabula, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, utapeli umeendelea, lakini watu wetu wa *TCRA* wameendelea na kazi nzuri sana ya kuhakikisha matapeli wote wanafahamika na wanakomeshwa. Hili tunaendelea kujipanga kwa hatua ngumu zaidi kuona kwamba tunaenda kukomesha kabisa suala la utapeli na suala la Mheshimiwa Angeline Mabula nimeshalifikisha kwa *DG - TCRA* Dkt. Bakari. Nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge nitaendelea kuwasiliana na Dkt. Bakari kuona kwamba hili suala linakomeshwa kabisa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Minza.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kata ya Bukundi kuna maeneo ambayo mawasiliano ya simu hayapo kabisa. Pia kuna Mwagotolo, Mwashimba, Mwashigela, Kasela na Mwanjolo. Je, ni lini Serikali itaimarisha mawasiliano?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILINAO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kata hii aliyoitaja Mheshimiwa Minza kama ni tatizo ni suala la umeme, watoa huduma wetu wamekuwa wakitumia *source* ya umeme kama *solar,* lakini maeneo mengine ambayo tayari *TANESCO* wamefanya kazi nzuri tunaendelea kuwahimiza watoa huduma wahakikishe wanapeleka umeme wa *REA* kwenye minara hii, hivyo maeneo ambayo ameyataja Mheshimiwa Minza na yenyewe tutaendelea kuyafuatilia na kuyasimamia kuhakikisha mawasiliano yanakuwa ya uhakika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kigua ajiandae Mheshimiwa Kunti.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Lwande kuna mnara wa *Halotel,* lakini kwa kweli kiuhalisia mawasiliano hakuna. Sasa ninaomba nimuulize Naibu Waziri ni nini mpango mkakati kuhakikisha kwamba Kata hii ya Lwande mawasiliano hasa ya *Halotel* yanapatikana muda wote? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILINAO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kigua kuhusu Kata ya Lwande mnara wa *Halotel* upo, lakini haufanyi vizuri, Mheshimiwa ninamhakikishia kwamba nitaufuatilia kuona tatizo ni nini, kama ni suala la umeme basi tutaendelea kuwashauri watoa huduma hawa kuimarisha mnara huu ili lengo la kusababisha mawasiliano ya uhakika liweze kutimia.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kunti.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Kata ya Ovada, Kata ya Lalta Wilaya ya Chemba ina changamoto kubwa sana ya mawasiliano pamoja na uwepo wa minara ya *TTCL,* lakini wananchi hawa mawasiliano yao yamekuwa ni ya taabu ambayo hayana uhakika. Je, ni nini mkakati wa Serikali wa kuboresha mawasiliano katika hizo Kata mbili?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILINAO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kunti kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kata hizi mbili alizozitaja katika Wilaya ya Chemba, *TTCL* tayari wamejenga mnara tutakachohakikisha kukisimamia kama Wizara ni kuona kwanza waweze kufanya huduma ya mashirikiano kwa pamoja ili hata watoa huduma wengine waweze kutumia mnara huu kusambaza

huduma ya mawasiliano, *TTCL* pia kuhakikisha mnara huu wana u-*upgrade* wanauwekea uwezo wa kuona kwamba mawasiliano yaliyokusudiwa yanaweza kuwafikia wananchi.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Maji Mheshimiwa Gulamali.

Na.191

**Hitaji la Maji ya Ziwa Victoria Kata za Manonga**

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itatenga fedha ili wananchi wa Kata za Igoweko, Uswaya na Tambalale – Manonga wapate maji ya Ziwa Victoria?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua changamoto ya upatikanaji wa huduma ya maji katika baadhi ya Kata zilizopo Jimbo la Manonga Wilaya ya Igunga ikiwemo Kata za Igoweko, Uswaya na Tambalale. Katika kutatua changamoto kwenye Kata hizo, Serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi miwili mikubwa ya Ziba - Nkinga awamu ya pili pamoja na Nkinga - Simbo ambayo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Kukamilika kwa miradi hiyo kutanufaisha zaidi ya wakazi 70,000 waishio kwenye vijiji 17 vya Jimbo la Manonga, Wilaya ya Igunga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali vilevile inaendelea na uchimbaji wa visima vitano katika Jimbo la Manonga unaoambatana na ujenzi wa miundombinu rahisi ya kutolea huduma *(point source)* katika baadhi ya vijiji vya Kata za Igoweko na Tambalale kupitia programu maalum ya uchimbaji wa visima 900.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuboresha huduma ya maji kwa maeneo ambayo hayajafikiwa na huduma hiyo kadri fedha zinavyopatikana. Ninakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gulamali.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali madogo ya nyongeza. Ni kweli tumepata utanuzi wa mradi wa maji ya Ziwa Victoria Ziba - Nkinga. Ni kweli tumepata mkandarasi wa kupeleka maji ya Ziwa Victoria Nkinga – Nsimbo. Ni kweli tumepata gari la kuchimba visima vitano kila Jimbo nasi tukiwemo, hasa katika maeneo ya Kata alizozitaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ule mradi wa visima vitano kwenye kila Jimbo tumepata gari kwenye Kata ya Igoweko, Kata ya Uswaya na Kata ya Tambalale, katika maeneo yote haya matatu tumekosa maji chini ya ardhi, ndiyo tunaiomba sasa Serikali kupitia Wizara ya Maji kwamba, mradi ule wa maji ya Ziwa Victoria unapofika Nsimbo tuwekewe fedha za maji kutoka Nsimbo kwenda kwenye hizo Kata ya Igoweko, Kata ya Uswaya na Kata ya Tambalale. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mbona sauti ipo chini leo?*(Kicheko)*

Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa ninakushukuru wewe na nimshukuru Mheshimiwa Seif Khamis Said Gulamali Mbunge wa Manonga kwa ushirikiano mzuri anaotupatia sekta ya maji na vilevile kwa kutoa ushirikiano pale ambapo tunapata changamoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa tumechimba visima vitano na visima vitatu hatukupata maji lakini tukaongeza kingine vikafika vitatu, visima viwili vinatoa maji mpaka sasa, lakini kimoja tunaendelea na ujenzi wa miundombinu. Vilevile ombi lake na ushauri wake Serikali tunaendelea kupokea ushauri wa wadau nasi kwa sababu maji ya Ziwa Victoria ambayo Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Hassan Suluhu alitoa Bilioni 680, kutoka Ziwa Viktoria mpaka Nzega - Igunga na *extension* yake ya Sikonge - Urambo pamoja na Kaliua bilioni 143 haya maji ni mengi sana. Kwa hiyo, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaweka katika

bajeti yetu ijayo ili tuweze kuhakikisha kwamba, tunafanya *extension* katika maeneo ambayo tumekosa maji chini ya ardhi kutokana na uchimbaji wa kisima. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chikota.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Ujenzi wa Mradi wa Makonde unasuasua kwa sababu, kuna changamoto ambazo mkandarasi bado anazo. Je, Serikali ina mkakati gani wa haraka wa kutatua changamoto za mkandarasi huyo, ili ujenzi uendelee?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana. Ninatambua kwamba, Mradi huu wa Makonde ni mradi wa kimkakati kwa Kanda ya Kusini. Serikali imekaa chini na mkandarasi kujadiliana namna ya kuzimaliza changamoto hizi, ili mradi huu uendelee. Pia, tunatambua kwamba, alikuwa na madai yake na wenzetu Wizara ya Fedha, tumeshaongea, tuko katika hatua nzuri, ili mkandarasi huyu aweze kurudi *site* mradi huu ukimbie kwa haraka na wananchi wapate wanachokitarajia kutokana na Mradi huu wa Makonde. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shamsia.

**MHE. SHAMSIA A. MATAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipatia nafasi, ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Je, ni lini Serikali itatatua changamoto ya maji ambayo ipo kwa muda mrefu katika Kata ya Mango, Pacha Nne?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru na ninamshukuru sana Mheshimiwa Mbunge. Bahati nzuri nilikuwepo Mtwara na tulifanya naye ziara na natambua changamoto hiyo na tayari tulishaipokea, Wizarani

tunaifanyia kazi. Nimwombe Mheshimiwa Mbunge awe na subira wakati tukiwa tunapata fedha, kwa ajili ya kwenda kutekeleza mradi huu. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria ni mradi muhimu sana kwa sababu, tunatarajia kutatua changamoto ya maji kwa Wakazi wa Rorya, Mji wa Tarime na *Tarime DC*, ambao ulitarajiwa kukamilika Mwaka 2025. Ninataka tu kujua kwa sasa umefikia asilimia ngapi? Ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana na ninamshukuru sana dada yangu, Mheshimiwa Esther Matiko, kwa kazi nzuri anayoifanya. Mradi huu ambao unaanzia Tarime, Rorya unaenda mpaka Serengeti, Mugumu. Kwa hiyo, tunaamini kabisa kwamba, huu mradi utaenda kusaidia sana katika wilaya kadhaa ambapo wananchi wa pale watapata huduma ya maji safi, lakini tunapotoa takwimu sahihi Mheshimiwa Mbunge anikubalie kwa sababu, ni suala la takwimu na Serikali haitakiwi kutoa takwimu ambazo siyo sahihi. Nimuombe baada ya hapa nilifanyie kazi, halafu nimpatie takwimu halisi kwamba, umefika asilimia ngapi *exactly,* kwa ajili ya manufaa ya wananchi wake wote. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Samweli.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni lini wananchi wa Bassodesh, Mureru na Gijetamohog watapata maji safi na salama bombani, ikiwa visima vimeshachimbwa na mabomba yako *site* zaidi ya mwaka sasa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa Mhandisi kwa kazi kubwa

anayoifanya kwa wananchi wake na mradi huo ambao tayari hatua ya kwanza tulichimba visima, lakini baadaye pia, tukanunua vifaa, ikiwemo mabomba, matanki na kadhalika. Sasa, hatua ya mwisho ni kuhakikisha kwamba, tunaenda kulaza yale mabomba pia, kutengeneza maeneo ambayo wananchi wanaweza kupata hiyo huduma ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge changamoto iliyokuwepo sasa hivi tayari tumeshaifanyia kazi na mabomba hayo yataenda kulazwa, ili yaweze kutoa huduma ya maji safi na salama. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake. Mheshimiwa Mwantum Dau.

Na. 192

**Kudhibiti Mimba za Utotoni Nchini**

**MHE. MWATUMU DAU HAJI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti mimba za utotoni, nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya visababishi vya mimba za utotoni ni pamoja na uelewa mdogo wa watoto kuhusu elimu ya afya ya uzazi na uwajibikaji duni wa wazazi na walezi katika kutunza na kulea watoto kikamilifu. Katika kukabiliana na tatizo hilo, Serikali inatekeleza Mpango kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto wa mwaka wa fedha 2024/2025 hadi 2028/2029, ambao moja ya kipaumbele ni kupunguza mimba za utotoni kwa 50% ifikapo Mwaka 2029, inaunda madawati ya ulinzi na usalama wa mtoto katika shule za

msingi na sekondari, inawakumbusha wazazi au walezi wajibu wao wa msingi wa kulea na kutunza watoto na imefanya marekebisho ya Sheria ya Elimu na Sheria ya Mtoto kwa kuongeza adhabu kwa wanaowapa watoto mimba, watoto na wazazi wasiotunza na kulea watoto.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwantumu Dau.

**MHE. MWANTUM DAU HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nimeridhika na majibu ya Serikali, ninashukuru ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Amina.

**MHE. AMINA DAUD HASSAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa, Serikali imeamua kuwarejesha wanafunzi waliopata mimba za utotoni shuleni. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwawekea mazingira mazuri ili kuepuka kunyanyapaa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Amina kwa kujali na kumuunga mkono Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuwarejesha watoto waliopata changamoto kwenye masomo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan imeelekeza watoto wote wanaopata changamoto za mimba za utotoni, baada ya kujifungua warudi shuleni. Mheshimiwa Rais akaliona hilo na akaelekeza mikoa yote ya Tanzania zijengwe shule za bweni, ili watoto hawa waweze kunusurika na kuondokana na changamoto za mimba za utotoni na ukatili. Ahsante. *(Makofi)*.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, angalizo. Serikali inasema imefanya marekebisho ya Sheria ya Elimu ya Sheria ya

Mtoto kwa kuongeza adhabu kwa wanaowapa Watoto ujauzito na wazazi wasiotunza na kulea watoto. Kwa maana wananchi na wazazi wanahusika kulea watoto wao.

Ahsante Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri. Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Mwakibete.

Na. 193

**Ujenzi wa Barabara Inayounganisha Jimbo la Busokelo Hadi Mbeya**

**MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE** aliuliza:-

Je, lini Barabara inayounganisha Jimbo la Busokelo na Mbeya yenye kilometa 28, itajengwa ili wananchi wasisafiri umbali mrefu kupitia Suma hadi Katumba?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara inayounganisha Jimbo la Busokelo na Mbeya, kupitia Halmashauri ya Busokelo, inajulikana kwa jina la *Number One* – Lugombo, yenye urefu wa kilometa 30. Barabara hii ni ya Wilaya iliyokasimiwa *TANROADS* kutoka *TARURA* mwaka 2023. Serikali imepanga katika mwaka wa fedha 2026/2027 kuanza maandalizi ya kuijenga barabara hii kwa kuifanyia upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ili ijengwe kwa kiwango cha lami. Kwa sasa, Serikali inaendelea kuifanyia barabara hii matengenezo ya kawaida ili iweze kupitika katika majira yote ya mwaka.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwakibete.

**MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, nitoe pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kutoa fedha kujenga

Barabara ya kutoka Katumba – Suma – Mpombo – Isange mpaka Ruangwa kwa kiwango cha lami. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais katika historia hii imeandikwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; Barabara hii ya *Number One* – Ngumburu imefungwa kutokana na mvua nyingi zinazonyesha na hakuna gari wala pikipiki inayopita katika barabara hii. Je, Serikali ina mpango gani wa dharura wa kuhakikisha barabara hii inafunguliwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Barabara kutoka Kandete Mjini – Luteba nayo imefungwa kutokana na mvua nyingi zinazoendelea kunyesha katika Jimbo hili la Busokelo. Je, Serikali ina mpango gani pia wa kupeleka vifusi, kwa ajili ya kufungua Barabara hii ya Kandete – Luteba? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI**: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mwakibete, yote kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii, kama nilivyosema, imekasimiwa *TANROADS* na ilikuwa ni barabara ya udongo. Kwa hiyo, tumeshaomba fedha za dharura na katika kipindi hiki ambacho mvua zinaendelea kunyesha, nyingi sana, katika huo ukanda. Nitumie nafasi hii kumwelekeza Meneja wa Mkoa wa Mbeya aende akafanye tathmini ya barabara zote mbili ambazo zimefungwa; na Kwa kuwa, wakandarasi wako jirani waweze kutusaidia kufungua na kama kutakuwa na changamoto inayohitaji nguvu kutoka Wizarani, basi aweze kutoa taarifa haraka, lakini ikiwezekana leo aende, ili akafanye tathmini na barabara hizo zote mbili ziweze kufunguliwa. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Issay.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kipande cha Barabara kati ya Mbulu – Garbabi hadi Hydom imekuwa na changamoto kubwa sana kwa wananchi katika

kipindi hiki cha mvua; na Kwa kuwa, mkandarasi wa Kichina ametekeleza kipande hicho. Je, Serikali inatoa kauli gani kumwagiza yule mkandarasi kwenda kujenga barabara ya kawaida ya wananchi ili wananchi waendelee kupata huduma? Ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, suala lina Wabunge wengi. Nikuombe ujibu kwa usahihi, lakini kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ziko barabara ambazo zilikuwa ziko na wakandarasi na zikawa zimesimama kwa sababu ya kutokulipa, ama *advance payment* ama *certificate,* kwa maana ya hati ambazo walikuwa wanazidai. Ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wengine kwamba, tayari Serikali imeshaanza kupeleka fedha na mkandarasi huyo aliyemtaja wa Mbulu – Garbabi, tayari ameshapelekewa *advance,* ameshapelekewa malipo ya *certificate,* ambayo alikuwa ameomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe wito kwa mameneja wote kwamba, pale ambapo pana wakandarasi wajibu wao ni kuhakikisha kwamba, zile barabara zinapitika, ziwe barabara kubwa zile ama za michepuko ili tusikatishe mawasiliano ambayo yapo. Ni wajibu wa wakandarasi na ipo kwenye mikataba yao, ikiwepo na Barabara ya Mbulu – Garbabi. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nancy.

**MHE. NANCY H. NYALUSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Kinyanambo – Madibira ni barabara ya kimkakati. Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara hii? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI**: Mheshimiwa Naibu Spika, barabara aliyoitaja imeshafanyiwa usanifu. Serikali inaendelea kutafuta fedha, kwa ajili ya kuanza kuijenga kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maimuna.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa nafasi hii. Ni lini Serikali itatenga fedha, kwa ajili ya ujenzi wa kiwango cha lami barabara ambayo inaunganisha Mkoa wa Mtwara na Lindi kupitia Mtama – Kitangali hadi Newala, kilometa 74? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI**: Mheshimiwa Naibu Spika, barabara aliyoitaja amekuwa anaiulizia mara kwa mara. Ni barabara ambayo tayari tumeshajenga maeneo baadhi korofi kwa vipande vile ambavyo vinasumbua, lakini mpango ni kuijenga barabara hiyo yote kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kamonga.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara kipande kinachoanzia Itoni hadi Lusitu imekuwa na hali mbaya sana kwa sasa na kusababisha kero kwa wananchi. Je, ni lini Serikali itamaliza majadiliano na mkandarasi, ili aendelee kufanya kazi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mkandarasi wa Itoni – Lusitu tayari tumeshamlipa sehemu ya malipo yake. Kwa hiyo, tunamwagiza Meneja wa Mkoa wa Njombe ahakikishe anamsimamia, ili aweze kwenda kazini na ahakikishe kwamba, ile barabara ambayo ilikuwa imekwama maeneo yote anayafungua na wananchi wasipate hiyo changamoto. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tarimo, wajiandae Mheshimiwa Bupe, Mheshimiwa Amar na Mheshimiwa Sanga.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, Mheshimiwa Rais ameshatoa fedha, kwa ajili ya kilometa 11

za njia mbili Barabara ya Moshi – Arusha, kipande cha Maili Sita mpaka Kiboroloni, Moshi; na Kwa kuwa, *TARURA* nao wana fedha, kwa ajili ya kutengeneza barabara ya njia mbili kutoka *NBC Roundabout* mpaka *YMCA* na tutapata fedha, kwa ajili ya *YMCA – KCMC*. Je, mko tayari kukaa na *TARURA,* ili kutengeneza *design* nzuri ya *Roundabout* ya *YMCA?* Ninashukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI**: Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wote taasisi hizi mbili zinashirikiana kwa ukaribu sana, *TARURA* na *TANROADS,* kwa sababu, barabara zao zinahusiana sana. Ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na niwape maelekezo watendaji wakuu wa hizi taasisi, kama tupokee ujumbe wa Mheshimiwa Mbunge, wakae na washirikiane. Ikiwezekana, kama una mawazo tukukaribishe ili uweze kutoa mawazo yako nini unafikiri kinaweza kikafanyika kwa ubora zaidi. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bupe, wajiandae Mheshimiwa Amar na Mheshimiwa Sanga.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini Serikali itajenga Barabara ya kutoka Namanyele Mjini – Kipili kwa kiwango cha lami? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, hii barabara tulishakamilisha usanifu. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, nina hakika katika bajeti ambayo tutakuja kuisoma hapa pia, itaonekana, kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Amar, jiandae Mheshimiwa Sanga.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, kipande cha Barabara inayotoka Kahama kuunganisha Sengerema

kuanzia Nyangulongo – Bukwimba – Karumwa – Nyidundu – Bosolwa hadi Wingi Tatu chenye kilometa 70, sasa hivi barabara ile ni mbovu sana. Je, unaweza ukamwelekeza Meneja wa *TANROADS,* Mkoa wa Geita, apeleke mashine ili kuweza kukwangua barabara ile?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara zote zinatakiwa zipitike na kama barabara hii imefungwa kwa upande wa Mkoa wa Geita kwa sababu, ninajua ina kipande cha Mwanza – Shinyanga na Geita. Ninamwelekeza Meneja wa Geita aende akafanye tathmini na kupeleka mitambo, ili barabara hiyo iweze kufunguliwa katika kipindi hiki cha mvua. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sanga.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Madihani – Busokelo – Kitulo – Busokelo ni barabara ambayo *TANROADS* mlianza kujenga, lakini imesimama. Ni ipi Kauli ya Serikali kujenga barabara hii, ili ikamilike wananchi wasizunguke Mbeya kuelekea Busokelo, waweze kukatisha?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli, eneo hili analolisema ni eneo ambalo lina mvua nyingi na ni la miinuko. Kwa hiyo, wamesimama si kwa sababu hawapo, lakini kwa sababu wanapisha hii hali ya hewa ambayo hata wakijenga leo, barabara yote inaweza kuondolewa. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, mpango upo na wakandarasi wataendelea kuijenga hiyo barabara. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Mheshimiwa Njelu Kasaka.

Na. 194

**Barabara ya Makongolosi hadi Mkiwa**

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE K.n.y. MHE. MASACHE NJELU KASAKA** aliuliza:-

Je, lini Selikali itaanza kujenga kwa kiwango cha lami Barabara ya kuanzia Makongolosi hadi Mkiwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Makongolosi – Rungwa – Itigi – Mkiwa yenye urefu wa kilometa 413 ni sehemu ya Barabara ya Mbeya – Lwanjilo – Chunya – Makongolosi – Rungwa – Itigi – Mkiwa yenye urefu wa kilometa 524. Ujenzi wa barabara hii unafanyika kwa awamu, ambapo sehemu ya Mbeya hadi Makongolosi, kilometa 111, ujenzi umekamilika. Sehemu ya Noranga – Itigi, Mlongoji, kilometa 25 ujenzi unaendelea na umefikia 76% na sehemu ya Itigi, Mlongoji – Mkiwa, kilometa 31.57, mkandarasi yupo kwenye maandalizi ya kuanza kazi. Kwa sehemu iliyobaki ya kutoka Makongolosi hadi Noranga, kilometa 356.43 Serikali inaendelea kutafuta fedha za kuendelea na ujenzi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jumbe.

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; wananchi wa Chunya na Wanambeya kwa ujumla wangetamani sana kuona barabara hii inaanza kujengwa mara moja na hasa ikianzia upande wa Chunya. Je, Serikali itaanza lini ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami kutokea Makongorosi – Lupa – Mkiwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Wilaya ya Chunya haijaunganishwa na Mkoa wa Songwe kwa lami na eneo hilo ni lile linalounganisha Mbalizi na Makongolosi. Ni lini barabara ya

kutoka Mbalizi – Makongolosi ikienda mpaka Mkwajuni, itaanza kujengwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge ambaye ameuliza swali kwa niaba ya Mbunge wa Chunya. Tunatambua kama Wizara kwamba sera ni kuunganisha mikoa yote kwa kiwango cha lami; na kati ya barabara kubwa ambazo zimebaki, ambazo pia ni *trunk,* barabara kuu, ni hii ya Chunya kwenda Itigi na vilevile Barabara ya Chunya kwenda Tabora kupitia Ipole.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuendelea kujenga kwa hatua kulingana na upatikanaji wa fedha ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba mpango wa Serikali ni kutafuta chanzo cha uhakika cha fedha ili barabara hiyo iweze kuunganishwa mikoa Nyanda za Juu Kusini na mikoa ya Kaskazini. Tunaiona kama ni barabara moja muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, kwa swali la pili pia tayari tumeishaanza, tumekwishatangaza kuanzia Mbalizi kwenda Mkwajuni na pia kuanzia Mkwajuni kwenda Mbalizi ili kuanza kujenga kipande hicho kwa lami. Kwa kutambua umuhimu huo Mheshimiwa Mbunge atakubaliana na nami kwamba tulikuwa na changamoto ya madaraja mawili makubwa ambayo yalikuwa yanasumbua, madaraja ya Lupa – Tinga na Binti Manyanga ambapo tayari Mheshimiwa Samia amekwishatoa fedha kwa ajili ya kuyajenga hayo madaraja ili kusiwe na mkwamo tena.  Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Oran.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni lini Serikali itaanza kujenga kwa kiwango cha lami kilometa 22 za Barabara ya Isyonje – Kikondo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii inakwenda hadi Makete. Tumekwishaanza upande wa Makete na katika mwaka huu tunategemea fedha ili tuanze pia upande wa Mbeya kwenda Makete ili tuweze kukamilisha hicho kipande chote. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtenga, Mtenga.

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Mtwara Mjini kuna barabara ambayo ilijengwa na *TANROAD* kutoka *keep left* hadi bandarini na barabara ile iliharibiwa na Kiwanda cha Dangote ambao walikuwa wanapitisha mitambo mikubwa. Tukalalamika na Serikali wakasema kwamba watazungumza na watu wa Dangote ili warekebishe barabara ile. Je, ni lini watakuja kuirekebisha barabara ile?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimwelekeze Meneja wa *TANROAD* Mkoa wa Mtwara. Pia nitawasiliana na Mheshimiwa Mbunge ili tujue changamoto iliyokuwepo. Tuliijenga barabara hiyo na Dangote ni kwa nini kama aliamuliwa ajenge na hajajenga ili tuweze kutoa majibu ya uhakika. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nyoka, umekwishaitwa.

**MHE. MARIAM M. NYOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni lini Barabara ya kutoka Lizaboni – Londoni – Lupapila hadi Litapwasi itajengwa kwa kiwango cha lami? Ninakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, sijalisikia hilo jina la hiyo barabara.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mariam, uliza tena swali lako. Washa *microphone* yako. Akili iko Jimboni nini?

**MHE. MARIAM M. NYOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kutoka Lizaboni kwenda Londoni – Lupapila hadi Litapwasi kwa kiwango cha lami.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, hii barabara kwanza tunakamilisha usanifu. Tulitambua kwamba kuna shida kubwa sana ya kuvuka mto mitoni. Tunavyoongea sasa hivi hilo daraja ambalo ndilo lilikuwa changamoto kubwa tunalijenga kuanzia sasa na wakandarasi wako *site*. Kwanza tukamilishe hiyo ili ipitike halafu tuanze mipango ya kuijenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami. ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Suma Fyandomo.

Na. 195

**Upungufu wa Magari ya Polisi Mkoa wa Mbeya**

**MHE. SUMA I. FYANDOMO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka magari kwenye vituo vya Polisi Mkoani Mbeya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Jeshi la Polisi hugawa vitendea kazi kama magari kwa uwiano sawa katika mikoa yote hapa nchini. Katika ugawaji huo pia huzingatia ukubwa wa eneo, wingi wa watu, shughuli za kiuchumi, matukio ya uhalifu na wingi wa makosa ya usalama barabarani. Katika mwaka wa fedha 2023/2024 na 2024/2025 Mkoa wa Mbeya umepata magari mapya 12, hivyo kufanya kuwa na jumla ya magari 43 yanayofanya kazi. Serikali itaendelea kutenga fedha

toka kwenye bajeti kila mwaka kwa ajili ya kununulia vitendea kazi kwa ajili ya Jeshi la Polisi ikiwemo magari. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Suma.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa niishukuru Serikali kwa namna ambavyo imetupatia hizo gari 12. Hata hivyo, Mkoa wa Mbeya ni mkoa ambao ni mkubwa sana. Pamoja na gari hizo 12 Wilaya ya Rungwe kuna gari ya *double cabin* ambayo Serikali wametupatia. Gari hiyo haiwezi kutosheleza mahitaji kwa sababu kama kumetokea uhalifu, mauaji, gari haiwezi hiyo ya *double cabin* kupakia mwili wa marehemu. Vilevile, Busokelo hakuna gari. Ukienda Mbarali kuna shida kwa sababu gari ipo moja ambayo ni nzima na inatakiwa ifike mpaka kule Madibila, Chimala, Lwiwa na Luhanga, lakini gari hakuna. Pamoja na hayo, Mbeya Mjini kuna gari lakini gari hizo hazitoshelezi. *Mbeya DC* hakuna gari kabisa. Mbalizi nako ni Mji mkubwa sana na hivyo kunakuwa na uhalifu wa mara kwa mara; bado Uyole hakuna gari yoyote, mpakani mwa Inyala hakuna gari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakwenda kuuliza swali langu la kwanza; Chunya ni kubwa mno ipo mpaka mpakani mwa Tabora hakuna gereza, gari hiyo hiyo itumike kutafuta waharifu lakini ipeleke watuhumiwa Mbeya Mjini. Je, ni lini Serikali itapeleka magari ya kutosheleza mahitaji ya Mkoa wa Mbeya?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; Mkoa wa Mbeya pale kwa masikitiko makubwa, pamoja na gari hizo ambazo zipo *service* inapelekwa fedha kiasi cha shilingi milioni moja na laki tano kwa mkoa mzima, ndizo zinapelekwa pale, ilhali magari 10 ni mabovu na yanatakiwa kutengenezwa pesa hakuna lakini pamoja na hilo magari ambayo ni mabovu kabisa hayatengenezeki yapo 11…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Suma, Waziri ameshakuelewa.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, lakini Ziwa Nyasa kule kuna *boat* ambalo linatakiwa

kukamata wahalifu, *boat* lile limeharibika muda mrefu, ninaomba Serikali iseme hapa itatengeneza lini magari? *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ahsante, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana kwa maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Mbeya. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum kwa ufatiliaji wake mkubwa kuhusiana na vitendea kazi katika Mkoa wa Mbeya yakiwemo magari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nijibu maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kweli tunajua kwamba Mkoa wa Mbeya ni mkubwa, na ndiyo maana ndani ya miaka miwili, mwaka wa fedha 2022/2023 na 2024/2025 tumepeleka gari 12. Hata hivyo, bado mahitaji ni makubwa. Nimhakikishie Mbunge kwamba Serikali ya Awamu ya Sita imeboresha sana vitendea kazi katika vyombo vyetu vya ulinzi na usalama likiwemo Jeshi la Polisi. Kwa hiyo bado Mkoa wa Mbeya utaendelea kuangaliwa kwa jicho la tofauti kwa ukubwa wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *service* ya magari; ni kweli fedha hutengwa kila mwaka kwa ajili ya *service* ya magari. Nimhakikishie kwamba Jeshi la Polisi lipo makini litaendelea kufanya *service* ya magari hayo ili yaweze kuhudumia wananchi wa Mbeya na Wilaya zote ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitaja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa maswali yamekwisha na muda wetu umekwisha, sasa ni matangazo. Wageni waliopo Bunge asubuhi hii:-

Wageni waliokaa Jukwaa la Spika, wageni 20 wa Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Waziri wa Katiba na Sheria, Ndugu Eliakim Maswi, Katibu Mkuu wa Wizara; Ndugu

Franklin Rwezimula, Naibu Mkuu Wizara; na Profesa Elisante Ole Grabriel Mtendaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania, ahsante. *(Makofi)*

Yupo Mheshimiwa Jaji Mstaafu Mathew Pauwa, Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; Ndungu Saulo Malauri, Mwenyekiti wa Bodi ya Huduma ya Msaada wa Kisheria; Dkt. Mary Levira, Mwenyekiti wa Baraza la Chuo cha Uongozi wa Mahakama; Mheshimiwa Jaji Winfrida Karroso, Mwenyekiti wa Tume ya Kurekebisha Sheria. *(Makofi)*

Yupo Mheshimiwa Mohamed Hamad, Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; Mheshimiwa Eva Nkya, Msajili Mkuu wa Mahakama; Ndugu Sylivester Mwakitalu, Mkurugenzi wa Mashtaka; Dkt. Ally Posi, Wakili Mkuu wa Serikali; Profesa Sist Mramba, Mkuu wa Taasisi Mafunzo ya Uanasheria wa vitendo Tanzania *(Law School of Tanzania);* Mheshimiwa Samweli Maneno, Naibu Mwanzasheria Mkuu wa Serikali. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Frank Kanyusi Frank, Kabidhi Wasii Mkuu na Mtendaji Mkuu wa *RITA;* Ndungu George Mandepo, Katibu Mtendaji Tume ya Kurebisha Sheria; Ndugu Patience Ntwina, Katibu Mtendaji Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; Ndugu Onorius Njole, Mwandishi Mkuu wa Sheria; na Ndugu Onesmo Olengurumwa, Mratibu wa Kitaifa wa Mtandao wa Haki za Kibinadamu Tanzania. *(Makofi)*

Wapo pia viongozi wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Ruvuma; yupo Ndugu Odo Mwisho, Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Ruvuma; Ndugu Mohamed Halfani, Katibu wa CCM Mkoa wa Ruvuma; Ndugu Malko Mbawala, Mwenezi Wilaya ya Songea. *(Makofi)*

Wageni wengine ni, familia ya Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro; Ndugu Florah Mdima, mke wa Mheshimiwa Ndumbaro; Ndugu Raphael Ndumbaro, mtoto wa Mheshimiwa Ndumbaro; Ndugu Daniel Ndumbaro, mtoto wa Mheshimiwa Ndumbaro; na Ndugu Brian Ndumbaro, mtoto wa Mheshimiwa Ndumbaro. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Jumanne Abdallah Sagini, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria ambao ni Sekretarieti ya CCM kutoka Wilaya ya Butiama; Ndugu Christopher Marwa, Mwenyekiti wa CCM Wilaya; Ndugu Mary Kananda, Katibu wa CCM Wilaya; na Ndugu Abuu Kawawa, Katibu Mwenezi Wilaya. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Sagini ni familia yake ambao ni, Ndugu Mariam Sagini, Mke wa Mheshimiwa; na Ndugu Leyla Sagini, Mtoto wa Mheshimiwa. Ahsanteni. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; Wageni 120 wa Mheshimiwa William Lukuvi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) ambao ni wapiga kura wake kutoka Isimani Mkoani Iringa, wakiwemo Wenyeviti wa Matawi wa CCM Jimbo la Isimani, Makatibu wa Matawi CCM Isimani, Makatibu Wenezi wa Matawi Isimani. *(Makofi)*

Wageni 46 wa Mheshimiwa George Simbachawene, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Utumishi na Utawala Bora, Watumishi wa Kata ya Pwaga kutoka Kibakwe Mkoani Dodoma. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Jumaa Hamidu Aweso, Waziri wa Maji, ambaye ni Ndugu Akida, Mtoto Mwenyekiti wa Shina la Stahabu Pwani kutoka Wilaya ya Pangani Mkoani Tanga. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, rafiki zake kutoka Katumba Tukuyu Mkoani Mbeya. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, ndugu zake kutoka Mlalo Mkoani Tanga, Ndugu Zainab Shangazi na Ndugu Ummy Shangazi. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Festo Richard Sanga ambao ni ndugu zake kutoka Mkoani Iringa. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda ambao ni wajumbe wa Bodi ya Umoja wa Wakulima wa Maparachichi Rungwe na Chama cha Ushirika wa Kilimo na Masoko kutoka Rungwe Mkoani Mbeya. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, marafiki zake kutoka Kibaha, Mkoa wa Pwani. *(Makofi)*

Wageni sita wa Joseph Zacharius Kamonga, Mtetezi wa Mama kutoka Ludewa, Mkoa wa Njombe. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo:-

Wapo Ndugu Joseph Mkakanze na Ndugu Joseline Mkakanze kutoka Ntyuka Mkoani Dodoma. *(Makofi)*

Wengine ni viongozi 60 wa Serikali ya wanafunzi kutoka Taasisi ya Uhasibu Tanzania *(TIA)* ya Jijini Dar es Salaam.

Katibu.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Mwongozo wa Spika.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa mujibu wa Kanuni Namba 76, ninaomba nisiisome kwa ajili ya muda; ningependa kuomba mwongozo wako kutokana na suala la mawasiliano ambalo nimeuliza katika swali la nyongeza, swali Namba 190. Suala hili pia niliwahi kuuliza Bunge lililopita na Mheshimiwa Spika akalitolea maelekezo kwa Waziri ili alifanyie kazi**.**

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeendelea kutumia maelekezo yao, pale ambapo inatokea changamoto ya jina lako kutumika katika utapeli, wanasema tutoe taarifa kwenye simu namba 15040 ambayo ni ya *TCRA*, unatuma kwa *SMS*. Kila tukituma wanapokea na wanasema wanashughulikia. Tangu nimeripoti, leo hii sasa tena nimeshapata malalamiko zaidi ya matano kwamba watu wanatapeliwa kwa jina langu na wanahusisha Ofisi ya Rais ya kwamba pengine kuna *tender* kwa Mheshimiwa Rais

na mimi ndiyo ninaisimamia kwa hiyo, watu wanatakiwa waende. Pia, wanahusisha Waziri Mkuu na ofisi mbalimbali za Serikali, na jina linalotumika ni jina langu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hili limekuwa la muda mrefu. Wakati niko Waziri nilishatoa *Press Release* kwani jina hili pia lilikuwa linatumika lakini hakuna hatua zinazochukuliwa ili kuweza kukomesha hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ningependa kujua, nini kauli ya Serikali kutokana na hawa matapeli ambao wanatufanyia uadui katika jamii kwa sababu mtu anaibiwa pesa anajua umehusika kumbe hukuhusika. Kwangu mimi limekuwa ni mateso zaidi kwa sababu ni mengi. Waheshimiwa Mawaziri nimewashirikisha, tangu Mheshimiwa Waziri Nape na Waziri ambaye yupo sasa, lakini hakuna hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba mwongozo wako. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, swali hili ni la siku nyingi sana. Mheshimiwa Naibu Waziri nilikuomba uonane na mhusika takribani sasa wiki ya pili lakini bado linaendelea.

Sasa mwongozo wangu ni kwamba, nikuombe Waziri wa Mawasiliano uonane na Mheshimiwa Mjumbe mjaribu kuli-*sort out* na mtafute njia ya kumsaidia. *(Makofi)*

Waheshimiwa tunaendelea.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia taarifa zilizowasilishwa leo katika Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria; Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti. Ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako sasa likubali kupokea, kujadili na kupitisha Mpango na Makadirio na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema kwa kutujaalia afya njema na kutuwezesha kukutana hapa leo kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na mwelekeo wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima na taadhima ninaomba kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kuniteua kwa mara ya pili kuongoza Wizara ya Katiba na Sheria. Ninaahidi kuitumikia nafasi hii kwa uaminifu na uadilifu ili kuwaletea maendeleo Wananchi na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa umahiri wake katika kuiongoza nchi yetu. Katika kipindi cha uongozi wake tunaendelea kushuhudia maendeleo na mafanikio makubwa katika Sekta mbalimbali ikiwemo Sekta ya Sheria. Ninaomba niungane na Waheshimiwa Wabunge na wananchi wenzangu kuendelea kumwombea Rais wetu kwa Mwenyezi

Mungu amjalie afya njema, hekima na busara katika kuliongoza Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa unyenyekevu mkubwa ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kupitishwa na Chama Cha Mapinduzi kuwa Mgombea wa Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kipindi cha Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ninapenda kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Balozi Emmanuel John Nchimbi, Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi kwa kuteuliwa kuwa Mgombea Mwenza na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuwa Mgombea wa Urais wa Zanzibar. Vilevile ninapenda kumpongeza ndugu Stephen Masato Wasira kwa kuchaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa CCM Tanzania Bara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nitumie fursa hii pia kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Phillip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa uongozi kwa wao mahiri na kwa ushirikiano mkubwa ninaoupata kutoka kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa Mbunge, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwasilisha hotuba ambayo imefafanua utendaji wa Serikali kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na kutoa mwelekeo wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Aidha, ninawapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote waliowasilisha Hotuba za Bajeti za Wizara wanazozisimamia kwa mawasilisho yao mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye pia ni Rais wa Mabunge ya

Dunia, pia na wewe kwa kuliongoza Bunge kwa umahiri na weledi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutumia fursa hii kuwapongeza Mawaziri walioteuliwa na Mheshimiwa Rais kutekeleza majukumu katika Wizara mbalimbali katika kipindi cha kuanzia Julai, 2024 hadi Machi, 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipekee ninapenda kumpongeza bwana Eliakim Chacha Maswi kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria. Kwa dhati kabisa ninakiri kuwa kupitia utendaji kazi wake mahiri na mzuri ndugu Maswi, amekuwa msaada mkubwa katika kuboresha Sekta ya Sheria, ambapo kwa kipindi kifupi cha takribani miezi tisa tangu alipoteuliwa kuwa Katibu Mkuu amewezesha maboresho mbalimbali kwa Wizara na Taasisi za Wizara na hivyo kuchochea ufanisi katika utendaji kazi na kuimarisha upatikanaji haki kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uzoefu wangu kama Waziri sina shaka kumtamka bwana Eliakim Maswi kuwa ni miongoni mwa Makatibu wakuu bora kufanya nao kazi. Huwa ninajisikia faraja kufanya kazi na Katibu Mkuu wa aina yake, kwa kuwa ndani ya muda mfupi mnaweza kufanya maboresho makubwa na yanayoonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uteuzi wa bwana Eliakim Chacha Maswi kuwa Katibu Mkuu na Dkt. Franklin Jasson Rwezimula kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria ni ishara ya imani kubwa aliyonayo Mheshimiwa Rais juu ya utendaji kazi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ilipokea kwa masikitiko makubwa taarifa ya kifo cha Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kigamboni na Mkurugenzi Mteule wa Shirika la Afya Duniani Kanda ya Afrika, kilichotokea tarehe 27 Novemba, 2024. Wizara inawapa pole familia ya marehemu, Wananchi wa Jimbo la Kigamboni na

Watanzania kwa ujumla. Mwenyezi Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nyakati tofauti nchi yetu imekumbwa na ajali na maafa katika maeneo mbalimbali zilizosababisha vifo, majeruhi, uharibifu wa mali na mazingira. Itakumbukwa tarehe 16 Novemba, 2024 kulitokea maafa ya kuanguka kwa jengo la ghorofa nne katika eneo la Kariakoo, Jijini Dar es Salaam na kusababisha vifo, majeruhi na upotevu wa mali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee natoa pole kwa waathirika wa tukio hili na kumwomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. Amina. Aidha, nitoe pole kwa waathirika na manusura wote wa matukio yote yaliyotokea nchini katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 umezingatia Dira ya Maendeleo ya Taifa ya Mwaka 2025 na miongozo mbalimbali ya kitaifa na kimataifa ikiwemo; Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Dunia (2030); Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2021/2022 - 2025/2026); Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020; na Maelekezo ya Viongozi Wakuu wa Serikali pamoja na Mipango Mikakati ya Wizara na Taasisi zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ilibainisha masuala ya kipaumbele ambayo yameainishwa kwenye Ibara ya 18 katika Kitabu cha Hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara pamoja na Taasisi zake ilipanga kukusanya maduhuli yenye jumla ya shilingi 12,676,199,000. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025 Wizara na Taasisi zake imekusanya jumla ya shilingi 9,036,054,037 sawa na 71.28% ya lengo la makusanyo ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na 85.54% kwa lengo la kipindi cha miezi 10.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara iliidhinishiwa jumla ya shilingi 486,296,754,555 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi 112,497,549,000 ni kwa ajili ya mishahara ya Watumishi, shilingi 228,180,396,571 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na shilingi 145,597,319,000 ni kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025, Wizara imepokea jumla ya shilingi 391,960,643,596.72 sawa na 80.60% ya iliyoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2024/2025. Kati ya fedha hizo zilizopokelewa, shilingi 94,741,018,477.30 ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi, shilingi 193,647,671,495.78 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na shilingi 103,571,953,623.64 ni fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Tunaishukuru sana Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mtiririko wa fedha mzuri kwa Wizara na Taasisi zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa majukumu kwa kuzingatia vipaumbele ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inaendelea kutekeleza Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia *(Mama Samia Legal Aid Campaign*). Tangu kuzinduliwa kwa Kampeni hii tarehe 27 Aprili, 2023, jumla ya Mikoa 25 ya Tanzania Bara imefikiwa na Kampeni. Mikoa hiyo ni: Dodoma, Manyara, Shinyanga, Ruvuma, Simiyu, Singida, Iringa, Mara, Songwe, Morogoro, Njombe, Katavi, Tabora, Geita, Kigoma, Mtwara, Mwanza, Kilimanjaro, Mbeya, Lindi, Rukwa, Pwani, Arusha, Tanga, na Kagera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhitimisha nchi nzima, kwa upande wa Tanzania Bara Mkoa uliobaki ni Dar es Salaam ambapo Kampeni itatekelezwa mwanzoni mwa mwezi Juni, 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Tanzania Zanzibar utekelezaji wa Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia umefanyika katika Mikoa mitatu ambayo ni: Kaskazini Pemba,

Mjini Magharibi, na Kaskazini Unguja. Aidha, mikoa ya Kusini Pemba na Kusini Unguja Kampeni itatekelezwa sasa na itakamilka ndani ya mwezi huu wa tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa Kampeni hii wananchi wamepatiwa huduma mbalimbali ikiwemo elimu kuhusu masuala ya haki na wajibu; umiliki na utatuzi wa migogoro ya ardhi; matunzo ya watoto; ukatili wa kijinsia na haki za binadamu. Kupitia Kampeni hii, jumla ya Mikoa 25 ya Tanzania Bara na Halmashauri 179, Kata 1,907 na Vijiji na Mitaa 5,702 zilifikiwa na jumla ya wananchi 2,698,908 (Wanaume 1,347,325 na Wanawake 1,351,583) walifikiwa na kupata elimu, huduma na msaada wa kisheria kupitia mikutano ya ana kwa ana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia ya Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia, jumla ya migogoro 24,691 iliyodumu kwa muda mrefu ilipokelewa ambapo baadhi ilidumu kwa zaidi ya miaka kumi. Utatuzi wa migogoro hiyo umewezesha kuimarisha amani, utulivu na utengamano miongoni mwa wanajamii. Migogoro hii ilihusisha masuala ya ardhi, ndoa za utotoni, matunzo ya watoto, ndoa, jinai na ukatili wa kijinsia. Aidha, jumla ya migogoro 5,704 ilitatuliwa na kuhitimishwa kwa njia mbadala kati ya migogoro 23,399 ya muda mrefu iliyopokelewa. Utatuzi wa migogoro 18,987 unaendelea katika ngazi mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuimarisha uratibu wa huduma za msaada wa kisheria katika ngazi ya Halmashauri, Kata, Vijiji na Mitaa, Wizara imeanzisha Madawati ya Msaada wa Kisheria katika Mamlaka za Serikali za Mitaa Tanzania Bara 184. Madawati hayo yanasaidia kusogeza huduma za msaada wa kisheria kwa wananchi pamoja na uendelevu wa huduma ya msaada wa kisheria nchini kote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeandaa Rasimu ya Sera ya Taifa ya Jinai na Mkakati wa utekelezaji wa Sera hiyo. Lengo la Sera hii ni kuhakikisha kunakuwa na Mfumo Jumuishi wa Ushughulikiaji wa Masuala ya Haki Jinai. Sera hiyo inatarajiwa kuidhinishwa na Serikali katika Mwaka wa Fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara ilitoa mafunzo ya elimu ya uraia na utawala bora kwa wajumbe wa Kamati za Usalama za Mikoa na za Wilaya; Watendaji wa Kata; na Menejimenti na Wataalamu katika Halmashauri 122 zilizopo katika mikoa 17. Aidha, katika kujenga kizazi chenye uzalendo, maadili na uwajibikaji kwa nchi, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwemo Ofisi ya Rais TAMISEMI; na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, iliandaa maudhui ya Elimu ya Katiba na Uraia kwa Shule za Awali, Msingi, Sekondari na Vyuo vya Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kuiwakilisha Serikali katika mikutano mbalimbali ya kisheria ya kikanda na kimataifa katika Sekta ya Sheria. Ikiwemo Mkutano wa kawaida wa Kumi wa Kamati Maalum ya Mawaziri wa Sheria na Haki ya Umoja wa Afrika uliofanyika Zanzibar. Katika mkutano huo, Tanzania ilichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati hiyo. Aidha, nafasi hii inatoa fursa kwa nchi kuwasilisha na kupitisha *agenda* zake kwa maslahi ya Taifa. Mikutano mingine imeainishwa kwenye Ibara ya 43 na 44 katika Kitabu cha Hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuongeza kasi ya utendaji kazi, Mahakama imeendelea kuongeza idadi ya Maafisa Mahakama. Katika mwaka wa fedha 2024/2025, jumla ya Majaji 10 wameteuliwa na hivyo kufanya idadi ya Majaji waliopo kufikia 146. Vilevile, Mahakimu 91 wameajiriwa na hivyo kufanya idadi ya Mahakimu kufikia 1,426.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 kulikuwa na jumla ya mashauri 238,154 mahakamani, kati ya hayo 63,050 yalikuwepo mwanzoni mwa Julai, 2024 na mashauri 175,104 yalifunguliwa katika kipindi husika. Kati ya mashauri 238,154 yaliyokuwepo, mashauri 174,581 yalisikilizwa na kuhitimishwa na mashauri 63,573 yanaendelea katika hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai 2024, hadi Aprili 2025, ujenzi na ukarabati wa majengo mbalimbali ya mahakama unaendelea. Ambapo ujenzi wa jengo la Makao

Makuu ya Mahakama na Nyumba za Makazi ya Majaji Jijini Dodoma umekamilika na ulizinduliwa na Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukarabati wa majengo ya zamani Mahakama Kuu Dodoma na Mahakama Kuu Iringa unaendelea. Pia, ujenzi wa vituo jumuishi vya utoaji haki unaendelea katika Mikoa tisa ifuatayo: Katavi, Njombe, Ruvuma, Songwe, Singida, Geita, Simiyu, Lindi na Pemba. Ujenzi wa Mahakama za wilaya unaendelea katika wilaya 11 na Mahakama za Mwanzo 72 katika mikoa mbalimbali nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Utumishi wa Mahakama ilipokea na kutolea uamuzi mashauri 27 ya nidhamu ambapo kati ya mashahuri hayo, saba yaliwahusu Maafisa wa Mahakama na 20 watumishi wasio Maafisa wa Mahakama. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025, Tume imeratibu utendaji wa Kamati za Maadili za Maafisa wa Mahakama katika mikoa nane ambayo ni, Arusha, Manyara, Iringa, Pwani, Mtwara, Lindi, Njombe, na Ruvuma. Wizara kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, imeendelea kuhakikisha kuwa sheria za nchi zinakwenda na wakati na zinaakisi sera na vipaumbele vya Serikali katika nyanja za kisiasa, kiuchumi, kijamii, kiutamaduni, kimazingira na kiteknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili 2025, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliandaa miswada ya sheria 16. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili 2025, Wizara kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilihakiki na kuchapisha jumla ya sheria ndogo 903 ikilinganishwa na sheria ndogo 885 zilizohakikiwa na kuchapishwa katika kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili 2025, Wizara kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imekamilisha ufasili na uhakiki wa mwisho wa sheria kuu 300 kati ya sheria kuu 446 ambazo zimetafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imekamilisha urekebu wa sheria kuu 446 za nchi na kuandaa toleo la sheria zilizofanyiwa urekebu la mwaka 2023. Toleo hili ni la pili tangu nchi yetu ilipopata uhuru. Toleo la kwanza lilitolewa mwaka 2002 kupitia ufadhili wa Benki ya Dunia. Toleo la sheria zilizofanyiwa urekebu kwa mwaka 2023 limeandaliwa kwa fedha za ndani na wataalam wa ndani. Aidha, Toleo hili lilizinduliwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 23 Aprili, 2025. Toleo hili litaanza kutumika rasmi tarehe 01 Julai, 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025, jumla ya majalada 16,956 yalipokelewa katika vyombo vya upelelezi ikilinganishwa na majalada 14,925 yaliyopokelewa katika kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Kati ya majalada hayo, majalada 14,925 yaliandaliwa hati za mashitaka sawa na 88.4% ikilinganishwa na majalada 10,007 yaliyoandaliwa hati za mashtaka katika kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2023/2024 sawa na 67%.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai ,2024 hadi Aprili, 2025, jumla ya kesi za jinai 27,523 ziliendeshwa katika Mahakama za wilaya na Hakimu Mkazi ikilinganishwa na kesi 25,037 zilizoendeshwa katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024. Aidha, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2024 hadi Aprili, 2025, jumla ya kesi 21,232 sawa na 77% zilihitimishwa ikilinganishwa na kesi 15,084 sawa na 60% ya kesi hizo zilizohitimishwa katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 hadi Aprili 2025, Ofisi ya Taifa ya Mashitaka iliendesha kesi kubwa 177 katika Mahakama Kuu *Division* ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi ikilinganishwa na kesi 60 zilizoendeshwa katika kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2023/2024. Aidha, kesi 108 zilihitimishwa zikilinganishwa na kesi 22 zilizohitimishwa katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imeendelea kusogeza huduma za Mashtaka kwa

wananchi katika ngazi za mikoa na wilaya. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025, Ofisi inaendelea kutoa huduma za kimashitaka katika mikoa 30 ya kimashitaka na ofisi 108 za wilaya. Aidha, katika kipindi husika ofisi imekamilisha ujenzi wa majengo ya Taifa ya mashtaka katika mikoa minne ambayo ni, Shinyanga, Manyara, Katavi na Rukwa. Vilevile, Ofisi ya Taifa ya Mashitaka inaendelea na ujenzi wa ofisi katika Mikoa ya Morogoro, Mbeya, Njombe, Geita, Kinondoni na Temeke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025, Serikali imeendesha jumla ya mashauri ya madai 9,013. Katika kuendesha mashauri hayo, mashauri 966 yalimalizika. Kwa kumalizika kwa mashauri hayo, Serikali imefanikisha kushinda mashauri 750 sawa na 77.6% ya mashauri yaliyomalizika kwa kipindi husika na kufanikiwa kuokoa kiasi cha shilingi bilioni 51.02 kiasi ambacho Serikali ingelipa endapo ingeshindwa mashauri hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa mashauri ya usuluhishi katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025, jumla ya mashauri ya usuluhishi 209 yameshughulikiwa. Katika kipindi husika, mashauri 21 yalimalizika. Kati ya hayo, Serikali imefanikiwa kushinda mashauri 16 sawa na 76.2% ya mashauri yaliyomalizika. Kutokana na kumalizika kwa mashauri hayo, Serikali imeokoa jumla ya shilingi bilioni 16.92 na dola za kimarekani milioni 63.34.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2024 Wizara imefanya mapitio ya Sheria ya Usuluhishi, Sura ya 15 na kanuni zake ili kuwezesha uanzishwaji na uendeshaji wa Kituo cha Usuluhishi wa Migogoro Tanzania. Uwepo wa mifumo thabiti ya utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala ni msingi muhimu katika maendeleo ya kibiashara na uwekezaji kwa kuwa huwezesha kutunza amani ya pande zinazovutana, kupunguza muda ambao pande hizo zinatumia Mahakamani pamoja na hasara inayoweza kujitokeza katika biashara au uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuimarisha upatikanaji haki na utawala bora, Serikali kupitia Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Sekta za Sheria, namba 11 ya Mwaka 2023 ilifanya

marekebisho ya muundo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuanzisha Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria. Lengo la maboresho hayo ni kuongeza tija na ufanisi katika shughuli za uandishi wa sheria, urekebu wa sheria na ufasili wa sheria. Muundo wa kiutawala wa ofisi hii uliidhinishwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan, tarehe 14 Januari, 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2026, Tanzania inafanyiwa tathmini ya utekelezaji wa haki za binadamu chini ya mfumo wa umoja wa mataifa wa haki za binadamu wa mapitio katika kipindi maalum (*Universal Periodic Review – UPR)*. Hivyo, katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025, Wizara iliratibu mafunzo ya maafisa 40 wa Wizara na taasisi zake za umma kutoka Tanzania bara na Zanzibar na asasi za kiraia 55 ya kuandaa kuwasilisha taarifa katika maeneo yao mahususi kuhusu haki za binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025, Wizara ilishiriki katika vikao vya 56, 57 na 58 vya Baraza la Haki za Binadamu na Umoja wa Mataifa. Kupitia ushiriki huu, Wizara imewasilisha taarifa muhimu kwa umoja wa mataifa kuhusu jitihada na mafanikio katika kulinda, kuhifadhi na kukuza haki mbalimbali za binadamu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Serikali imetoa elimu kwa umma ya Haki za Binadamu na misingi ya utawala bora kwa njia za mikutano ya hadhara 92 kwenye mikoa tisa ya Tanzania bara na Tanzania Zanzibar, ambapo wananchi 64,550 walifikiwa. Pia, elimu hiyo imetolewa kupitia mitandao ya kijamii. Wizara kupitia Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ilifanya ukaguzi katika Magereza 29 na vituo vya Polisi 23 katika mikoa 14 ya Tanzania Bara na miwili ya Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025, jumla ya vyeti vya kuzaliwa 1,241,765 vimesajiliwa na kutolewa sawa na 105% ikilinganishwa na lengo la kusajili na kutoa

vyeti vya kuzaliwa 1,181,123. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025, jumla ya vyeti vya vifo 34,504 vimesajiliwa na kutolewa. Vilevile, marejesho ya shahada za ndoa 31,641 yamesajiliwa sawa na 64.7% ya lengo la kusajili ndoa 48,750.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Kurekebisha Sheria ya Tanzania imefanya tathmini ya utekelezaji wa sheria zilizosimamia michezo ya kubahatisha sura ya 41. Lengo la tathmini hii ni kubaini kama malengo ya kutungwa kwa Sheria hiyo yamefikiwa. Tume ya Kurekebisha Sheria ya Tanzania imefanya utafiti wa mfumo wa sheria unaosimamia utatuzi wa migogoro ya kibenki ili kubaini changamoto ya migogoro na mikopo. Lengo la utafiti huu ni kuishauri Serikali kuchukua hatua stahiki ili kuwa na mfumo madhubuti, nafuu na wa haraka wa utatuzi wa migogoro ya kibenki.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi, 2025, Wizara ilipitia na ilisajili jumla ya mikataba 483 ya uwekezaji katika utajiri asili na maliasilia za nchi iliyoingiwa kati ya Serikali na wawekezaji kwa lengo la kuhakiki uzingatiwaji wa matakwa ya kisheria. Wizara imeandaa mkakati wa Taifa wa uangalizi wa utajiri asilia na mali asilia za nchi ili kuwezesha utekelezaji wa misingi ya sheria za maliasilia kwa kipindi cha miaka mitano cha kuanzia Mwaka wa Fedha 2025/2026 hadi 2029/2030. Lengo la mkakati huu ni kuweka mfumo wa pamoja katika usimamizi na uangalizi wa rasilimali za nchi ili kuhakikisha kuwa uwekezaji katika utajiri asili na maliasili za nchi unanufaisha Taifa na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025, Wizara imekamilisha mikataba ya urejeshaji wa wahalifu watoro kutoka Nchi tatu za Ethiopia, Iran na Kenya. Majadiliano ya mikataba ya kubadilishana wahalifu na nchi nyingine nne za shirikisho za Urusi, Qatar, Umoja wa Falme za Kiarabu, na Burundi yanaendelea. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025, Wizara kupitia Ofisi ya Taifa ya Mashitaka ilipokea maombi ya kupatiwa Ushahidi wa watuhumiwa waliofanya makosa ya jinai katika nchi tano za Thailand, India, Shelisheli, Zambia na Uganda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara na taasisi zake imeendelea kuboresha mifumo mbalimbali ya TEHAMA kwa lengo la kufikisha huduma za kisheria karibu na wananchi. Hadi kufikia Aprili 2025, 75% ya mifumo ya TEHAMA katika Sekta ya Sheria imeunganishwa. Tarehe 5 Sptemba, 2024 Wizara ilizindua kituo cha huduma kwa mteja ambapo mwananchi hupata fursa ya kuwasilisha malalamiko na hoja mbalimbali za kisheria moja kwa moja kupitia namba za simu *0262160360* na namba ya *WhatsApp 0739101910* na barua pepe kupitia *malalamiko@sheria.go.tz.*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025, Taasisi ya Mafunzo ya Wanasheria kwa Vitendo Tanzania iliendesha mafunzo ya uanasheria kwa vitendo kwa wanafunzi wa kundi la 37 hadi 40 ambapo kundi la 37 limehitimu, kundi la 38 limemaliza mafunzo ya uandani, kundi la 39 lipo kwenye mafunzo ya uandani baada ya mafunzo ya darasani na kundi la 40 linaendelea na mafunzo ya darasani. Aidha, taasisi ilisajili wanafunzi 1,240 sawa na 82.7% ya lengo la usajili wa wanafunzi 1,500 kwa kundi la 39 na 40.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto, imeendelea kuimarisha upatikanaji wa haki nchini kwa kuwajengea uwezo Waheshimiwa Majaji, Wasajili wa Mahakama, Mahakimu, Maafisa wa Mahakama na watumishi wengine wa Sekta ya Sheria. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025, Chuo kiliendesha na kuratibu mafunzo aina 28 kwa washiriki 1,723. Taarifa ya maboresho ya utendaji wa maendeleo ya rasilimaliwatu iliyo chini ya Wizara na taasisi zake imeainishwa katika ibara ya 148 hadi 159 katika kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 hadi kufikia Machi, 2025, fursa kadhaa na mikakati ya kutumia fursa hizo imebainika kama ilivyoainishwa katika ibara ya 160 na ibara ya 161 katika kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shukrani; ninapenda kutumia fursa hii kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito

Mhagama, Mwenyekiti wa Kamati na Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, Makamu Mwenyekiti wa Kamati na Kamati yote kwa ujumla yake na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti chini ya uongozi wa Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mwenyekiti wa Kamati na Mheshimiwa Twaha Ally Mpembenwe, Makamu Mwenyekiti wa Kamati kwa maelekezo na ushauri wao ambao umeleta mchango mkubwa katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuliarifu Bunge kuwa, ushauri, maelekezo na maoni yote yaliyotolewa na Kamati yamezingatiwa kikamilifu katika maandalizi ya bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ninapenda kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Songea Mjini ambao walinichagua na kunifanya nisimame hapa katika siku ya leo. Pia ninaomba niwashukuru viongozi na wanachama wa Chama Cha Mapinduzi katika Wilaya ya Songea Mjini, ambao baadhi yao wapo leo hapa. Pia viongozi wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Ruvuma kwa ushirikiano wanaoendelea kunipa katika kuwawakilisha na kuwatumikia katika Bunge hili pamoja na kuratibu utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo katika Jimbo la Songea Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuchukua fursa hii kuwapa ujumbe kwamba, huu ndiyo mwaka alioufanya bwana, ninaomba waendelee kuniunga mkono tuendelee kuleta maendeleo Songea Mjini. Ninapenda kutumia fursa hii kuwashukuru wale wote waliochangia kwa namna moja au nyingine katika kuwezesha Wizara kufanikisha majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio yaliyopatikana katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 yametokana na ushirikiano na misaada ya kifedha na kiufundi kutoka kwa washirika wa maendeleo wakiwemo Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa *(UNDP),* Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (*UNICEF*), Umoja wa Ulaya *(EU),* Ujerumani kupitia *GIZ*, Benki ya Dunia, bila kusahau ushiriki wa wananchi katika kutii na kuheshimu

Katiba na sheria za nchi wakiongozwa na Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nitumie fursa hii kuwashukuru Viongozi wenzangu wa Wizara ya Katiba na Sheria akiwemo Mheshimiwa Jumanne Abdallah Sagini, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, ambaye ameninong'oneza kwamba anarudi Butiama. Kwa niaba yake ninawaomba wananchi wa Butiama waendelee kumuunga mkono. Pia, ninamshukuru Mheshimiwa Eliakim Chacha Maswi, Katibu Mkuu na Dkt. Franklin Jasson Rwezimula, Naibu Katibu Mkuu kwa ushirikiano wanaonipatia katika utekelezaji wa shughuli za Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba vilevile nitoe shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Profesa Ibrahimu Hamisi Juma, Jaji Mkuu wa Tanzania na Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Mahakama; Mheshimiwa Dkt. Mustapher Mohamed Siyani, Jaji Kiongozi; Mheshimiwa Hamza Saidi Johari, Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Mheshimiwa Eva Kiaki Nkya, Msajili Mkuu wa Mahakama ya Tanzania; Mheshimiwa Samwel Maneno, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali; pamoja na Wakuu wa Taasisi na Watendaji Wakuu wote wa Taasisi na Wizara pamoja na Wenyeviti ambao wameungana nami katika bajeti hii ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee, ninaishukuru familia yangu, hususan mke wangu kipenzi Ndugu Flora Ndumbaro na watoto wangu kwa ushirikiano wanaoendelea kunipatia kwa kunivumilia na kunitia moyo wakati ninapokuwa ninatekeleza majukumu yangu ya kulitumikia Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako ninaomba pia nimshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuisaidia timu ya Simba *Sports Club* kuingia katika fainali ya mashindano ya *CAF*, Simba inaingia fainali kwa mara ya pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako, ninawaombea ruhusa Waheshimiwa Wabunge wafuatao ili waambatane na

Simba kwenda Morocco. Mheshimiwa Gulamali, Mheshimiwa Tarimba, Mheshimiwa Mavunde, Mheshimiwa Mwigulu na Waheshimiwa Wabunge wengine. Kwa ruhusa yako waende Morocco tarehe 17 Mei ili wakaishangilie Simba ikifanya mambo yake kule ugenini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara, Taasisi zake na Mhimili wa Mahakama itaendelea kuboresha utoaji wa huduma za kisheria na utoaji haki kwa umma. Katika kufikia azma hiyo, Wizara imeainisha maeneo mahsusi ya kipaumbele ambayo yameainishwa katika Ibara ya 169 katika kitabu cha hotuba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa, baadhi ya kazi zitakazotekelezwa na Mafungu yote ya Wizara katika mwaka wa fedha 2025/2026 zimeainishwa kwenye Ibara ya 170 hadi 178 katika kitabu cha hotuba. Katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara na taasisi zake na zinatarajia kukusanya jumla ya Shilingi 13,656,199,000. Ili kufanikisha utekelezaji wa vipaumbele vilivyoainishwa, Wizara inaomba kuidhinishiwa jumla ya fedha kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara na Taasisi zake inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 687,698,489,000. Kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya kina na mchanganuo wa maombi ya fedha za bajeti ya kila Fungu umeainishwa katika vitabu vya randama za Mafungu husika ambavyo vimegawiwa kwa Waheshimiwa Wabunge kupitia mfumo wa kidijitali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. DAMAS DANIEL NDUMBARO (MB.), WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA AKIWASILISHA BUNGENI MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## A. UTANGULIZI

***1. Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kutoa hoja kwamba kutokana na taarifa zilizowasilishwa leo katika Bunge lako na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti zilizochambua Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria na Mfuko wa Mahakama, Bunge lako sasa likubali kupokea, kujadili na kupitisha taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, pamoja na kujadili na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Katiba na Sheria, Taasisi zake pamoja na Mahakama ya Tanzania kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

***2. Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote, ninamshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa fadhili zake na kutujalia afya njema na kutuwezesha kukutana hapa leo kwa ajili ya kujadili taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na Mwelekeo wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

***3. Mheshimiwa Spika,*** kwa heshima na taadhima ninaomba kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa **Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kuniteua kwa mara ya pili kuiongoza Wizara ya Katiba na Sheria. Ninaahidi kuitumikia nafasi hii kwa uaminifu na uadilifu ili kuwaletea maendeleo wananchi na Taifa kwa ujumla.

### *Pongezi*

***4. Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya pekee nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania kwa umahiri wake katika kuiongoza nchi yetu. Katika kipindi cha uongozi wake, tunaendelea kushuhudia maendeleo na mafanikio makubwa katika sekta mbalimbali ikiwemo Sekta ya Sheria, ambapo tumeshuhudia kuimarika kwa mfumo wa utoaji haki, huduma za msaada wa kisheria, kukuza na kulinda haki za binadamu na watu pamoja na misingi ya utawala bora. Naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge na Wananchi wenzangu kuendelea kumuombea Rais wetu kwa Mwenyezi Mungu amjaalie afya njema, hekima na busara katika kuliongoza Taifa letu la Tanzania.

***5. Mheshimiwa Spika,*** kwa unyenyekevu mkubwa ninapenda kumpongeza Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuthibitishwa na Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuwa mgombea wa Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2025. Aidha, ninapenda kuwapongeza Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi kwa kuteuliwa kuwa mgombea mwenza na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuwa mgombea wa Urais wa Zanzibar. Vilevile, ninapenda kumpongeza Ndugu Stephen Masato Wasira kwa kuchaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa CCM Tanzania Bara.

***6. Mheshimiwa Spika,*** ninaomba nitumie fursa hii pia kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb.), Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa uongozi wao mahiri na uliotukuka katika kulitumikia Taifa letu.

***7. Mheshimiwa Spika,*** nitumie nafasi hii kumshukuru na kumpongeza Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwasilisha hotuba ambayo imefafanua utendaji wa Serikali kwa mwaka 2024/2025 na kutoa mwelekeo wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Aidha, ninawapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote

waliowasilisha Hotuba za Bajeti za Wizara wanazozisimamia kwa mawasilisho yao mazuri.

***8. Mheshimiwa Spika,*** ninaomba nitumie nafasi hii kukupongeza wewe binafsi pamoja na Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuliongoza Bunge kwa umahiri na weledi mkubwa. Aidha, kwa namna ya pekee naomba kutumia nafasi hii kukupongeza Mheshimiwa Spika kwa kazi nzuri unayoendelea kuifanya katika kusimamia Umoja wa Mabunge Duniani. Vilevile, nitoe pongezi kwa Wenyeviti wa Bunge ambao huendesha Vikao vya Bunge kwa niaba ya Spika.

***9. Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kutumia fursa hii kuwapongeza Mawaziri walioteuliwa na Mheshimiwa Rais kutekeleza majukumu katika Wizara mbalimbali katika kipindi cha kuanzia Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 ambao ni Mhe. William Vangimembe Lukuvi (Mb.), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu); Mhe. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi (Mb.), Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo; Mhe. Jerry William Silaa (Mb.), Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari; Mhe. Mhandisi Hamad Yusuf Masauni (Mb.), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira); Mhe. Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji (Mb.), Waziri wa Mifugo na Uvuvi; Mhe. Abdallah Hamis Ulega (Mb.), Waziri wa Ujenzi; Mhe. Innocent Lugha Bashungwa (Mb.), Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi; Mhe. Jenista Joackim Mhagama (Mb.), Waziri wa Afya; Mhe. Balozi Mahmoud Thabit Kombo (Mb.), Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki; Mhe. Dkt. Selemani Saidi Jafo (Mb.), Waziri wa Viwanda na Biashara; Mhe. Balozi Dkt. Pindi Hazara Chana (Mb.), Waziri wa Maliasiali na Utalii; Mhe. Deogratius John Ndejembi (Mb.), Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; na Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete (Mb.), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu).

***10. Mheshimiwa Spika,*** nichukue nafasi hii pia kuwapongeza Naibu Mawaziri walioteuliwa ambao ni Mhe. Deus Clement Sangu (Mb.), Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Mhe. Cosato David Chumi (Mb.), Naibu

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki anayeshughulikia Masuala ya Mambo ya Nje; na Mhe. Dennis Lazaro Londo (Mb.), Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki anayeshughulikia Masuala ya Afrika Mashariki.

***11. Mheshimiwa Spika,*** kwa kipekee ninapenda kumpongeza Bw. Eliakim Chacha Maswi kwa kuteuliwa na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria na Dkt. Franklin Jasson Rwezimula kwa kuteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria. Uteuzi wao ni ishara ya imani kubwa aliyonayo Mhe. Rais juu ya uhodari na utendaji kazi wao.

***Salam za Pole***

***12.*** **Mheshimiwa Spika,** Wizara ilipokea kwa masikitiko makubwa taarifa ya kifo cha Mhe. Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile (Mb.), aliyekuwa Mbunge wa jimbo la Kigamboni (CCM) na Mkurugenzi Mteule wa Shirika la Afya Duniani (WHO) Kanda ya Afrika, kilichotokea tarehe 27 Novemba, 2024. Wizara inawapa pole familia ya marehemu, Wananchi wa Jimbo la Kigamboni na Watanzania kwa ujumla. Mwenyezi Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi, AMINA.

***13. Mheshimiwa Spika,*** kwa nyakati tofauti nchi yetu imekumbwa na ajali na maafa katika maeneo mbalimbali zilizosababisha vifo, majeruhi, uharibifu wa mali na mazingira. Itakumbukwa tarehe 16 Novemba, 2024 kulitokea maafa ya kuanguka kwa jengo la ghorofa nne (**4**) katika eneo la Kariakoo, Jijini Dar es Salaam na kusababisha vifo, majeruhi na upotevu wa mali. Kwa namna ya pekee natoa pole kwa waathirika wa tukio hili. Aidha, ninaomba kutoa pole kwa waathirika na manusura wote wa matukio yote yaliyotokea nchini katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2024/2025. Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi, AMINA.

### B. DIRA NA DHIMA

***14. Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Katiba na Sheria inaongozwa na Dira ambayo ni "Katiba na Sheria wezeshi kwa maendeleo ya Taifa". Aidha, Dhima ya Wizara ni "kuwa na mfumo madhubuti wa kikatiba na kisheria wenye kufanikisha utekelezaji wa sera na mipango kwa maendeleo ya Taifa".

### C. MUUNDO NA MAJUKUMU YA WIZARA

***15. Mheshimiwa Spika***, Wizara ya Katiba na Sheria inajumuisha Mhimili wa Mahakama ya Tanzania, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na Tume ya Utumishi wa Mahakama. Taasisi nyingine ni Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria, Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini (RITA), Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo na Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto.

***16. Mheshimiwa Spika***, kwa mujibu wa Hati Idhini iliyotolewa kupitia Tangazo la Serikali Na. 619B la tarehe 30 Agosti, 2023 Wizara ina majukumu yafuatayo: -

(i) Kuratibu utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria;

(ii) Kusimamia mfumo wa haki na utoaji haki;

(iii) Kutunga sera zinazohusu masuala ya kisheria na kusimamia utekelezaji wake;

(iv) Kushughulikia masuala ya kikatiba;

(v) Uandishi wa sheria;

(vi) Kuendesha mashtaka ya jinai;

(vii) Kushughulikia uendeshaji wa mashauri ya madai na usuluhishi;

(viii) Kuratibu masuala ya haki za binadamu;

(ix) Usuluhishi wa migogoro ya kibiashara, sheria za kimataifa na mikataba;

(x) Kuratibu usajili wa matukio muhimu ya binadamu, ufilisi na udhamini;

(xi) Kuratibu tathmini na maboresho ya sheria;

(xii) Kuratibu ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa sheria za utajiri asili na maliasilia za nchi;

(xiii) Kushughulikia urejeshwaji wa wahalifu na masuala ya ushirikiano wa kimataifa kwenye makosa ya jinai;

(xiv) Kuboresha utendaji na maendeleo ya rasilimali watu iliyo chini ya Wizara; na

(xv) Kuratibu majukumu ya taasisi, mipango na miradi chini ya Wizara.

**D. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025**

***17. Mheshimiwa Spika***, utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2024/2025 umezingatia Dira na miongozo mbalimbali ya kitaifa na kimataifa ambayo ni pamoja na; Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Dunia (2030); Mpango wa Maendeleo wa Afrika (2063); Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025; Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/2022 - 2025/2026); Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020; Ahadi za Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizozitoa wakati akifungua Bunge la 11 mwaka 2021; maelekezo ya Viongozi Wakuu wa Serikali pamoja na Mipango Mikakati ya Wizara na Taasisi zake.

***18. Mheshimiwa Spika,*** katika bajeti ya mwaka 2024/2025, Wizara ilibainisha masuala ya kipaumbele kama ifuatavyo: -

(i) Kuratibu utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria;

(ii) Kutunga Sera ya Taifa ya Haki Jinai;

(iii) Kuwezesha urekebu wa Sheria za Tanzania;

(iv) Uandishi wa sheria ikiwa ni pamoja na kuandaa Toleo la Sheria Ndogo zilizofanyiwa urekebu mwaka 2025 na kuimarisha marejeo na ufuatiliaji wa utekelezaji wa mikataba iliyosainiwa;

(i) Kushughulikia masuala ya kikatiba ikiwa ni pamoja na kutoa elimu ya uraia na utawala bora kwa umma;

(ii) Kusimamia mfumo wa haki na utoaji haki ikiwa ni pamoja na kuimarisha miundombinu ya Mahakama, kuharakisha mashauri ya kawaida na kumaliza mashauri ya muda mrefu;

(iii) Kuendesha mashtaka ya jinai, kuimarisha utenganishaji wa shughuli za mashtaka na upelelezi;

(iv) Kushughulikia uendeshaji wa mashauri ya madai na usuluhishi wa migogoro ya kibiashara, sheria za kimataifa na mikataba;

(v) Kuwezesha uanzishwaji wa Kituo cha Usuluhishi wa Migogoro;

(vi) Kuwezesha Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria kuanza kutekeleza majukumu yake;

(vii) Kuratibu masuala ya haki za binadamu, utawala bora;

(viii) Kuimarisha usajili wa matukio muhimu ya binadamu pamoja na usajili na ufilisi katika Mikoa yote ya Tanzania Bara;

(ix) Kuratibu tathmini na maboresho ya sheria ikiwa ni pamoja na Kufanya Mapitio ya Mifumo wa Sheria inayosimamia Elimu, Michezo ya Kubahatisha na Kufanya Utafiti wa Mfumo wa Sheria Unaosimamia Utatuzi wa Migogoro ya Kibenki na Taasisi za fedha;

(x) Kuratibu ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa sheria za utajiri asili na maliasilia za nchi;

(xi) Kushughulikia urejeshwaji wa wahalifu na masuala ya ushirikiano wa kimataifa kwenye makosa ya jinai;

(xii) Kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji haki na huduma za kisheria; na

(xiii) Kuboresha utendaji na maendeleo ya rasilimaliwatu ya Wizara na taasisi zake ikiwemo ajira, uteuzi, nidhamu na maadili.

## E. MWENENDO WA BAJETI NA FEDHA ZILIZOPOKELEWA NA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

### (i) Makusanyo ya Maduhuli

***19. Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara pamoja na Taasisi zilizo chini ya Wizara ilipanga kukusanya maduhuli yenye jumla ya Shilingi **12,676,199,000.00** kutoka kwenye vyanzo mbalimbali vya mapato ambavyo ni pamoja na ada ya watoa huduma za msaada wa kisheria, ada za kusajili mashauri, faini zinazotokana na mashauri mbalimbali pamoja na pango la ofisi. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 Wizara na Taasisi zake imekusanya jumla ya Shilingi **9,036,054,037.00** sawa na asilimia **71.28** ya lengo la makusanyo ya maduhuli kwa mwaka 2024/2025 na asilimia **85.54** kwa lengo la kipindi cha miezi 10 kama ilivyoainishwa katika **Kiambatisho Na.1.** Sababu za kutofikia lengo la ukusanyaji wa maduhuli ni kuwepo kwa maombi pungufu ya usajili wa Watoa Huduma kwa Njia Mbadala na Watoa Huduma ya Msaada Kisheria ikilinganishwa na lengo lililowekwa.

(ii) Bajeti Iliyoidhinishwa

***20. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara iliidhinishiwa jumla ya Shilingi **486,296,754,555.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo Shilingi **112,497,549,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi, Shilingi **228,180,396,571.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na Shilingi **145,597,319,000.00** ni kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha za maendeleo Shilingi **85,640,600,984.00** ni fedha za ndani na Shilingi **59,978,208,000.00** ni fedha za nje **(Kiambatisho Na.2).**

(iii) Fedha Zilizopokelewa

***21. Mheshimiwa Spika*****,** katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025, Wizara imepokea jumla ya Shilingi **391,960,643,596.72** sawa na asilimia **80.60** ya Bajeti ya Shilingi **486,296,754,555.00** iliyoidhinishwa katika mwaka 2024/2025. Kati ya fedha zilizopokelewa, Shilingi **94,741,018,477.30** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi, Shilingi **193,647,671,495.78** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na Shilingi **103,571,953,623.64** ni fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Aidha, fedha za Miradi ya Maendeleo zinajumuisha Shilingi **66,045,048,103.65** fedha za ndani na Shilingi **37,526,905,519.99** fedha za nje. Muhtasari wa mchanganuo wa Bajeti iliyoidhinishwa na kiasi cha fedha kilichopokelewa na Wizara na Taasisi kwa kipindi hicho zimeainishwa katika **Kiambatisho Na. 3a** na **3b.**

## F. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU KWA KUZINGATIA VIPAUMBELE

***22. Mheshimiwa Spika****,* utekelezaji wa mpango na bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 umezingatia vipaumbele vilivyowekwa na Wizara kama ifuatavyo:-

### *(i) Kuratibu Utoaji wa Huduma ya Msaada wa Kisheria*

***23. Mheshimiwa Spika*****,** katika kuimarisha upatikanaji haki kwa watu wote kupitia huduma ya msaada wa kisheria, Wizara

inaendelea kuimarisha uratibu na usimamizi wa huduma za msaada wa kisheria katika ngazi za kijamii. Katika kuhakikisha wananchi wanafikiwa kwa urahisi, Wizara inatekeleza Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia (***Mama Samia Legal Aid Campaign - MSLAC***). Tangu kuzinduliwa kwa Kampeni hii tarehe 27 Aprili, 2023, jumla ya Mikoa **25** imefikiwa na Kampeni. Mikoa hiyo ni Dodoma, Manyara, Shinyanga, Ruvuma, Simiyu, Singida, Iringa, Mara, Songwe, Morogoro, Njombe, Katavi, Tabora, Geita, Kigoma, Mtwara, Kilimanjaro, Mwanza, Mbeya, Lindi, Rukwa, Pwani, Arusha, Tanga na Kagera. Ili kuhitimisha nchi nzima, kwa upande wa Tanzania Bara Mkoa uliobaki ni Dar es Salaam ambapo Kampeni itatekelezwa Juni, 2025.

***24. Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa Tanzania Zanzibar utekelezaji wa Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia umefanyika katika mikoa mitatu (**3**) ambayo ni Kaskazini Pemba, Mjini Magharibi na Kaskazini Unguja. Aidha, mikoa ya Kusini Pemba na Kusini Unguja Kampeni itatekelezwa Mei, 2025 na hivyo kukamilisha maeneo yote ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

***25. Mheshimiwa Spika***, katika utekelezaji wa Kampeni hiyo wananchi wamepatiwa huduma mbalimbali ikiwemo elimu kuhusu masuala ya haki na wajibu; umiliki na utatuzi wa migogoro ya ardhi; matunzo ya watoto; utatuzi wa migogoro ya ajira na mahusiano kazini; ukatili wa kijinsia; wosia, mirathi, ndoa na familia; usajili wa matukio muhimu ya binadamu; na haki za binadamu. Aidha, kupitia mada zinazotolewa, wananchi wamepata fursa ya kuuliza maswali kuhusu masuala ya kisheria na kupatiwa majibu papo kwa hapo. Kupitia Kampeni hiyo, jumla ya Halmashauri **180**, Kata **1,907** na Vijiji/Mitaa **5,702** ilifikiwa na jumla ya wananchi **2,698,908** (Wanaume **1,347,325** na Wanawake **1,351,583**) walifikiwa na kupata elimu na huduma za kisheria kupitia mikutano ya ana kwa ana.

***26. Mheshimiwa Spika***, katika utekelezaji wa Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia, elimu ya sheria pia imekuwa ikitolewa kupitia vyombo vya habari ikiwemo redio za kitaifa na kijamii; televisheni na mitandao ya kijamii; na vipeperushi. Ninapenda kuchukua nafasi hii kuvipongeza na

kuvishukuru vyombo vya habari kwa kuwa wadau muhimu kwa kipindi chote cha utekelezaji wa Kampeni ambapo kupitia wao jamii inaendelea kupata elimu na taarifa mbalimbali za utekelezaji wa Kampeni na vimesaidia kuongeza uelewa wa masuala ya kisheria na mwitikio wa wananchi kuhusu Kampeni. Hadi kufikia Aprili, 2025 maudhui ya elimu ya Sheria na masuala ya utawala bora kupitia Kampeni hii yametazamwa mara **43,035,493.**

***27. Mheshimiwa Spika***, kupitia Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia, jumla ya migogoro **24,691** iliyodumu kwa muda mrefu ilipokelewa ambapo baadhi ilidumu kwa zaidi ya miaka kumi. Utatuzi wa migogoro hiyo umewezesha kuimarisha amani, utulivu na utengamano miongoni mwa wanajamii kwani unaacha pande zilizokuwa na migogoro zimeelewana. Migogoro hii ilihusisha masuala ya ardhi, ndoa za utotoni, matunzo ya watoto, madai, ndoa, jinai, ukatili wa kijinsia, ardhi, ajira na mengineyo. Aidha, jumla ya migogoro **5,704** ilitatuliwa na kuhitimishwa kwa njia mbadala kati ya migogoro **23,399** ya muda mrefu iliyopokelewa. Utatuzi wa migogoro **18,987** unaendelea katika ngazi mbalimbali.

***28. Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha uratibu wa huduma za msaada wa kisheria katika ngazi ya Halmashauri, Kata, Vijiji na Mitaa, Wizara imeanzisha Madawati ya Msaada wa Kisheria katika Mamlaka za Serikali za Mitaa **184**. Madawati hayo yamesaidia kusogeza huduma za msaada wa kisheria kwa wananchi pamoja na uendelevu wa huduma ya msaada wa kisheria. Aidha, jumla ya watumishi **449** wameajiriwa ili kuwezesha Madawati hayo kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Kupitia madawati haya, Wananchi wanawasilisha malalamiko na changamoto zao za kisheria na kupatiwa ufumbuzi.

***29. Mheshimiwa Spika***, tangu kuanzishwa kwa Madawati ya Msaada wa Kisheria, jumla ya wananchi **6,427,738** (Wanaume **2,905,356** na Wanawake **3,522,382**) wamepatiwa elimu juu ya masuala ya kisheria na haki za binadamu. Aidha, migogoro **16,041** ilisajiliwa ambapo migogoro **7,889** ilipatiwa ufumbuzi na migogoro mingine **8,152** inaendelea kufanyiwa kazi. Migogoro hiyo ilijumisha masuala ya ardhi, ukatili wa kijinsia, matunzo ya Watoto, ndoa,

ukiukwaji wa misingi ya utawala bora, masuala ya ndoa na familia, ajira na mahusiano kazini, madai na jinai. Uwepo wa Madawati umeongeza uendelevu wa huduma za msaada wa kisheria na kuongeza wigo wa upatikanaji wa huduma za msaada wa kisheria hususan ngazi za chini katika kijamii.

***30. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025 Wizara iliwezesha vikao vitatu vya Bodi ya Kitaifa ya Ushauri ya Msaada wa Kisheria. Pamoja na mambo mengine, Bodi iliishauri Wizara kuandaa sera ya msaada wa kisheria, mfuko wa huduma za msaada wa kisheria na kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa mashirika yanayotoa huduma za msaada wa kisheria nchini ili kuhakikisha kuwa huduma inayotolewa inakuwa kwenye kiwango kinachoridhisha. Masuala yaliyojadiliwa kwenye bodi yamefanyiwa kazi na Wizara imeandaa rasimu ya Sera ya Taifa ya Msaada wa Kisheria na ukaguzi wa Mashirika yanayotoa msaada wa Kisheria unaendelea kufanyika kama ilivyopangwa.

***31. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuongeza wigo wa upatikanaji wa huduma za msaada wa kisheria kwa kutumia Kliniki za Msaada wa Kisheria za Vyuo Vikuu vinavyofundisha taaluma ya Sheria kwa kuandaa Mwongozo wenye lengo la kuimarisha huduma za msaada wa kisheria kupitia wanachuo wa taaluma ya sheria na wakufunzi. Jumla ya Vyuo Vikuu **15** vimeanzisha na kuendesha Kliniki za Msaada wa Kisheria. Aidha, Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo (LST) imekuwa na Program ya lazima kwa wanafunzi wake kushiriki kutoa huduma ya msaada wa kisheria kwa wananchi katika ngazi za Kata ikiwa ni sehemu ya mafunzo kwa vitendo. Kwa kufanya hivyo, wanachuo wanakuwa na uelewa juu ya masuala ya msaada wa kisheria na kutengeneza ari ya kusaidia wananchi mara watakapohitimu mafunzo yao. Vilevile, jumla ya wanafunzi **1,944** wameshiriki katika program na kutoa huduma za msaada wa kisheria kwa wananchi **17,074** kati yao wanaume **8,554** wanawake **8,520** katika mikoa yote **26** ya Tanzania Bara.

***32. Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha uratibu wa utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria nchini, Wizara imekamilisha ujenzi wa mfumo wa kielektroniki wa Huduma za Msaada wa Kisheria

(Haki Sheria) ambao unapatikana kupitia anuani https://tlegalaid.sheria.go.tz. Hatua inayofuata ni kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo watoa huduma ya msaada wa kisheria ili waweze kutumia mfumo wa huduma za msaada wa kisheria. Mfumo huu unawezesha upokeaji wa taarifa za utekelezaji wa huduma za msaada wa kisheria kutoka kwa Mashirika ya Msaada wa Kisheria na kuhifadhi taarifa za utekelezaji wa Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia. Pia, mfumo huu unalenga kurahisisha upatikanaji wa takwimu zinazotokana na utoaji wa huduma za msaada wa kisheria.

***33. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili, 2025, jumla ya Mashirika **183** yamesajiliwa kutoa Huduma za Msaada wa Kisheria nchini ikilinganishwa na Mashirika **99** yaliyosajiliwa kipindi kama hicho katika mwaka 2023/2024. Kutokana na usajili huo, jumla ya mashirika yaliyosajiliwa yamefikia **377**. Aidha, Wizara imefanya mafunzo kwa Wasaidizi wa Kisheria wapatao **216** (wanaume **99** na wanawake **117).** Lengo la mafunzo hayo ni kuhakikisha huduma za msaada wa kisheria zinasogezwa karibu zaidi na Wananchi. Hadi Aprili, 2025 kuna jumla ya Wasaidizi wa Kisheria **2,205** waliosajiliwa katika Mfumo wa Usajili wa Msaada wa Kisheria.

***34. Mheshimiwa Spika***, katika jitihada za kufikisha huduma za msaada wa kisheria kwa wananchi, Wizara ilishiriki kwenye Maonesho ya Kimataifa ya Biashara (Sabasaba), Maonesho ya Wakulima (Nanenane) na Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wanawake ambapo huduma za msaada wa kisheria zilitolewa na kuwafikia jumla ya wananchi **1,914** (wanaume **1,056** na Wanawake **858**). Aidha, jumla ya migogoro **141** ilihitimishwa kati ya **233** iliyopokelewa. Migogoro **92** inaendelea kufanyiwa kazi katika ngazi mbalimbali za kimahakama na kiutawala kwa ajili ya hatua za utatuzi.

***35. Mheshimiwa Spika,*** tarehe 18 Oktoba, 2024 Wizara kwa kushirikiana na Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS) iliratibu na kuwezesha Matembezi ya Amani na Msaada wa Kisheria dhidi ya Vitendo vya Ukatili na Mauaji ya Watoto ambapo jumla ya Wanasheria wa kujitegemea **150** walishiriki. Lengo kuu la

matembezi hayo lilikuwa kuhamasisha na kupinga vitendo vya ukatili na mauaji ya watoto. Jumla ya wananchi **24** (Wanaume **9** na Wanawake **15**) waliokuwa na uhitaji walipata huduma za msaada wa kisheria ambapo mashauri yao yaliwasilishwa TLS na kupatiwa ufumbuzi.

***36. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2024/ 2025, Wizara imekamilisha rasimu ya Mpango Mkakati wa Jukwaa la Haki Mwanamke. Aidha, tarehe 04 na 05 Agosti, 2024 Wizara ilishiriki katika Jukwaa la Mwaka la Mashirika yasiyo ya Kiserikali na uzinduzi wa Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) iliyofanyika mkoani Dodoma mtawalia. Kupitia ushiriki huo, jumla ya wananchi **637** (wanaume **318**, wanawake **319**) walipatiwa huduma za msaada wa kisheria kutoka katika Kata za Chamwino Ikulu, Chang'ombe, Mpunguzi na Viwanja vya Chinangali.

***(ii) Kutunga Sera ya Taifa ya Haki Jinai***

***36. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeandaa rasimu ya Sera ya Taifa ya Haki Jinai na Mkakati wa Utekelezaji wa Sera hiyo. Rasimu hiyo imeweka mwelekeo wa jinsi ya kushughulikia changamoto zilizopo katika mnyororo wa haki jinai kwa kuzingatia mapendekezo yaliyoainishwa katika Taarifa ya Tume ya Kuangalia Jinsi ya Kuboresha Mfumo wa Haki Jinai Nchini. Lengo la Sera hii ni kuhakikisha kunakuwepo mfumo jumuishi wa ushughulikiaji wa masuala ya haki jinai nchini. Mfumo huo unahusisha kuzuia uhalifu; kubaini uhalifu; upelelezi; ukamataji watuhumiwa; uendeshaji wa mashtaka; utoaji wa haki ya uwakilishi kwa watuhumiwa; utoaji wa hukumu na adhabu; urekebishaji wa wafungwa; na uangalizi na ufuatiliaji wa wafungwa au watuhumiwa walio katika maeneo ya vizuizini. Sera hii itachangia katika kuimarisha utawala wa sheria na kuendeleza uwepo wa amani na utulivu nchini. Serikali inakamilisha uchambuzi wa maoni ya wadau ili yazingatiwe ipasavyo. Sera hiyo inatarajiwa kuidhinishwa na Serikali katika mwaka wa fedha 2025/2026.

***(iii) Kushughulikia Masuala ya Kikatiba ikiwa ni Pamoja na Kutoa Elimu ya Utawala bora na uraia kwa Umma***

***37. Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia Wizara ya Katiba na Sheria inatoa elimu ya uraia kwa umma na utawala bora kwa viongozi na watendaji katika ngazi ya Mkoa na Wilaya. Malengo ya elimu hiyo ni kuwajengea uwezo watendaji wa Serikali za Mitaa na Vyombo vya Usalama kwenye masuala ya uraia, haki za binadamu, misingi ya utawala bora na demokrasia.

***38. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025, Wizara ilitoa mafunzo ya elimu ya uraia na utawala bora kwa wajumbe wa Kamati za Usalama za Mikoa na za Wilaya; Watendaji wa Kata; na Menejimenti na Wataalam katika Halmashauri **122** zilizopo katika Mikoa **17** sawa na asilimia **244** ya lengo la kuzifikia Halmashauri **50** katika mwaka 2024/2025. Mikoa na idadi ya Halmashauri hizo ni Rukwa (**5**), Iringa (**5**), Morogoro (**9**), Mara (**9**), Geita (**6**), Kigoma (**8**), Tabora (**8**), Katavi (**5**), Kilimanjaro (**7**), Songwe (**5**), Mtwara (**8**), Mwanza (**8**), Mbeya (**6**), Lindi (**6**), Pwani (**9**) Tanga (**11**) na Arusha (**7**).

***39. Mheshimiwa Spika***, katika kujenga kizazi chenye uzalendo, maadili na uwajibikaji kwa nchi, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya RaisTAMISEMI; Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia; Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA); na Chuo cha Uongozi wa Mahakama iliandaa maudhui ya Elimu ya Katiba na Uraia kwa Shule za Awali, Msingi, Sekondari na Vyuo vya Mafunzo ya Ufundi Stadi. Maudhui hayo yatachopekwa katika mitaala ya Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ufundi Stadi ili kuwezesha wanafunzi kupata elimu ya Katiba na uraia wakiwa masomoni.

***40. Mheshimiwa Spika,*** ili kuimarisha ushirikiano katika Sekta ya Sheria baina ya pande mbili za Muungano, Wizara ya Katiba na Sheria na Afisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar zilikutana na kujadili masuala mbalimbali ya kisheria na kikatiba kwa lengo la kubadilishana uzoefu, utaalam na tafiti za kisheria hususan katika maeneo tunayoshahabiana ili kutatua changamoto mbalimbali za kisheria kwa pande zote mbili za Muungano. Aidha, kupitia vikao viwili (**2**)

vilivyofanyika, pande mbili za Muungano zilibadilishana uzoefu kuhusu masuala ya Mahakama ya Rufani; mfumo wa uendeshaji wa kesi kielektroniki; mashtaka katika makosa ya uhujumu uchumi na uhalifu wa kupangwa; na namna ya kushughulikia makosa ya udhalilishaji na usafirishaji haramu wa binadamu.

***(iv) Kusimamia Mfumo wa Haki na Utoaji Haki ikiwa ni Pamoja na Kuimarisha Miundombinu ya Mahakama, Kuharakisha Uhitimishaji wa Mashauri Mapya na* Kumaliza Mashauri ya Muda Mrefu**

***a. Kusimamia Utekelezaji wa Mfumo wa Utoaji Haki***

***41. Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kuratibu maboresho ya mfumo wa haki kwa kuzingatia mapendekezo ya Tume ya Kuangalia Jinsi ya Kuboresha Taasisi za Haki Jinai Nchini. Kukamilika kwa maboresho hayo kutaongeza imani katika mfumo wa utoaji haki nchini.

***42. Mheshimiwa Spika***, kwa mujibu wa kifungu cha 219(5) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20, Waziri mwenye dhamana ya sheria amepewa mamlaka ya kuwaachilia huru wafungwa waliotenda makosa wakiwa na changamoto ya afya ya akili ambao wamehifadhiwa katika Taasisi ya Afya ya Akili Isanga kwa uangalizi. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 Wizara ilitoa amri za kuwaachilia huru wakosaji **68** baada ya kuthibitika afya zao za akili zimeimarika na wanaweza kurudi uraiani kuendelea na shughuli za kiuchumi.

***b. Ushirikiano wa Masuala ya Kisheria Kikanda na Kimataifa***

***43. Mheshimiwa Spika*,** Wizara imeendelea kuiwakilisha Serikali katika mikutano mbalimbali ya kisheria ya kikanda na kimataifa katika Sekta ya Sheria. Baadhi ya mikutano ambayo Wizara ilishiriki katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 ni Pamoja na Mkutano wa kawaida wa 10 wa Kamati Maalum ya Mawaziri wa Sheria na Haki ya Umoja wa Afrika uliofanyika Zanzibar. Katika mkutano huo, Tanzania ilichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati hiyo. Aidha, nafasi hii inatoa fursa kwa Nchi

kuwasilisha na kupitisha agenda zake kwa maslahi ya Taifa. Pia, Kamati hiyo iliwasilisha nyaraka za kisheria katika Mkutano wa 38 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika kwa ajili ya maamuzi. Nyaraka hizo ni:-

(i) Rasimu ya mapendekezo ya mkataba wa Afrika wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na wasichana;

(ii) Rasimu ya sheria ya kuanzisha Kituo cha Afrika cha kusimamia usalama wa chakula; na

(iii) Viambatisho tisa **(9)** vya Itifaki ya eneo la soko huru la biashara Afrika.

***44. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 Wizara ilishiriki katika Mkutano wa Nchi Wanachama wa Shirika la Mashauriano ya Sheria za Kimataifa kwa Nchi za Afrika na Asia (AALCO) mbao ulifanyika Bangkok, Thailand. Mkutano huo ulihusisha nchi za Afrika na Asia ambapo nchi hizo zilikubaliana kuhusu masuala mbalimbali ikiwemo kuongeza makosa ya uhalifu wa kivita, kuwa na mashirikiano katika masuala ya ushahidi katika eneo la utaifishaji mali na ulinzi katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari (*Exclusive Economic Zone - EEZ*). Aidha, katika mkutano uliofanyika nchini Kenya, Tanzania iliwasilisha taarifa za ziada ili kuwezesha kuondolewa katika orodha ya nchi hatarishi katika masuala ya Utakatishaji Fedha na Ugaidi.

***c. Kuimarisha Usikilizaji wa Mashauri,Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Mahakama***

***45. Mheshimiwa Spika,*** ili kuongeza kasi ya utendaji kazi, Mahakama imeendelea kuongeza idadi ya Maafisa Mahakama. Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 jumla ya Majaji **10** wameteuliwa (Mahakama Kuu – **5** na Mahakama ya Rufani – **5**) na hivyo kufanya idadi ya Majaji waliopo kufikia **146** (Mahakama Kuu – **107** na Mahakama ya Rufani - **39**). Vilevile, Mahakimu **91** wameajiriwa na hivyo kufanya idadi ya Mahakimu kufikia **1,426** (Mahakama za Mwanzo - **195** na Mahakama za Hakimu Mkazi - **1,231**).

***46. Mheshimiwa Spika***, suala la kupunguza mlundikano wa mashauri mahakamani ni moja ya vipaumbele muhimu vya Serikali katika kuhakikisha kuwa wananchi wote wanapata haki kwa wakati. Kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 kulikuwa na jumla ya mashauri **238,154** mahakamani; kati ya hayo **63,050** yalikuwepo mwanzoni mwa Julai, 2024 na mashauri **175,104** yalifunguliwa. Kati ya mashauri **238,154** yaliyokuwepo, mashauri **174,581** yalisikilizwa na kuhitimishwa na mashauri **63,573** yanaendelea katika hatua mbalimbali. Aidha, mashauri yenye umri mrefu Mahakamani ni **2,780** sawa na asilimia **4** ya mashauri yote yaliyobaki Mahakamani. Kati ya mashauri yenye umri mrefu yaliyopo mahakamani, mashauri **1,325** yapo Mahakama ya Rufani; **189** yapo Mahakama Kuu; **553** yapo Mahakama za Hakimu Mkazi na Wilaya; na **713** yapo Mahakama za mwanzo. Pia, katika Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, jumla ya mashauri **59** yalibakia mwishoni mwa Juni 2024, **118** yalisajiliwa, **108** yalisikilizwa na **69** yalibakia.

***47. Mheshimiwa Spika***, vigezo vinavyotumika kubainisha umri mrefu wa mashauri ni miaka miwili (**2**) kwa Mahakama ya Rufani na Mahakama Kuu; mwaka mmoja (**1**) kwa Mahakama za Hakimu Mkazi na Wilaya; na miezi sita (**6**) kwa Mahakama za Mwanzo.

***48.*** **Mheshimiwa Spika,** Mahakama imeendelea kufanya ukaguzi na usimamizi wa shughuli za Mahakama katika Mahakama za Hakimu Mkazi, Wilaya na Mwanzo kwa Kanda **18** za kimahakama ambapo ukaguzi umefanyika kwa asilimia **99.7** ikilinganishwa na Ukaguzi wa kipindi kama hiki kwa mwaka 2023/2024 ambapo ulifanyika kwa asilimia **99.3**. Matokeo ya ukaguzi huo, yamewezesha kuongeza kasi ya umalizaji mashauri mahakamani kwa kuwa huambatana na ukaguzi wa jalada moja baada ya jingine. Vilevile, magereza **103** kati ya **129** yaliyopo yalikaguliwa, sawa na asilimia **80.2**.

***49. Mheshimiwa Spika,*** Mahakama ya Tanzania imeendelea kushirikiana na wadau wake katika mnyororo wa haki jinai ili kuhakikisha mashauri yanamalizika kwa wakati. Tarehe 06 Aprili

2025 Mahakama iliitisha kikao kazi cha pamoja kilichohusisha wadau kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Chama cha Mawakili Tanganyika, Idara ya Ustawi wa Jamii, Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza pamoja na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya. Kupitia kikao hicho, wajumbe walijadili taarifa ya hali ya mashauri ya mlundikano mpaka kufikia Desemba -2024, hali ya mahabusu magerezani na mkakati wa kupunguza mlundikano na matumizi ya TEHAMA kwenye usikilizaji wa rufaa na maombi.

***50. Mheshimiwa Spika,*** Mahakama ya Tanzania imeendelea na utekelezaji wa Mpango wa Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Mahakama wa Miaka Mitano (2021/2022 – 2025/2026). Lengo la Mpango huo ni kuboresha na kusogeza huduma za Mahakama karibu na Wananchi ili kuwapunguzia gharama na muda wanaoutumia kupata huduma za mahakama. Katika mwaka wa fedha 2024/2025 hadi kufikia Aprili, 2025 hali ya ujenzi na ukarabati wa majengo mbalimbali ya Mahakama ni kama ifuatavyo:-

(i) Ujenzi wa Vituo Jumuishi vya Utoaji Haki tisa **(9**) unaendelea ambapo ujenzi Katika Kituo cha Katavi umefikia (asilimia **42**), Songea (asilimia **51**), Songwe (asilimia **27**), Njombe (asilimia **68**), Simiyu (asilimia **35**), Lindi (asilimia **47**), Singida (asilimia **5**), Tunduru – Ruvuma (asilimia **18**), Korogwe – Tanga (asilimia 95), Ulanga-Morogoro (asilimia **99**) Pemba (asilimia **25**) na Geita (asilimia **78**); Chamwimo – Dodoma (asilimia **55**);

(ii) Ujenzi wa majengo ya Mahakama za Wilaya 11 unaendelea ambapo ujenzi katika Mahakama ya Kibiti umefikia (asilimia **53**), Ubungo (asilimia **98**), Nachingwea (asilimia **9**), Simanjiro (asilimia **18**), Hanang-Manyara (asilimia 19), Mbulu-Manyara (asilimia **50**) na Mkalama-Singida (asilimia **8**);

(iii) Ukarabati wa jengo la zamani la Mahakama Kuu Dodoma umefikia asilimia **57**;

(iv) Ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Mahakama umekamilika na kuzinduliwa tarehe 05 Aprili, 2025;

(v) Ujenzi wa nyumba za Majaji eneo la Iyumbu Dodoma umekamilika na kuzinduliwa tarehe 05 Aprili, 2025;

(vi) Ujenzi wa nyumba ya Jaji Mkuu, jijini Dodoma unaendelea ambapo ujenzi umefikia asilimia **56**; na

(vii) Ujenzi wa Mahakama za Mwanzo **72** unaendelea ambapo ujenzi katika Mahakama za Izigo, Nyakakika-Kagera na Kigoma Kaskazini, Heru Juu, Manyovu-Kigoma umefikia asilimia **22**; Mipingo, Mtandi, Ndomoni - Lindi na Chikundi-Mtwara (asilimia **72**); Msata, Bungu, Somangila na Kimanzichana-Pwani na Mbagala Dar es Salaam (asilimia **28**); Unyamikubi, Minyughe-Singida; KwamtoroDodoma; Bwakila Chini, Minepa - Morogoro (asimilia **60**); Chikongola, Kitangari -Mtwara na Nalasi, Likuyu Sekamaganga, LilondoRuvuma (asilimia **31**); Manda, LupembeNjombe; Izazi, Mafinga-Iringa na NgoherangaMorogoro (asilimia **82**); Kabila, Inonelwa, Nyatukala-Mwanza na Muganza-Geita (asilimia **38**); Mugumu-Musoma na Lagangabilili, Ngulyati, Nyalikungu-Simiyu (asilimia **55**); Malunga, Majengo-Shinyanga na Ng'azo-Geita (asilimia **87**); Engasment, TarakeaKilimanjaro, Terrat-Manyara, Gonja na Sanya Juu - Kilimanjaro (asilimia **70**); Minjingu-Manyara, Terat, Maji ya Chai na Makuyuni-Arusha (asilimia **72**); Kasanga, Namanyere na Nambogo-Rukwa, Ugalla, Sibwesa, Mamba -Katavi (asilimia **36**); Lupa Tingatinga, Ndobo, Rujewa-Mbeya na Kanga, Msangano-Songwe (asilimia **85**), IlangalaMwanza (asilimia **38**), Mbalizi-Mbeya (asilimia **75**), na Machame-Kilimanjaro (asilimia **24**), Haubi-Dodoma (asilimia **69**), Kinusi-Dodoma (asilimia **50**), Rugwa-Singida (asilimia **20**), Magubike–Morogoro (asilimia **5**), Kipili– Tabora (asilimia **2**), Nanjilinji–Lindi (asilimia **15**) na Kitumbeine-Arusha (asilimia **97**).

### *d. Usimamizi wa Utumishi wa Mahakama*

***51. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili, 2025 Tume ya Utumishi wa Mahakama imeendelea kusimamia watumishi wa Mahakama ya Tanzania ikiwa ni pamoja na uteuzi, ajira mpya, maslahi ya watumishi, masuala ya nidhamu na maadili. Katika kipindi husika, Tume ilimshauri Mheshimiwa Rais juu ya Uteuzi wa Jaji mmoja **(1)** wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Tume iliteua Naibu Wasajili sita **(6),** Mkurugenzi wa Sheria Mkurugenzi Msaidizi wa TEHAMA na Watendaji wa Mahakama wanne **(4),** Tume imeajiri watumishi **498** wa Mahakama wa kada mbalimbali. Tume iliwathibitisha kwenye cheo cha uongozi Msajili Mkuu, Msajili wa Mahakama ya Rufani, Msajili wa Mahakama Kuu, Naibu Wasajili **34**, Mtendaji wa Mahakama ya Rufani, Mtendaji wa Mahakama Kuu Divisheni na Watendaji wawili **(2)** wa Mahakama Kanda. Aidha, Tume iliwathibitisha kazini jumla ya watumishi **283** wa kada mbalimbali.

***52. Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha nidhamu na maadili kwa watumishi wa Mahakama yanasimamiwa ipasavyo, Tume ilishughulikia mashauri **27** ya nidhamu na kutolewa uamuzi ambapo kati ya mashauri hayo, saba (**7**) yaliwahusu Maafisa Mahakama na **20** watumishi wasio Maafisa Mahakama.

***53. Mheshimiwa Spika***, Tume ya Utumishi wa Mahakama pia imeendelea kuimarisha Kamati za Maadili za Maafisa Mahakama ngazi ya Mikoa na Wilaya kwa kuhakikisha kunakuwepo usimamizi madhubuti wa utekelezaji wa majukumu yao. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 Tume imeratibu ukaguzi wa Kamati za Maadili za Maafisa Mahakama katika mikoa saba (**8**) ya Arusha, Manyara, Iringa, Pwani, Mtwara, Lindi, Njombe na Ruvuma na wilaya **49** ndani ya mikoa hiyo. Ukaguzi huu ulilenga kutathmini namna Kamati zinavyotekeleza majukumu yake, kutoa ushauri wa kuboresha utendaji, na kupokea maoni kutoka kwa wajumbe wa Kamati. Hivyo, kuimarisha utendaji wa Kamati na nidhamu katika Mahakama na kuongeza imani ya wananchi katika mfumo wa utoaji haki.

***54. Mheshimiwa Spika***, Tume ya Utumishi wa Mahakama imeendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu majukumu yake na uwepo wa Kamati za Maadili za Mikoa na Wilaya katika mikoa ya Manyara, Kigoma, Mbeya, Mwanza, Mtwara, Kagera na Mara. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025, vipindi nane (**8**) vya redio vilirushwa kupitia redio za kijamii za Manyara *FM, Smile FM, TBC, Joy Fm Redio, Morning Star Redio, Safari Fm Redio, Redio Free Africa* pamoja na mitandao ya kijamii ya *Facebook, Instagram, x* (uliojulikana kama *Twitter*) na *Youtube*.

***(v) Uandishi wa Sheria Ikiwa ni Pamoja na Kuandaa Toleo la Sheria Ndogo Zilizofanyiwa Urekebu mwaka 2025 na Kuimarisha Marejeo na Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Mikataba Iliyosainiwa***

***55. Mheshimiwa Spika*,** Wizara kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (OMMS) imeendelea kuhakikisha kuwa sheria za nchi zinakwenda na wakati na zinaakisi sera na vipaumbele vya Serikali katika nyanja za kisiasa, kiuchumi, kijamii, kiutamaduni, kimazingira na kiteknolojia. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 Ofisi iliandaa Miswada ya sheria **16**. Miswada iliyoandaliwa ni kama ilivyoainishwa kwenye **Kiambatisho Na.4**. Aidha, katika kipindi husika, Wizara kupitia OMMS ilisimamia utangazaji wa Sheria Kuu mpya **15** ambazo zilisainiwa na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali (**Kiambatisho Na.5).**

***56. Mheshimiwa Spika*,** katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025, Wizara kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilihakiki na kuchapisha jumla ya Sheria Ndogo **903**, ikilinganishwa na Sheria Ndogo **885** zilizohakikiwa na kuchapishwa katika kipindi kama hicho Mwaka 2023/2024. Lengo la kutengenezwa kwa sheria ndogo ni kufafanua maudhui yaliyobainishwa kwenye Sheria Kuu. Sheria hizo zinajumuisha Kanuni **125**, Amri **171**, Notisi **408**, Sheria Ndogo **182**, Matamko tisa **(9)** na Hati nane (**8**). Orodha ya Sheria Ndogo zilizoandaliwa kuanzia Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 ni kama zinavyoonekana kwenye **Kiambatisho Na.6**.

***57. Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2024/2025, jumla ya Sheria Ndogo Kifani **(*Model By-Laws*) 40** ziliandaliwa kwa ajili ya

kuziongoza Wizara, Taasisi na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika uandaaji wa Sheria Ndogo. Sheria zilizoandaliwa zinajumuisha Sheria **32** za Wizara na Taasisi za Serikali na nane **(8)** za Halmashauri. Aidha, Sheria Ndogo Kifani zinaandaliwa kwa ajili ya kuingizwa katika Mfumo wa kielektroniki wa OAGMIS ili kupunguza dosari za uandishi pamoja na kurahisisha mchakato wa uhakiki. Kati ya Sheria hizo, Sheria nane **(8)** zimekamilika na zimewekwa kwenye Mfumo wa OAGMIS baada ya kuhakikiwa na kuanza kutumika tarehe 01 Machi, 2025. Orodha ya Sheria Ndogo Kifani zilizoandaliwa na kukamilika kuanzia Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 ni kama zinavyoonekana kwenye **Kiambatisho Na.7.**

***58. Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza programu ya kutumia lugha ya Kiswahili kwenye utoaji haki na kuwawezesha wananchi kuzielewa Sheria za nchi, Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa Sheria zote za nchi zinapatikana katika lugha ya Kiswahili na Kiingereza ikiwa ni utekelezaji wa Sheria ya Tafsiri ya Sheria Sura ya 1 mapitio ya Mwaka 2021 inayoelekeza kutafsiri sheria zote zilizopo katika lugha ya Kiingereza kuwa katika lugha ya Kiswahili. Hivyo, katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025, Wizara kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imekamilisha uhakiki wa mwisho wa Sheria Kuu **300** kati ya **446** zilizotafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili kama zinavyoonekana kwenye **Kiambatisho Na.8**.

***59. Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha kuwa sheria zote za nchi zinaendana na wakati na kuwarahisisshia watumiaji katika kufanya rejea ya sheria husika hususan wakati wa utoaji wa haki na utekelezaji wa wajibu ikiwemo huduma za kimahakama na ukusanyaji mapato, Wizara kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imekamilisha urekebu wa Sheria Kuu **446** za nchi na kuandaa Toleo la Sheria Zilizofanyiwa Urekebu la Mwaka 2023. Zoezi hili limefanyika kwa mujibu wa Sheria ya Urekebu wa Sheria, Sura ya 4. Toleo hili ni la pili tangu Nchi yetu ilipopata uhuru. Toleo la Kwanza lilitolewa mwaka 2002 na liliandaliwa kwa ufadhili Benki ya Dunia. Toleo la Sheria Zilizofanyiwa Urekebu la Mwaka 2023 limeandaliwa kwa fedha za ndani na wataalaam wa ndani. Aidha, kwa kuzingatia uzito na umuhimu wa urekebu wa sheria, Toleo hili lilizinduliwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa hafla maalum

iliyofanyika tarehe 23 Aprili, 2025 Ikulu-Chamwino. Toleo hili litaanza kutumika tarehe 1 Julai, 2025. Hatua hii ni sehemu ya jitahada za Serikali ya Awamu ya Sita katika kuimarisha utawala bora, utawala wa sheria na kuimarisha misingi ya utoaji haki.

***60. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, imeendelea kushiriki na kutoa ushauri wa kisheria katika majadiliano mbalimbali ya mikataba ya kibishara, mikutano ya kitaifa, kikanda na kimataifa. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 jumla ya Mikataba ya Kitaifa na Kimataifa **2,574** kutoka Wizara, Idara zinazojitegemea, Mashirika ya Umma, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ilifanyiwa upekuzi ikilinganishwa na Mikataba **1,280** iliyofanyiwa upekuzi katika kipindi kama hicho mwaka 2023/2024 sawa na ongezeko la asilimia **101**. Ongezeko hili linatokana na juhudi za Serikali kuongeza idadi ya miradi kwa ajili ya kutoa huduma kwa wananchi na miradi inayofadhiliwa na Wadau wa Maendeleo. Aidha, Hati za Makubaliano **514** zilifanyiwa upekuzi katika kipindi husika ikilinganishwa na **341** zilizofanyiwa upekuzi katika kipindi kama hicho mwaka 2023/2024. Ongezeko hili linaakisi jitihada za Serikali kuhamasisha uwekezaji na diplomasia ya ushirikiano wa kikanda na kimataifa.

***61. Mheshimiwa Spika***, kati ya mikataba **2,574** iliyofanyiwa upekuzi katika mwaka 2024/2025, mikataba **733** ilithaminishwa katika sarafu mbalimbali katika mchanganuo ufuatao: Mikataba **659** ilikuwa na thamani ya Shilingi **Trilioni 16.82**; Mikataba **50** ilikuwa na thamani ya **Dola za Marekani 582,190,396.71** sawa na Shilingi **Trilioni 1.49**; Mikataba **22** ilikuwa na thamani ya Fedha ya Jumuiya ya Ulaya (Euro) **196,535,051.81** sawa na Shilingi **Trilioni 0.58** na Mkataba mmoja **(1)** ulikuwa na thamani ya fedha ya **Yen ya Japan 390,000** sawa na Shilingi **6,704,061.00**. Mikataba iliyofanyiwa upekuzi ilihusisha masuala ya ununuzi, ujenzi, ukarabati wa majengo na utoaji huduma za jamii kama vile ujenzi wa shule, hospitali na barabara.

***62. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ina jukumu la kutoa ushauri wa kisheria kwa Serikali Kuu, Idara zinazojitegemea, Mashirika ya Umma, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na kwa wananchi. Lengo ni kuhakikisha

Serikali na Taasisi zake zinapata faida kutokana na utekelezaji wa majukumu yake na hivyo, kuikinga Serikali kuingia katika kesi mbalimbali kwa kuhakikisha sheria, kanuni na taratibu za nchi zinafuatwa. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 jumla ya maombi ya ushauri wa kisheria **2,844** yalipokelewa na kufanyiwa kazi ikilinganishwa na maombi **1,707** katika kipindi kama hicho katika mwaka 2023/2024 sawa na ongezeko la asilimia **67.** Kati ya maombi hayo, **347** yalitoka Serikali Kuu (Wizara), **411** Taasisi za Serikali, **83** Mashirika ya Umma, **174** Mamlaka za Serikali zinazojitegemea, **159** Wakala wa Serikali, **230** Mamlaka za Serikali za Mitaa, **69** Makampuni; na **1,373** wadau wengine.

***(vi) Kuratibu Shughuli za Upelelezi, Kuendesha Mashtaka ya Jinai na Kusimamia Utenganishaji wa Shughuli za Mashtaka na Upelelezi***

***63. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Ofisi ya Taifa ya Mashtaka (OTM) ina wajibu wa kuratibu shughuli za upelelezi, kuendesha mashtaka na kusimamia utenganishaji wa shughuli za mashtaka na upelelezi. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili, 2025 OTM ilipokea jumla ya majalada **16,956** kutoka vyombo vya upelelezi ikilinganishwa na majalada **14,925** yaliyopokelewa katika kipindi kama hicho mwaka 2023/2024. Kati ya majalada hayo, majalada **14,925** yaliandaliwa hati za mashtaka sawa na asilimia **88.4** ikilinganishwa na majalada **10,007** yaliyoandaliwa hati za mashtaka katika kipindi hicho mwaka 2023/2024 sawa na asilimia **67.**

***64. Mheshimiwa Spika,*** Kati ya majarada yaliyoshughulikiwa katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili 2025, Majalada **316** yalifungwa ikilinganishwa na majalada **1,028** yaliyofungwa kipindi kama hicho katika mwaka 2023/2024. Aidha, majalada **785** yalirejeshwa kwa upelelezi zaidi ikilinganishwa na majalada **3,087** yaliyorejeshwa kwa upelelezi zaidi katika kipindi kama hicho katika mwaka 2023/2024. Hivyo, kufanya majalada yaliyofanyiwa kazi katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili, 2025 kuwa **16,091** sawa na asilimia **94** ya majalada yaliyopokelewa ikilinganishwa na majalada **14,122** sawa na asilimia **95** ya majalada yaliyofanyiwa kazi katika kipindi kama hicho mwaka 2023/2024. Vilevile,

majalada **863** yalikuwa yanaendelea kufanyiwa kazi kote nchini ikilinganishwa na majalada **803** yaliyokuwa yanaendelea kufanyiwa kazi katika kipindi kama hicho mwaka 2023/2024.

***65. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2024 hadi April, 2025 OTM iliendesha kesi za jinai katika Mahakama za Wilaya, Hakimu Mkazi, Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani. Jumla ya kesi za jinai **27,523** ziliendeshwa katika Mahakama za Wilaya na Hakimu Mkazi ikilinganishwa na kesi **25,037** zilizoendeshwa katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024. Aidha, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2024 hadi Aprili, 2025, jumla ya kesi **21,232** sawa na asilimia **77** zilihitimishwa ikilinganishwa na kesi **15,084** sawa na asilimia **60** ya kesi zilizohitimishwa katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2023/2024. Kati ya kesi zilizohitimishwa, **13,409** zilihitimishwa kwa washtakiwa kutiwa hatiani sawa na asilimia **63** ikilinganishwa na kesi **10,444** sawa na asilimia **69** zilizohitimishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2023/2024.

***66. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka iliendesha jumla ya kesi **707** katika Mahakama za watoto ikilinganishwa na kesi **622** zilizoendeshwa katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2023/2024 ambapo kesi **590** zilihitimishwa sawa na asilimia 83**,** ikilinganishwa na kesi **454** sawa na asilimia **67** zilizohitimishwa mwaka 2023/2024. Kati ya kesi **590** zilizohitimishwa kesi **438** sawa na asilimia **74** zilihitimishwa kwa watuhumiwa kutiwa hatianai.

***67. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili, 2025, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka iliendesha jumla ya kesi **2,638** katika Mahakama Kuu ya Tanzania ikilinganishwa na kesi **6,409** zilizoendeshwa katika kipindi kama hicho mwaka 023/2024. Aidha, kesi **1,135** sawa na asilimia **43** zilihitimishwa ikilinganishwa na kesi **754** zilizohitimishwa kwa kipindi kama hicho mwaka 2023/2024 sawa na asilimia **12** ya kesi zilizoendeshwa.

***68. Mheshimiwa Spika****,* katika mwaka 2024/2025 hadi Aprili, 2025, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka iliendesha kesi kubwa **177** katika Mahakama Kuu – Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi ikilinganishwa na kesi **60** zilizoendeshwa kipindi

kama hicho mwaka 2023/2024. Aidha, kesi **108** sawa na asilimia **61** zilihitimishwa ikilinganishwa na kesi **22** zilizohitimishwa katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 na kesi **69** sawa na asilimia **38** zinaendelea katika hatua mbalimbali.

***69. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka iliendesha jumla ya rufaa na maombi **1,842** ya jinai katika Mahakama ya Rufani ikilinganishwa na rufaa na maombi **2,905** yaliyoendeshwa kipindi kama hicho katika mwaka 2023/24. Kati ya kesi hizo, rufaa na maombi **655** yalihitimishwa sawa na asilimia **36** ya Rufaa na Maombi yaliyoendeshwa ikilinganishwa na rufaa na maombi **414** yaliyohitimishwa kipindi kama hicho mwaka 2023/2024 sawa na asilimia **14** ya rufaa na maombi yaliyokuwa yanasikilizwa.

***70. Mheshimiwa Spika*****,** Wizara kupitia Ofisi ya Taifa ya Mashtaka inaendelea kukagua magereza na vituo vya polisi nchini kwa lengo la kuainisha changamoto za kiutendaji na kiupelelezi na kutoa maelekezo stahiki ya kutatua changamoto hizo kwa mujibu wa sheria. Katika mwaka 2024/2025, hadi kufikia Aprili, 2025 jumla ya magereza **109** yalikaguliwa ikilinganishwa na magereza **107** yaliyokaguliwa kipindi kama hicho katika mwaka 2023/2024 sawa na ongezeko la magereza **2**. Pia, ukaguzi umefanyika katika vituo vya Polisi **289** ikilinganishwa na vituo **251** vilivyokaguliwa katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2023/2024 ikiwa ni ongezeko la vituo **38**. Katika ukaguzi huo jumla ya mahabusi **1,296** waliachiwa ikilinganishwa na mahabusi **1,250** walioachiwa kipindi kama hicho kwa mwaka 2023/2024 (**Kiambatisho Na.9).**

***71. Mheshimiwa Spika***, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imeendelea kutekeleza Mpango wa Kutenganisha Shughuli za Mashtaka na Upelelezi kwa kuendelea kuongeza idadi ya Mawakili wa Serikali na kuendelea kutoa vibali vya kuendesha mashtaka kwa Waendesha Mashtaka kutoka Ofisi na Taasisi mbalimbali. Lengo la mpango huu ni kusogeza huduma za kimashtaka kwa wananchi katika ngazi za Mikoa na Wilaya. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025, Ofisi ilihuisha Kanzidata ya Waendesha Mashtaka waliopewa kibali cha kuendesha mashtaka na Mkurugenzi wa Mashtaka na Daftari la Mawakili wa Serikali. Hadi Aprili, 2025, Ofisi

ya Taifa ya Mashtaka ina jumla ya Mawakili **680** pamoja na Waendesha Mashtaka waliopewa kibali na Mkurugenzi wa Mashtaka wapatao **964** nchi nzima. Aidha, jumla ya wataalam **206** wanaohusika na upelelezi katika maeneo ya maandishi, picha, alama za vidole na milipuko wametangazwa katika Gazeti la Serikali.

***72. Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imeendelea kusogeza huduma za kimashtaka kwa wananchi katika ngazi za Mikoa na Wilaya. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025, Ofisi inaendelea kutoa huduma za kimashtaka katika mikoa **30** ya Kimashtaka na Ofisi **108** za Wilaya. Aidha, katika kipindi husika, Ofisi imekamilisha ujenzi wa majengo ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka katika Mikoa minne (**4**) ya Shinyanga, Manyara, Katavi na Rukwa. Vilevile, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka inaendelea na ujenzi wa Ofisi katika mikoa ya Morogoro (asilimia **90**), Mbeya (asilimia **92**), Njombe (asilimia **60**), Geita (asilimia **60**), Kinondoni (asilimia **70**) na Temeke (asilimia **70**)

***(vii) Kushughulikia Uendeshaji wa Mashauri ya Madai na Usuluhishi wa Migogoro ya Kibiashara, Sheria za Kimataifa na Mikataba***

***73. Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (OWMS) inaendelea kuiwakilisha Serikali katika kuratibu, kusimamia na kuendesha mashauri ya madai na usuluhishi yaliyopo na yatakayofunguliwa katika Mahakama na Mabaraza ya Usuluhishi ndani na nje ya nchi. Mahakama na Mabaraza hayo ni Mahakama ya Rufaa, Mahakama Kuu ya Tanzania, Mahakama za Wilaya, Mahakama nje ya nchi na Mabaraza ya Usuluhishi ya ndani na nje ya nchi (*NCC, Tiarb, Ad hoc Arbitral Tribunals, ICSID, ICC, PCA* na *LCIA*).

***74. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeendesha jumla ya mashauri ya Madai **9,013**. Kati ya Mashauri hayo, Mashauri **8,347** ni madai ya kitaifa, Mashauri **33** ni ya madai ya kimataifa na mashauri **633** ni mashauri ya Kikatiba na Haki za Binadamu. Katika kuendesha mashauri hayo, mashauri **966** yalimalizika. Kati ya

mashauri yaliyomalizika, mashauri **814** ni ya madai ya kitaifa, shauri **moja (01)** ni la madai ya kimataifa na mashauri **151** ni ya Kikatiba na Haki za Binadamu. Kwa kumalizika kwa mashauri hayo, Ofisi imefanikiwa kushinda mashauri **750** sawa na asilimia **77.6%** ya mashauri yaliyomalizika kwa kipindi husika na kuokoa kiasi cha Shilingi **51,022,810,719.81** kiasi ambacho Serikali ingelipa endapo ingeshindwa mashauri hayo.

***75. Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeendesha mashauri **70** yaliyotokana na Uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliofanyika mwezi Novemba,2024. Kati ya mashauri hayo, mashauri matano **(5)** yaliyofunguliwa kabla ya uchaguzi na mashauri **65** yalifunguliwa baada ya uchaguzi. Katika kuendesha mashauri hayo, mashauri **57** yalihitimishwa kwa Ofisi kushinda mashauri **56** sawa na asilimia **98.2%** ya mashauri yaliyomalizika na kushindwa shauri moja **(01)** ambalo limekatiwa rufaa na Mashauri **13** yaliyobaki yanaendelea katika Mahakama mbalimbali nchini.

***76. Mheshimiwa Spika***, mashauri yaliyofunguliwa kabla ya uchaguzi yalikuwa yakipinga Ofisi ya Rais, TAMISEMI kusimamia uendeshaji wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Katika mashauri hayo, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ilisimamia na kuendesha mashauri hayo na kufanikisha Serikali kushinda. Hayo ni mafanikio makubwa kwani endapo Serikali ingeshindwa katika mashauri hayo, ingesimamisha kufanyika kwa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa muda uliopangwa na kuongeza gharama kwa Serikali.

***77. Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa mashauri ya usuluhishi, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 imeshughulikia jumla ya mashauri ya usuluhishi **209.** Ambapo, kati ya mashauri hayo, **180** ni ya usuluhishi wa kitaifa na mashauri **29** ni ya usuluhishi wa kimataifa. Katika kipindi husika, mashauri **21** yalimalizika kati ya hayo, Ofisi imefanikiwa kushinda mashauri **16** sawa na asilimia **76.2** ya mashauri yaliyomalizika.

***78. Mheshimiwa Spika,*** kutokana na kumalizika kwa mashauri hayo, Serikali imeokoa kiasi cha shilingi **16,937,954,066.64** na Dola

za Marekani **63,341,890.03** kiasi ambacho Serikali ingelipa endapo ingeshindwa mashauri hayo.

***79. Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeendelea kusimamia, kufuatilia na kupitia taratibu za uendeshaji wa mashauri ya madai na usuluhishi. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025, Ofisi imeshughulikia notisi **754** za siku tisini zenye nia ya kuishtaki Serikali na kuandaa taarifa **28** kwa lengo la kuzuia uzalishaji wa mashauri mapya, kutatua migogoro kwa njia ya usuluhishi na kuweka mikakati ya kuzuia kutokea tena kwa mashauri, hivyo kupunguza mlundikano wa mashauri mahakamani.

***80. Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeendelea kubuni mikakati mbalimbali ya kuzuia uzalishaji wa mashauri mapya na kutatua migogoro kwa njia ya usuluhishi. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025, Ofisi ilifanya ukaguzi wa majalada na namna ya uendeshaji wa mashauri yanayoendelea mahakamani katika Mikoa tisa (**9)** ikiwemo Tabora, Kilimanjaro, Mwanza, Kagera, Mara, Arusha, Mbeya, Iringa, na Manyara ili kubaini changamoto za kisheria na kiutendaji katika uendeshaji wa mashauri mathalani kubaini kama Mawakili wa Serikali wanafuata miongozo na taratibu zilizowekwa za uendeshaji wa mashauri. Aidha, katika kipindi husika Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ilitoa kibali kwa Mawakili wa Serikali **2,746** cha uendeshaji wa mashauri ya Madai na kutoa mafunzo kwa Mawakili wa Serikali **35** kuhusu miongozo ya viwango vya uendeshaji wa mashauri vya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

#### *(viii) Kuwezesha Uanzishwaji wa Kituo cha Usuluhishi wa Migogoro*

***81. Mheshimiwa Spika***, uwepo wa mifumo thabiti ya utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala ni msingi muhimu katika maendeleo ya kibiashara na uwekezaji kwa kuwa huwezesha kutunza amani ya pande zinazovutana, kupunguza muda ambao pande hizo zingetumia mahakamani pamoja na hasara inayoweza kujitokeza katika biashara au uwekezaji. Katika mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara imepata jengo kwa ajili ya kuanzisha Kituo cha Taifa cha

Usuluhishi wa Migogoro kwa njia Mbadala Tanzania ambapo jitihada za ukarabati wa jengo hilo unaendelea. Aidha, Wizara inaendelea na mapitio ya Sheria ya Usuluhishi, Sura ya 15 na Kanuni zake ili kuwezesha Kituo kufanya kazi kwa ufanisi; pamoja na kuboresha Mfumo wa Kieletroniki wa Utambuzi, Usajili na Usimamizi wa Watoa Huduma za Utatuzi wa Migogoro kwa Njia Mbadala.

***82. Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili, 2025, Wizara imeimarisha mfumo wa utatuzi wa migogoro nje ya Mahakama kwa kutumia njia za majadiliano, maridhiano, upatanishi na usuluhishi ambapo:-

(i) Kikao cha Jopo la Ithibati kimefanyika, katika kikao hicho, jumla ya maombi **78** ya watatuzi wa migogoro kwa njia mbadala na taasisi moja yalijadiliwa na kupitishwa wakiwemo Wasuluhishi **26**; Waendesha Majadiliano **16**; Wapatanishi **23**; Waendesha Maridhiano **12** na Taasisi ya moja (**1)**;

(ii) Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano baina ya Wizara, Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo na Kituo cha Usuluhishi wa Migogoro kwa Njia mbadalaTanzania, (*Tanzania International Arbitration Centre - TIAC*) imesainiwa. Hati hiyo imebainisha ushirikiano katika eneo la utoaji mafunzo ya masuala ya utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala;

(iii) Watatuzi wa Migogoro kwa njia Mbadala **50** walipatiwa mafunzo kuhusu mbinu za usuluhishi na utatuzi wa migogoro; na

(iv) Mfumo wa Kielektroniki wa Maombi ya Usajili wa Watatuzi wa Migogoro kwa Njia Mbadala umeboreshwa ambapo kwa sasa unaruhusu watumiaji kupata na kuhuisha vyeti vyao kwenye mfumo na kuwezesha kufanya malipo bila kulazimika kuja Wizarani.

***(ix) Kuwezesha Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria Kuanza Kutekeleza Majukumu Yake***

***83. Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha upatikanaji haki na utawala bora, Serikali kupitia Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Sekta ya Sheria, Na. 11/2023 ilifanya marekebisho ya muundo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuanzisha Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria. Lengo la maboresho haya ni kuongeza tija na ufanisi katika shughuli za uandishi wa sheria, urekebu na ufasiri wa sheria. Muundo wa kiutawala wa Ofisi hii uliidhinishwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 14 Januari, 2025 ili kuiwezesha kuendelea kutekeleza majukumu yake. Aidha, tayari Ofisi imepewa fungu la kibajeti ambalo ni Fungu 101 kwa ajili ya kuiwezesha Ofisi hiyo kuandaa Mpango na Bajeti kila mwaka.

***(x) Kuratibu Masuala ya Haki za Binadamu na Utawala Bora***

***84. Mheshimiwa Spika***, Tanzania ni miongoni mwa nchi mwanachama wa Umoja wa Mataifa ambapo kama mwanachama, imeridhia mikataba na itifaki mbalimbali zinazohusu masuala ya haki za binadamu ambazo utekelezaji wake unapaswa kutolewa taarifa kwa vipindi husika. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 Wizara iliandaa rasimu mbili (**2**) za taarifa ambazo ni: -

(i) Taarifa ya Utekelezaji wa Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu wa mwaka 1981; na

(ii) Taarifa ya Utekelezaji wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Watu wenye Ulemavu wa mwaka 2006.

***85. Mheshimiwa Spika***, rasimu za taarifa hizo za utekelezaji wa mikataba na itifaki zinatarajiwa kuwasilishwa kwenye Kamati za Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika zinazosimamia utekelezaji wa Mikataba hiyo na Itifaki ndani ya mwaka 2025. Uwasilishaji wa taarifa ya Mikataba na Itifaki una manufaa kwa Nchi kwa kuwa taarifa hizo zitaonesha hatua mbalimbali ambazo nchi imechukua katika kuhakikisha kuna mazingira wezeshi kupitia

sheria na maboresho mbalimbali ya kisekta kwa wananchi. Aidha, kupitia uwasilishaji wa taarifa hizo nchi itaonekana kimataifa namna ambavyo imechukua hatua za kulinda na kukuza haki za binadamu na hivyo kuvutia na kukuza uwekezaji wa kigeni na utalii nchini.

***86. Mheshimiwa Spika,*** katika uendelevu wa usimamizi wa haki za binadamu kimataifa, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hufanyiwa tathmini ya utekelezaji wa haki za binadamu chini ya mfumo wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Binadamu wa Mapitio Katika Kipindi Maalum (*Universal Periodic Review-UPR*). Kwa upande wa Tanzania, tathmini hiyo itafanyika mwaka 2026, hivyo, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025, Asasi za Kiraia **55** zilijengewa uwezo wa namna ya kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa haki za binadamu katika maeneo mahsusi. Aidha, Wizara iliratibu mafunzo ya kuwajengea uwezo maafisa **40** kutoka katika Wizara na Taasisi za Umma kutoka Tanzania Bara na Zanzibar**.** Mafunzo hayo yalihusu Mapitio katika Kipindi Maalum (UPR) na uandaaji wa taarifa mahsusi za utekelezaji wa mikataba ya haki za binadamu ambayo nchi imeridhia.

***87. Mheshimiwa Spika***, katika kukuza ushirikiano wa kimataifa na kulinda haki za binadamu, katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili 2025 Serikali iliratibu na kuwa Nchi Mwenyeji wa Warsha ya Kikanda ya kujenga uwezo kwa Nchi za Afrika Wanachama wa Jumuiya ya Madola kuhusu uwasilishaji wa Ripoti za Mikataba na Kuimarisha Mifumo ya Kimataifa ya Utekelezaji, Uwasilishaji na Ufuatiliaji wa Mikataba ya haki za binadamu. Warsha hiyo ilihudhuriwa na washiriki **42** kutoka Nchi **15** Wanachama.

***88. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025, Wizara ilishiriki katika vikao vya 56, 57 na 58 vya Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa, Geneva-Uswisi, na Kikao cha Kamati ya Tatu cha Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa. Kupitia ushiriki huu, Wizara imewasilisha taarifa muhimu kwa Umoja wa Mataifa kuhusu jitihada na mafanikio katika kulinda, kuhifadhi na kukuza haki za wanawake, watoto, watu wenye ulemavu, haki ya maendeleo, haki ya kufikia haki na usawa mbele ya sheria, haki ya kupata afya na elimu na mafanikio katika kukuza demokrasia

na kuimarisha haki za kiraia, kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni na kijamii.

***89. Mheshimiwa Spika,*** ili kuimarisha uratibu wa usimamizi wa masuala ya haki za binadamu nchini, katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 Wizara imeandaa rasimu ya Mpango Kazi wa Pili wa Kitaifa wa Haki za Binadamu kwa kipindi cha mwaka 2025/2026 – 2028/2029. Vilevile, Mpango Kazi huo unalenga makundi maalum yakiwemo; wanawake, watoto, watu wenye ulemavu na wazee. Mpango Kazi huo utawezesha Serikali kutekeleza majukumu yake kwa kuwa na mipango ya muda mfupi na wa kati katika kuboresha upatikanaji wa haki hizo kwa wakati. Mpango Kazi huo utazinduliwa mwishoni mwa mwaka, 2025.

***90. Mheshimiwa Spika,*** katika jitihada za kuboresha utendaji kazi wa watumishi na kuongeza ufanisi katika kushughulikia masuala ya haki za binadamu, Watumishi **700** wa Serikali kutoka Wizara na Taasisi mbalimbali walijengewa uelewa juu ya Mfumo wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Binadamu, Mfumo wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu pamoja na wajibu wa kutekeleza na kutoa taarifa za utekelezaji wa Mikataba ya haki za binadamu ambayo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeridhia. Aidha, watumishi hao walijengewa uelewa kuhusu maadili na haki za binadamu.

***91. Mheshimiwa Spika,*** katika kusimamia hifadhi ya haki za binadamu na misingi ya utawala bora nchini, Wizara kupitia Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) imeendelea kupokea na kushughulikia malalamiko yanayohusu uvunjwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025 THBUB ilianza na malalamiko **759** na kusajili malalamiko mapya **160** kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 hivyo kufanya jumla ya malalamiko hayo kuwa **919**. Kati ya malalamiko hayo, **480** yalihusu uvunjwaji wa haki za binadamu, **37** uvunjwaji wa haki za binadamu kwa makundi maalum na **469** ukiukwaji wa misingi ya utawala bora.

***92. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2024/2025, Wizara kupitia THBUB ilifanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo

yaliyotolewa katika mamlaka mbalimbali kwenye malalamiko saba (**7**) yenye mapendekezo **46** kuhusiana na migogoro ya ardhi kati ya wananchi na taasisi mbalimbali na uvunjwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora katika Mikoa ya Morogoro, Shinyanga, Kigoma na Rukwa. Lengo la kufanya ufuatiliaji huo, ni kuweza kubaini namna ambavyo mapendekezo hayo yametekelezwa. Kati ya mapendekezo **46** yaliyotolewa Tume, **23** yametekelezwa na kukamilika na **23** yanaendelea kutekelezwa.

***93. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi husika Wizara kupitia Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ilifanya uchunguzi maalum wa malalamiko **105** ambapo ilitembelea maeneo ya tukio ili kukusanya ushahidi na vielelezo kuhusu tuhuma za uvunjwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora. Uchunguzi huo ulihusu masuala mbalimbali ikiwemo ardhi, ukatili wa kijinsia, ndoa, wafanyakazi kutopatiwa haki zao, tuhuma za watu kupotea na vitendo vya mauaji. Taarifa zenye mapendekezo zimeandaliwa na kuwasilishwa kwenye Taasisi husika kwa ajili ya kuchukua hatua stahiki.

***94. Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha elimu kuhusu masuala ya haki za binadamu na misingi ya utawala bora inawafikia wananchi hasa katika maeneo ya pembezoni, Wizara kupita THBUB imeendelea kutoa elimu hiyo kwa wananchi na Viongozi mbalimbali wa Serikali. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 THBUB ilifanya mikutano ya hadhara na wananchi katika Mikoa tisa (**9**) na Halmashauri **47** kama ifuatavyo; (Mkoa wa Kigoma Halmashauri nane (**8**), Tabora Halmashauri nane (**8**), Singida Halmashauri saba (**7**) Kagera Halmashauri tano (**5**), Dodoma Halmashauri tatu (**3**), Iringa Halmashauri tano (**5**) Njombe Halmashauri sita (**6**); Manyara Halmashauri tano (**5**) na Mkoa wa Mjini katika Manispaa ya Mjini Zanzibar (**2**).

***95. Mheshimiwa Spika***, katika kujenga uelewa wa wananchi kuhusu Haki za Binadamu na namna ya kulinda haki hizo, Wananchi **64,550** walipatiwa elimu katika mikutano ya hadhara **92** iliyofanyika katika mikoa tisa (**9**). Katika mikutano hiyo, malalamiko **103** yaliwasilishwa na wananchi ambapo **52**

yalishughulikiwa na kuhitimishwa kwa kushirikiana na mamlaka nyingine zilizokuwa zinahusika ama kulalamikiwa na wananchi wa eneo husika. Pia, jumla ya vipeperushi **14,020** vyenye jumbe mbalimbali za kuelimisha ikiwemo "*Utaratibu wa kuwasilisha malalamiko Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Utawala Bora* na *Ijue THBUB*" vilitolewa. Vilevile, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025 Jumla ya vipindi vya redio na televisheni **30** viliandaliwa na kurushwa vikiwa na maudhui mbalimbali ya utoaji elimu kwa umma.

**96. *Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) imeanzisha utaratibu wa kutoa elimu kwa njia ya Jumbe Fupi (*Bulk SMS*) kupitia simu za mkononi ambapo kwa sasa, jumbe moja inawafikia takribani wananchi **87,557**. Katika kuhakikisha THBUB inawafikia wananchi wanaotumia mitandao ya kijamii imefungua akaunti katika Mtandao wa Jamii Forums. Mtandao huu unatembelewa na zaidi ya watu **milioni 1** kwa siku hivyo kufanya jumbe zinazotolewa na THBUB kwa siku kutembelewa na wananchi takribani **Milioni 1**. THBUB inaendelea kuimarisha akaunti zake za Mitandao mingine ya kijamii (Facebook, Instagram na Youtube); ambapo, kupitia akaunti hizo THBUB inatoa elimu na kuweka midahalo mbalimbali yenye lengo la kutoa elimu ya haki za binadamu na misingi ya utawala bora.

**97. *Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia THBUB ilifanya ukaguzi katika Magereza **29** na Vituo vya Polisi **23** katika mikoa **14** ya Tanzania Bara, na miwili (**2**) Tanzania Zanzibar kama ifuatavyo: -

(i) Gereza la ukonga, Segerea, Keko na kituo cha polisi Stakishari katika Mkoa wa Dar es Salaam;

(ii) Gereza la Mahabusu Morogoro mjini na Gereza la Mifugo Mtego wa Simba Mkoa wa Morogoro;

(iii) Gereza la Iringa, Pawaga, Isupilo, gereza la Mgagao na kituo cha Polisi mjini Kati Mkoa wa Iringa;

(iv) Gereza la Singida, Manyoni, Kiomboi na vituo vya Polisi, Kiomboi na Manyoni Mkoa wa Singida;

(v) Gereza la Kibondo, na kituo cha Polisi Kibondo Mkoa wa Kigoma;

(vi) Gereza la Njombe, Ludewa na Kituo cha Polisi kati Njombe na Ludewa;

(vii) Gereza la Babati, Mbulu na Vituo vya Polisi Babati, Mbulu na Simanjiro Mkoa wa Manyara;

(viii) Gereza la Urambo, Uyui na vituo vya Polisi Nzega, Igunga, Urambo na Kituo cha kati Tabora katika Mkoa wa Tabora;

(ix) Gereza la Mkuza pamoja na vituo vya Polisi Mlandizi na Kibaha Mkoa wa Pwani;

(x) Gereza la Ruanda, Tukuyu na kituo cha Polisi Kati Mbeya;

(xi) Gereza la Biharamulo na kituo cha Polisi Wilaya Biharamulo Mkoa wa Kagera;

(xii) Gereza kuu Butimba, Magu, na kituo cha Polisi Buhongwa na Buswelu Mkoa wa Mwanza;

(xiii) Gereza la Chato na Geita Mkoa wa Geita;

(xiv) Gereza la Arusha;

(xv) Chuo cha Mafunzo cha Kiinuamiguu na Kinumoshi Wilaya ya kati Mkoa wa Kusini Unguja pamoja; na

(xvi) Vituo vya Polisi Mwembemadema na Fumba katika Mkoa wa Mjini Magharibi na shule ya maadilisho Zanzibar.

***98. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia THBUB inaendelea na programu ya uanzishwaji wa klabu za haki za binadamu katika taasisi za elimu kwa lengo la kujenga na kuimarisha kizazi kinachoheshimu haki za binadamu na misingi ya utawala bora nchini. Katika kipindi husika, jumla ya klabu za haki za binadamu **55** katika shule za Msingi, Shule za Sekondari, Vyuo vya Kati na Vyuo Vikuu Nchini zimeanzishwa na kufanya kuwa na jumla ya klabu za haki za binadamu **364.**

***99. Mheshimiwa Spika***, kifungu cha 6(1)(k) cha Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Sura ya 391 kimeipa wajibu THBUB kutoa mapendekezo kwa sheria zote ili kuhakikisha zimezingatia haki za binadamu na misingi ya utawala bora. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025 Wizara kupitia Tume imepitia sheria nne (**4**) za hifadhi za maliasili na kupendekeza maeneo yanayohitaji kufanyiwa marekebisho. Sheria hizo ni: -

(i) Sheria ya Hifadhi ya Mamlaka ya Eneo la Ngorongoro, Sura ya 284;

(ii) Sheria ya Hifadhi ya Wanyamapori Sura ya 283;

(iii) Sheria ya Hifadhi za Taifa, Sura ya 282; na

(iv) Sheria ya Misitu, Sura ya 323.

***100. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia THBUB imeendelea na zoezi la kuratibu uandaaji wa Mpango Kazi wa Kitaifa wa Haki za Binadamu na Biashara wa miaka mitano (2025/2026- 2029/2030). Lengo la Mpango Kazi huu ni kubainisha vipaumbele vya nchi katika kutekeleza Mwongozo wa Kanuni za Umoja wa Mataifa Kuhusu Haki za Binadamu na Biashara - *(United Nations Guiding Principles on Business and Human Rights (UNGPs-BHR*) wa mwaka 2011. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 THBUB imekusanya maoni ya wadau katika mikoa nane (**8**) ya Tanzania Bara na minne (**4**) ya Zanzibar yaliyopelekea kuandaliwa kwa rasimu ya awali ya mpango husika. Rasimu ya Mpango Kazi wa Kitaifa iliwasilishwa katika kamati ya Kitaifa ya Usimamizi wa Uandaaji Mpango huo kwa hatua ya mapitio.

***(xi) Kuimarisha Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu pamoja na Usajili na Ufilisi katika Mikoa yote ya Tanzania Bara***

***101.*** **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini - RITA inaendelea na utekelezaji wa programu mbalimbali za usajili wa matukio muhimu ya binadamu ikiwemo usajili wa watoto walio chini ya umri wa miaka mitano, usajili wa watoto walio na umri wa miaka 5 hadi 17 na watu walio na umri wa miaka 18 na kuendelea. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 Wakala umesajili na kutoa vyeti vya kuzaliwa **1,338,618** (Wanaume **667,970** na Wanawake **670,648**) sawa na asilimia **102** ikilinganishwa na lengo la kusajili na kutoa vyeti vya kuzaliwa **1,312,359**. Usajili huo umegawanyika katika makundi yafuatayo:-

(a) Usajili na utoaji vyeti vya kuzaliwa kwa watoto walio na umri chini ya miaka mitano. Wizara kupitia Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 Wakala umesajili na kutoa vyeti vya kuzaliwa **653,841**kwa watoto walio na umri chini ya miaka mitano sawa na **asilimia 101** ikilinganishwa na shabaha ya kusajili watoto **645,737.** Kati yao, wa kike **326,267** na wa kiume ni **327,574.** Usajili huu umefanya jumla ya idadi ya watoto waliosajiliwa kupitia kundi hili kuanzia mwaka 2013 hadi kufikia Aprili, 2025 kuwa **10,824,267** (wa kiume **5,354,561** na wa kike **5,469,707**). Wakala unaendelea kuhamasisha wananchi kujitokeza ili kuwezesha usajili na utoaji vyeti vya kuzaliwa kwa kila tukio la kizazi linalotokea kwenye vituo vya afya na kwenye jamii bila malipo ndani ya siku 90.

Katika kuboresha usajili na utoaji wa vyeti kwa wakati kwa watoto wanaozaliwa, Wizara kupitia Wakala kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais-TAMISEMI imeendelea kutoa maelekezo na kufanya ufuatiliaji kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa 184. Lengo ni kuhakikisha kuwa, watoto wanapozaliwa wanasajiliwa na kupatiwa nyaraka ya kisheria ili kuthibitisha kutokea kwa tukio husika ikiwa ni sehemu ya haki ya mtoto. Aidha, nitumie fursa hii kutoa wito kwa Watendaji wa Vituo vya kutolea huduma za Tiba na Ofisi za Kata kuingiza taarifa za usajili wa watoto kwenye

kanzidata ya RITA ili kuiwezesha Serikali kupata takwimu za watoto waliozaliwa kwa ajili ya mipango ya maendeleo.

(b) Usajili wa watoto walio na umri wa miaka 5 hadi 17 waliopo shuleni. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 Wakala umesajili na kutoa vyeti **239,672**sawa na **asilimia 119** ya lengo la kusajili watoto **201,389.** Kati ya watoto waliosajiliwa watoto wa kike ni **120,315**na watoto wa kiume ni **119,357**.

(c) Usajili wa watu wenye umri wa miaka 18 na kuendelea. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 Wakala umesajili na kutoa vyeti vya kuzaliwa **445,105** (wanawake **222,107** na wanaume **222,998**) sawa na asilimia 100.47 ya lengo la kusajili na kutoa vyeti **465,233**. Aidha, Wakala umefanya uhakiki wa vyeti vya kuzaliwa **142,356** kwa ajili ya kuwawezesha wanafunzi wanaoomba mikopo kwenye Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu pamoja na wananchi kupata huduma za bima ya afya.

***102. Mheshimiwa Spika,*** Wakala umeendelea kuratibu na kusimamia usajili wa matukio ya vifo, ndoa, talaka na watoto wa kuasili nchini kwa lengo la kuwezesha wananchi kupata haki zinazotokana na nyaraka husika. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 Wakala umesajili na kutoa vyeti vya vifo **35,163.** Vilevile, Wakala umefanya uhakiki wa vyeti vya vifo **25,032** kwa ajili ya kuwawezesha wanafunzi wanaoomba mikopo kwenye Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu pamoja na wananchi kupata huduma za bima ya afya.

***103. Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 Wakala umesajili marejesho ya shahada za Ndoa **35,052** zilizofungwa sawa na asilimia **65** ya lengo la kusajili ndoa **54,167**. Aidha, jumla ya leseni mpya **2,994** za kufungisha ndoa zilitolewa kwa viongozi wa dini na leseni **986** za kufungisha ndoa zilihuishwa. Vilevile, katika kipindi husika nakala ngumu **233,514** za ndoa zimehifadhiwa katika mfumo wa kielektroniki.

***104. Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 Wakala umesajili na kutoa vyeti **675** vya talaka sawa na asilimia **116** ya lengo la kusajili talaka **583**. Natoa wito kwa viongozi wote waliopewa dhamana ya kufungisha ndoa, wazazi na walezi kuendelea kutoa elimu ya maadili kwa wanandoa. Vilevile, natoa wito kwa wanandoa kujenga utamaduni wa kuvumiliana na kutatua changamoto zinazojitokeza kwa njia ya majadiliano ili kupunguza talaka zinazoathiri malezi ya watoto kwa mustakabali wa haki zao.

***105. Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza Kampeni ya Kitaifa ya Kulinda Maadili, Haki na Ukatili Dhidi ya Watoto, katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 Wakala umesajili na kutoa vyeti **29** vya kuasili watoto sawa na **asilimia 79** ya lengo la kusajili watoto wa kuasili **37.**

***106. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 Wizara kupitia Wakala ilipokea jumla ya maombi ya huduma za bodi za wadhamini **1,211.** Kati ya maombi hayo **1,161** yalihitimishwa na **56** yanaendelea kufanyiwa kazi kama yanavyobainishwa katika **kiambatisho Na.10**. Vilevile, Wakala ulipokea migogoro **33** ya bodi za wadhamini ambapo migogoro **18** ilitatuliwa kwa njia ya majadiliano na migogoro **15** ipo katika hatua mbalimbali ya usuluhishi. Aidha, katika kupunguza migogoro, Wakala umeanza kuwajengea uwezo Wajumbe wa Bodi za Wadhamini na wadau wengine **423.**

***107. Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia Wakala imeendelea kuimarisha upatikanaji haki kwa wakati kwa wananchi hususan katika masuala ya mirathi. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 Wakala ulipokea mashauri mapya ya mirathi **14** na kufanya jumla ya mirathi inayosimamiwa kufikia **140**. Katika kipindi husika mirathi sita (**6**) imefungwa baada ya kugawa mali kwa wanufaika na **134** inaendelea kufanyiwa kazi.

***108. Mheshimiwa Spika***, Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025, Wakala umeandika na kutunza wosia **109** na kuendelea kutoa elimu zaidi kwa wanachi kuhusu faida za kuandika na kuhifadhi wosia ili kupunguza migogoro ya mirathi inayojitokeza

katika jamii. Aidha, Wakala umetoa elimu kuhusu uandishi wa wosia na masuala ya mirathi kwa wananchi **10,858** (wanawake **6,063** na wanaume **4,795**) kupitia makongamano na maonesho ya Kitaifa ikiwemo Wiki ya Sheria, Nanenane, Sabasaba na Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia katika mikoa ya Kigoma, Katavi, Rukwa, Geita na Lindi.

***109. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025, Wakala umehudhuria mashauri **59** yaliyopo katika Mahakama mbalimbali pamoja na Mabaraza ya Ardhi na Nyumba yanayohusu masuala ya mirathi na Bodi za Wadhamini zinazosimamiwa na Wakala. Hadi kufikia Aprili, 2025, jumla ya mashauri **33** yamemalizika na mashauri **26** yanaendelea kufanyiwa kazi.

***(xii) Kuratibu Tathmini na Maboresho ya Sheria ikiwa ni pamoja na Kufanya Mapitio ya Mifumo ya Sheria inayosimamia Elimu, Michezo ya Kubahatisha na Kufanya Utafiti wa Mfumo wa Sheria Unaosimamia Utatuzi wa Migogoro ya Kibenki na Taasisi za fedha***

***110. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025, Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania iliendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia maeneo mahsusi ya vipaumbele kama msingi wa kutekeleza dhima ya Tume ya "*Kufanya mapitio na utafiti ili kuboresha sheria za Jamhuri ya Muuungano wa Tanzania kulingana na misingi ya Katiba kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii*".

***111. Mheshimiwa Spika,*** Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania imefanya Tathmini ya Utekelezaji wa Sheria Zinazosimamia Michezo ya Kubahatisha, Sura ya 41, ili kubaini kama malengo ya kutungwa kwa sheria hiyo yamefikiwa. Tathmini hii imejikita katika kuangalia ni kwa kiasi gani utekelezaji wa sheria unalinda washiriki wa michezo ya kubahatisha wasiathirike na uraibu. Vilevile, kuangalia ikiwa utekelezaji wa sheria hii umeweza kulinda watoto chini ya miaka 18 wasishiriki katika michezo ya kubahatisha na kupata uraibu wa kushiriki michezo hiyo. Taarifa ya Tathmini ya

Utekelezaji wa Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Sura ya 41 itakamilika kabla au ifikapo Juni, 2025.

***112. Mheshimiwa Spika,*** kutokana na kuongezeka kwa mashauri yanayotokana na migogoro ya kibenki na taasisi za fedha kuhusiana na mikopo, Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania imefanya utafiti wa mfumo wa sheria unaosimamia utatuzi wa migogoro ya kibenki na taasisi za fedha kuhusu mikopo. Utafiti huo unalenga kubainisha changamoto zinazoukabili mfumo wa utatuzi wa migogoro tajwa na kuishauri Serikali hatua stahiki za kuchukua ili kuwa na mfumo madhubuti, nafuu na wa haraka wa utatuzi wa migogoro ya kibenki. Taarifa ya utafiti huu itakamilika mwaka wa fedha 2025/2026.

***113. Mheshimiwa Spika,*** Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania imefanya Mapitio ya Sheria ya Makampuni, Sura ya 212 na Sheria ya Majina ya Biashara, Sura ya 213. Lengo la mapitio hayo ni kubaini changamoto zinazoathiri ufanisi wa utekelezaji wa sheria hizo na kutoa mapendekezo yatakayoiwezesha Serikali kuchukua hatua stahiki kwa kuhakikisha kunakuwa na sheria bora zitakazorahisisha mazingira ya kufanya biashara na kuvutia wawekezaji. Taarifa za Mapitio ya Sheria hizi imekamilika.

***114. Mheshimiwa Spika,*** kutokana na kuongezeka kwa wimbi la matumizi ya "Shisha" na athari za kiafya zinazoweza kutokana na matumizi ya bidhaa hiyo hasa kwa upande wa vijana, Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania inafanya Mapitio ya Mfumo wa sheria zinazosimamia Matumizi ya Bidhaa za Tumbaku kwa lengo la kuishauri Serikali kuhusu namna bora ya kudhibiti matumizi ya "Shisha" ili kulinda afya za Watanzania hasa vijana. Andiko la Majadiliano limeshaandaliwa na hatua inayofuata ni ukusanyaji wa maoni ya wadau. Taarifa ya Mapitio ya Mfumo wa Sheria tajwa itakamilika mwaka wa fedha 2025/2026.

***115. Mheshimiwa Spika,*** Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania imefanya Mapitio ya Sheria ya Takwimu, Sura ya 351 kwa lengo la kuweka Mfumo wa kurahisisha upatikanaji wa takwimu kutoka katika mamlaka mbalimbali na kupatikana katika mamlaka moja badala ya njia inayotumika sasa na kurahisisha utekelezaji wa

majukumu ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu na kuongeza ufanisi. Taarifa ya mapitio ya sheria hiyo imekamilika.

***116. Mheshimiwa Spika,*** Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania inafanya Mapitio ya Sheria ya Usuluhishi, Sura ya 15 ili kubaini mapungufu yaliyopo katika sheria na kanuni zake na kupendekeza marekebisho ya sheria hiyo kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utatuzi wa migogoro ya kibiashara na uwekezaji. Ukusanyaji wa maoni ya wadau umekamilika. Taarifa ya Mapitio ya Sheria ya Usuluhishi itakamilika kabla au ifikapo Juni 2025.

***117. Mheshimiwa Spika,*** kutokana na baadhi ya shughuli za mapitio, tathmini na utafiti wa sheria kukamilika mwishoni mwa mwaka wa fedha 2023/24, Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania iliwasilisha taarifa za shughuli hizo mwanzoni mwa mwaka wa fedha 2024/25. Taarifa hizo ni pamoja na Taarifa ya Mapitio ya Sheria zinazosimamia Adhabu ya Viboko, Taarifa ya Tathmini ya Utekelezaji wa Sheria zinazosimamia Usafiri Majini, Taarifa ya Tathmini ya Utekelezaji wa Sheria zinazosimamia Usafiri Ardhini, Taarifa ya Tathmini ya Utekelezaji wa Kifungu 91(3) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai (uondoshaji wa mashauri Mahakamani), na Taarifa ya Utafiti kuhusu Mfumo wa Sheria zinazosimamia Makosa ya Uhujumu Uchumi na Uhalifu wa Kupangwa.

***118. Mheshimiwa Spika,*** sambamba na shughuli za Utafiti wa Sheria, Mapitio ya Sheria, na Tathmini ya Utekelezaji wa Sheria, Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania imeendelea kutoa Elimu ya Sheria kwa Umma kupitia Kampeni ya Kitaifa ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia ambapo Tume ilitoa elimu ya sheria kwa wananchi katika maeneo mbalimbali ya sheria na kutoa vipeperushi vya masuala ya sheria; kushiriki katika Maonesho ya Nane Nane na Tamasha la Utamaduni; na kuandaa makala inayojulikana kama "*The Law Reformer Journal*" iliyozinduliwa jijini Dodoma tarehe 24 Agosti 2024; kushiriki katika Tamasha la Tatu la Utamaduni la Kitaifa lililofanyika katika Uwanja wa Majimaji, Manispaa ya Songea tarehe 20 – 23 Septemba, 2024 na kutoa elimu ya sheria kwa wananchi kupitia maongezi na vipeperushi vya masuala mbalimbali ya sheria.

***119. Mheshimiwa Spika,*** Tume pia iliandaa na kurusha vipindi **12** vya luninga na vipindi **12** vya redio na kutoa elimu kuhusu mada mbalimbali zikiwemo; Haki za Mshtakiwa katika Mfumo wa Jinai, Sheria ya Mapato Yatokanayo na Uhalifu, Taratibu na Faida za Usuluhishi katika Migogoro ya Ardhi, Taratibu za Ufunguaji wa Mashauri ya Mirathi, haki na Ulinzi wa Mtoto Kisheria, Sheria ya Ndoa, Dhamana, Makubaliano ya Kukiri Kosa, Haki na Ustawi wa Wanyama, na Masuala Muhimu ya kuzingatia katika Mikataba, na nafasi ya Utafiti wa Sheria katika Maendeleo ya Kiuchumi na Kijamii. Vipindi hivyo vilirushwa kupitia TUMESHERIA TV, AZAM TV, TBC, na radio za kijamii katika mikoa ya Katavi, Rukwa, Kigoma, Arusha, Manyara na Kilimanjaro.

***120. Mheshimiwa Spika,*** Tume pia iliandaa na kusambaza vipeperushi katika maeneo **10** ya sheria yaliyojielekeza katika masuala ya haki jinai, haki za kiraia na haki za kijamii ambazo ni Utetezi katika Makosa ya Jinai, Makubaliano ya Kukiri Kosa, Masuala Muhimu katika Ukamataji wa Mtuhumiwa, Upekuzi, Masuala ya Kuzingatiwa katika Uchukuwaji wa Maelezo ya Mtuhumiwa, Makosa dhidi ya Maadili, Hatua za Utoaji Ushahidi, Sheria ya Vyama vya Siasa, Sura ya 258, Sheria ya Ustawi wa Wanyama, Sura ya 154 na Sheria ya Madaktari wa Mifugo, Sura ya 316.

### *(xiii) Kuratibu Ufuatiliaji na Tathmini ya Utekelezaji wa Sheria za Utajiri Asili na Maliasilia za Nchi*

***121. Mheshimiwa Spika,*** usimamizi na uangalizi wa utajiri asili na maliasilia za nchi ni suala ambalo linapewa kipaumbele cha kipekee na nchi zote duniani ikiwemo Tanzania. Lengo likiwa ni kuhakikisha kuwa uvunaji na matumizi ya utajiri asili na maliasilia za nchi unakua wenye tija katika kuinua Pato la Taifa na kuleta maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi.

***122. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha kuanzia Julai 2024 hadi Aprili 2025 Wizara imeendelea kutekeleza jukumu lake la kusimamia utekelezaji wa Sheria za Uangalizi wa Utajiri Asili na Maliasilia za Nchi, Sura ya 449 na 450 ambapo jumla ya Mikataba **483** ya uwekezaji katika utajiri asili na maliasilia za nchi iliyoingiwa

kati ya Serikali na wawekezaji ilisajiliwa na kupitiwa kwa lengo la kuhakiki uzingatiwaji wa matakwa ya Sheria, ili kuhakikisha uwekezaji katika utajiri asili na maliasilia za nchi unaleta faida za kiuchumi na maendeleo endelevu ya jamii.

***123. Mheshimiwa Spika,*** katika kufanikisha utekelezaji wa Sheria hizi, Wizara imeandaa Mkakati wa Taifa wa Uangalizi wa Utajiri Asili na Maliasilia za nchi ili kuwezesha utekelezaji wa misingi ya sheria tajwa kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia 2025/2026 – 2029/2030. Lengo la Mkakati huu ni kuweka mfumo wa pamoja katika usimamizi na uangalizi wa rasilimali za nchi ili kuhakikisha kuwa uwekezaji katika utajiri asili na maliasilia za nchi unachangia ipasavyo katika uchumi na ustawi wa wananchi.

***124. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuwajengea uwezo watendaji Serikalini kuhusu usimamizi na uangalizi wa utajiri asili na maliasilia za nchi. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 jumla ya watendaji 52 wamejengewa uwezo wakiwemo Wataalam kutoka kwenye Wizara, Idara, Taasisi na Wakala za Serikali. Lengo likiwa ni kutoa elimu kuhusu usimamizi na uangalizi wa utajiri asili na maliasilia za nchi.

***125. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025, Wizara ilitoa mafunzo kwa viongozi wa Serikali katika ngazi za Mikoa, Wilaya na Halmashauri katika Mkoa wa Mbeya. Mafunzo hayo yalilenga kukuza na kujenga uzalendo na utaifa katika kusimamia utajiri asili na maliasilia za nchi kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia, mafunzo haya yaliwezesha kuongeza uelewa kuhusu fursa zilizopo katika masuala ya utajiri asili na maliasilia za nchi na namna bora ya kuzifikia na kuzitumia fursa hizo ili zilete maendeleo endelevu kwa wananchi. Mafunzo hayo yalihusisha jumla ya viongozi na watendaji **150** wa Serikali.

***(xiv) Kushughulikia Urejeshwaji wa Wahalifu na Masuala ya Ushirikiano wa Kimataifa kwenye Makosa ya Jinai***

***126.* Mheshimiwa Spika,** Tanzania imeendelea kushirikiana na mataifa mengine katika kusimamia urejeshwaji kwa watuhumiwa wa uhalifu katika nchi walikofanya makosa. Katika kipindi cha

Julai 2024 hadi Aprili, 2025 Wizara imekamilisha mikataba ya urejeshwaji wa wahalifu watoro kutoka nchi tatu (**3**) za Ethiopia, Iran na Kenya. Majadiliano ya mikataba ya kubadilishana wahalifu na nchi nyingine nne (**4**), za Shirikisho la Urusi, Qatar, Umoja wa Falme za Kiarabu na Burundi yanaendelea. Aidha, maombi tisa (**9**) kutoka nchi tisa (**9**) tofauti yamepokelewa ambapo kati ya maombi hayo maombi mawili (**2**) yameshughulikiwa na wahalifu watoro wamerejeshwa katika nchi zao maombi saba (**7**) hayakukidhi vigezo hivyo yamerudishwa kwa ajili ya marekebisho. Vilevile, Tanzania imetuma maombi matatu (**3**) ya kurejeshwa wahalifu watoro katika nchi tatu.

***127. Mheshimiwa Spika***, Tanzania imeendelea kushirikiana na mataifa mengine katika masuala ya kimataifa kwenye makosa ya jinai kwa lengo la kupata au kutoa ushahidi kuhusiana na watuhumiwa waliopo nje ya nchi au waliopo nchini. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili, 2025, Wizara kupitia Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ilipokea maombi ya kupatiwa ushahidi wa watuhumiwa waliofanya makosa ya jinai katika nchi tano (**5**) za Thailand, India, Shelisheli, Zambia na Uganda. Maombi yaliyopokelewa kutoka Thailand na Zambia yalifanyiwa kazi na ushahidi ulioombwa ulitumwa huku maombi ya India yakikataliwa kwa kukosa vigezo na maombi kutoka Uganda na Shelisheli yanaendelea kushughulikiwa. Ofisi ya Taifa ya Mashtaka (OTM) pia, imetuma ombi moja (**1**) katika Jamhuri ya Zambia ambalo bado halijajibiwa.

***128. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imeendelea kuimarisha ushirikiano ya Kikanda na Kimataifa katika kuzuia uhalifu wa kupangwa na unaovuka mipaka. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 Ofisi ilishiriki vikao vitano (**5**) vilivyohusu makosa yanayovuka mipaka na uhalifu wa kupangwa. Vikao hivi vimewezesha nchi wanachama kubadilishana uzoefu katika kukabiliana na makosa ya kupangwa na kushughulikia masuala ya jinai.

***129. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ilishiriki Kongamano la Jukwaa la Ukanda wa Bahari ya Hindi nchini *Mauritius* kuanzia tarehe 20 – 24 Januari, 2025 kujadili

namna ya kukabiliana na makosa ya dawa za kulevya pamoja na uvuvi haramu. Vilevile, Wizara kupitia OTM ilishiriki kikao kazi cha kuandaa Mwongozo wa Wapelelezi na Waendesha Mashtaka Jijini Nairobi, Kenya tarehe 22 – 27 Septemba, 2024 kilichohusu makosa yanayovuka mipaka na uhalifu wa kupangwa.

***130. Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha ushirikiano wa masuala ya kisheria katika ngazi za kikanda na kimataifa, Wizara kupitia Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ili shiriki katika kongamano linalohusu namna nchi wanachama zinavyokabiliana na matukio ya ugaidi ikiwemo kudhibiti ufadhili wa ugaidi na makosa yanayoambatana nayo. Kongamano hilo lilifanyika tarehe 24 – 26 Septemba, 2024 Jijini Pretoria, Afrika Kusini.

***131. Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha ushirikiano wa masuala ya kisheria katika ngazi za kikanda na kimataifa, Wizara kupitia Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ilishiriki katika mkutano wa Umoja wa Mataifa kuhusu majadiliano ya Mkataba wa Kimataifa dhidi ya Uhalifu wa Mtandao (*Reconvened concluding Session of International Convention on countering the use of ICTS for criminal purposes*) uliofanyika New York, Marekani kuanzia tarehe 29 Julai – 09 Agosti, 2024. Moja wapo ya maazimio ya mkutano huo ni kuandaa rasimu ya Mkataba wa Kimataifa wa kushughulikia Makosa ya kimtandao ambao utatumiwa na nchi wanachama kuomba ushahidi wa Kimtandao nje ya nchi.

***132. Mheshimiwa Spika***, ziara na mikutano mingine ambayo Wizara kupitia Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ilishiriki ni pamoja na ziara ya Kamati ya Usalama ya Umoja wa Mataifa (*UN Security Council Counter-Terrorism Committee - CTED*) iliyofanyika nchini tarehe 19-23 Agosti, 2024; Mkutano wa Umoja wa Nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika wa Kudhibiti Fedha Haramu (*Eastern and Southern Africa Anti-Money Laundering Group-ESAAMLG*) uliofanyika Diani, Kenya tarehe 23 – 31 Agosti, 2024; na Kongamano linalohusiana na upatikanaji haki sawa kwa wote nchini Brazil tarehe 9 – 12 Disemba, 2024.

***(xv) Kuimarisha Matumizi ya TEHAMA katika Utoaji Haki na Huduma za Kisheria***

***133. Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha azma ya Serikali ya kuboresha mifumo ya TEHAMA katika utoaji huduma za kisheria, Wizara imeunganisha mifumo ya TEHAMA inayotoa huduma za kisheria. Hadi kufikia Aprili, 2025; asilimia **75** ya mifumo ya TEHAMA katika Sekta ya Sheria imeunganishwa ambapo, Wizara imeunganisha mfumo wake na Mifumo ya Mahakama ya Tanzania; Ofisi ya Taifa ya Mashtaka; Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali; na Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini. Aidha, kazi ya kuunganisha mifumo ya TEHAMA katika Sekta ya Sheria inaendelea ili kuwezesha mifumo hiyo kusomana na mifumo ya NIDA; TAKUKURU; Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum; na Jeshi la Polisi Tanzania. Pia, Wizara imeimarisha matumizi ya mfumo wa *Portal* ya HAKI SHERIA ambao unatumiwa na Wananchi na maafisa Dawati la Msaada wa Kisheria katika Mamlaka za Serikali za Mitaa **184** nchini.

***134. Mheshimiwa Spika,*** tarehe 5 Septemba, 2024 Wizara ilizindua Kituo cha Huduma kwa Mteja ambapo Mwananchi hupata fursa ya kuwasilisha malalamiko na hoja mbalimbali za kisheria moja kwa moja kupitia namba ya simu **0262160360,** namba ya *Whatsapp* **0739101910 na** barua pepe kupitia malalamiko@sheria.go.tz. Aidha, tangu kuzinduliwa kwake, Kituo kimepokea jumla ya malalamiko **1,154**, kati ya hayo **775** yameshughulikiwa na **379** yapo katika hatua mbalimbali za kushughulikiwa.

***135. Mheshimiwa Spika***, Pamoja na kupokea malalamiko kupitia kituo cha huduma kwa mteja, Wizara pia imeendelea kupokea na kushughulikia malalamiko ya kisheria yaliyowasilishwa na wananchi kwa njia ya barua. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025, jumla ya malalamiko **278** yalipokelewa na kufanyiwa uchambuzi. Kati ya malalamiko hayo 126 yaliwasilishwa katika taasisi mbalimbali za Serikali; na **152** yaliwasilishwa kwenye Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS) na Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania (TAWLA) ambapo yanaendelea kufanyiwa kazi.

***136. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025 maboresho ya mifumo ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za Mahakama yameendelea kwa lengo la kuimarisha upatikanaji haki kwa wananchi. Hadi kufikia Aprili, 2025 mifumo ifuatayo ya TEHAMA imeendelea kutumika katika utekelezaji wa majukumu ya Mahakama: Mfumo wa usikilizaji mashauri (JOT eCMS); Mfumo wa Kunukuu na Kutafsiri Mwenendo wa Mashauri (TTS); Mfumo wa Takwimu (*Data Hub*); Mfumo wa Taarifa za Hukumu na Sheria Tanzania (TAnzLII); na Mahakama Mtandao (*Virtual Court*).

*137.* **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Tume ya Utumishi wa Mahakama inakamilisha ujenzi wa Mfumo wa TEHAMA wa Ajira, Maadili na Nidhamu kwa Watumishi wa Mahakama. Mfumo huo unahusisha moduli kuu tatu (**3**) ambazo zinajengwa kwa awamu: *Recruitment Module* kwa ajili ya ajira ambao umekamilika kwa asilimia **60**, *Ethics and Discipline Module* kwa ajili ya usimamizi wa maadili na nidhamu ambao umekamilika kwa asilimia **80** na *Human Resources Information Management Module* ambao utahusisha uthibitisho wa ajira, kupandishwa vyeo, mabadiliko ya kada na uteuzi. Aidha, ujenzi wa moduli hii utaanza baada ya moduli mbili (**2**) za awali kukamilika.

***138. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini - RITA imeendelea kusogeza na kuimarisha utoaji wa huduma kwa wananchi kupitia TEHAMA. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 huduma za usajili wa Vizazi, Vifo, Ndoa, Talaka na Bodi za Wadhamini zimewezeshwa kupatikana kidijitali kupitia *eRITA* ambapo mwananchi anaweza kutuma maombi popote alipo bila kufika ofisi za Wakala na kuchagua Ofisi ya Mkuu wa Wilaya iliyo karibu kwa ajili ya kuchukua nyaraka za huduma aliyoomba. Aidha, katika kipindi husika Wakala unaendelea kuboresha mfumo wa huduma za Wakala ili kuhakikisha huduma zote za Wakala zinapatikana kidigitali.

***139. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025, Wizara kupitia RITA imeongeza idadi ya Taasisi za Serikali ambazo zimeunganishwa na kuwezesha kubadilishana taarifa ya mifumo yake na kufikia taasisi **29** ili kurahisisha utoaji wa huduma kwa Wananchi. Mifumo ambayo RITA imeunganishwa nayo ni pamoja

na GoTHOMIS wa Ofisi ya Rais -TAMISEMI unaowezesha kubadilishana taarifa za vizazi; eHMS wa Wizara ya Afya unaowezesha kubadilishana taarifa za vizazi na vifo na PREM na PREMS wa NECTA ambao unawezesha usajili wa watoto ambao hawana vyeti waliopo shuleni.

***140. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali iliendelea na maboresho ya Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Mashauri (*CIMS*) ili kukusanya, kuhifadhi na kutoa taarifa za mienendo ya mashauri kwa wakati. Aidha, maboresho yanaendelea ili kuhakikisha Mfumo huo unasomana na Mifumo ya Mahakama.

***141. Mheshimiwa Spika,*** Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania inaendelea na ujenzi wa Mfumo wa Kielekroniki wa Utendaji Kazi (*LRMIS*) ambapo mfumo huu unatarajiwa kukamilika kabla au ifikapo Juni, 2025. Manufaa yanayotarajiwa baada ya kukamilika kwa mfumo huo ni ukusanyaji wa taarifa za kisheria, kutunza kumbukumbu za kisheria na kurahisisha utatuzi wa haraka wa changamoto, kuwezesha watumishi kufanya kazi popote walipo, kuunganishwa na mifumo mingine kama OAGMIS na kupunguza matumizi ya karatasi. Pia, Tume inaendelea na usanifu wa mfumo wa Maktaba Mtandao ili kuifanya maktaba ya Tume kuwa ya kidigitali na kwenda sambamba na maendeleo ya kiteknolojia ikiwa ni pamoja na kurahisisha matumizi ya maktaba hiyo.

***142.* Mheshimiwa Spika*,*** katika kuongeza ufanisi wa utoaji wa huduma za ushauri wa kisheria pamoja na kubadilishana taarifa mbalimbali ikiwemo mwenendo wa uendeshaji wa mashauri nchini, Wizara kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeunganisha Mfumo wake wa TEHAMA wa OAGMIS na Mifumo ya Taasisi nyingine. Hadi kufikia Aprili, 2025, Mfumo wa OAGMIS umeunganishwa na Mfumo wa Usimamizi na Uendeshaji Mashauri wa Mahakama ya Tanzania (*e-Case Management System*) na Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Mashauri wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

***143. Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali pia imeendelea kufanya maboresho katika mfumo wa OAGMIS

kwa kuanzisha Moduli ya Upekuzi wa Mikataba (*e-Vetting*). Aidha, mafunzo juu ya matumizi ya moduli hiyo yanaendelea kutolewa kwa Watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na wadau. Moduli hiyo inatarajiwa kuanza kutumika mwaka wa fedha 2025/2026.

***(xvi) Kuimarisha Mfumo wa Elimu ya Sheria***

**a. Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania**

***144. Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania (*The Law School of Tanzania – LST*) iliendesha mafunzo ya uanasheria kwa vitendo kwa wanafunzi **451** wa kundi la 37, wanafunzi **791** kwa kundi la 38, wanafunzi **458** wa kundi la 39 na wanafunzi **782** wa kundi la 40. Wanafunzi wa kundi la 37 wamemaliza masomo yao na kupata matokeo, wanafunzi wa kundi la 38 wamemaliza masomo yao na wanasubiri matokeo ya mwisho, wanafunzi wa kundi la 39 wamemaliza masomo ya darasani na wapo kwenye mafunzo uwandani na wanafunzi wa kundi la **40** wapo kwenye mafunzo ya darasani.

***145. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania iliendelea kusimamia na kutekeleza falsafa ya kujifunza kwa vitendo (*Learning by doing*) ambapo mbinu mbalimbali za ufundishaji na ujifunzaji zilitumika ikiwa ni pamoja na: Visa (*Case studies*), mazoezi ya vitendo kupitia semina, mahakama za kimaigizo (*moot courts*), kupangiwa majukumu na kuigiza (*role plays and simulations*), kazi za vikundi, uwasilishaji (*presentations*), filamu, na mafunzo uwandani (*Field Placement*). Mbinu hizi ni muhimu kwa maendeleo ya wanafunzi ili kuwajenga na kuwaandaa vyema katika mazingira yote ya utendaji wao pindi wanapohitimu mafunzo. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania ilisajili jumla ya wanafunzi **1,240** sawa na asilimia **82.7** ya lengo la usajili wa wanafunzi **1,500** kwa kundi la 39 na 40. Aidha, katika kipindi husika, Taasisi imetoa wahitimu **282** waliofanya mitihani katika kundi la **37**. Pamoja na hao watahiniwa 1,938 walifaulu

baadhi ya vipengele vya masomo na hivyo kuruhusiwa kufanya mitihani ya marudio ili kukamilisha vipengele hivyo.

**b. Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto**

***146. Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto (IJA) imeendelea kutoa elimu ya Sheria katika ngazi ya Astashahada na Stashahada ya Sheria kwa lengo la kuandaa wataalamu wenye weledi na maadili katika masuala ya sheria na utawala wa haki. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 Chuo kimesajili jumla ya wanafunzi **780** sawa na asilimia **82.1** ya lengo la udahili wa wanafunzi **950.** Aidha, katika kipindi hicho jumla ya wanafunzi **766** walihitimu mafunzo ya ngazi ya Astahashada na Stashahada ya Sheria ukilinganisha na wahitimu **608** waliohitimu katika mwaka 2023/2024 ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia **26.**

***147. Mheshimiwa Spika**,* Wizara kupitia Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto imeendelea kuimarisha upatikanaji wa haki nchini kwa kuwajengea uwezo Waheshimiwa Majaji, Wasajili wa Mahakama, Mahakimu, maafisa wa Mahakama na watumishi wengine wa Sekta ya Sheria. Lengo la mafunzo hayo ni kuongeza ufanisi na weledi katika utekelezaji wa majukumu yao. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili, 2025, Chuo kiliendesha na kuratibu mafunzo ya aina **28** kwa washiriki **1,723**. Mafunzo hayo yaligawanyika katika makundi mawili (**2**)**;** mafunzo ya ana kwa ana na mafunzo ya masafa ambapo mafunzo ya ana kwa ana ni **16** yaliyokuwa na washiriki **454** (**Kiambatisho Na.11a**) na mafunzo kwa njia ya masafa ni **12** yaliyokuwa na washiriki **1,269** (**Kiambatisho Na.11b**).

***(xvii) Kuboresha Utendaji na Maendeleo ya Rasilimaliwatu wa Wizara na Taasisi Zake Ikiwemo Ajira, Uteuzi, Nidhamu na Maadili***

**(a) Wizara ya Katiba na Sheria**

***148. Mheshimiwa Spika*,** Wizara imeendelea kuratibu na kushughulikia upatikanaji wa watumishi kulingana na mahitaji,

ambapo katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 watumishi **451** wameajiriwa na watumishi **29** wamehamia kutoka Taasisi mbalimbali. Hivyo, kufikia mwezi Aprili, 2025 Wizara ina jumla ya watumishi **616.** Aidha, jumla ya nafasi **11** za uongozi kulingana na muundo wa Wizara ambazo zilikuwa wazi zimejazwa kwa nafasi za Wakurugenzi sita (**6**) na Wakurugenzi Wasaidizi watano (**5**). Aidha, watumishi **13** walithibitishwa vyeo, **53** walipandishwa vyeo na mmoja (**1**) alibadilishwa kada.

***149. Mheshimiwa spika,*** katika kuboresha na kuongeza ufanisi na weledi katika utendaji kazi jumla ya watumishi nane **(8)** wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu, **42** wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi, **35** wamepatiwa mafunzo ya ndani (*Inhouse training*) kuhusu usalama mahali pa kazi yaliyotolewa na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, watumishi wapya **449** walipatiwa mafunzo elekezi, watumishi **80** walipatiwa mafunzo kuhusu Miongozo ya uandishi na matumizi ya nyaraka za Serikali na watumishi **100** wamepatiwa mafunzo ya Usalama na matumizi sahihi ya Mifumo ya TEHAMA. Aidha, Wizara imeendelea kuwapatia watumishi wake mafunzo ya Mfumo wa Kielektroniki wa Ununuzi wa Umma (NeST).

**(b) Mahakama ya Tanzania**

***150. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 Mahakama imeajiri watumishi **522**, kuwapandisha madaraja **1,867** na kuwabadilisha kada **109.** Hadi kufikia Aprili, 2025, Mahakama ilikuwa na watumishi **6,067**. Aidha, Mahakama imewezesha watumishi **173** kushiriki mafunzo ya muda mrefu na **443** kushiriki mafunzo ya muda mfupi.

**(c) Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali**

***150. Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeajiri watumishi watano **(5)** wa kada mbalimbali. Watumishi **44** walipandishwa vyeo, watumishi wawili **(2)** walibadilishiwa kada na watumishi tisa **(9)** walithibitishwa kazini. Hadi Aprili 2025, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilikuwa na jumla ya watumishi **214**. Aidha,

watumishi **13** wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu na **14** walipatiwa mafunzo ya muda mfupi.

**(d) Ofisi ya Taifa ya Mashtaka**

***152. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha kuanzia Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imeendelea kutekeleza masuala mbalimbali kwa ajili ya maendeleo ya rasilimaliwatu. Hadi kufikia Aprili, 2025 Ofisi ilikuwa na jumla ya watumishi **1,070** kati ya hao, Mawakili wa Serikali ni **774***,* Makatibu Sheria ni **144** na kada nyingine ni **192.** Kati ya watumishi hao, watumishi ***145*** ni ajira mpya ambao wameajiriwa katika kipindi hiki (Mawakili wa Serikali ***100****,* Makatibu Sheria ***20*** na Madereva ***25).*** Aidha, Ofisi imethibitisha kazini watumishi ***36,*** na kuratibu mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi kwa watumishi. Vilevile, watumishi ***126*** walishiriki mafunzo ya muda mrefu na watumishi ***268*** mafunzo ya muda mfupi.

**(e) Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali**

***153. Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ina jumla watumishi **255**. Kati ya watumishi waliopo Mawakili wa Serikali wapo **117**, Makatibu Sheria wapo **19** na watumishi wa kada nyingine wapo **119**. Kati ya watumishi hao, watumishi **19** ni ajira mpya ambao wameajiriwa katika kipindi hiki. Vilevile, watumishi **32** walihudhuria mafunzo ya muda mrefu na watumishi **231** walihudhuria mafunzo ya muda mfupi. Pia watumishi **176** waliwezeshwa kushiriki katika mikutano mbalimbali ya kitaaluma.

**(f) Tume ya Utumishi wa Mahakama**

***154. Mheshimiwa Spika*****,** katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 Sekretarieti ya Tume ya Utumishi wa Mahakama, ilikuwa na watumishi **32** kati ya watumishi **54** wanaohitajika kwa mujibu wa ikama. Aidha, mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi watatu **(3)** na watumishi 11 mafunzo ya muda mfupi yametolewa.

### (g) Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora

***155. Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ina jumla watumishi, **174** wa kada mbalimbali na Makamishna sita (**6**). na**.** Kati ya watumishi hao, watumishi **23** ni ajira mpya, watumishi watano (**5**) wamehamia kutoka taasisi nyingine na watumishi **12** wameazimwa kutoka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) ambao wamepangiwa kufanya kazi katika ofisi za THBUB zilizopo Zanzibar na Pemba. Vilevile, watumishi wawili (**2**) walihudhuria mafunzo ya muda mrefu na watumishi sita (**6**) walihudhuria mafunzo ya muda mfupi, saba (**7**) walipata mafunzo ya kustaafu na watumishi **41** wamethibitishwa vyeo.

### (h) Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania

***156. Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia Aprili 2025, Tume ilikuwa na jumla ya Watumishi 54 wa fani mbalimbali. Katika kipindi husika Watumishi wanne (**4**) walihamia, Mtumishi mmoja (**1**) aliajiriwa, nafasi sita (**6**) za uongozi zilijazwa na mtumishi mmoja (**1**) alistaafu. Aidha, katika kipindi husika, Watumishi **40** walipatiwa mafunzo katika maeneo mbalimbali kwa lengo la kuwajengea uwezo katika maeneo yao ya kitaaluma. Aidha, Watumishi nane (**8**) wanaendelea na mafunzo katika ngazi ya Shahada ya kwanza na Shahada ya Uzamili.

### (i) Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini

***157. Mheshimiwa Spika*****,** Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini - RITA una jumla ya watumishi **208**. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 Wizara kupitia Wakala imeajiri watumishi wapya wanne (**4**), imepandisha vyeo watumishi **76 na** imewathibitishakwenye vyeo watumishi **50.** Aidha, watumishi **141** walipatiwa mafunzo ikiwemo **126** mafunzo ya muda mfupi na **15** mafunzo ya muda mrefu.

### (j) Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania

***158. Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha kuanzia Julai 2024 hadi Aprili, 2025 Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania iliajiri watumishi wapya watano (**5**), watumishi wawili (**2**) walithibitishwa kazini, watumishi **13** walipandishwa vyeo na mtumishi mmoja (**1**) aliteuliwa katika nafasi ya uongozi. Hivyo, hadi kufikia Aprili, 2025 Taasisi ilikuwa na watumishi **66**. Aidha, watumishi wanne **(4)** wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu na **38** walipatiwa mafunzo ya muda mfupi.

### (k) Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto

***159. Mheshimiwa Spika*****,** hadi kufikia Aprili, 2025 Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto kilikuwa na jumla ya watumishi **110**. Katika kipindi hicho, Chuo kimeajiri watumishi wanne (**4**), kuthibitisha kazini watumishi **10** na kuthibitishwa kwenye vyeo watumishi wawili (**2**). Vilevile, katika kipindi husika, mtumishi mmoja (**1**) alihamia, watatu (**3**) walihama, na mmoja (**1**) alistaafu. Aidha, watumishi **32** walipatiwa mafunzo ya muda mfupi na **14** mafunzo ya muda mrefu.

## G. FURSA NA MIKAKATI YA KUTUMIA FURSA

### Fursa Zilizopo

***160. Mheshimiwa Spika*****,** pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika mwaka wa fedha 2024/25 hadi kufikia Aprili, 2025 fursa kadhaa zimebainika ikiwemo:-

(i) Kuendelea kuongeza kasi ya kufungamanisha mifumo ya TEHAMA ya Taasisi za utoaji haki ili kuboresha upatikanaji haki kwa wakati kwa Wananchi;

(ii) Ongezeko kubwa la Wananchi wanaohitaji huduma ya msaada wa kisheria ikilinganishwa na rasilimali zilizopo kutokana na wigo wa elimu ya msaada wa kisheria kuongezeka;

(iii) Kuendelea kuongeza rasilimaliwatu ili majukumu ya Wizara yatekelezwe ipasavyo;

(iv) Kuendelea kuwajengea uwezo Watumishi ili kukabiliana na upungufu wa Mawakili wa Serikali wenye ubobezi katika maeneo ya uchambuzi wa mikataba ya uwekezaji katika utajiri asili na maliasilia; uendeshaji wa mashauri ya kimataifa, uchambuzi wa mikataba ya mafuta na gesi, na uendeshaji wa mashauri yanayohusu uhalifu wa kimtandao;

(v) Kuendelea kuboresha mfumo wa kisheria na kitaasisi ili kuwezesha utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala;

(vi) Kuongeza uelewa wa umma kuhusu Sheria za Nchi ili wazitii bila shuruti na hivyo kupunguza matukio ya uhalifu na uvunjaji wa haki za binadamu;

(vii) Kuongeza uelewa kwa wajumbe wa Kamati za Maadili ya Maafisa Mahakama ngazi ya Mikoa na Wilaya hususan wapya wanaobadilika mara kwa mara ili watekeleze majukumu yao kwa weledi;

(viii) Hitaji la kuendelea kuboresha mfumo wa kisheria ili kuimarisha usimamizi wa mikataba ya uwekezaji;

(ix) Hitaji la kuendelea kufikisha huduma za kimashtaka kwa wananchi;

(x) Hitaji la kuboresha uratibu wa masuala ya mirathi na bodi za wadhamini; na

(xi) Uwezekano wa kufanya mabadiliko ya Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania ili kuwezesha kuwa na sheria zenye tija nchini.

**Mikakati ya Kutumia Fursa**

***161. Mheshimiwa Spika,*** ili kutumia fursa tajwa, Wizara imebuni mikakati mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

(i) Kushirikiana na Wakala wa Serikali Mtandao (eGA) kuboresha, kutengeneza na kufungamanisha mifumo ya TEHAMA katika Sekta ya Sheria;

(ii) Kuimarisha Madawati ya Msaada wa Kisheria yaliyoanzishwa katika Mamlaka zote 184 za Serikali za Mitaa Pamoja na kuimarisha Kituo cha Huduma kwa Mteja na kuongeza wigo wa utekelezaji wa Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia ili wananchi wengi wafikiwe na huduma ya msaada wa kisheria;

(iii) Kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ili kupata vibali vya ajira mpya pamoja na uhamisho wa Watumishi kuja Wizara ya Katiba na Sheria;

(iv) Kuwezesha Watumishi kushiriki katika mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu kwenye maeneo yenye uhitaji ikiwemo uchambuzi wa mikataba ya Uwekezaji katika utajiri asili na maliasilia za Nchi na utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala;

(v) Kuanzisha Kituo cha Usuluhishi Tanzania pamoja na kufanya mapitio ya mfumo wa sheria zinazohusu masuala ya utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala;

(vi) Kuanzisha na kutekeleza programu na vipindi mbalimbali kwa ajili ya kutoa elimu ya masuala ya kisheria kwa umma ikiwa ni pamoja na kutafsiri nyaraka za kisheria na Sheria za Nchi katika lugha ya Kiswahili ili kuongeza wigo wa uelewa kwa Wananchi;

(vii) Kuhamasisha wakuu wa Mikoa na Wilaya kutoa elimu kwenye mikutano ya hadhara ya wananchi kuhusu uwepo wa Kamati za Maadili na majukumu yake;

(viii) Kuendelea kuwajengea uwezo wajumbe wa bodi za wadhamini ili wasimamie bodi kwa mujibu wa Katiba na sheria na kuwa na vikao vya usuluhishi wa wanufaika wa mirathi ili kuhakikisha migogoro inahitimishwa kwa wakati; na

(ix) Kufanya marekebisho ya Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Sura ya 171 ili kuwezesha sheria zinazotungwa au kufanyiwa marekebisho kufanyiwa utafiti wa kina ili ziweze kukidhi mahitaji ya Taifa kwa wakati husika na kwa maendeleo endelevu.

**H. SHUKRANI**

***162. Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kutumia fursa hii kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama (Mb.), Mwenyekiti wa Kamati na Mhe. Florent Laurent Kyombo (Mb.), Makamu Mwenyekiti na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti chini ya uongozi wa Mheshimiwa Oran Manase Njeza (Mb) mwenyekiti wa kamati, na Mheshimiwa Twaha Ally Mpembenue (Mb) Makamu mwenyekiti kwa maelekezo na ushauri wao ambao umeleta mchango mkubwa katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Nitoe shukrani zangu pia, kwa wajumbe wa Kamati kwa uchambuzi wa kina wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na kwa kupitisha kwa kauli moja Makadirio ya Mpango na Bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026. Ninapenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa ushauri, maelekezo na maoni yote yaliyotolewa na Kamati yamezingatiwa kikamilifu katika maandalizi ya bajeti hii. Nawashukuru sana kwa uongozi wao na ushirikiano wanaotupatia.

***163. Mheshimiwa Spika,*** vilevile, naomba kuwashukuru sana Wananchi wa Jimbo la Songea Mjini, Viongozi na Wanachama wa Chama Cha Mapinduzi katika Mkoa wa Ruvuma, kwa

ushirikiano wanaoendelea kunipa katika kuwawakilisha na kuwatumikia katika Bunge hili pamoja na kuratibu utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo katika Mkoa huo.

***164. Mheshimiwa Spika,*** naomba kutumia fursa hii kuwashukuru wale wote waliochangia kwa namna moja au nyingine katika kuiwezesha Wizara kufanikisha majukumu yake. Mafanikio yaliyopatikana katika mwaka 2024/2025 yametokana na ushirikiano na misaada ya kifedha na kiufundi kutoka kwa nchi wahisani ikiwemo Ujerumani kupitia GIZ, mashirika mbalimbali ya kitaifa na kimataifa, Taasisi za fedha za Kitaifa na Kimataifa ikiwemo Benki ya Dunia, Asasi za Kiraia (AZAKI), Taasisi za hiari zisizokuwa za kiserikali na mashirika ya kidini bila kusahau ushiriki wa Wananchi katika kutii na kuheshimu Katiba na Sheria za nchi wakiongozwa na Waheshimiwa Wabunge.

***165. Mheshimiwa Spika,*** pia, ninaomba nitumie fursa hii kuwashukuru Viongozi wenzangu wa Wizara ya Katiba na Sheria akiwemo Mhe. Jumanne Abdallah Sagini (Mb.), Naibu Waziri wa Katiba na Sheria; Bw.Eliakim Chacha Maswi, Katibu Mkuu; na Dkt. Franklin Jasson Rwezimula, Naibu Katibu Mkuu kwa ushirikiano wanaonipatia katika utekelezaji wa shughuli za Wizara.

***166. Mheshimiwa Spika,*** vilevile, natoa shukrani za dhati kwa Mhe. Prof. Ibrahimu Hamisi Juma, Jaji Mkuu wa Tanzania na Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Mahakama; Mhe. Hamza Saidi Johari, Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Mhe. Dkt. Mustapher Mohamed Siyani, Jaji Kiongozi wa Mahakama Kuu ya Tanzania; Prof. Elisante Ole Gabriel, Mtendaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Mahakama; na Mhe. Eva Kiaki Nkya, Msajili Mkuu wa Mahakama ya Tanzania.

***167. Mheshimiwa Spika,*** sambamba na hao, ninapenda pia kuwashukuru Wakuu na Watendaji Wakuu wa Taasisi za Wizara wakiwemo Mhe. Prof. Paul Faustine Kihwelo, Jaji wa Mahakama ya Rufani na Mkuu wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto; Bw. Samwel Marco Maneno, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Bw. Sylvester Anthony Mwakitalu, Mkurugenzi wa Mashtaka; Dkt. Ally Saleh Possi, Wakili Mkuu wa Serikali; Bw.

Onorius John Njole, Mwandishi Mkuu wa Sheria; Bw. Frank Kanyusi Frank, Kabidhi Wasii Mkuu na Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini; Prof. Sist Joseph Mramba, Mkuu wa Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania; Bi. Bibiana J. Kileo, Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka; Bi. Alice E. Mtulo, Naibu Wakili Mkuu wa Serikali; Bi. Irene Lesulie, Naibu Kabidhi Wasii Mkuu wa Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini; Mhe. Winifrida B. Korosso, Jaji wa Mahakama ya Rufani na Mwenyekiti wa Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania; Bw. George Nathaniel Mandepo, Katibu Mtendaji wa Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania; Mhe. Mathew P. Mwaimu, Jaji Mstaafu wa Mahakama Kuu na Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; Bw. Mohamed Khamis Hamad, Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; na Bw. Patience Kilanga Ntwina, Katibu Mtendaji wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.

***168. Mheshimiwa Spika,*** mwisho ila siyo kwa umuhimu, ninaomba kuwashukuru Wakuu wa Idara na Vitengo na Watumishi wote wa Wizara na Taasisi zake. Pia, ninaomba nichukue fursa hii kuwashukuru wadau wote wa Wizara kwa ushirikiano wanaotupatia katika utekelezaji wa majukumu ambayo Wizara imekasimiwa na Serikali. Aidha, kwa namna ya pekee, ninaishukuru familia yangu hususan Mke wangu kipenzi Bi. Flora Ndumbaro na watoto wangu kwa ushirikiano wanaoendelea kunipatia kwa kunivumilia na kunitia moyo wakati ninapokuwa natekeleza majukumu yangu ya kulitumikia Taifa.

## I. MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

### *(a) Vipaumbele vya Wizara*

***169. Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Wizara, Taasisi zake na Mhimili wa Mahakama itaendelea kuboresha utoaji wa huduma za kisheria na utoaji haki kwa umma ili kuendana na Mipango ya Sekta ya Sheria nchini; na Mipango ya Kikanda na Kimataifa ili kufikia malengo yaliyopangwa kwa kipindi husika. Katika kufikia azma hiyo maeneo mahsusi ya kipaumbele yameainishwa ambayo ni:-

(i) Kuimarisha huduma za msaada wa kisheria kwa watu wenye uhitaji;

(ii) Kushughulikia masuala ya kikatiba pamoja na kutoa elimu ya Katiba na Uraia kwa umma;

(iii) Kutekeleza mapendekezo ya Tume ya Kuangalia Jinsi ya Kuboresha Taasisi za Haki Jinai Nchini;

(iv) Kubainisha na kutatua migogoro ya kisheria kwa wananchi na wadau wengine;

(v) Kuimarisha mifumo ya utoaji haki ili haki ipatikane kwa wote na kwa wakati;

(vi) Kuboresha mfumo wa kitaifa na kuzingatia mifumo ya kikanda na kimataifa kuhusu haki za binadamu na utawala bora;

(vii) Kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa katika masuala ya haki jinai na haki madai;

(viii) Kuwezesha matumizi ya lugha ya Kiswahili katika Sekta ya Sheria nchini;

(ix) Kuimarisha mifumo kisheria na kitaasisi katika Utatuzi wa Migogoro kwa Njia Mbadala;

(x) Kuimarisha usimamizi wa mikataba ya utajiri asili na maliasilia za nchi ambazo Wizara, Idara na Taasisi za Serikali zimeingia na wawekezaji;

(xi) Kuimarisha usimamizi, ufuatiliaji na majadiliano ya mikataba;

(xii) Kuimarisha mfumo wa uandishi, ufasiri na urekebu wa sheria

(xiii) Kuongeza uelewa kwa Watendaji wa Serikali na Wananchi kuhusu Sheria za Nchi;

(xiv) Kuimarisha utafiti, tathmini na mapitio ya sheria;

(xv) Kuendesha mashtaka ya jinai na kuimarisha shughuli za utenganishaji wa mashtaka na upelelezi;

(xvi) Kuimarisha uratibu, usimamizi na uwakilishi katika kuendesha mashauri ya madai na usuluhishi;

(xvii) Ujenzi na ukarabati wa miundombinu katika sekta ya sheria;

(xviii) Kusimamia na kuendeleza elimu na taaluma ya Sheria nchini;

(xix) Kuwezesha usajili wa matukio muhimu ya binadamu na kusimamia masuala ya ufilisi na udhamini;

(xx) Kuwezesha ajira, uteuzi, kuimarisha nidhamu na maadili ya watumishi wa Mahakama.

(xxi) Kuimarisha mifumo ya TEHAMA kwa ajili ya kuboresha huduma za kisheria nchini; na

(xxii) Kuendeleza rasilimali watu katika Sekta ya Sheria.

***(b) Kazi Zitakazotekelezwa katika Mwaka wa Fedha 2025/2026***

***170. Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa, baadhi ya kazi zitakazotekelezwa na Wizara ya Katiba na Sheria (Fungu 41) katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 ni pamoja na:-

(i) Kuandaa Sera ya Taifa ya Msaada wa Kisheria;

(ii) Kutoa huduma za msaada wa kisheria ikiwemo kutekeleza Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia;

(iii) Kutoa elimu kwa umma kuhusu Sera ya Taifa ya Haki Jinai;

(iv) Kutoa Elimu ya Uraia kwa umma na utawala bora kwa Viongozi na watendaji kwa Halmashauri 100 kwa kuzingatia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yam waka 1977;

(v) Kuimarisha mfumo wa usimamizi, uratibu na kuwajengea uwezo wataalam wa Utatuzi wa Migogoro kwa Njia Mbadala;

(vi) Kuratibu na kuwezesha Mapitio ya Sheria zinazohusu Haki jinai;

(vii) Kuwezesha uandaaji wa miongozo ya ufuatiliaji wa masuala ya haki za binadamu na uandishi wa taarifa za Haki za Binadamu;

(viii) Kuratibu na kushiriki mikutano ya Kikanda na ya Kimataifa;

(ix) Kujenga uwezo kwa wananchi kuhusu uelewa wa Sheria za Utajiri na Maliasilia za Nchini Sura 449 na 450;

(x) Kuangalia Sheria zinazodhibiti masuala ya Utajiri Asili na Maliasili kama zinakidhi matakwa ya Sheria Sura ya 449 na 450;

(xi) Kufanya tathmini na ufuatiliaji wa utekelezaji wa mfumo wa utoaji haki;

(xii) Kuratibu na kusimamia usajili wa matukio muhimu ya binadamu ya vifo, ndoa, talaka na watoto wa kuasili;

(xiii) Kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za kisheria;

(xiv) Kuimarisha mifumo ya upatikanaji haki madai; na

(xv) Kutoa mafunzo ya uanasheria kwa vitendo kwa wanafunzi 1,300.

***171. Mheshimiwa Spika,*** baadhi ya kazi zitakazotekelezwa na Tume ya Utumishi wa Mahakama (Fungu 12) katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 ni pamoja na:-

(i) Kuendelea kuwezesha Ajira na uteuzi kwa watumishi wa Mahakama;

(ii) Kuendelea kusimamia Nidhamu na Maadili ya watumishi wa Mahakama;

(iii) Kuimarisha Kamati za Maadili za Maafisa Mahakama za Mikoa na Wilaya; na

(iv) Kuimarisha Mfumo wa TEHAMA wa ajira na maadili na nidhamu.

***172. Mheshimiwa Spika,*** baadhi ya kazi zitakazotekelezwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (Fungu 16) katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 ni pamoja na:-

(i) Kuimarisha Usimamizi na Ufuatiliaji wa Mikataba iliyosainiwa na kuingiwa na Serikali; na

(ii) Kutoa elimu ya kisheria kwa jamii kupitia Kliniki za Sheria ili kuwaongezea uelewa wananchi kuhusu wajibu na haki zao.

(iii) Kuboresha mifumo ya TEHAMA na kuimarisha matumizi yake katika utoaji wa huduma za kisheria;

(iv) Ujenzi wa majengo ya Ofisi za Vituo Jumuishi vya Taasisi za Serikalza Kisheria Nchini katika mikoa ya Mtwara na Tabora;

***173. Mheshimiwa Spika,*** baadhi ya kazi zitakazotekelezwa na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (Fungu 19) katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 ni pamoja na:-

(i) Kuratibu, kusimamia na kuendesha mashauri ya Madai na Usuluhishi yaliyopo na yatakayofunguliwa na au dhidi ya Serikali na Taasisi zake;

(ii) Kuanzisha Ujenzi wa ofisi za Wakili Mkuu wa Serikali katika mikoa iliyo na Masjala za Mahakama Kuu;

(iii) Kuimarisha mfumo wa kielektroniki wa usimamizi wa mashauri ili kuwa na mfumo thabiti katika kukusanya, kuhifadhi na kutoa taarifa sahihi; na

(iv) Kuboresha ufanisi na utendaji kazi kwa kununua vitendea kazi na kutoa mafunzo kwa watumishi.

***174. Mheshimiwa Spika,*** baadhi ya kazi zitakazotekelezwa na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka (Fungu 35) katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 ni pamoja na:-

(i) Kuendelea na uendeshaji wa kesi za jinai;

(ii) Kufanya ukaguzi katika maeneo yanayohifadhi mahabusi na wafungwa;

(iii) Kuendesha mashauri ya utaifishaji wa mali zinazotokana na uhalifu; na

(iv) Kuendelea na ujenzi wa Majengo ya Ofisi za Mashtaka katika Mikoa na Wilaya.

***175. Mheshimiwa Spika,*** baadhi ya kazi zitakazotekelezwa na Mfuko wa Mahakama (Fungu 40) katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 ni pamoja na:-

(i) Kuharakisha utatuzi wa mashauri ya kawaida na mkakati wa kumaliza mashauri ya muda mrefu (Backlog);

(ii) Kuimarisha uwezo katika ukaguzi na usimamizi wa shughuli za Mahakama;

(iii) Kuendelea kutekeleza mpango wa ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya mahakama;

(iv) Kuboresha mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA); na

(v) Kuimarisha na kuboresha huduma za mafunzo endelevu ya kimahakama na sheria kwa watumishi wa mahakama na wadau wengine.

***176. Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa, baadhi ya kazi zitakazotekelezwa na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (Fungu 55) katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 ni pamoja na:-

(i) Kutoa elimu kwa umma kuhusu haki za binadamu na misingi ya utawala bora katika Mikoa 26 ya Tanzania bara na Mikoa mitano (5) ya Zanzibar;

(ii) Kushughulikia malalamiko ya uvunjwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora na kufanya ufuatiliaji wa mapendekezo ya THBUB yaliyowasilishwa kwenye Taasisi za umma na binafsi;

(iii) Kufanya ukaguzi wa maeneo walimozuiliwa watu kwa mujibu wa sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Magereza, Vituo vya Polisi, Mahabusu za Watoto, na vyuo vya mafunzo); na

(iv) Kufanya ufuatiliaji, utafiti na tathmini ya hali ya haki za binadamu na utawala bora nchini.

***177. Mheshimiwa Spika,*** baadhi ya kazi zitakazotekelezwa na Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania (Fungu 59) katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 ni pamoja na:-

(i) Kufanya utafiti wa mfumo wa sheria zinazosimamia usajili wa Mawakili wa Kujitegemea Tanzania;

(ii) Kufanya utafiti wa mfumo wa sheria zinazosimamia biashara ya hewa ukaa (carbon trading);

(iii) Kufanya utafiti utakaowezesha kutungwa kwa sheria ya matumizi ya akili unde (AI);

(iv) Kufanya utafiti wa mfumo wa sheria zinazosimamia mfumo wa kupinga maamuzi ya kiutawala nchini;

(v) Kufanya Tathmini ya Utekelezaji wa Sheria za Mamlaka ya Nchi kuhusu Umiliki wa Utajiri Asili na Maliasili za Nchi, Sura ya 449 na sheria ya Mapitio na Majadiliano kuhusu Masharti Hasi katika Mikataba ya Utajiri Asili na Maliasilia za Nchi, Sura ya 450;

(vi) Kufanya mapitio ya mfumo wa sheria za bima za magari;

(vii) Kufanya mapitio ya Sheria ya Afya na Usalama Mahala pa Kazi, Sura ya 297;

(viii) Kufanya tathmini ya utekelezaji wa Sheria ya Ugaidi, Sura ya 19;

(ix) Kuendelea na utoaji wa elimu ya sheria na kusambaza taarifa za sheria kwa umma kwa kupanua wigo wa utoaji wa huduma hiyo ili kuwafikia wananchi na wadau wa sheria wengi zaidi nchini; na

(x) Kujenga uwezo wa Watumishi kwa kuanza utekelezaji wa Mpango wa Mafunzo wa Taasisi wa mwaka 2025/26 – 2029/30.

***178. Mheshimiwa Spika,*** baadhi ya kazi zitakazotekelezwa na – Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria (Fungu 101) katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 ni pamoja na:-

(i) Kuandaa Miswada ya Sheria 10, Sheria Ndogo 1,200 na Kutengeneza Sheria Ndogo Kifani 20;

(ii) Kuandaa Toleo la Urekebu wa Sheria Ndogo la Mwaka 2025 na Toleo la Urekebu wa Sheria za Afrika Mashariki la Mwaka 2025.

(iii) Kuboresha/kuimarisha Mifumo ya TEHAMA na matumizi yake katika Uandishi, Ufasiri na Urekebu wa Sheria hususan kujenga Mfumo wa *e-Drafting, e-Translation, na eLibrary*;

(iv) Kutoa mafunzo kwa Watumishi katika maeneo ya kimkakati ili kuhakikisha kunakuwa na wataalam wa kutosha na wenye ujuzi katika nyanja mbalimbali za uandishi wa sheria; na

(v) Kuongeza uelewa wa Wananchi kuhusu Sheria kwa kukamilia tafsiri ya Sheria Kuu **446** na kuanza kutafsiri Sheria Ndogo **900**.

***(c) Makusanyo ya Maduhuli***

***179. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara, Taasisi zake na Mhimili wa Mahakama inatarajia kukusanya jumla ya Shilingi **13,656,199,000** ikiwa ni maduhuli kama ilivyoainishwa katika **Kiambatisho Na.12**

***(d) Makadirio ya Fedha kwa ajili ya Kutekeleza Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026***

***180. Mheshimiwa Spika,*** ili kufanikisha utekelezaji wa vipaumbele vilivyoainishwa, Wizara inaomba kuidhinishiwa jumla ya Shilingi **687,698,489,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Mchanganuo wa makadirio ya bajeti kwa mafungu Tisa **(9)** ya Wizara na taasisi zake ni kama ilivyoainishwa kwenye **Jedwali Na. 1.**

**Jedwali Na. 1: Mchanganuo wa Makadirio ya Bajeti kwa Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi Zake kwa Mwaka wa Fedha, 2025/2026**

| **Fungu la Matumizi** | | **Bajeti 2025/2026** |
|---|---|---|
| (i) | Mishahara ya watumishi | 135,995,670,000 |
| (ii) | Matumizi Mengineyo | 389,464,032,000 |
| (iii) | Miradi ya Maendeleo-Ndani | 79,671,467,000 |
| (iv) | Miradi ya Maendeleo- Nje | 82,567,320,000 |
| | **JUMLA** | **687,698,489,000** |

***181. Mheshimiwa Spika***, kiasi hicho cha fedha kinaombwa kupitia mafungu ya bajeti yaliyo chini ya Wizara kama inavyoonekana hapo chini:-

**Fungu 12: Tume ya Utumishi wa Mahakama**

| | | |
|---|---|---|
| Matumizi ya Mishahara | - Sh. | 1,125,247,000 |
| Matumizi Mengineyo | - Sh. | 5,841,720,000 |
| Matumizi ya Maendeleo (Ndani) | - Sh. | |
| Matumizi ya Maendeleo (Nje) | - Sh. | |
| **Jumla Ndogo** | **- Sh.** | **6,966,967,000** |

**Fungu 16: Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali**

| | | |
|---|---|---|
| Matumizi ya Mishahara | - Sh. | 4,671,816,000 |
| Matumizi Mengineyo | - Sh. | 35,481,434,000 |
| Matumizi ya Maendeleo (Ndani) | - Sh. | 788,704,000 |

| | | |
|---|---|---|
| Matumizi ya Maendeleo (Nje) | - Sh. | |
| **Jumla Ndogo** | **- Sh.** | **40,941,954,000** |

**Fungu 19: Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali**

| | | |
|---|---|---|
| Matumizi ya Mishahara | - Sh. | 4,779,918,000 |
| Matumizi Mengineyo | - Sh. | 33,717,836,000 |
| Matumizi ya Maendeleo (Ndani) | - Sh. | |
| Matumizi ya Maendeleo (Nje | - Sh. | |
| **Jumla Ndogo** | **- Sh.** | **38,497,754,000** |

**Fungu 35: Ofisi ya Taifa ya Mashtaka**

| | | |
|---|---|---|
| Matumizi ya Mishahara | - Sh. | 20,434,283,000 |
| Matumizi Mengineyo | - Sh. | 109,671,664,000 |
| Matumizi ya Maendeleo (Ndani) | - Sh. | 15,866,110,000 |
| Matumizi ya Maendeleo (Nje) | - Sh. | |
| **Jumla Ndogo** | **- Sh.** | **145,972,057,000** |

**Fungu 40: Mahakama ya Tanzania**

| | | |
|---|---|---|
| Matumizi ya Mishahara | - Sh. | 84,645,042,000 |
| Matumizi Mengineyo | - Sh. | 143,385,988,000 |
| Matumizi ya Maendeleo (Ndani) | - Sh. | 18,601,200,000 |
| Matumizi ya Maendeleo (Nje) | - Sh. | 74,424,000,000 |
| **Jumla Ndogo** | **- Sh.** | **321,056,230,000** |

**Fungu 41: Wizara ya Katiba na Sheria (RITA na LST)**

| | | |
|---|---|---|
| Matumizi ya Mishahara | - Sh. | 14,182,689,000 |
| Matumizi Mengineyo | - Sh. | 30,992,606,000 |
| Matumizi ya Maendeleo (Ndani) | - Sh. | 44,415,453,000 |
| Matumizi ya Maendeleo (Nje) | - Sh. | 8,143,320,000 |
| **Jumla Ndogo** | **- Sh.** | **97,734,068,000** |

**Fungu 55: Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora**

| | | |
|---|---|---|
| Matumizi ya Mishahara | - Sh. | 3,452,519,000 |
| Matumizi Mengineyo | - Sh. | 8,291,446,000 |
| Matumizi ya Maendeleo (Ndani) | - Sh. | - |
| Matumizi ya Maendeleo (Nje) | - Sh. | - |
| **Jumla Ndogo** | **- Sh.** | **11,743,965,000** |

**Fungu 59: Tume ya Kurekebisha Sheria**

| | | |
|---|---|---|
| Matumizi ya Mishahara | - Sh. | 1,775,350,000 |
| Matumizi Mengineyo | - Sh. | 5,627,180,000 |
| Matumizi ya Maendeleo (Ndani) | - Sh. | - |
| Matumizi ya Maendeleo (Nje) | - Sh. | - |
| **Jumla Ndogo** | **- Sh.** | **7,402,530,000** |

**Fungu 101: Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria**

| | | |
|---|---|---|
| Matumizi ya Mishahara | - Sh. | 928,806,000 |
| Matumizi Mengineyo | - Sh. | 16,454,158,000 |
| Matumizi ya Maendeleo (Ndani) | - Sh. | |
| Matumizi ya Maendeleo (Nje) | - Sh. | |
| **Jumla Ndogo** | **- Sh.** | **17,382,964,000** |

***182. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2025/2026 Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake inaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi **687,698,489,000**. Kati ya fedha hizo shilingi **135,995,670,000** ni kwa ajili ya mishahara ya Watumishi, Shilingi **389,464,032,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na shilingi **162,238,787,000** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

***183. Mheshimiwa Spika***, maelezo ya kina na mchanganuo wa maombi ya fedha za bajeti ya kila Fungu umeainishwa kwenye vitabu vya Randama za mafungu husika ambavyo vimegawiwa kwa Waheshimiwa Wabunge kupitia Mfumo wa Kielektroniki wa Bunge.

***184. Mheshimiwa Spika***, ninaomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono, sasa kabla sijawaita Wenyeviti wa Kamati, tunao wanafunzi 50 na walimu wanne kutoka Klabu ya Wapinga Rushwa Shule ya Sekondari Dkt. John Samwel Malecela kutoka Dodoma. Karibuni na hongereni kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Utawala, Katiba na Sheria.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA - MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE, UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote ninaomba taarifa hii yote iingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, ninaomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge, Utawala, Katiba na Sheria kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria inahusika na Mafungu Saba chini ya Wizara hii ambayo ni Fungu 41 - Wizara ya Katiba na Sheria; Fungu 16 - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Fungu 35 - Ofisi ya Taifa ya Mashtaka; Fungu 12 - Tume ya Utumishi wa Mahakama; Fungu 55 -Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; Fungu 59 - Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania; Fungu 19 - Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali; Fungu 101 - Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiwa ninaendelea na taarifa yangu ninaomba nifanye nukuu chache: Martin Luther King anaeleza "*Injustice anywhere is a threat to justice everywhere*." Akiwa na maana kuwa, kukosekana kwa haki sehemu moja ni tishio kwa upatikanaji wa haki sehemu nyingine. Pia, Seneca *the*

*Elder* naye ninamnukuu anasema: "*It is a denial of justice not to stretch out a helping hand to the fallen; that is the common right of humanity.*" Akiwa na maana, kutokuwasaidia watu wanyonge ni kuwanyima haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bila shaka utakubaliana nami kuwa, hakuna katika kipindi chochote katika historia ya nchi yetu ambapo Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na ofisi zilizo chini ya Wizara hii zimekuwa karibu na wananchi kama kipindi hiki cha Awamu ya Sita chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia *(Mama Samia Legal Aid Campaign)* sambamba na ujenzi wa ofisi za Mashtaka pamoja na Mahakama nyingi mpya nchini kote ni kielelezo cha dhamira ya dhati ya Mheshimiwa Rais kuwafikia watanzania kote nchini na hasa vijijini ili kuhakikisha kuwa, kila Mtanzania anapata haki yake kwa ukaribu, kwa uharaka na kwa uhakika na anachochea amani na utulivu nchini kwani amani ni tunda la haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muktadha huo, ninaliomba Bunge lako Tukufu liungane na Kamati yetu ya kudumu ya Utawala, Katiba na Sheria, kutoa pongezi za dhati na za kipekee, kwanza kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Pili, kwa Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro, Waziri; Mheshimiwa Jumanne Abdallah Jumanne Sagini, Naibu Waziri; Mheshimiwa Hamza Johari, Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Ndugu Eliakimu Maswi, Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria; pamoja na Watendaji wote waliopo chini yake kwa ubunifu na utekelezaji bora wa majukumu chini ya Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno hayo ya pongezi kwa Mheshimiwa Rais na Wizara, uniruhusu sasa niendelee na sehemu ya pili ya taarifa yetu na sehemu hii inahusu uchambuzi wa makusanyo ya maduhuli pia inahusu matumizi ya bajeti kwa mwaka uliopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba uridhie sehemu hii ya taarifa iingie kwenye kumbukumbu kama ilivyowasilishwa kwa Mafungu yote kama nitakavyoyataja. Kwanza, 41 - Wizara ya Katiba na Sheria; Fungu 16 - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Fungu 35 - Ofisi ya Taifa ya Mashtaka; Fungu 12 - Tume ya Utumishi wa Mahakama; Fungu 55 - Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; Fungu 59 - Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania; Fungu 19 - Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali; Fungu 101 - Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa upatikanaji wa fedha katika Wizara unaonesha kwamba, kwa ujumla Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2024/2025 hadi kufikia Februari 2025, ofisi hii imepokea 59.79% ya bajeti iliyopitishwa na Bunge kipindi ambacho ilitakiwa kuwa 75% ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha husika. Kwa maana hiyo, mtiririko wa upatikanaji wa fedha ulipaswa kuboreshwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wizara hii, Taasisi tano kati ya Taasisi saba zilizopo chini ya Ofisi hii zimefanikiwa kupata kiasi cha fedha ambacho kinaendana na uwiano wa upatikanaji wa fedha kwa 66.6% hadi kufikia Februari, 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchanganuo wa fedha hizo kwa taasisi za Wizara ya Katiba na Sheria ni kama inavyoonekana katika Jedwali Na.2 na Jedwali Na.3 yaliyomo kwenye taarifa yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na uzingatiaji wa ushauri wa Kamati. Wakati wa uchambuzi wa bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Kamati ilitoa maoni na ushauri kuhusu mambo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Wizara hiyo. Naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba kwa sehemu kubwa Serikali imezingatia ushauri wa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, upo ushauri ambao ulianza kuzingatiwa, lakini haujakamilika, na ushauri mwingine umepokelewa lakini haujafanyiwa kazi. Kwa mfano, kuhusu Usajili

wa matukio muhimu kama vile ndoa na talaka, Kamati iliishauri Wizara iendeshe *program* za elimu kwa umma ili kuhamasisha wananchi juu ya umuhimu wa usajili wa matukio hayo. Taarifa ya utekelezaji ilionesha kuwa Wizara haikufanyia kazi ushauri huo na hivyo ni maoni ya Kamati kuwa, jambo hilo linahitaji kipaumbele katika utekelezaji wa bajeti wa Fungu 41. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba uniruhusu niende kwenye Sehemu ya Tatu ya taarifa yetu ambayo inahusu Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kuhusu maduhuli; katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara ya Katiba na Sheria inaomba kuidhinishiwa kukusanya jumla ya shilingi milioni 85 ikilinganishwa na shilingi 108,332,000, katika mwaka wa fedha 2024/2025 kama ambavyo imeainishwa katika Jedwali Na.4 lililopo kwenye taarifa hii. Lengo hili limepungua kwa 21.54% likilinganishwa na na lengo la ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha unaoisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi unaonesha kuwa, kati ya Mafungu Nane (8) yaliyopo chini ya Wizara hii ni Mafungu Mawili pekee ndiyo yenye makadirio ya ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Hata hivyo, hali hiyo inatokana na asili na majukumu ya kila Fungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu matumizi ya kawaida; katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na taasisi zilizo chini yake inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 297,426,672,000, ikiwa ni fedha za matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi 51,350,628,000 ni mishahara na shilingi 243,078,090,000 ni matumizi mengineyo, kama ambavyo imechanganuliwa katika Jedwali Na. 5.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya matumizi ya kawaida; katika mwaka wa fedha 2025/2026 imeongezeka kwa asilimia 58.61 Ikilinganisha na mwaka wa fedha unaoisha ambapo bajeti ya matumizi ya kawaida ndani ya ukomo wa bajeti ilikuwa shilingi

187,116,892,571. Kamati imebaini kwamba, moja kati ya sababu ya ongezeko hili ni maoni ya Kamati kwamba Serikali ipange bajeti kulingana na mahitaji halisi. Aidha, ongezeko hilo linaakisi mahitaji ya kifedha kulingana na sababu mbalimbali za kiuchumi ikiwemo kupanda kwa bei ya bidhaa na huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu miradi ya maendeleo; katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ya Katiba na Sheria inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 71,113,634,000 kwa ajili ya utekelezaji wa mpango wa maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 63,070,314,000 ni fedha za ndani na shilingi 8,143,320,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya maendeleo katika mwaka wa fedha 2025/2026 imeongezeka kwa kiasi cha shilingi 14,578,473,000 sawa na 25.74% ikilinganisha na Bajeti ya mwaka wa fedha unaoisha. Kamati iliambiwa kuwa, sababu ya ongezeko hilo, linachangiwa na ongezeko la gharama za bei ya bidhaa na huduma. Mchanganuo wa Miradi ya Maendeleo ni kama ulivyoainishwa katika Jedwali Na.6 lililopo kwenye Taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inapongeza jitihada za Serikali kuendelea kupanga bajeti ili kutekeleza miradi mingi zaidi kwa kutumia fedha za ndani. Sehemu ya Nne ya Taarifa yetu ni Maoni na Ushauri na kwa Sehemu ya Kwanza ni Maoni ya Jumla, ambayo uniruhusu nisiyasome, lakini Sehemu ya Pili inahusu Maoni na Ushauri mahsusi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maoni ya jumla yaliyopo katika Ukurasa wa 15 na 16 wa Taarifa hii ninayoisoma, ambayo ni mtazamo wa jumla wa Kamati, sasa ninaomba kutoa ushauri wa Kamati, kama ifuatavyo:-

(a) Wizara ya Katiba na Sheria ihakikishe kwamba, inaweka makadirio ya makusanyo ya maduhuli yanayoakisi uwezo wa ukusanyaji na hali halisi ya vyanzo vyake;

(b) Wizara ianzishe programu na kiliniki za kutoa Elimu kwa Umma kuhusu haki za binadamu na madhara ya uvunjifu wa haki hizo za msingi;

(c) *RITA* chini ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ianze utaratibu wa kutoa elimu kwa wananchi kuhusu usajili wa ndoa zilizofungwa kidini na kimila na taratibu za usajili wa talaka nchini;

(d) Wizara ya Katiba na Sheria ihakikishe kwamba, Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia *(Mama Samia Legal Aid Campaign)* zinakuwa endelevu, ili kuwafikia watu wengi zaidi kwa ukaribu; na

(e) Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora iendelee kuwezeshwa zaidi kibajeti hususani bajeti ya maendeleo ili kuipa uwezo mkubwa zaidi wa kutekeleza majukumu yake kikamilifu na kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kumshukuru sana Spika, wewe, pamoja na Wenyeviti wote wa Bunge kwa uongozi wenu na kutupatia nafasi ya kuwasilisha taarifa hii. Ninapenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi wa hali ya juu na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Ninaomba majina yao yaingizwe kwenye Taarifa Rasmi za Bunge, kama yalivyowasilishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati, ninaomba nichukue fursa hii kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Waziri wa Katiba na Sheria, pamoja na Mheshimiwa Mbunge Jumanne Abdallah Sagini, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, kwa ushirikiano walioipatia Kamati, ambao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, Kamati inamshukuru

Mheshimiwa Hamza Johari, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa ushirikiano ambao ameendelea kuipa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba pia niwashukuru watendaji wote wa Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na taasisi zake kwa ushirikiano walioupatia Kamati wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo, Bwana Eliakim Maswi; Ndugu Franklin Jasson Rwezimula, Naibu Katibu Mkuu; Profesa Elisante Ole Gabriel, Mtendaji Mkuu wa Mahakama na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Mahakama; Ndugu Sylvester Mwakitalu, Mkurugenzi wa Mashtaka; Ndugu Patience Ntwina, Katibu Mtendaji wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; Ndugu George Mandepo Katibu Mtendaji wa Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania na Dkt. Ally Possi, Wakili Mkuu wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, ninapenda kumshukuru sana Katibu wa Bunge Ndugu Baraka Leonard, kwa kuratibu vema Shughuli za Kamati na Bunge kwa mujibu wa Katiba ya Nchi yetu. Aidha, kipekee nawashukuru Sekretarieti ya Kamati kwa kuratibu shughuli za Kamati na kufanikisha kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii tukiwa mwaka wetu wa mwisho wa utendaji, kama Wabunge, kabla ya uchaguzi ujao, ninaomba nitumie nafasi hii kuwashukuru wananchi wote wa Madaba ambao wamenipatia imani kwa muda wote huu wa kutekeleza majukumu yangu ya uwakilishi kwa wananchi. Heshima ambayo wamenipatia imeniwezesha pia, kutekeleza majukumu ya Bunge kwa ufanisi mkubwa. Aidha, niwashukuru sana viongozi wetu wa Chama Cha Mapinduzi, ngazi ya mkoa, wilaya, kata na matawi ambao wakati wote wameendelea kutoa ushirikiano mkubwa ili kuhakikisha Mbunge wao, Joseph Kizito Mhagama, niwapo Bungeni ninafanya kazi kwa utulivu na kwa ufanisi mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahadi yangu, nitaendelea kutoa ushirikiano kwa wananchi wangu na kuhakikisha kwamba, tunaendelea kumsemea na kumtetea Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, sasa ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

**SEHEMU YA KWANZA**

**1.0 UTANGULIZI**

**1.1. Maelezo ya Awali**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa **Kanuni ya 118 (9)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika**, ili kukidhi masharti ya Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Bunge, na kwa madhumuni ya kurahisisha ufuatiliaji na mtiririko, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu zifuatazo: -

(a) Sehemu ya Kwanza inayotoa maelezo ya jumla na kuonesha misingi, muundo na namna Kamati ilivyofanya kazi;

(b) Sehemu ya Pili inayohusu uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti, makusanyo ya maduhuli, mwenendo wa upatikanaji wa fedha, utekelezaji wa miradi ya maendeleo na uzingatiaji wa ushauri wa Kamati;

(c) Sehemu ya tatu inayohusu uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026;

(d) Sehemu ya Nne inayofanya majumuisho ya maoni na kutoa ushauri wa Kamati; na

(e) Sehemu ya tano na ya Mwisho ni Hitimisho.

### 1.2. Msingi wa Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, Msingi wa Kamati kufanya uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Wizara ya Katiba na Sheria ni Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Kifungu cha 6(2)(e) kikisomwa kwa pamoja na Kifungu cha 7 (1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, zinatambua jukumu la Kamati hii kufanya uchambuzi huo. Aidha, Kanuni ya 118(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge imeweka masharti yanayotaka Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio hayo kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni. Naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa masharti hayo yamezingatiwa.

### 1.3. Mawanda ya Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, Katika uchambuzi huo, Kamati ilipitia jumla ya mafungu Saba (7) ambayo ni: -

(a) **Fungu 41** – Wizara ya Katiba na Sheria;

(b) **Fungu 16** – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;

(c) **Fungu 35** – Ofisi ya Taifa ya Mashtaka;

(d) **Fungu 12** – Tume ya Utumishi wa Mahakama;

(e) **Fungu 55** – Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora;

(f) **Fungu 59** – Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania;

(g) **Fungu 19** – Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali; na

(h) **Fungu 101** – Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI NA TATHIMINI

### 2.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** matokeo ya uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi yanaweka msingi wa ushauri wa Kamati kuhusu hoja hii ya Wizara ya Katiba na Sheria. Kwa sababu hiyo, ili kuwezesha ufuatiliaji mzuri wa wasilisho hili, naomba kubainisha mambo makuu manne yaliyochambuliwa kama ifuatavyo: -

(a) Makusanyo ya maduhuli;

(b) Mwenendo wa Upatikanaji wa fedha za Bajeti ya Matumizi ya kawaida na Bajeti ya Maendeleo;

(c) Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria;

(d) Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati; na

**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi huo, njia ya kukokotoa Asilimia ilitumika. Aidha, Kamati ilifanya ulinganisho wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

## 2.2 Uchambuzi wa Makusanyo ya Maduhuli

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Katiba na Sheria ililenga kukusanya maduhuli ya jumla ya **Sh. 108,332,000**, kati ya fedha hizo **Fungu 41** – Wizara ya Katiba na Sheria ililenga kukusanya **Sh. 45,000,000**, **Fungu 35** – Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ililenga kukusanya **Sh. 60,000,000** na **Fungu 16** – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ililenga kukusanya **Sh. 3,332,000**.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli unaonesha yafuatayo: -

(a) **Fungu 41** – Wizara ya Katiba na Sheria imekusanya chini ya lengo, hadi kufika hadi kufikia Mwezi Februari, 2025 makusanyo ni **Sh 20,521,000** kati ya **Sh. 45,000,000** sawa na **asilimia 45.60** tu.

**Mheshimiwa Spika;** Kamati ilielezwa kuwa, kutokufikiwa kwa lengo ni kutokana na maombi ya usajili wa watoa huduma kwa njia mbadala na Watoa Huduma ya Msaada Kisheria kuwa machache ikilinganishwa na lengo lililowekwa. Sababu nyingine ni kutoanza kufanya kazi kwa Kituo cha Usuluhishi Tanzania kilichotarajiwa kuanzishwa.

(b) **Fungu 35** – Ofisi ya Taifa ya Mashtaka hadi kufika Februari, 2025 imekusanya kiasi cha **Sh. 56,000,000** kati ya **Sh. 60,000,000** sawa na **asilimia 93.33** ya lengo la Makusanyo. Makusanyo hayo, yanatokana na uzingatiaji wa masharti ya upangishaji.

(c) **Fungu 16** – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali hadi kufikia Mwezi Februari, 2025 haikuwa imeweza kukusanya kiasi chochote cha fedha, hata hivyo lengo la makusanyo ya ofisi hiyo ni Sh. 3,332,000 kama ilivyoidhinishwa na Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa Maduhuli yaliyopangwa kukusanywa yalitarajiwa kutokana na huduma mbalimbali zinazotolewa na Ofisi kama vile nyaraka za zabuni,

ada mbalimbali na urejeshwaji wa fedha za umma, hadi kufikia Mwezi Februari, 2025 hakuna mauzo yoyote ya zabuni yaliyofanyika na huduma iliyotolewa kwa malipo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ina maoni kuwa, makusanyo hafifu ya **Fungu 41** na **Fungu 16** chini ya Wizara, yanaweza kutafsiriwa kwamba malengo ya ukusanyaji yaliyowekwa hayakuwa halisi, au vyanzo vya maduhuli vilivyoanishwa havikuwa vya uhakika na si endelevu. Kwa msingi huo, ni vyema Wizara na taasisi zake zote izingatie uhalisia wa makadirio ya makusanyo ya maduhuli. Aidha kwa utaratibu bora wa makadirio ya bajeti, itafaa **Fungu 16** lisiwekewe lengo la makusanyo ya Maduhuli mpaka pale Serikali itakapojiridhisha na uhalisia wa makusanyo ya Maduhuli.

**Mheshimiwa Spika,** mchanganuo wa maduhuli kwa kila fungu unaoneshwa katika **Jedwali Na. 1.**

**JEDWALI NA. 1 MAKUSANYO YA MADHUHULI 2024/2025**

| FUNGU | MAKADIRIO YA MAKUSANYO YA MADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 | MAKUSANYO YA MADUHULI HADI KUFIKIA FEBRUARI, 2025 | ASILIMIA YA MAKUSANYO |
|---|---|---|---|
| **Fungu 41** – Wizara ya Katiba na Sheria | 45,000,000 | 20,521,000 | 45.60 |
| **Fungu 35** – Ofisi ya Taifa ya Mashtaka | 60,000,000 | 56,000,000 | 93.33 |
| **Fungu 16** – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali | 3,332,000 | 0 | 0 |
| **JUMLA KUU** | **108,332,000** | **76,521,000** | **70.64** |

***Chanzo:*** *Randama za Wizara ya Katiba na Sheria na Usanifu wa Kamati.*

### 2.3 Uchambuzi wa Matumizi ya Bajeti

#### 2.3.1 Fungu 41 – Wizara ya Katiba na Sheria

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2024/2025, fungu hili iliidhinishiwa jumla ya **Sh. 85,184,265,931.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo, kati ya fedha hizo **Asilimia 47** ilikuwa ni matumizi ya Kawaida na **Asilimia 53** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Mwezi Februari, 2025 fedha za Matumizi ya Kawaida zilizopokelewa ni **Sh**. **26,989,913,491.57** sawa na asilimia **67.08** ya bajeti ya matumizi ya Kawaida iliyopitishwa na Bunge. Aidha, hadi kufikia mwezi Februari, 2025 Wizara **Fungu 41** lilipokea **Sh. 37,284,206,408.00** sawa na **asilimia 96.77** ya fedha zilipokelewa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

#### 2.3.2 Fungu 16 - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliidhinishiwa jumla ya **Sh. 31,499,071,640** kwa ajili ya bajeti ya Matumizi ya Kawaida na bajeti ya Maendeleo, Kati ya Fedha hizo **Asilimia 94** ni bajeti ya matumizi ya Kawaid ana **Asilimia 6** ni Bajeti ya Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Hadi kufikia mwezi Februari, 2025 Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilipokea jumla ya **Sh. 14,562,671,325.01** sawa na **asilimia 49** ya bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili matumizi ya Kawaida. Aidha, Hadi kufikia mwezi Februari 2025, Ofisi imepokea na kutumia kiasi cha **Sh. 92,297,975.33** kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo sawa na **Asilimia 05** ya Bajeti iliyoidhinishwa.

#### 2.3.3 Fungu 35 - Ofisi ya Taifa ya Mashtaka

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka iliidhinishiwa jumla ya **Sh. 87,483,894,000** ilitengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya

Maendeleo. Kati ya fedha hizo **Asilimia 89** ni kwa ajili ya matumizi ya Kawaida na **Asilimia 11** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia mwezi Februari, 2025, Ofisi ilipokea jumla ya **Sh. 41,063,245,442.20** sawa na **Asilimia 52.96** ya bajeti ya Matumizi ya Kawaida na **Sh. 3,153,642,711.66** sawa na **asilimia 31.72** zilipokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

**2.3.4 Fungu 12 – Tume ya Utumishi wa Mahakama;**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Tume ya Utumishi wa Mahakama iliidhinishiwa jumla ya **Sh. 5,498,652,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, kati ya fedha hizo ni Mishahara (PE) ni **Asilimia 14** na **Asilimia 86** kwa ajili ya kugharamia gharama za uendeshaji wa ofisi.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi Februari, 2025 Tume ya Utumishi wa Mahakama ilipokea jumla ya **Sh. 3,665,768,000** sawa na asilima **66.66** ya bajeti iliyoidhinishwa. Ambapo **Asilimia 64.3** zilipokelewa kwa ajilii ya Mishahara (PE) na **Asilimia 62.89** zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC). Mtiririko huo ni ishara kuwa shughuli za uendeshaji wa shughuli za Tume ya Utumishi wa Mahakama zilitekelezwa kama zilivyopangwa.

**2.3.5 Fungu 55 – Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora iliidhinishiwa jumla ya **Sh. 8,685,660,000** ambapo kati ya fedha hizo **Asilimia 41** ni Mishahara (PE) na **Asilimia 59** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC).

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari, 2025 Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora jumla ya **Sh. 6,478,650,577.65** sawa na asilima **74.59** ya bajeti iliyoidhinishwa; ambapo **Asilimia 54.67** zilipokelewa kwa ajilii ya Mishahara (PE) na Asilimia **88.19** zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC).

### 2.3.6 Fungu 59 – Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania iliidhinishiwa jumla ya **Sh. 5,051,790,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, kati ya fedha hizo **Asilimia 18** ni Mishahara (PE) na **Asilimia 82** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC).

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Mwezi Februari, 2025 Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania ilipokea jumla ya **Sh. 3,360,265,436.33** sawa na asilimia **66.5** ya bajeti iliyoidhinishwa ambapo asilimia **76.96** zilipokelewa kwa ajilii ya Mishahara (PE) na na asilimia **64.17** zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC).

### 2.3.7 Fungu 19 – Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali iliidhinishiwa jumla ya **Sh. 20,750,720,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, kati ya fedha hizo **Asilimia 21** ni Mishahara (PE) na **Asilimia 79** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC).

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Mwezi Februari, 2025 Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ilipokea jumla ya **Sh. 16,002,847,489.46** sawa na asilima **77.11** ya bajeti iliyoidhinishwa; ambapo Asilimia **61.18** zilipokelewa kwa ajilii ya Mishahara (PE) na asilimia **43.12** zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC).

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa upatikanaji wa fedha hizo unaonesha kwamba:

(a) Kwa ujumla, Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2024/2025, hadi kufikia Februari, 2025 Ofisi hii ilipokea **asilimia 59.79** ya bajeti iliyopitishwa na Bunge kipindi ambacho ilitakiwa kuwa Asilimia 75 ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025. Kwa maana hiyo, mtiririko wa upatikanaji wa fedha ulipaswa kuboreshwa Februari.

(b) Taasisi Tano (5) kati ya Taasisi saba (7) zilizopo chini ya Ofisi hii zimefanikiwa kupata kiasi cha fedha ambacho kinaendana na uwiano wa upatikanaji wa fedha kwa **asilimia 66.6** hadi kufikia Februari, 2025.

**Mheshimiwa Spika**, Mchanganuo wa fedha hizo kwa taasisi za Wizara ya Katiba na Sheria ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 2** na **Jedwali Na. 3.**

**JEDWALI NA. 2 MCHANGANUO WA MATUMIZI YA KAWAIDA 2024/2025**

| FUNGU | FEDHA YA MATUMIZI YA KAWAIDA ILIYOTENGWA KWA MWAKA 2024/2025 | FEDHA YA MATUMIZI YA KAWAIDA ILIYOPOKELEWA HADI KUFIKIA FEBRUARI, 2025 | ASILIMIA YA MAPOKEZI |
|---|---|---|---|
| **Fungu 41** – Wizara ya Katiba na Sheria | 40,232,527,931.00 | 26,989,913,491.57 | 67.08 |
| **Fungu 16** – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali | 29,759,165,640.00 | 14,562,671,325.01 | 49 |
| **Fungu 35** – Ofisi ya Taifa ya Mashtaka | 77,540,377,000.00 | 41,063,245,442.20 | 52.96 |
| **Fungu 12** – Tume ya Utumishi wa ahakama | 5,498,652,000.00 | 3,665,768,000.00 | 66.66 |
| **Fungu 55** – Tume ya Haki za Binadamu na Utawala | 8,685,660,000.00 | 6,478,650,577.65 | 74.59 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Bora | | | |
| **Fungu 59** – Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania | 5,051,790,000.00 | 3,360,265,436.33 | 66.5 |
| **Fungu 19** – Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali | 20,750,720,000.00 | 16,002,847,489.46 | 77.11 |
| **Fungu 101** – Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria | - | - | - |
| **JUMLA KUU** | **187,518,892,571.00** | **112,123,361,762.22** | **59.79** |

***Chanzo**: Randama za Wizara ya Katiba na Sheria na Usanifu wa Kamati*

**JEDWALI NA. 3 MCHANGANUO WA BAJETI YA MAENDELEO 2024/2025**

| FUNGU | FEDHA YA MAENDELEO ILIYOTENGWA KWA MWAKA 2024/2025 | FEDHA YA MAENDELEO ILIYOPOKELEWA HADI KUFIKIA FEBRUARI, 2025 | ASILIMIA YA MAPOKEZI |
|---|---|---|---|
| **Fungu 41** - Wizara ya Katiba na Sheria | 44,951,738,000.00 | 38,824,842,100.00 | 96.77 |
| **Fungu 16** - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali | 1,739,906,000.00 | 92,297,975.33 | 5.3 |
| **Fungu 35** - Ofisi ya Taifa ya Mashtaka | 9,943,517,000.00 | 3,153,642,711.66 | 31.72 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **JUMLA KUU** | **56,635,161,000.00** | **42,070,782,786.99** | **74.28** |

***Chanzo****: Randama za Wizara ya Katiba na Sheria na Usanifu wa Kamati*

### 2.4 Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Kamati ilitoa maoni na ushauri kuhusu mambo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Wizara hiyo. Naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba kwa sehemu kubwa Serikali imezingatia ushauri wa Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** upo ushauri ambao ulianza kuzingatiwa lakini haujakamilika, na ushauri mwingine umepokelewa lakini haujafanyiwa kazi, kwa mfano Kuhusu Usajili wa matukio muhimu kama vile ndoa na Talaka, Kamati iliishauri Wizara iendeshe program za Elimu kwa Umma ili kuhamasisha wananchi juu ya umuhimu wa usajili wa matukio hayo. Taarifa ya utekelezaji ilionesha kuwa Wizara haikufanyia kazi ushauri huo na hivyo ni maoni ya Kamati kuwa, jambo hilo linahitaji kipaumbele katika utekelezaji wa bajeti wa **Fungu 41.**

## SEHEMU YA TATU

### 3.0 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

### 3.1 Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Wizara ya Katiba na Sheria inaomba kuidhinishiwa kukusanya jumla ya **Sh. 85,000,000** ikilinganishwa na **Sh. 108,332,000.00** katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 kama ambavyo imeainishwa katika **Jedwali Na. 4**. Lengo hili limepungua kwa asilimia **21.54** likilinganishwa na na lengo la ukusanyaji wa Maduhuli kwa mwaka wa fedha unaoisha.

**JEDWALI NA. 4 MADUHULI KWA MWAKA 2025/2026**

| FUNGU | MAKADIRIO YA MAKUSANYO YA MADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 | MAKADIRIO YA MAKUSANYO YA MADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 |
|---|---|---|
| **Fungu 41** - Wizara ya Katiba na Sheria | 45,000,000.00 | 25,000,000.00 |
| **Fungu 35** - Ofisi ya Taifa ya Mashtaka | 60,000,000.00 | 60,000,000.00 |
| **Fungu 16** - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali | 3,332,000.00 | |
| **JUMLA KUU** | **108,332,000.00** | **85,000,000.00** |

***Chanzo:*** *Randama za Wizara ya Katiba na Sheria na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi unaonesha kuwa, kati ya Mafungu manane (8) yaliyopo chini ya Wizara hii, ni Mafungu Mawili pekee ndiyo yenye Makadirio ya Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Hata hivyo, hali hiyo inatokana na asili na majukumu ya kila Fungu. **Aidha,** kwa Mafungu hayo Mawili yenye makadirio ya ukusanyaji wa Madhuhuli yanakadiriwa kuwa **Sh. 85,000,000**.

### 3.2 Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na taasisi zilizo chini yake inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Sh. 297,428,672,000.00** ikiwa ni Fedha za Matumizi ya Kawaida, kati ya fedha hizo **Sh. 51,350,628,000.00** ni Mishahara (PE) na **Sh. 243,078,090,000.00** ni Matumizi Mengineyo (OC), kama ambavyo imechanganuliwa katika **Jedwali Na. 5.**

**JEDWALI NA. 5 MCHANGANUO WA MATUMIZI YA KAWAIDA 2025/2026**

| FUNGU | MISHAHARA | MATUMIZI MENGINEYO | JUMLA YA MATUMIZI YA KAWAIDA |
|---|---|---|---|
| **Fungu 41** - Wizara ya Katiba na Sheria | 14,182,689,000.00 | 30,992,606,000.00 | 45,175,295,000.00 |
| **Fungu 16** – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali | 4,671,816,000.00 | 35,481,434,000.00 | 40,153,250,000.00 |
| **Fungu 35** - Ofisi ya Taifa ya Mashtaka | 20,434,283,000.00 | 109,671,664,000.00 | 130,105,947,000.00 |
| **Fungu 12** - Tume ya Utumishi wa Mahakama | 1,125,247,000.00 | 5,841,720,000.00 | 6,966,967,000.00 |
| **Fungu 55** - Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora | 3,452,519,000.00 | 8,291,446,000.00 | 11,743,965,000.00 |
| **Fungu 59** - Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania | 1,775,350,000.00 | 5,627,180,000.00 | 7,402,530,000.00 |
| **Fungu 19** - Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali | 4,779,918,000.00 | 33,717,836,000.00 | 38,497,754,000.00 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **FUNGU 101 –** Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria | 928,806,000.00 | 16,454,158,000.00 | 17,382,964,000.00 |
| **JUMLA KUU** | **51,350,628,000.00** | **243,078,090,000.00** | **297,428,672,000.00** |

***Chanzo**: Randama za Wizara ya Katiba na Sheria na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya Matumizi ya Kawaida katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 imeongezeka kwa asilimia **58.61** ukilinganisha na Mwaka wa Fedha unaoisha ambapo bajeti ya Matumizi ya kawaida ndani ya ukomo bajeti ilikuwa **Sh. 187,518,892,571.00**. Kamati imebaini kwamba, moja kati ya sababu ya ongezeko hili ni maoni ya Kamati kwamba Serikali ipange bajeti kulingana na mahitaji halisi. Aidha, ongezeko hilo linaakisi mahitaji ya kifedha kulingana na sababu mbalimbali za kiuchumi ikiwemo kupanda kwa bei ya bidhaa na huduma.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ina maoni kuwa upo umuhimu wa Seriklai kuhakikisha kwamba fedha zinazoombwa zinatumika vizuri. Na ili kuhakikisha hili linatekelezwa ipasavyo,Serikali iendelee kuzingatia taratibu za kuwasilisha taarifa mbalimbali za utekelezaji wa bajeti mbele ya Kamati.

### 3.3 Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Wizara ya Katiba na Sheria inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Sh. 71,213,634,000.00** kwa ajili ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Sh. 63,070,314,000.00** ni fedha za ndani, na **Sh. 8,143,320,000.00** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, bajeti ya maendeleo katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 imeongezeka kwa kiasi cha **Sh. 14,578,473,000.00** sawa na asilimia **25.74** ukilinganisha na bajeti ya Mwaka wa Fedha unaoisha, kamati iliambiwa kuwa sababu ya ongezeko hilo linachangiwa na ongezeko la gharama za bei za

bidhaa. Mchanganuo wa Miradi ya Maendeleo ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 6.**

**JEDWALI NA. 6 MCHANGANUO WA BAJETI YA MAENDELEO 2025/2026**

| FUNGU | BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 | |
|---|---|---|
| | FEDHA ZA NDANI | FEDHA ZA NJE |
| **Fungu 41** - Wizara ya Katiba na Sheria | 46,415,500,000.00 | 8,143,320,000.00 |
| **Fungu 16** - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali | 788,704,000.00 | - |
| **FUNGU 35 –** Ofisi ya Taifa ya Mashitaka | 15,866,110,000.00 | - |
| **JUMLA NDOGO** | **63,070,314,000.00** | **8,143,320,000.00** |
| **JUMLA KUU** | **71,213,634,000.00** | |

***Chanzo***: *Randama za Wizara ya Katiba na Sheria na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza jitihada za Serikali kuendelea kupanga bajeti ili kutekeleza miradi mingi zaidi kwa kutumia fedha za ndani.

## SEHEMU YA NNE

### 4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 4.1 Maoni ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, naomba kukamilisha uchambuzi kwa kubainisha Maoni ya Kamati

yanayojenga mtazamo ambao ni msingi wa Ushauri wa Kamati. Maoni hayo ni kama ifuatavyo: -

(a) Kutokuwepo kwa makadirio ya makusanyo ya maduhuli yanayoakisi uwezo wa ukusanyaji na hali halisi ya vyanzo vyake, husababisha kuonekana kuwa hakuna tathmini ya kutosha juu ya vyanzo hivyo vya ukusanyaji wa maduhuli. Kwa hiyo, Serikali inahitaji kujiwekea malengo ya ukusanyaji maduhuli yenye uhalisia;

(b) Kutokuwepo kwa Elimu ya haki za binadamu kwa umma, kunasababisha wananchi kuendelea kuwepo kwa matukio makubwa ya uvunjifu wa haki za Binadamu katika Jamii;

(c) Kutosajiliwa kwa ndoa za kimila na Talaka kwa mujibu wa Sheria, kutokana na elimu ndogo na mwamko hafifu kwa wananchi, kunafifisha Azma ya RITA kuwa na taarifa sahihi na halisi za ndoa zilizofungwa kimila na matukio ya Talaka;

(d) Kutokusomana kwa Mfumo wa Tume ya Haki za Binadamu unaohusisha utoaji wa taarifa za matukio ya uvunjifu wa haki za Binadamu na Utawala Bora na mifumo mingine ya Taasisi za utoaji haki nchini kunaweza kudhoofisha ushirikiano baina ya Taasisi hizo katika kuwezesha uzingatiaji wa misingi ya Haki za Binadamu na Utawala Bora;

(e) Kukosekana kwa Mfumo wa wazi wa Utoaji Taarifa za matukio ya uvunjifu wa Haki za Binadamu nchini, kunaweza kusababisha Tume ya Haki za Bindamu na Utawala Bora ionekana haitekelezi majukumu yake kikamilifu; na

(f) Utekelezaji wa Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia (Mama Samia Legal Aid Campaign)

umechangia manufaa makubwa katika misingi ya haki, ustawi wa watu Mshikamano ndani ya jamii.

**Mheshimiwa Spika**, kwa maoni hayo Serikali ya awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inahitaji kupongezwa, kuungwa mkono na kuzingatiwa inavyostahili kwa wakati wa sasa; Aidha mtazamo huu unaendana na lengo la Serikali kwa mujibu wa **Ibara ya 8 (1)(b)** ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 ambao ni Ustawi wa wananchi.

**4.2 Ushauri**

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kutoa maoni hayo ambayo ni mtazamo wa jumla wa Kamati, sasa naomba kutoa Ushauri wa Kamati kama ifuatavyo: -

(a) Wizara ya Katiba na Sheria ihakikishe kwamba inaweka makadirio ya makusanyo ya maduhuli yanayoakisi uwezo wa ukusanyaji na hali halisi ya vyanzo vyake;

(b) Wizara ianzishe programu na kiliniki za kutoa Elimu kwa Umma kuhusu haki za binadamu na madhara ya uvunjifu wa haki hizo za msingi;

(c) RITA chini ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ianze utaratibu wa kutoa elimu kwa wananchi kuhusu Usajili wa ndoa zilizofungwa kidini na kimila na taratibu za usajili wa talaka nchini;

(d) Wizara ya Katiba na Sheria ihakikishe kwamba Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia (Mama Samia Legal Aid Campaign) zinakuwa endelevu ili kuwafikia watu wengi zaidi kwa ukaribu; na

(e) Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora iendelee kuwezeshwa zaidi kibajeti hususani bajeti ya maendeleo ili kuipa uwezo mkubwa zaidi wa kutekeleza majukumu yake kikamilifu na kwa ufanisi.

## 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa Uongozi wenu na kutupatia nafasi ya kuwasilisha taarifa hii. Napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi wa hali ya juu na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao yaingizwe kwenye taarifa rasmi za Bunge kama yalivyowasilishwa.

1. Mhe. Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mb - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Florent Laurent Kyombo, Mb. - **M/Mwenyekiti**
3. Mhe. Abdullah Ali Mwinyi, Mb. - Mjumbe
4. Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb. - Mjumbe
5. Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mb. - Mjumbe
6. Mhe. Edward Olelekaita Kisau, Mb. - Mjumbe
7. Mhe. Boniphace Nyangindu Butondo, Mb. – Mjumbe
8. Mhe. Dkt. Alice Karungi Kaijage, Mb. - Mjumbe
9. Mhe. Joseph Anania Tadayo, Mb. - Mjumbe
10. Mhe. Jonas Van Zeeland, Mb. - Mjumbe
11. Mhe. Selemani Jumanne Zedi, Mb. - Mjumbe
12. Mhe. Seif Khamis Said Gulamali, Mb. - Mjumbe
13. Mhe. Salum Mohammed Shaafi, Mb. - Mjumbe
14. Mhe. Yahya Omary Massare, Mb. - Mjumbe
15. Mhe. Agnesta Lambert Kaiza, Mb. - Mjumbe
16. Mhe. Abeid Ighondo Ramadhani, Mb. - Mjumbe
17. Mhe. Suma Ikenda Fyandomo, Mb. - Mjumbe
18. Mhe. Hussein Nassor Amar, Mb. - Mjumbe
19. Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb. - Mjumbe
20. Mhe. Omar Issa Kombo, Mb. – Mjumbe
21. Mhe. Aziza Seylum Ally, Mb. – Mjumbe
22. Mhe. Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mb. - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nichukue fursa hii kumpongeza na kumshukuru Mhe. Balozi Dkt. Damas Daniel Ndumbaro (Mb), Waziri wa Katiba na Sheria Pamoja na Mhe. Jumanne Abdallah Sagini (Mb, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria kwa ushirikiano walioipatia Kamati,

ambao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha; Kamati inamshukuru Mhe. Hamza Johari Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushirikiano ambao ameendelea kuipa Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, naomba pia niwashukuru watendaji wote wa Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na taasisi zake kwa ushirikiano walioupatia Kamati wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo Bw. Eliakimu Maswi, Ndg. Dkt Franklin Jasson Rwezimula Naibu Katibu Mkuu, Prof. Elisante Ole Gabriel Mtendaji Mkuu wa Mahakama na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Mahakama, Ndg. Sylvester A. Mwakitalu Mkurugenzi wa Mashtaka, Ndg. Patience Ntwina Katibu Mtendaji wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Ndg. George Mandepo Katibu Mtendaji wa Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania na Dkt. Ally Possi Wakili Mkuu wa Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini sio kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Baraka I. Leonard, kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Bunge kwa mujibu wa Katiba ya Nchi. Aidha, kiupekee nawashukuru Sekretarieti ya Kamati kwa kuratibu shughuli za Kamati na kufanikisha kukamilika kwa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako tukufu likubali kujadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa kuna wageni waliopo Bungeni asubuhi hii:-

Wageni wengine wa Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro; Watendaji na Maafisa kutoka Wizara na Taasisi zake, Kamati ya Siasa ya Mkoa wa Ruvuma na Maafisa wa *National Microfinance Bank.*

Mheshimiwa Ndumbaro hiyo safari ya Morocco kuna baadhi ya viongozi wapo pale juu, wewe unawajua. Waongeze kwenye orodha hiyo, mimi ninakuruhusu. Sitaki kuwataja, waende huko Morocco wakatazame mambo. *(Makofi/Kicheko)*

Mgeni wa Mheshimiwa Priscus Tarimo, rafiki na ndugu Maxwell Machange, Mzee Shayo kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Sasa, ninamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti. *(Makofi)*

**MHE. ZAYTUN S. SWAI K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, ninaomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bajeti Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama, Fungu 40 kwa mwaka wa fedha 2024/2025, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Vilevile, ninaomba Taarifa hii yote iingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahakama ya Tanzania ni moja kati ya Mihimili mitatu ya Dola na majukumu yake makubwa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ni kutafsiri Sheria na kutolea maamuzi mashauri mbalimbali yanayoletwa Mahakamani. Aidha, Ibara ya 107(1) (A) ya Katiba, imeipa Mahakama Mamlaka ya kuwa chombo pekee cha usimamizi wa utoaji haki na chenye mamlaka ya mwisho katika kutekelezaji wa utoaji wa haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo tarehe 5 Aprili, 2025 historia iliwekwa katika Mhimili wa Mahakama, ambapo Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alizindua rasmi Jengo la Makao Makuu ya Mahakama ya Tanzania. Uzinduzi wa Jengo hilo ni hatua kubwa kwa historia ya Mhimili huu nchini kufuatia ukweli kwamba, Mhimili huo haukuwahi kuwa na Jengo la Makao Makuu kwa kipindi cha miaka 104 tangu kuanzishwa kwake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jengo hilo ni la kipekee na ni kubwa zaidi Barani Afrika kati ya majengo ya Makao Makuu ya Mahakama na kushika nafasi ya sita kwa ukubwa duniani. Kamati inapenda kutoa pongezi zake za dhati kwa Serikali ya Awamu ya Sita, chini ya Rais wake Jemedari Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuthamini suala la utoaji haki kwa Wananchi wa Tanzania. Hakika ametekeleza falsafa yake ya *4R* kwa vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa hii inatoa tathmini ya utekelezaji wa Bajeti na Majukumu ya Mfuko wa Mahakama kuanzia Mwezi Julai, 2024 hadi kufikia Tarehe 22 Aprili, 2025 pamoja na vipaumbele na masuala muhimu yanayopendekezwa katika Mpango na Bajeti ya Mfuko wa Mahakama kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mapitio ya utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama kwa Mwaka 2024/2025. Katika mwaka wa fedha 2024/2025 Mfuko wa Mahakama uliidhinishiwa na Bunge jumla ya shilingi bilioni 241.6 kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 71.9 ni mishahara ya Mahakama, shilingi 2.6 mishahara ya Chuo cha Uongozi wa Mahakama, Lushoto na shilingi bilioni 78.6 ni, kwa ajili ya matumizi mengineyo *(OC)*. Aidha, fedha za maendeleo zilizoidhinishwa ni shilingi bilioni 88.4 ambapo, shilingi bilioni 31 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 57.4 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi tarehe 22 Aprili, 2025 Mfuko wa Mahakama ulikuwa umepokea jumla ya shilingi bilioni 182.9 sawa na 75.74% ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Kati ya fedha hizo zilizopokelewa shilingi bilioni 60.2 zilikuwa ni, kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 75.7, kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa fedha za maendeleo, fedha zilizopokelewa katika kipindi hicho ni jumla ya shilingi bilioni 47. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 9.9 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 37 ni fedha za nje. Mwenendo wa utekelezaji Bajeti ya Mfuko wa Mahakama kwa mwaka wa fedha 2024/2025 umeainishwa katika Jedwali Na.1, kama Taarifa ya Kamati inavyoonesha.

Mheshimiwa Spika, asilimia kubwa ya fedha zilizopokelewa ni fedha, kwa ajili ya matumizi mengineyo ambazo zimetolewa kwa 96.33%. Ufanisi huo umetokana na Serikali kuendelea kutoa fedha, kwa ajili ya kugharamia mahitaji maalum ya Mahakama. Mahitaji hayo ni kama vile kugharamia stahiki mbalimbali za majaji wapya walioteuliwa, pamoja na kugharamia mashauri ambayo yana maslahi mapana kwa Taifa, ambayo hayakuwa sehemu ya mipango na Bajeti ya Mahakama kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kutoa fedha kwa Fungu hili, pale ambapo mahitaji ya ziada na ya lazima yanapojitokeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Mfuko wa Mahakama ulipanga kukusanya maduhuli yenye jumla ya shilingi bilioni 12.5. Hadi tarehe 22 Aprili, 2025 jumla ya shilingi bilioni 8.9 zilikusanywa, sawa na 71.22% ya lengo. Kwa kuwa, maduhuli ya Mahakama yanakusanywa kutoka kwenye vyanzo viwili vya msingi ambavyo ni faini na Ada za Mahakama, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa, viwango hivyo hususan Ada za Mahakama vinaendelea kuwa chini na rafiki, ili wananchi wengi waweze kupata haki wanayostahili na siyo kukwamishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Mafanikio na Changamoto ya Utekelezaji wa Majukumu ya Mahakama kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Katika mwaka wa fedha 2024/2025, Mfuko wa Mahakama umefanikiwa kutekeleza masuala yafuatayo:-

a) Utatuzi wa Mashauri na Mkakati wa Kumaliza Mashauri ya Muda Mrefu; *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwezi Julai, 2024 hadi Aprili, 2025, Mahakama ilikuwa na jumla ya mashauri 191,617. Kati ya mashauri hayo mashauri 63,050 ni ya zamani yaliyovuka mwaka 2023/2024 na mashauri 128,567 ni mashauri mapya yaliyofunguliwa katika kipindi husika. Kati ya mashauri yote, mashauri 140,986 yalihitimishwa katika kipindi tajwa na mashauri 50,631 yalikuwa yanaendelea kusikilizwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kati ya mashauri yote yaliyobaki Mahakamani, mashauri yenye umri mrefu ni 1,724 sawa na 3% ambapo, Mahakama inaendelea na mkakati wa kumaliza mashauri hayo. Kiwango cha mashauri ya muda mrefu yaliyobaki mahakamani yanaifanya Mahakama ya Tanzania kuongoza Barani Afrika kwa kuwa na kiwango kidogo cha mashauri ya muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Mahakama kuwa ni Mahakama inayoongoza Afrika kwa kuwa na kiwango cha chini cha mashauri yenye muda mrefu. Mafanikio haya kwa kiasi kikubwa yamechagizwa na matumizi ya TEHAMA, ikiwa ni pamoja na matumizi ya Akili Mnemba *(Artificial Intelligence)* katika kutafsiri na kuandika hukumu, ambapo Mahakama imewekeza kwa kiasi kikubwa na hivyo kusaidia kusikiliza na kuhitimisha mashauri. Hatua hii imesababisha Mahakama kuongoza kwa Afrika na kushika nafasi ya pili duniani, baada ya Jamhuri ya Kazakhstan.

b) Kuboresha Mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano Kama Nyenzo Muhimu ya Kuboresha Utoaji Haki;

Mheshimiwa Spika, Mahakama imekuwa inatumia mifumo mbalimbali ya TEHAMA katika utekelezaji wa majukumu yake. Mfano, Mfumo wa Usikilizaji Mashauri; Mfumo wa Kunukuu na Kutafsiri Mwenendo wa Mashauri na Mfumo wa Takwimu *(Data Hub)*. Matumizi ya Mifumo ya TEHAMA imeifanya Mahakama kuwa miongoni mwa Mahakama zinazoongoza Afrika kwa kutumia Mifumo ya TEHAMA katika majukumu yake. Matumizi ya TEHAMA yameonesha mafanikio makubwa, siyo tu katika kushughulikia mashauri ya Mahakama, lakini pia, katika kuokoa muda na baadhi ya gharama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Mahakama kwa kuwa mfano mzuri wa matumizi ya TEHAMA na hivyo inashauri taasisi nyingine, hususan zile zinazofanya kazi pamoja na Mahakama kuiga mfano huo.

c) Kuboresha Upatikanaji wa Kumbukumbu na Taarifa kwa Wakati.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025, Mahakama ilifanya zoezi la kutunza kumbukumbu za mashauri ya jinai na madai katika mfumo wa kidigitali kwa Mahakama ya Rufani na Mahakama Kuu, Kanda ya Dar es Salaam, zilizozalishwa katika kipindi cha ukoloni (1920 – 1960). Kulingana na Taarifa ya Mahakama, jumla ya majalada 13,095 yenye kurasa 326,474 yamebadilishwa kwenda kwenye mfumo wa kidigitali. Kamati inaipongeza Mahakama kwa hatua hii muhimu kwa nchi yetu ukizingatia kuwa, kumbukumbu hizo ni za kudumu na zimebeba historia ya Mahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahakama pia imeendelea na utekelezaji wa Mpango wa Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Mahakama wa Miaka Mitano, ambapo hadi kufikia Aprili 2025 Miradi imefikia katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Kwa kuwa, Mpango wa Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Mahakama unahitimishwa mwaka 2025/2026, Mahakama imepanga kufanya tathmini ya utekelezaji wa mpango huo mwezi Septemba, 2025, kwa lengo la kupata hali ya utekelezaji wa mpango pamoja na kufanya maandalizi ya kuwa na Mpango Mpya wa Ujenzi kwa mwaka 2026/2027 ambao utaenda sambamba na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano chini ya Dira ya Taifa ya Maendeleo (2050).

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Changamoto; pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa majukumu ya Mahakama kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Mfuko wa Mahakama unaendelea kukabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(a) Upungufu wa watumishi kwa kada mbalimbali;

(b) Ufinyu wa Bajeti ya Matumizi Mengineyo kukidhi mahitaji ya huduma zilizoongezeka pamoja na uanzishwaji wa Mahakama mpya katika baadhi ya mikoa;

(c) Uhaba na uchakavu wa majengo ya ofisi na makazi ya Mahakimu na Majaji hususan katika Mahakama za Mwanzo na Wilaya; na

(d) Upungufu wa vitendea kazi hususan magari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko wa Mahakama kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Mfuko wa Mahakama umetengewa jumla ya shilingi bilioni 321, sawa na ongezeko la 32.89% ikilinganishwa na Bajeti ya mwaka 2024/2025 ya shilingi bilioni 241.6. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 82.1 ni, kwa ajili ya mishahara ya Mahakama, shilingi bilioni 2.6 ni, kwa ajili ya mishahara ya Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto na shilingi bilioni 143.4 ni, kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, fedha za matumizi ya maendeleo zilizotengwa ni shilingi bilioni 93. Kati ya fedha hizo shilingi biloni18.6 ni fedha za ndani na shilingi 74.4 ni fedha za nje. Mchanganuo wa ongezeko la bajeti umeainishwa kwenye Jedwali la pili, kama Taarifa ya Kamati inavyoonesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti hiyo imeongezeka, ili kukidhi mahitaji muhimu ya huduma mbalimbali za utolewaji haki kutokana na kuanzishwa kwa Mahakama mpya katika baadhi ya mikoa, ununuzi wa magari, uendeshaji wa mashauri ya uchaguzi pamoja na kugharamia stahiki za msingi za majaji wapya walioteuliwa na mahakimu. Hatua hii inaonesha dhamira ya dhati ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuhakikisha kwamba, Watanzania wanapata haki na kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2024/25 Mahakama ilitarajia kuajiri watumishi 1,562. Hadi Tarehe 22 Aprili, 2025, Mahakama imepata vibali vya kuajiri watumishi wapya 545 na watumishi wa ajira mbadala 216 na hivyo kuwa na upungufu wa watumishi 1,071. Vilevile, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Mahakama ilitenga nafasi za kupandisha vyeo watumishi 2,464 na kuwabadilisha Kada watumishi 64. Hata hivyo, Mahakama

imeshindwa kutekeleza suala hili kutokana na kuchelewa kupata vibali vya kupandisha vyeo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Mahakama imepanga kuajiri jumla ya watumishi 522. Idadi hii bado haikidhi mahitaji halisi ya watumishi 10,351 wanaohitajika ambapo hivi sasa kuna watumishi 6,070 tu. Pamoja na uwekezaji mkubwa uliofanywa na Mahakama katika TEHAMA unaosaidia kupunguza changamoto za upungufu wa watumishi bado uhitaji wa watumishi ni mkubwa kutokana na ongezeko la Mahakama mpya kufuatia kupanuka kwa huduma kulingana na uhitaji uliopo, ambapo kwa sasa upungufu ni watumishi 4,281. Kada zenye upungufu mkubwa ni Afisa TEHAMA, Afisa Hesabu, Msaidizi wa Hesabu, Walinzi, Wasaidizi wa Ofisi na Mahakimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa upatikanaji wa nafasi za kuajiri unategemea idhini ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora, Kamati inaishauri Serikali kutoa kipaumbele kwa Mhimili huu muhimu kwa utolewaji wa haki. Ujenzi wa majengo ya Mahakama utakuwa hauna maana endapo kuna uhaba wa rasilimali watu katika maeneo mbalimbali nchini kuendesha vituo hivyo. Aidha, ujenzi wa majengo hayo uende sambamba na upatikanaji wa watumishi wa kutosha na vitendea kazi ili juhudi hizo zilete matunda yaliyokusudiwa na kuongeza ufanisi na utendaji kazi wa Mahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upungufu wa magari. Katika kutekeleza majukumu yake, Muhimili wa Mahakama unahitaji magari ya kutosha. Hata hivyo, idadi iliyopo ya magari takribani 460, idadi ambayo haikidhi mahitaji halisi ya magari yanayohitajika. Aidha, magari yaliyopo mengi ni chakavu na ni ya muda mrefu; ambayo yanahitaji fedha nyingi kwa ajili ya matengenezo na hivyo kuongeza bajeti ya matengenezo. Hadi sasa Mahakama ina upungufu wa magari 40; na katika mwaka wa fedha 2025/2026 Mahakama imepanga kununua magari tisa tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Mahakama umekuwa ukitumia Wakala wa Ununuzi Serikalini *(GPSA)*. Hata hivyo, wakala

huyo amekuwa akichelewa kuwasilisha magari pamoja na kwamba amekwishalipwa. Mathalani kati ya magari 19 yaliyoagizwa mwaka wa fedha 2023/2024 ni magari 13 tu yamekabidhiwa. Hivyo, Kamati inaitaka *GPSA* kuhakikisha kuwa inakabidhi magari hayo haraka iwezekanavyo. Vilevile, Kamati inaiomba Serikali kuangalia uwezekano wa kuiwezesha Mahakama kununua magari mengi zaidi wakati wa mapitio ya utekelezaji wa bajeti katika kipindi cha nusu mwaka ili iweze kutatua changamoto ya upungufu wa magari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upungufu wa Mahakama za Mwanzo. Hadi sasa mahakama za mwanzo zilizopo ni 960 ikilinganishwa na idadi ya kata zilizopo nchini ambazo ni 3,956. Hivyo, kuna uhaba wa mahakama za mwanzo takribani 2,996.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe kuwa takribani asilimia 70.84 ya mashauri yote ya Mahakama yanatoka katika ngazi ya mahakama za mwanzo. Katika mwaka wa fedha 2024/2025, Mahakama ilitarajia kukamilisha ujenzi wa mahakama za mwanzo za Machame (Hai), Ilangala (Ukerewe), Mbalizi (Mbeya) na Kinusi (Mpwapwa). Hata hivyo, kutokana na mwenendo wa utolewaji wa fedha za maendeleo za ndani hadi tarehe 22 Aprili, 2025, hakuna jengo lolote lililokuwa limekamilika. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa inatoa fedha kama zilivyopangwa ili kukamilisha miradi hii kwa wakati ili kupunguza uhaba wa mahakama za mwanzo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia hatua kubwa iliyopigwa na Mahakama katika eneo la matumizi ya TEHAMA, ikiwemo kuwepo na chumba maalum cha mifumo ya kutolea taarifa mbalimbali za Mahakama katika jengo la Mahakama Kuu. Kamati inaishauri Serikali kuona umuhimu wa kuhakikisha kuwa mifumo hii inalindwa, inaendelezwa na inaboreshwa ili iweze kuwa himilivu na kuleta tija iliyokusudiwa. Aidha, suala hilo liende sambamba na mafunzo ya mara kwa mara kwa watumishi wa Mahakama pamoja na kulinda rasilimali watu kwa kuboresha stahiki zao na kuwa na mpango wa kubakiza watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upungufu wa majopo kwa Mahakama ya Rufani. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa kwa asilimia kubwa mlundikano wa mashauri hususan mashauri ya muda mrefu umesababishwa na upungufu wa majopo kwa Mahakama ya Rufani. Mahakama ya Rufani ina jumla ya majopo 12; kila jopo lina wastani wa mashauri 754 kwa mwaka badala ya mashauri 220 kwa mwaka yanayokubalika. Hii inafanya Mahakama ya Rufani kuelemewa na mzigo mkubwa wa mashauri. Hivyo basi, Serikali ione umuhimu wa kuhakikisha kuwa inaongeza majopo ya Mahakama ili kuondokana na changamoto ya mlundikano wa mashauri nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mahakama zilizo katika makasha *(Containerised Courts)*. Kufuatia changamoto za uhaba wa mahakama za mwanzo nchini Kamati inaishauri Mahakama kutumia mfumo wa mahakama za makasha kama suluhu ya muda mfupi wakati Mahakama ikiendelea na mipango ya ujenzi wa Mahakama katika kila kata nchini. Mfumo huu pamoja na kuwa ni wa gharama nafuu utasaidia pia kupunguza mahitaji ya kuwa na Mahakama za Mwanzo katika kila Kata. Vilevile, mfumo huu utapunguza uhitaji wa kusafirisha mahabusu umbali mrefu ili kwenda kusikiliza kesi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mahakama Zinazotembea. Mahakama zinazotembea zimeleta ufanisi mkubwa katika utoaji haki. Tangu kuanzishwa kwake mwaka 2019 hadi tarehe 22 Aprili, 2025, jumla ya mashauri 7,181 yalifunguliwa na mashauri 7,134 yalimalizika, sawa na asilimia 99 ya mashauri yote yaliyofunguliwa kupitia mahakama zinazotembea; na mashauri 47 yanaendelea na usikilizaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, jumla wa wananchi 85,608 wamenufaika na huduma mbalimbali zinazotolewa na Mahakama inayotembea. Hadi sasa kuna jumla ya magari matano ambayo yanatoa huduma katika Mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Tabora, Mbeya na Mwanza. Hivyo basi, Kamati inaishauri Serikali kuongeza idadi ya magari haya, hususan katika maeneo ambayo yana uhitaji mkubwa, ili kusogeza huduma ya utolewaji haki karibu na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujenzi wa vituo jumuishi vya utoaji haki. Kamati inaipongeza Mahakama kwa kuendeleza ujenzi wa vituo jumuishi. Vituo hivi kimsingi vinajumuisha zaidi ya mahakama moja katika jengo moja la ghorofa ambapo ghorofa ya kwanza kunakuwa na Mahakama ya Mwanzo, ghorofa ya pili Mahakama ya Wilaya, ghorofa ya tatu Mahakama Kuu na ghorofa ya nne kunakuwa na Mahakama Kuu pamoja na ofisi za baadhi wa wadau wa Mahakama wakiwemo polisi, ustawi wa jamii, mawakili na waendesha mashtaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu huu wa vituo jumuishi si tu kwamba unarahisisha upatikanaji wa huduma katika eneo moja bali pia umewezesha wananchi kupata haki kwa wakati, kupunguza mrundikano wa mashauri mahakamani, kuongeza kasi ya uondoshaji wa mashauri pamoja na kupunguza gharama za uendeshaji wa mashauri kwa Mahakama na wananchi. Kutokana na mafanikio haya Kamati ingependa kutoa rai kwa Serikali kuendelea kutoa kipaumbele katika ujenzi wa vituo jumuishi kwa kuwa ni hatua muhimu ya kusogeza huduma karibu zaidi na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nihitimishe kwa kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Tulia Akson, Spika wa Bunge na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani pamoja na wewe Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Naibu Spika kwa miongozo yenu katika kuendesha shughuli za Bunge. Aidha nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, Waziri wa Fedha; Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro, Waziri wa Katiba na Sheria; Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, Naibu Waziri wa Fedha; na Mheshimiwa Jumanne Abdallah Sagini, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria kwa ushirikiano wao wakati Kamati inajadili bajeti ya Mfuko wa Mahakama. Aidha, Kamati inamshukuru Dkt. Natu El-maamry Mwamba, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha; Profesa Elisante Ole Gabriel, Mtendaji Mkuu wa Mahakama; pamoja na wataalam wote wa Ofisi ya Mahakama na Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na Kamati wakati wa majadiliano ya Bajeti ya Mfuko huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee ninaomba kumshukuru Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mwenyekiti wa

Kamati na Mheshimiwa Twaha Mpembenwe, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti kwa namna wanavyoiongoza vyema Kamati ya Bajeti. Aidha, ninaomba niwashukuru Wajumbe wote kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati kwa umakini wao katika kujadili na kutoa maoni na mapendekezo mbalimbali kuhusu Bajeti ya Mfuko wa Mahakama. Ninaomba kuwatambua Wajumbe hao kama wanavyoonekana kwenye Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda vilevile kuwashukuru wananchi wa Mkoa wa Arusha na hasa akinamama kwa ushirikiano walionipa muda wote kama Mbunge wa Viti Maalum wa Mkoa wa Arusha. Ninaendelea kuwaomba tuwe pamoja na sitawaangusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuchukua fursa hii kumshukuru Ndugu Baraka Leonard, Katibu wa Bunge kwa niaba ya watumishi wote kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, ninaliomba Bunge lako Tukufu sasa lipokee, lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko wa Mahakama (Fungu 40) kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kama yalivyowasilishwa na Waziri wa Katiba na Sheria yenye jumla ya shilingi 321.1, ambapo kiasi cha Shilingi 82.1 ni kwa ajili ya Mishahara ya Mahakama, shilingi 2.6 ni Mishahara ya Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto *(IJA)*, shilingi 143.3 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na shilingi 93 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

# TAARIFA YA KAMATI YA BAJETI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MFUKO WA MAHAKAMA – FUNGU 40 KWA MWAKA WA FEDHA 2024/25 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/26 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

## 1.0. UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Maoni ya Kamati ya Bajeti, kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama (Fungu 40) kwa mwaka wa fedha 2024/25 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/26.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa kifungu cha 9(1)(c) cha Sheria ya Bajeti Sura ya 439, Kamati ya Bunge ya Bajeti ilikutana na Mheshimiwa Hamad Hassan Chande (Mb), Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Jumanne Abdallah Sagini (Mb), Naibu Waziri wa Katiba na Sheria pamoja na Profesa Elisante Ole Gabriel, Mtendaji Mkuu wa Mahakama ili kufanya mashauriano kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama kwa Mwaka wa Fedha 2024/25 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko huo kwa Mwaka wa Fedha wa 2025/26.

**Mheshimiwa Spika**, Mahakama ya Tanzania ni moja kati ya Mihimili mitatu ya Dola na majukumu yake makubwa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ni kutafsiri Sheria na kutolea maamuzi mashauri mbalimbali yanayoletwa Mahakamani. Aidha, Ibara 107(A) (1) ya Katiba, imeipa Mahakama Mamlaka ya kuwa chombo pekee cha Usimamizi wa utoaji haki na chenye Mamlaka ya mwisho katika kutekeleza utoaji wa haki.

**Mheshimiwa Spika**, mnamo tarehe 05 Aprili, 2025 historia iliwekwa katika Muhimili wa Mahakama, ambapo Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alizindua rasmi Jengo la Makao Makuu ya Mahakama ya Tanzania. Uzinduzi wa Jengo hilo ni hatua kubwa kwa historia ya Muhimili huu nchini kufuatia ukweli kwamba, Muhimili huo

haukuwahi kuwa na jengo la Makao Makuu kwa kipindi cha miaka 104 tangu kuanzishwa kwake. Jengo hilo ni la kipekee na ni kubwa zaidi barani Afrika kati ya majengo ya makao makuu ya mahakama na kushika nafasi ya sita kwa ukubwa duniani. Kamati inapenda kutoa pongezi zake za dhati kwa Serikali ya awamu ya Sita chini ya Rais wake, Jemedari Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuthamini suala la utoaji haki kwa wananchi wa Tanzania. Hakika ametekeleza falsafa yake ya 4R kwa vitendo.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii inatoa tathmini ya utekelezaji wa Bajeti na majukumu ya Mfuko wa Mahakama kuanzia mwezi Julai 2024 hadi kufikia tarehe 22 Aprili, 2025, pamoja na vipaumbele na masuala muhimu yanayopendekezwa katika Mpango na Bajeti ya Mfuko wa Mahakama kwa mwaka wa Fedha 2025/26.

## 2.0. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MFUKO WA MAHAKAMA KWA MWAKA 2024/25

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/25 Mfuko wa Mahakama uliidhinishiwa na Bunge jumla ya **Shilingi 241,599,553,000.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 71,922,320,000** ni mishahara ya Mahakama, **Shilingi 2,616,257,000** ni mishahara ya Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto (Institute of Judiciary Administration - IJA) na **Shilingi 78, 620,476,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC). Aidha, fedha za maendeleo zilizoidhinishwa ni **Shilingi 88,440,500,000** ambapo **Shilingi 31,002,000,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 57,438,500,000** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** hadi tarehe 22 Aprili, 2025 Mfuko wa Mahakama ulikuwa umepokea jumla ya **Shilingi 182,983,483,871.56** sawa na **asilimia 75.74** ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Kati ya fedha zilizopokelewa **Shilingi 60,248,339,676.90** zilikuwa ni kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 75,734,289,786.97** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Kwa upande wa fedha za maendeleo, fedha zilizopokelewa katika kipindi hicho ni jumla ya **Shilingi 47,000,854,408**. Kati ya Fedha hizo **Shilingi 9,992,854,407.69**

ni fedha za ndani na **Shilingi 37,008,000,000** ni fedha za nje. Mwenendo wa utekelezaji Bajeti ya Mfuko wa Mahakama kwa mwaka wa Fedha 2024/25 umeainishwa katika **jedwali Na.1.**

**Jedwali Na. 1: Utekelezaji wa Bajeti ya Fungu 40 kwa mwaka 2024/25 hadi kufikia 22 Aprili 2025**

| Matumizi | Bajetiiliyoidhinishwa 2024/25 | Fedha iliyotolewa hadi 22 Aprili 2025 | Asilimia |
|---|---|---|---|
| Mishahara (Mahakama na IJA) | 74,538,577,000 | 60,248,339,676.90 | 80.83 |
| Matumizi mengineyo | 78, 620,476,000 | 75,734,289,786.97 | 96.33 |
| Fedha za Maendeleo | **88,440,500,000** | **47,000,854,407.69** | **53.14** |
| •Maendeleo Ndani | 31,002,000,000 | 9,992,854,407.69 | 32.23 |
| • Maendeleo Nje | 57,438,500,000 | 37,008,000,000 | 64.43 |
| **JUMLA** | **241,599,553,000** | **182,983,483,871.56** | **75.74** |

***Chanzo*: Randama ya Fungu 40.**

**Mheshimiwa Spika,** asilimia kubwa ya fedha zilizotolewa ni fedha kwa ajili ya matumizi mengineyo ambazo zimetolewa kwa **asilimia 96.33.** Ufanisi huo umetokana na Serikali kuendelea kutoa fedha kwa ajili ya kugharamia mahitaji maalumu ya Mahakama. Mahitaji hayo ni kama vile kugharamia stahiki mbalimbali za majaji wapya walioteuliwa pamoja na kugharamia mashauri ambayo yana maslahi mapana kwa Taifa ambayo hayakuwa sehemu ya mipango na bajeti ya Mahakama kwa mwaka wa fedha 2024/25. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kutoa fedha kwa fungu hili pale ambapo mahitaji ya ziada na ya lazima yanapojitokeza.

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2024/25 Mfuko wa Mahakama ulipanga kukusanya maduhuli yenye jumla ya

**Shilingi 12,571,199,000**. Hadi tarehe 22 Aprili 2025, jumla ya **Shilingi 8,952,973,536.63** zilikusanywa sawa na **asilimia 71.22** ya lengo. Kwa kuwa maduhuli ya Mahakama yanakusanywa kutoka kwenye vyanzo viwili vya msingi ambavyo ni faini na ada za Mahakama ***(Fines and Court Fees),*** Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa viwango hivyo hususan ada za Mahakama vinaendelea kuwa chini na rafiki ili wananchi wengi waweze kupata haki wanayostahili na sio kuwakwamisha.

## 3.0. MAFANIKIO NA CHANGAMOTO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA MAHAKAMA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/25

### 3.1. Mafanikio

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/25, Mfuko wa Mahakama umefanikiwa kutekeleza masuala yafuatayo;

#### a) Utatuzi wa mashauri ya kawaida na mkakati wa kumaliza mashauri ya muda mrefu (*backlog*)

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Mwezi Julai 2024 hadi Aprili, 2025, Mahakama ilikuwa na jumla ya mashauri **191,617**. Kati ya mashauri hayo mashauri **63,050** ni ya zamani yaliyovuka mwaka 2023/24 na mashauri **128,567** ni mashauri mapya yaliyofunguliwa katika kipindi husika. Kati ya mashauri yote **191,617**, mashauri **140,986** yalihitimishwa katika kipindi tajwa na mashauri **50,631** yalikuwa yanaendelea kusikilizwa. Aidha, kati ya mashauri yote yaliyobaki Mahakamani, mashauri yenye umri mrefu (kati ya miezi 6 na miaka 2 kulingana na ngazi ya Mahakama) ni **1,724** sawa na **asilimia 3** ambapo, Mahakama imeandaa mkakati wa kumaliza mashauri hayo. Kiwango cha Mashauri ya Muda mrefu yaliyobaki mahakamani, yanaifanya Mahakama ya Tanzania kuongoza barani Afrika kwa kuwa na kiwango kidogo cha mashauri ya muda mrefu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Mahakama kuwa ni Mahakama inayoongoza Afrika kwa kuwa na kiwango cha chini zaidi cha **asilimia 3** cha mashauri yenye umri mrefu. Mafanikio haya kwa kiasi kikubwa yamechagizwa na matumizi ya TEHAMA

ikiwa ni pamoja na matumizi ya akili mnemba (Artificial Intelligence) katika kutafsiri na kuandika hukumu ambapo Mahakama imewekeza kwa kiasi kikubwa na hivyo kusaidia kusikiliza na kuhitimisha mashauri. Hatua hii imesababisha Mahakama kuongoza kwa Afrika na kushika nafasi ya pili (2) Duniani baada ya Jamhuri ya Kazakhstan.

**b) Kuboresha mifumo ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) kama nyenzo muhimu ya kuboresha utoaji haki.**

**Mheshimiwa Spika,** Mahakama imekuwa inatumia mifumo mbalimbali ya TEHAMA katika utekelezaji wa majukumu yake mfano, Mfumo wa usikilizaji mashauri *(JoT e-CMS);* Mfumo wa Kunukuu na kutafsiri mwenendo wa Mashauri (TTS); na Mfumo wa Takwimu *(Data Hub)*. Matumizi ya mifumo ya TEHAMA imeifanya Mahakama kuwa miongoni mwaMahakama zinazoongoza Afrika kwa kutumia mifumo ya TEHAMA katika majukumu yake. Matumizi ya TEHAMA yameonyesha mafanikio makubwa sio tu katika kushughulikia mashauri ya Mahakama lakini pia katika kuokoa muda na baadhi ya gharama.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Mahakama kwa kuwa mfano mzuri wa matumizi ya TEHAMA na hivyo inaishauri Taasisi zingine hususan zile zinazofanya kazi pamoja na Mahakama kuiga mfano. Matumizi ya TEHAMA yameonyesha mafanikio chanya na kurahisisha utendaji kazi, kuongeza uwazi katika mnyororo wa utoaji haki na kukabiliana na changamoto mbalimbali ikiwemo upungufu wa watumishi.

**c) Kuimarisha uwezo wa Ukaguzi na usimamizi wa shughuli katika ngazi zote za Mahakama na Magereza**.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai, 2024– Aprili, 2025, Ukaguzi wa Mahakama za Hakimu Mkazi, Wilaya na Mwanzo kwa Kanda zote umefanyika kwa **asilimia 99.7**. Vilevile, magereza **103** kati ya **129** yalikaguliwa, sawa na **asilimia 80.2**.

**d) Kuboresha upatikanaji wa Kumbukumbu na taarifa kwa wakati**.

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025, Mahakama, ilifanya zoezi la kutunza kumbukumbu za mashauri ya jinai na madai katika mfumo wa kidigitali kwa Mahakama ya Rufani na Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam zilizozalishwa kipindi cha ukoloni (1920-1960). Kulingana na Taarifa ya Mahakama, jumla ya majalada **13,095** yenye kurasa **326,474** yamebadilishwa kwenda kwenye mfumo wa kidigitali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Mahakama kwa hatua hii muhimu kwa nchi yetu ukizingatia kuwa kumbukumbu hizo ni za kudumu na zimebeba historia ya Mahakama. Aidha, Kamati ilijulishwa kuwa Mahakama kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali mtandao-eGA ipo kwenye maandalizi ya kujenga Mfumo wa uhifadhi wa kumbukumbu hizo (repository) na kwa majalada ya Rufani yanayoendelea hadi sasa zoezi la ujenzi wa mfumo wa uhifadhi wa kumbukumbu linaendelea.

**e) Utekelezaji wa Mpango wa Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Mahakama**.

**Mheshimiwa Spika,** Mahakama imeendelea na utekelezaji wa Mpango wa Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Mahakama wa Miaka Mitano (2021/22–2025/26) ambapo hadi kufikia Aprili 2025 Miradi imefikia katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa Mpango wa Ujenzi na ukarabati wa Miundombinu ya Mahakama unahitimishwa mwaka 2025/26, Mahakama imepanga kufanya tathmini ya utekelezaji wa Mpango huo mwezi Septemba 2025 kwa lengo la kupata hali ya utekelezaji wa mpango pamoja na kufanya maandalizi ya kuwa na Mpango mpya wa Ujenzi kwa mwaka 2026/27 ambao utaenda sambamba na Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano (2026/27- 2030/31) chini ya Dira ya Taifa ya Maendeleo (2050).

**f) Kuimarisha maendeleo ya rasilimali watu**.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025, Mahakama imewezesha watumishi **173** kushiriki mafunzo ya muda mrefu na watumishi **443** kushiriki mafunzo ya muda mfupi. Mafunzo ya muda mfupi yamehusisha mafunzo elekezi, mafunzo ya Uongozi na usimamizi wenye Ufanisi wa Mahakama, mafunzo ya Maadili na Huduma kwa Mteja, mafunzo ya Sheria ya Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi, mafunzo kwa njia ya mtandao *(Virtually)* ya Haki ya Uwakilishi katika Mahakama za Mwanzo na mafunzo kuhusu "*Artificial Inteligence and the Rule of Law*".

**3.2. Changamoto**

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa majukumu ya Mahakama kwa mwaka wa fedha 2024/25, Mfuko wa Mahakama unaendelea kukabiliwa na changamoto zifuatazo: -

a) Upungufu wa watumishi kwa kada mbalimbali;

b) Ufinyu wa bajeti ya Matumizi Mengineyo kukidhi mahitaji ya huduma zilizoongezeka pamoja na uanzishwaji wa Mahakama mpya katika baadhi ya mikoa;

c) Uhaba na uchakavu wa majengo ya ofisi na makazi ya Mahakimu na Majaji hususan katika Mahakama za Mwanzo na Wilaya; na

d) Upungufu wa vitendea kazi hususan magari.

**4.0. MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA MFUKO WA MAHAKAMA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/26**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2025/26, Mfuko wa Mahakama umepanga kutekeleza malengo yaliyoainishwa kwenye Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 hadi 2025/26), Mpango Mkakati wa Mahakama ya

Tanzania wa miaka mitano (2020/21-2024/25) na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti wa Mwaka 2025/26. Maeneo ya kipaumbele katika Bajeti ya 2025/26 kwa Mfuko wa Mahakama ni yafuatayo: -

i. Kuharakisha utatuzi wa mashauri ya kawaida pamoja na kutekeleza mkakati wa kumaliza mashauri ya muda mrefu (*Backlog*);

ii. Kuimarisha uwezo wa Ukaguzi na usimamizi wa shughuli za Mahakama;

iii. Kuendelea kutekeleza Mpango wa Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Mahakama;

iv. Kuboresha mifumo ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) kama nyenzo muhimu ya kuboresha utoaji wa huduma;

v. Kuongeza ushirikiano na wadau wa haki jinai na madai ili kuharakisha huduma ya utoaji haki; na

vi. Kuimarisha maendeleo ya rasilimali watu, ikiwa ni pamoja na kutoa mafunzo, na kuhimiza nidhamu kwa watumishi.

**4.1. Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka 2025/26**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2025/26, Mfuko wa Mahakama umetengewa jumla ya **Shilingi 321,056,230,000** sawa na ongezeko la **asilimia 32.89** ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2024/25 ya **Shilingi 241,599,553,000**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 82,028,785,000** ni kwa ajili ya mishahara ya Mahakama, **Shilingi 2,616,257,000** ni kwa ajili ya mishahara ya Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto (IJA) na **Shilingi 143,385,988,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, fedha za matumizi ya maendeleo zilizotengwa ni **Shilingi 93,025,200,00,** kati ya fedha hizo **Shilingi 18,601,200,000** ni fedha za ndani na **Shilingi**

**74,424,000,000** ni fedha za nje. Mchanganuo wa ongezeko la bajeti umeainishwa kwenye **jedwali Na. 2.**

**Jedwali Na.2. Ulinganisho wa Bajeti ya Fungu 40 kwa mwaka 2024/25 na 2025/26**

| Matumizi | 2024/25 | 2025/26 | Tofauti | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| **Matumizi ya kawaida** | **153,159,053,000** | **228,031,030,000** | **74,871,977,000** | **48.89** |
| **• Mishahara** | **74,538,577,000** | **84,645,042,000** | **10,106,465,000** | **13.56** |
| • Mishahara ya Mahakama | 71,922,320,000 | 82,028,785,000 | 10,106,465,000 | **14.05** |
| • Mishahara ya IJA | 2,616,257,000 | 2,616,257,000 | 0 | **-** |
| **• Matumizi Mengineyo** | **78,620,476,000** | **143,385,988,000** | **64,765,512,000** | **82.38** |
| **Matumizi ya Maendeleo** | **88,440,500 ,000** | **93,025,200,000** | **4,584,700,000** | **5.18** |
| • Ndani | 31,002,000,000 | 18,601,200,000 | -12,400,800,000 | **(40.00)** |
| • Nje | 57,438,500,000 | 74,424,000,000 | 16,985,500,000 | **29.57** |
| **JUMLA** | **241,599,553,000** | **321,056,230,000** | **79,456,677,000** | **32.89** |

*Chanzo: Randama Fungu 40*

**Mheshimiwa Spika,** ongezeka la Bajeti kwa kiasi kikubwa limetokana na ongezeko la fedha za matumizi mengineyo, ambapo zimeongezeka kutoka **Shilingi 78,620,476,000** mwaka 2024/25 hadi **Shilingi 143,385,988,000** mwaka 2025/26 sawa na ongezeko la **asilimia 82.38.** Bajeti hiyo imeongezeka ili kukidhi mahitaji muhimu ya huduma mbalimbali za utolewaji haki kutokana na kuanzishwa kwa Mahakama mpya katika baadhi ya mikoa, ununuzi wa magari, uendeshaji wa mashauri ya uchaguzi pamoja na kugharamia stahiki za msingi za majaji wapya walioteuliwa na mahakimu. Hatua hii inaonyesha dhamira ya dhati ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhakikisha kwamba wananchi wanapata haki na kwa wakati.

### 4.2. Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2025/26 Fungu 40 linatarajia kukusanya maduhuli yenye jumla ya **Shilingi 13,571,199,000** sawa na ongezeko la **asilimia 7.95** ikilinganishwa na **Shilingi 12,571,199,000** za mwaka 2024/25.

## 5.0. MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

### 5.1. Upungufu wa Watumishi

**Mheshimiwa Spika,** changamoto ya uhaba wa watumishi kwa Mahakama si changamoto mpya bali imekuwa ikiripotiwa mara kwa mara. Pamoja na kuwa kila mwaka Mahakama imekuwa ikitarajia kuajiri watumishi wapya ili kuziba pengo la uhaba, suala hilo limekuwa halitekelezeki kama ilivyokuwa imepangwa.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2024/25 Mahakama ilitarajia kuajiri watumishi **1,562.** Hadi tarehe 22 Aprili, 2025, Mahakama imepata vibali vya kuajiri watumishi wapya **545** na watumishi ajira mbadala **216** na hivyo kuwa na upungufu wa watumishi **1,071**. Vilevile, katika mwaka wa fedha 2024/25 Mahakama ilitenga nafasi za kupandisha vyeo watumishi **2,464** na kuwabadilisha Kada watumishi **64**. Hata hivyo, Mahakama imeshindwa kutekeleza suala hilo kutokana na kuchelewa kupata vibali vya kupandisha vyeo.

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2025/26 Mahakama imepanga kuajiri jumla ya watumishi **522.** Idadi hii bado haikidhi mahitaji halisi ya watumishi **10,351** wanaohitajika ambapo hivi sasa kuna watumishi **6,070**. Pamoja na uwekezaji mkubwa uliofanywa na Mahakama katika TEHAMA unaosaidia kupunguza changamoto za upungufu wa watumishi, bado uhitaji wa watumishi ni mkubwa kutokana na ongezeko la Mahakama mpya kufuatia kupanuka kwa huduma kulingana na uhitaji uliopo ambapo kwa sasa upungufu ni watumishi **4,281**. Kada zenye upungufu mkubwa ni Afisa TEHAMA, Afisa Hesabu, Msaidizi wa Hesabu, Walinzi, Wasaidizi wa Ofisi na Mahakimu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa upatikanaji wa nafasi za kuajiri unategemea idhini ya Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora (OR-MUUB), Kamati inaishauri Serikali kutoa kipaumbele kwa Muhimili huu muhimu kwa utolewaji wa haki. Ujenzi wa majengo ya Mahakama utakuwa hauna maana endapo kuna uhaba wa rasilimali watu katika maeneo mbalimbali nchini kuendesha vituo hivyo. Aidha, ujenzi wa majengo hayo uende sambamba na upatikanaji wa watumishi wa kutosha na vitendea kazi ili juhudi hizo zilete matunda yaliyokusudiwa na kuongeza ufanisi na utendaji kazi wa Mahakama.

### 5.2. Upungufu wa Magari

**Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza majukumu yake, Muhimili wa Mahakama unahitaji magari ya kutosha**.** Hata hivyo, idadi iliyopo ya magari takribani **460** haikidhi mahitaji halisi ya magari yanayohitajika. Aidha, magari yaliyopo mengi ni chakavu na ni ya muda mrefu ambayo yanahitaji fedha nyingi kwa ajili ya matengenezo na hivyo kuongeza bajeti ya matengenezo. Hadi sasa Mahakama ina upungufu wa magari **40** na katika mwaka wa fedha 2025/26 Mahakama imepanga kununua magari **9**.

**Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa Mahakama umekuwa ukitumia Wakala wa Ununuzi Serikalini (GPSA). Hata hivyo, wakala huyo amekuwa akichelewa kuwasilisha magari hayo pamoja na kwamba ameshalipwa. Mathalani kati ya magari **19** yaliyoagizwa mwaka wa fedha 2023/24 ni magari **13** tu yamekabidhiwa. Hivyo, Kamati inaitaka GPSA kuhakikisha kuwa inakabidhi magari hayo haraka iwezekanavyo. Vilevile, Kamati inaiomba Serikali kuangalia uwezekano wa kuiwezesha Mahakama kununua magari mengi zaidi wakati wa mapitio ya utekelezaji wa bajeti katika kipindi cha nusu mwaka ili iweze kutatua changamoto ya upungufu wa magari.

### 5.3. Upungufu wa Mahakama za Mwanzo

**Mheshimiwa Spika**, hadi hivi sasa Mahakama za Mwanzo zilizopo ni **960** ikilinganishwa na idadi ya Kata zilizopo nchi nzima

ambazo jumla zipo **3,956.** Hivyo, kuna uhaba wa Mahakama za Mwanzo takribani **2,996.**

**Mheshimiwa Spika,** ikumbukwe kuwa takribani **asilimia 70.84** ya mashauri yote ya Mahakama yanatoka katika ngazi ya Mahakama za Mwanzo. Katika mwaka 2024/25, Mahakama ilitarajia kukamilisha ujenzi wa Mahakama za Mwanzo Machame (Hai), Ilangala (Ukerewe), Mbalizi (Mbeya) na Kinusi (Mpwapwa). Hata hivyo, kutokana na mwenendo wa utolewaji wa fedha za maendeleo za ndani hadi tarehe 22 Aprili 2025 hakuna jengo lolote lililokuwa limekamilika. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa inatoa fedha kama zilivyopangwa ili kukamilisha miradi kwa wakati ili kupunguza uhaba wa Mahakama za mwanzo nchini.

**5.4. Kuendeleza na kutunza Mifumo ya TEHAMA pamoja na kulinda Rasilimali watu wa Mahakama**

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia hatua kubwa iliyopigwa na Mahakama katika eneo la matumizi ya TEHAMA ikiwemo kuwepo na chumba maalum cha mifumo ya kutolea taarifa mbalimbali za Mahakama – "*Judiciary Visual Situation Room*" uliosimikwa katika jengo la Mahakama Kuu. Kamati inaishauri Serikali kuona umuhimu wa kuhakikisha kuwa mifumo hii inalindwa, inaendelezwa na inaboreshwa ili iwe himilivu na kuleta tija iliyokusudiwa. Aidha, suala hilo liende sambamba na mafunzo ya mara kwa mara kwa Watumishi wa Mahakama pamoja na kulinda rasilimali watu kwa kuboresha stahiki zao na kuwa na mpango wa kubakiza watumishi.

**5.5. Upungufu wa Majopo kwa Mahakama ya Rufani**

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa kwa asilimia kubwa mlundikano wa mashauri hususan mashauri ya muda mrefu umesababishwa na upungufu wa majopo kwa Mahakama ya Rufani.

Mahakama ya Rufani ina jumla ya majopo **12** na kila jopo lina wastani wa mashauri **754** kwa mwaka badala ya mashauri

**220** kwa mwaka yanayokubalika. Hii inafanya Mahakama ya Rufani kuelemewa na mzigo mkubwa wa mashauri. Hivyo basi, Serikali ione umuhimu wa kuhakikisha kuwa inaongeza majopo ya Mahakama ili kuondokana na changamoto ya mlundikano wa mashauri nchini.

### *5.6. Mahakama zilizo katika makasha (Containerized courts)*

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia changamoto za uhaba wa Mahakama za Mwanzo nchini, Kamati inaishauri Mahakama kutumia mfumo wa Mahakama za makasha kama suluhu ya muda mfupi wakati Mahakama inaendelea na mipango ya ujenzi wa Mahakama katika kila Kata nchini. Mfumo huu pamoja na kuwa ni wa gharama nafuu, utasaidia pia kupunguza mahitaji ya kuwa na Mahakama za Mwanzo katika kila Kata. Vilevile, mfumo huu utapunguza uhitaji wa kusafirisha mahabusu umbali mrefu ili kwenda kusikiliza kesi zao.

### *5.7.* Mahakama zinazotembea *(Mobile Courts)*

**Mheshimiwa Spika,** Mahakama zinazotembea zimeleta ufanisi mkubwa katika utoaji haki. Tangia kuanzishwa kwake mwaka 2019 hadi tarehe 22 Aprili 2025, jumla ya mashauri **7,181** yalifunguliwa na mashauri **7,134** yalimalizika sawa na **asilimia 99** ya mashauri yote yaliyofunguliwa kupitia Mahakama zinazotembea na Mashauri **47** yanaendelea na usikilizaji. Aidha, jumla wa wananchi **85,608** wamenufaika na huduma mbalimbali zinazotolewa na Mahakama inayotembea. Hadi sasa kuna jumla ya magari **5** ambayo yanatoa huduma katika Mikoa ya Dar-es-salaam, Dodoma, Tabora, Mbeya na Mwanza. Hivyo basi, Kamati inaishauri Serikali kuongeza idadi ya magari haya hususan katika maeneo ambayo yanauhitaji mkubwa ili kusogeza huduma ya utolewaji haki karibu na wananchi.

### 5.8. Ujenzi wa Vituo Jumuishi vya Utoaji Haki

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Mahakama kwa kuendeleza ujenzi wa vituo jumuishi. Vituo hivi kimsingi vinajumuisha zaidi ya Mahakama moja katika jengo moja la

ghorofa ambapo ghorofa ya kwanza kunakuwa na Mahakama ya Mwanzo, ghorofa ya pili Mahakama ya Wilaya, ghorofa ya tatu Mahakama Kuu na ghorofa ya nne kunakuwa na Mahakama Kuu pamoja na Ofisi za baadhi wa wadau wa Mahakama wakiwemo Polisi, Ustawi wa Jamii, Mawakili na Waendesha Mashtaka.

**Mheshimiwa Spika,** utaratibu huu wa vituo jumuishi sio tu unarahisisha upatikanaji wa huduma katika eneo moja lakini pia umewezesha wananchi kupata haki kwa wakati, kupunguza mlundikano wa mashauri mahakamani, kuongeza kasi ya uondoshaji wa mashauri pamoja na kupunguza gharama za uendeshaji wa mashauri kwa Mahakama na za wananchi. Kutokana na mafanikio haya, Kamati ingependa kutoa rai kwa Serikali kuendelea kutoa kipaumbele katika ujenzi wa vituo jumuishi kwakuwa ni hatua muhimu ya kusogeza huduma karibu zaidi na wananchi.

**6.0. HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika,** naomba nihitimishe kwa kukushukuru wewe Mhe. Dkt. Tulia Akson, (Mb) Spika wa Bunge na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani pamoja na Mhe. Mussa Azzan Zungu (Mb), Naibu Spika kwa miongozo yenu katika kuendesha shughuli za Bunge. Aidha nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba (Mb), Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro (Mb), Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Hamad Hassan Chande (Mb), Naibu Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Jumanne Abdallah Sagini (Mb), Naibu Waziri wa Katiba na Sheria kwa ushirikiano wao wakati Kamati inajadili bajeti ya Mfuko wa Mahakama. Aidha, Kamati inamshukuru Dkt. Natu El-maamry Mwamba, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Prof. Elisante Ole Gabriel, Mtendaji Mkuu wa Mahakama pamoja na wataalamu wote wa Ofisi ya Mahakama na Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na Kamati wakati wa majadiliano ya Bajeti ya Mfuko huu.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa umakini wao katika kujadili na kutoa maoni na

mapendekezo mbalimbali kuhusu Bajeti ya Mfuko wa Mahakama. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Oran Manase Njeza, Mb | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe.Twaha Ally Mpembenwe, Mb | M/M/kiti |
| 3. | Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Mb | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Mariam Madalu Nyoka, Mb | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Dkt. Charles Stephen Kimei, Mb | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Josephat Sinkamba Kandege, Mb | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Leah Jeremiah Komanya, Mb | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Juma Hamad Omar, Mb | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Subira Khamis Mgalu, Mb | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Shally Josepha Raymond, Mb | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Stella Alex Ikupa, Mb | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Jonas William Mbunda, Mb | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Kwagilwa Reuben Nhamanilo, Mb | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Bahati Khamis Kombo, Mb | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Vedastus Manyinyi Mathayo, Mb | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Omar Ali Omar, Mb | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Zaytun Seif Swai,Mb | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Rashid Abdallah Rashid, Mb | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Joseph Zacharius Kamonga, Mb | Mjumbe |
| 20. | Mhe. Bahati Keneth Ndingo, Mb | Mjumbe |
| 21. | Mhe. Yahya Ally Mhata, Mb | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Ndg. Baraka I. Leonard, Katibu wa Bunge kwa niaba ya Watumishi wote kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako tukufu sasa lipokee, lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko wa Mahakama (Fungu 40) kwa Mwaka wa Fedha 2025/26 kama yalivyowasilishwa na Waziri wa Katiba na Sheria yenye jumla ya **Shilingi 321,056,230,000** ambapo kiasi cha **Shilingi 82,028,785,000** ni kwa ajili ya Mishahara ya Mahakama, **Shilingi 2,616,257,000** ni Mishahara ya Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto (IJA), **Shilingi 143,385,988,000** ni

kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **Shilingi 93,025,200,000** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Oran Manase Njeza, (Mb)
**MWENYEKITI KAMATI YA BUNGE YA BAJETI**
30 Aprili, 2025

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Sasa tunaanza michango/mijadala. Tunaanza na Mheshimiwa Swalle, wajiandae Mheshimiwa Nahodha na Mheshimiwa Timotheo Mnzava.

**MHE. SHAMSI VUAI NAHODHA:** Mheshimiwa Naibu Spika...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa tuna dharura ninaanza na Mheshimiwa swalle wewe utakuwa wa pili.

**MHE. SHAMSI VUAI NAHODHA:** Naam?

**NAIBU SPIKA:** Anaanza Mheshimiwa Swalle wewe utakuwa wa pili; ana dharura kidogo.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa heshima uliyonipa ili niweze kuwa mchangiaji wa kwanza mchana huu katika Wizara hii ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza, nimesoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri na mimi kama Mbunge wa wananchi wa Jimbo la Lupembe ukisoma katika bajeti hii ya Wizara ya Katiba na Sheria utabaini kwamba Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya *reforms* kubwa sana katika sekta ya sheria hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri, Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Naibu Waziri wake Mheshimiwa Jumanne Sagini, Jaji Mkuu wa Tanzania, Mtendaji Mkuu wa Mahakama, *SG, AG* wetu

na *DPP* kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya chini ya Wizara hii ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma kwenye hotuba hii; miongoni mwa maeneo ambayo Mheshimiwa Rais amekuja na maono makubwa ya kuwasaidia Watanzania ni pamoja na kampeni maalum ya Mama Samia *Legal Aid.* Sisi Wabunge wa vijijini ambao tunajua changamoto za wananchi wetu, ambapo wapo wananchi wengi hawana uwezo wa kuzifikia Mahakama kwa sababu ya umbali pamoja na gharama za kutafuta mawakili kuwa kubwa na pia wapo wanananchi ambao hawajui taratibu za kupata haki zao; Kampeni hii ya Mama Samia *(Mama Samia Legal Aid Campaign)* imekuwa msaada mkubwa sana kwa wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kumwomba Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, tumemwona katika nchi yetu kwenye mikoa mbalimbali akiongoza kwa vitendo kampeni hii; na nimhakikishie Mheshimiwa Waziri, katika awamu yake ameifanya Wizara ya Katiba na Sheria kuwa karibu zaidi na wananchi wa Tanzania. Hongera sana kwake na timu yake yote ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka pia nitoe ushauri kidogo katika eneo hili la msaada wa Mama Samia wa Kisheria. Ili huduma hii iweze kuwa endelevu, pamoja na mipango mizuri ya Wizara hii ninaishauri sana Serikali, wako watu kwenye mikoa na wilaya wanaitwa *paralegal;* hawa watu wana *NGO* mbalimbali. Ninataka nimwombe Mheshimiwa Waziri kwamba atakapokuja ku-*wind up* jioni atuambie wana mpango gani wa kufanya ushirikiano wa kutosha kuwasaidia *paralegal* hawa kuwajengea uwezo wa mafunzo na kuwasaidia vitendea kazi ili huduma hii ya Mama Samia iweze kuwa endelevu leo na vizazi vijavyo. Kwa mfano, Jimbo la Lupembe tunao watu wa *paralegal* pale Nyombo wanaitwa Nyomapace wakiongozwa na mzee wangu Joakim Mwinami pamoja na Lucas Payovela.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda pia kwenye Mkoa wa Njombe tunao watu wa *paralegal* kwenye taasisi kubwa ya

Mapao ikiongozwa na Mchungaji Sinene. Hawa watu wanahitaji kujengewa uwezo sana kupitia Wizara hii. Nimwombe Mheshimiwa Waziri atusaidie. Wengi hawana vifaa kama *computer* na hawana usafiri pia. Tukiwasaidia hawa, kwa kuwa wapo karibu na wananchi wataifanya huduma hii kuwa endelevu na kuwa na msaada zaidi kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, ninataka nitumie nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Lupembe kutoa shukrani maalumu kwa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kujenga Mahakama ya Mwanzo kwa zaidi ya shilingi bilioni moja pale Lupembe Barazani. Mahakama ya Lupembe pale Bararazani ilikuwa imechakaa sana na ilikuwa inavuja lakini Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ametujengea mahakama mpya ambayo itahudumia wananchi wa kata saba za Jimbo la Lupembe. Wananchi Idamba, Mfiriga, Lupembe yenyewe, Matembwe, Ukalawa, Ikondo hadi Kidegembye. Watapata huduma bora katika Mahakama ya Mwanzo ya Lupembe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri na Wizara husika, pia nilishatoa ombi kwa wananchi wa Tarafa kubwa ya Makambako ambao wanaomba kupata Mahakama ya Mwanzo pale Mtwango Barabarani. Mheshimiwa Waziri anapafahamu; anapita kila siku pale, umeshakuwa mji. Wananchi hawa kuna kata tano kubwa wananchi hawa: Kata ya Mtwango, Kichiwa, Ninga, Ikuna, na Igongolo. Wote hawa wanafuata mahakama mbali kule Mkoani Njombe au Makambako. Wanaomba Mahakama ya Mwanzo eneo hili ili wapate ukjaribu wa huduma za kisheria na mashauri yao yaende kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba pia nitumie nafasi hii kuiomba sana Wizara hii iendelee kutoa elimu kwa Watanzania kwamba haki ya kusikilizwa; na mimi nimefanya kazi kwenye sekta mbalimbali ikiwemo sehemu ya sheria; wapo watu hawajui umuhimu wa haki ya kusikilizwa. Wananchi wakiwa na changamoto mbalimbali, nimesoma kwenye hii taarifa, huduma ya Mama Samia imewafikia zaidi ya Watanzania milioni 6.4;

wamesikilizwa kesi zao. Wananchi wakisikilizwa kesi zao hata kama hawatapata ufumbuzi, lakini wanapata amani katika maisha yao. Ni muhimu sana haki ya kusikilizwa ikaendelea kujengewa msingi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ninataka nijielekeze kutoa ushauri kidogo kwenye eneo la haki ya kupiga kura kwa mwaka huu 2025. Ninataka nitumie nafasi hii ndani ya Bunge lako Tukufu kutoa shule kidogo kwa Chama cha CHADEMA na wafuasi wao. Haki ya kupiga kura ni haki ya Mtanzania. Ukisoma kwenye Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 5. Ninaomba nisome kwa manufaa ya wananchi wa Tanzania, inasema "Kila rai awa Tanzania aliyetimiza umri wa miaka 18 anayo haki ya kupiga kura katika uchaguzi nchini Tanzania"

Mheshimiwa Naibu Spika, haki ya kupiga kura ni haki ya uraia wa Tanzania. Hakuna mtu mwenye haki ya kuvuruga haki ya mtu mwingine ya kwenda kupiga kura. Maana yake haki pekee walionayo vyama ambavyo havishiriki uchaguzi, wana haki ya kutokushiriki uchaguzi na wana ya kutokupiga kura wao, lakini hawana haki ya kuzuia Watanzania wengine kupiga kura katika nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, ukisoma Ibara ya 30 ya Katiba hii imeeleza vizuri; kwamba uhuru wa watu wa kutumia haki yao ya kujieleza unapaswa ukome inapoanzia haki ya watu wengine. Mheshimiwa Rais alikuja na *4Rs* katika nchi yetu; zimekuwa ni matunda makubwa; zimefanya *reforms* katika sheria na zimesaidia kuleta utulivu nchini, lakini inaonekana wenzetu wa CHADEMA wamevimbiwa na *4Rs* za Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupata uhuru wa kujieleza na uhuru wa maandamano wameanza kuvuka mipaka kwenda kuvuruga haki za wengine kupiga kura. Ninataka niiombe Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara hii ya Katiba na Sheria, tunaomba mlinde haki zetu sisi Watanzania ambao tupo tayari kwenda kupiga kura Oktoba mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana niliangalia kule Ruvuma – Songea vyama 12 vimekaa vimesema vitashiriki uchaguzi; na sisi Wananchi wa Lupembe kwa kazi nzuri aliyoifanya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuleta maendeleo kwenye maji, shule, ujenzi wa Mahakama na barabara tumejiandaa kwenda kupiga kura. Tunaiomba Serikali isifanye mchezo na jambo hili. Lazima ilinde haki ya sisi Watanzania kwenda kupiga kura Oktoba mwaka huu 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho kwa mchana huu; ninataka pia nitoe wito kwa vyama vyote vya siasa. Kama alivyosema Dkt. Nchimbi kwamba uchaguzi wa mwaka huu siyo uchaguzi wa mwisho, upo uchaguzi mwingine baada ya 2025 watashiriki huo na ziko njia mbili tu za kufanya *reforms* kwenye sheria. Njia ya kwanza unafanya *reform* kupitia Bunge hili. Unaleta sheria ndani ya Bunge kisha unafanya *reform* na njia ya pili kwa mujibu wa sheria za nchi yetu unafanya *reform* kupitia Mahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama iko sheria ambayo haiku sawa Katiba imetoa nafasi ya mtu kwenda Mahakamani ku-*challenge* hiyo sheria ili iweze kurekebishwa. Ipo mifano mingi. Mwaka 2004 Bunge hili lilitunga sheria ambayo haikuwa nzuri, Sheria ya Takrima. Wanaharakati walienda Mahakamani sheria hii ikaondolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka nitoe wito, hatuwezi kufanya *reform* ya sheria kwa kufanya maandamano mtaani Kariakoo. Huwezi kufanya *reform* ya sheria kwa kuhamasisha watu wasiende kupiga kura, *reforms* zinakuja Bungeni.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kengele ya pili imelia ninakuongeza dakika moja.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninakushukuru na ninaunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Nahodha, Mheshimiwa Mnzava na Mheshimiwa Kunambi.

**MHE. SHAMSI VUAI NAHODHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ninaipongeza Wizara kwa kuchukua hatua mbalimbali za kuimarisha utendaji wa idara ya Mahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, napenda kusema kwamba, Idara ya Mahakama imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuimarisha mifumo ya TEHAMA na kutumia Mahakama zinazotembea, ili kuimarisha ufanisi na utendaji wa kesi hasa kwa kutumia mikutano ya kimtandao *(video conference)*. Hapana shaka matumizi haya ya teknolojia ya kisasa katika kuendesha kesi yamesaidia sana katika kupunguza gharama za uendeshaji na usafiri, hasa kwa Mahakimu na washtakiwa mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kwa maoni yangu, dhamira hii ya kutumia mifumo ya kisasa ya kiteknolojia katika kuongeza ufanisi na kupunguza gharama za uendeshaji wa kesi, inakwenda kinyume na dhamira ya kuongeza magari pamoja na matumizi makubwa ya kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika busara ya kawaida, unapokuwa na mifumo ya kisasa ya uendeshaji, matumizi ya magari yanataka kupungua kwa sababu kila magari yanapoongezeka na gharama zinazidi kuongezeka pamoja na ununuzi wa vipuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya pili ambayo nadhani ni vizuri nikaisemea, nafikiri Idara ya Mahakama ina haja ya kuangalia upya uamuzi wa kutaka kuanzisha karakana maalumu ya kutengeneza magari. Kwa maoni yangu, Mahakama ingepeleka magari yake katika karakana za Serikali ili Mahakama ikabakia na jambo lake la msingi la kuendesha kesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mtakubaliana nami kwamba, hivi sasa sisi kama Taifa tuna tatizo moja la msingi, na ni lazima tulisimamie kwa umakini sana. Makubaliano ya mikataba ya miradi yanachukua muda mrefu sana *(negotiation)*. Nimeanza

kusikia taarifa za kufanyiwa kazi miradi ya kusindika Gesi Asilia *(LNG)*, pamoja na Mradi wa Chuma na Makaa ya Mawe Liganga tangu nikiwa Waziri mwaka 2013, mpaka leo bado tuko kwenye mijadala ya mikataba hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua kuna haja ya kuifanyia kazi mikataba hii kwa umakini wa hali ya juu, lakini natambua pia iko tofauti kati ya umakini na kuchelewesha mambo. Athari yake ni nini kuchukua muda mrefu kuidhinisha mikataba hii? Kuna athari mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa duniani unafanyika utafiti wa matumizi ya Gesi ya *Hydrogen* kama chanzo cha nishati. Utafiti huu ukifanikiwa, gesi yetu itabakia chini ya ardhi kama makumbusho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, hivi sasa dunia inafanya utafiti juu ya kupata chanzo mbadala cha kutumia chuma. Badala ya kutumia chuma, watu wanafikiria kutumia madini ya *platinum* na *titanium*. Hilo likifanikiwa, chuma cha Tanzania kitabaki bila kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu, suala la matumizi ya makaa ya mawe kama chanzo cha nishati, hivi sasa dunia inazungumzia juu ya haja ya kutumia nishati iliyo safi. Makubaliano hayo yakifikiwa, basi hapana shaka kwamba makaa ya mawe ya Tanzania yatakuwa hayana matumizi. Ndiyo maana ninasisitiza kuna haja ya kukamilisha miradi hii, na majadiliano haya yakamilike haraka iwezekanavyo, ili miradi hii ianze kufanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mnasaba huo, naiomba sana Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuwapeleka vijana wake (wanasheria) nje ili wapatiwe mafunzo ya vitendo katika masuala ya majadiliano na maridhiano ya mikataba. Hapa sizungumzii shahada; unaweza ukawa na shahada moja, mbili, tatu, lakini weledi ukawa wa kiwango cha chini. Nazungumzia mafunzo ya vitendo ambayo utafundishwa maadili na mitazamo sahihi ya kufanya mambo, ndilo ninalolisisitiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mtakubaliana nami kwamba, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inapaswa kuimarisha kitengo chake cha usuluhishi wa migogoro kati ya wawekezaji na Serikali. Tumekuwa tukipoteza hapa kesi nyingi sana, tunashtakiwa Serikali inapoteza. Hatuwezi kuendelea hivyo, kwa sababu Serikali inapoteza fedha nyingi sana. Ndiyo maana napendekeza kuna haja ya kuimarisha utendaji pamoja na mafunzo ya vijana wetu, ili wawe na weledi na umahiri wa kufanya kazi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Timotheo Mnzava, jiandae Mheshimiwa Kunambi na Mheshimiwa Dkt. Kimei.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami naungana na wenzangu waliotangulia kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria kwa hotuba nzuri ya bajeti ambayo kwa kweli imebeba maono, imebeba mafanikio, lakini imeeleza hali halisi na hatua tuliyopiga kama Taifa kwenye upande wa sekta hizi muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mchango kwenye maeneo machache, kama manne, na kama muda utaruhusu, nitakuwa na mchango kwenye maeneo manne.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la kwanza, natumia nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa na nzuri anayofanya kwenye nchi yetu kwenye sekta zote. Kwenye eneo linalohusiana na hotuba na hoja iliyoko mbele yetu leo, Mheshimiwa Swalle amesema vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli kama kuna jambo limekuja kuwakomboa Watanzania hasa wa vijijini, ambao walilazimika kutafuta fedha nyingi kupata mawakili, lakini kutembea umbali mrefu kupata huduma za kisheria, ni Kampeni ya Mama Samia *(Legal Aid Campaign)*. Jambo hili ni jambo kubwa na zuri, na kwa kweli Wizara ya Katiba na Sheria mnastahili

pongezi. Kwa jambo hili, mmemtengenezea Mheshimiwa Rais *legacy* kubwa sana ya kuacha kwenye Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu na ushauri wangu kwenye eneo hili, kiu ya msaada wa kisheria ni ya muda mrefu sana, na hatimaye sasa tumeona imeanza kufikiwa. Tunaomba jambo hili liwekewe utaratibu wa kuwa jambo endelevu. Ni vizuri kama nchi tukawaza sasa namna ya kuwa na mfuko maalumu kwa ajili ya shughuli za msaada wa kisheria, ili hata kampeni hii ikiisha, si unajua kampeni hii ni mradi; jambo hili liwe endelevu kwa ajili ya kuwasaidia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, ni jambo la Wanakorogwe Vijijini Tarafa ya Bungu, wanatembea zaidi ya kilometa 50 kwenda Korogwe Mjini kufuata huduma za Mahakama. Jambo hili nimelisema muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunalo jengo la Mahakama pale Bungu, lakini ni chakavu, halitumiki. Tuliamua hata kutafuta jengo lingine tuwape wenzetu wa Mahakama ili angalau kuwe na huduma za Kimahakama pale Bungu. Wananchi wanatembea kilometa 50 kufuata viapo, kwenda kusikiliza kesi zao, kupeleka mashauri yao. Jambo hili siyo zuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Wizara, najua Mheshimiwa Waziri ni msikivu, ni mtu mzuri sana, tuwasaidie wananchi wa Tarafa ya Bungu wasitembee hatua nyingi kufuata huduma za Kimahakama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu, natambua kwamba Waziri wetu wa Katiba na Sheria ni Mwenyekiti wa lile Jukwaa la Mawaziri wa *AU*. Najua iko mikataba mikubwa tumeingia, ikiwemo ile *convention* ya kuzuia ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, sijajua sisi kama nchi tumefikia hatua gani kwenye kufuata taratibu zote za msingi ili tuweze kutekeleza mkataba ule. Kubwa ambalo nataka kulisema leo, tunayo timu ya wataalamu, tunao wanaharakati, tunazo Asasi za

Kiraia ambao walianzisha mchakato wa kutengeneza sheria maalumu ya kupinga ukatili wa kijinsia kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, walianzisha mchakato, ninawashukuru sana. Nawapongeza wenzetu wa *TANLAP* ndiyo waliongoza jahazi kwenye kazi hii. Kazi hii ilifanyika vizuri, ilishafika Serikalini. Mara ya mwisho mlisema mko kwenye hatua ya kuangalia, kukusanya maoni ili muweze kuyafanyia kazi. Natamani Mheshimiwa Waziri anapokuja kwenye kuhitimisha hoja, atuambie jambo hili limefikia wapi kama nchi kwenye kutengeneza sheria hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la nne na la mwisho ambalo nataka kuchangia kwa siku ya leo, Wizara ya Katiba na Sheria ndiyo *custodian* wa sheria za nchi hii. Ndiyo mna jukumu la kusimamia sera kwenye maeneo haya. Yako mambo ambayo inawezekana yakawa hayawagusi moja kwa moja Wizara ya Katiba na sheria, lakini hamwezi kukwepa jukumu lenu la kutusaidia kuwapa elimu Watanzania juu ya sheria mbalimbali tunazotunga kwenye nchi yetu ili mambo yawe mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko sana, wako watu wanazunguka huko mtaani wanawahadaa Watanzania, wanawadanganya na wanawaambia kama hakuna mabadiliko hakuna uchaguzi. Kimsingi ukiangalia mabadiliko wanayoyasema ni mabadiliko ambayo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa utashi wake mkubwa wa kisiasa aliamua kuyachukua, akaamua kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ikaleta Bungeni mapendekezo ya Miswada ya sheria tatu, tukafanya kazi ya kuchambua sheria hizo na tukatunga sheria ambayo lengo lake ni kufanya hayo maboresho ambayo hawa wenzetu ndiyo wanapita wanawaambia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali mkiendelea kukaa kimya, wasiokuwa na nia njema na Taifa letu wataendelea kuchafua nchi yetu, wataendelea kuwadanganya Watanzania, wataendelea kuichafua na kuiharibu nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii leo niiombe Serikali, pamoja na kwamba mambo ya uchaguzi ni mambo yanasimamiwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi, lakini jambo la uchaguzi ni jambo la kisheria. Serikali haiwezi kukwepa jukumu lake la msingi la kutoa elimu kuhusu sheria hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana 2024 tumepitisha sheria hapa, tumefanya maboresho makubwa sana. Nataka nitumie nafasi hii ya leo kuyasema ili Watanzania huko nje wajue kwamba Serikali na Bunge lao tulishafanya kazi kwenye eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara ya kwanza kwenye historia ya nchi yetu tumetengeneza Sheria Maalum ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi. Huko nyuma tulikotoka mambo yote ya Tume ya Uchaguzi, zaidi ya kwenye Katiba, lakini pia tulikuwa tunayakuta kwenye Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, kidogo na kwenye Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara ya kwanza kwenye nchi yetu tumetunga sheria maalum inayoshughulika na Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi. Kwenye sheria hii tumefanya maboresho makubwa sana ambayo ndiyo yalikuwa yakipigiwa kelele muda wote. Wenzetu hawa kwa miaka yote wamekuwa wakilalamika juu ya uteuzi wa Wajumbe wa Tume, kwa maana wale Makamishna.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Sheria ya Taifa ya Uchaguzi tuliyoitunga, ukienda Kifungu cha Tano, Sita, na cha Tisa, tumekuja na utaratibu mpya. Yako mambo makubwa matatu yamefanyika kwenye namna ya kuwapata Wajumbe wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza, kwa mara ya kwanza Mheshimiwa Rais pamoja na kupewa mamlaka na Katiba kuteua Wajumbe wa Tume, lakini tumeweka utaratibu mzuri wa kisheria unaoleta uwazi na usawa. Tumetengeneza Kamati ya Usaili ambayo itakuwa na jukumu moja la kupendekeza majina;

Jina la Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwenda kwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, pamoja na Katiba kumpa mamlaka Rais, lakini hayachagui tu mwenyewe. Kuna Kamati ya Usaili inayopendekeza majina kwenda kwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo tumefanya, tumetengeneza utaratibu wa Wajumbe wote wa Tume, kuomba nafasi kwenye Kamati ya Usaili. Kamati ya Usaili inawafanyia usaili, inatoa mapendekezo na kuchagua wale ambao watakuwa wamekidhi vigezo. Zaidi sana, tumeenda mbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii Kamati ya Usaili imewekwa watu ambao kwa nafasi zao, kwa mchakato wa upatikanaji wao, ni watu wasiotiliwa shaka kwenye nchi yetu. Kamati inaongozwa na Jaji Mkuu, inaongozwa na Jaji wa Zanzibar, inaongozwa na Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Unataka watu gani wengine? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda duniani kote huwezi kuutoa kabisa mchakato wa kutengeneza Tume na Serikali iliyopo. Tunaye Rais; hii nchi siyo kwamba ipo tu haina Rais, Rais yupo, huwezi kumtoa; lakini nchi zote wanachotumia ni utaratibu kama huu, unakuwa na Kamati au unapeleka Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi humu tungeweka sheria kwamba Wajumbe wa Tume waletwe wapitishwe Bungeni, bado wangepiga kelele, wangesema Wabunge wengi ni Wabunge wa CCM. Tumeunda Kamati ambayo ina watu kutoka kwenye Vyombo vinavyoaminika, vyenye sifa za kustahili kuwa na haki ya kutenda kazi kwa usawa kwenye nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo tumefanya, muda mrefu tumelalamikiwa kuhusu uteuzi wa Mkurugenzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Kwa mara ya kwanza Mheshimiwa Rais amekubali na tumepitisha sheria Bungeni. Mkurugenzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi hateuliwi tu na Rais mwenyewe, lakini

Tume ya Uchaguzi ndiyo imepewa jukumu la kutafuta na kupendekeza kwa Rais mtu wa kuwa Mkurugenzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Kuna *reform* gani nyingine inahitajika zaidi ya *reform* hizi ambazo zimefanyika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hilo tu, tumekuwa pia na muda mrefu tukilalamikia uteuzi wa wasimamizi wa uchaguzi. Sheria tuliyokuwanayo, Sheria ya Taifa ya Uchaguzi ilikuwa inatamka na kutoa sharti moja kwa moja kwamba, kila Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya, Mkurugenzi wa Manispaa, ndiyo atakuwa Msimamizi wa Uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye sheria hii tumempa nafasi Rais aweze kutafuta mtumishi yeyote wa Umma, Mwandamizi, ambaye mara nyingi huyu atakuwa siyo lazima awe mteule wa Rais, hali ambayo inamwondolea wasiwasi na kumfanya atende kazi hii kwa usawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi sana, kwa mara ya kwanza tumeweka sheria kwamba Msimamizi huyu wa Uchaguzi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa unazungumza mambo muhimu, nakuongeza dakika moja.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeweka kwenye sheria kwamba, msimamizi huyo wa uchaguzi, kuna na sifa ya ziada kwamba, ni lazima awe hajashika nafasi yoyote kwenye chama cha siasa kwa muda usiopungua miaka mitano. Hili ni jambo ambalo ni kubwa na jambo ambalo halikuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia mambo yaliyofanyika ni makubwa. Ukiangalia utaratibu uliowekwa ni utaratibu mzuri. Jambo hili limekaa kwenye namna ya kuwapata watumishi wa

kawaida mpaka wasimamizi wa vituo; mpaka wasimamizi wa vituo vya kuandikisha na vituo vya kupigia kura wanaomba kazi, wanafanyiwa usaili, wanaajiriwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara na niiombe Serikali; kwenye mambo ya msingi kama haya tusiwachekee watu wenye nia mbaya. Kama tumefanya yote haya na bado watu hawaoni, watu hawa wana jambo lao lingine. Tutoe elimu kwa Watanzania wajue ukweli, lakini tusimamie sheria nchi yetu iendelee kuongozwa kwa mujibu wa utaratibu wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kunambi, halafu Mheshimiwa Dkt. Kimei jiandae. *(Makofi)*

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nianze moja kwa moja kumshukuru Mheshimiwa Rais. Sote tunafahamu kuna mvua za masika zinazoendelea sasa na upande wa jimbo langu kule Mlimba, barabara zimekuwa zikiharibika sana, lakini kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kweli namshukuru Mheshimiwa Rais, amechukua hatua. Alimwelekeza Waziri wa Ujenzi kaka yangu Mheshimiwa Ulega, naye ninamshukuru sana. Alipanda helikopta kutoka Dodoma na amekwenda kuchukua hatua kule na Serikali ipo kazini. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nijielekeze kwenye hotuba hii ya bajeti ya leo. Nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa anayofanya, nami ninasema tu kwa dhati, ukiona Mheshimiwa Waziri unateuliwateuliwa kwenye Wizara moja mara mbili, maana yake wewe ni mbobezi katika eneo hilo. Hongera sana, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Rais kwa jambo lingine mahsusi. Jambo kubwa ambalo Mheshimiwa Rais amelifanya ni kukamilisha ujenzi wa Makao Makuu ya Mahakama

yetu ya Tanzania. Jambo hili ni la kumpongeza, kwani ameweka historia katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, namshukuru *His Lordship Prof. Ibrahim Juma,* Jaji Mkuu wa Mahakama yetu Tanzania. Namshukuru kwa sababu moja, amefanya mageuzi makubwa sana kwenye Mhimili huu wa Mahakama. Siyo tu kuhamisha Makao Makuu, kusimamia ujenzi wa Makao Makuu Dodoma, lakini amefanya mageuzi mengi kama vile matumizi ya TEHAMA ambayo inasaidia katika kuharakisha kesi zikamilike kwa wakati na Watanzania wanatendewa haki. Kwa hili, ninampongeza sana Mheshimiwa Prof. Ibrahim Juma, Jaji Mkuu wa Tanzania, hakika atakumbukwa kizazi hata kizazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa ninapompongeza Mheshimiwa Jaji Mkuu, ninanukuu maneno ya Rais wa Awamu ya 26 wa Marekani. Yeye alisema maneno haya, anaitwa Theodore Roosevelt. Anasema maneno haya; *"People don't care how much you know until they know how much you care."* Alikuwa na maana hii, unapopewa dhamana za kuhudumia watu, lazima utimize wajibu wako, kiasi cha kwamba unajali watu. Yaani unaacha matokeo, unaacha alama ili kusudi watu waone kweli wewe ulikuwa unajua katika kutimiza majukumu yako hayo uliyopewa. Sasa kwa hili, Jaji Mkuu wetu amefanya na Theodore Roosevelt anasema maneno haya, nami ninampongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nijielekeze kwenye eneo hili la Kampeni ya Msaada wa Kisheria wa Mama Samia. Yaani kama kuna jambo ambalo sisi Watanzania tuna kila sababu ya kujivunia ni kampeni hii. Wenzangu wamesema, Mheshimiwa Mnzava ameeleza hapa nami ninamuunga mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzishwa kwa Mfuko Maalum wa Msaada wa Kisheria, kimsingi tunaona jambo hili lina tija kwa Watanzania. Sasa, naongeza jambo lingine, kwani kuna dhambi gani tukifanya iwe taasisi kwa mujibu wa sheria? Kwa sababu nafahamu, Mheshimiwa Rais analifanya jambo kwa utashi wake yeye binafsi. Sasa, akienda akapata awamu hii nyingine ya pili

akahitimisha muda wake, sasa je, kampeni hii inakwenda kusimama?

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili lazima kama Serikali mchukue hatua. Tuanzishe taasisi kwa mujibu wa sheria ambayo kizazi hata kizazi kitamkumbuka Mheshimiwa Rais kwa ubunifu mkubwa wa kuwasaidia Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nijielekeze eneo lingine la huo msaada wa kisheria kuimarisha Huduma za Kisheria za Msingi *(Primary Legal Aid)*. Nataka kusema nini hapa? Tunafahamu kwamba pamoja na jitihada za Serikali katika kutoa msaada wa kisheria, kuna baadhi ya maeneo kama vile Magereza, kuna watuhumiwa na wafungwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa naomba ninukuu kundi moja la muziki huko nyuma linaitwa "Majitu", walimshirikisha *Inspector* Haruni, wanasema hivi, "siyo wote wanaokwenda jela wana hatia, wengine wanakwenda kwa kesi za kusingiziwa."

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hizi huduma za misaada ya kisheria zikienda kwenye maeneo kama Magereza, najua zipo, lakini zikaimarishwa, zikawa *funded,* zikawekewa mpango maalum wa fedha ili hawa *paralegal* pamoja na Serikali watengeneze mfumo ambao utafanikisha wafungwa kupata msaada wa kisheria ili waweze kujitetea na wasihukumiwe bila kuwa na hatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni suala la *RITA*. Tunafahamu kazi kubwa wanayofanya *RITA* (Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini), wanafanya kazi nzuri. Leo hii tunaona sasa hivi usajili wa vyeti vya kuzaliwa unafanyika kupitia mtandao. Jambo hili ni jema sana, lakini kwa sisi hasa Wabunge wa Vijijini kama pale Mlimba, mwananchi anayetoka Kata ya Masagati anatembea umbali wa kilometa takribani 223, anakuja Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Kilombero kufuata cheti cha kuzaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni ushauri wangu kwamba Serikali sasa ione haja ya kuwekeza fedha. Taasisi yetu

ya *RITA* ipewe fedha za kutosha ili kusudi vyeti vikiwa tayari, basi viende kwenye Kata zetu na mwananchi apate cheti kwa wakati kwa kutumia gharama nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine niende kwenye Mahakama yetu ya Mwanzo ya Mlimba. Hii naomba Mheshimiwa Waziri atusaidie, na nimpongeze Mheshimiwa Waziri na pia niendelee kumpongeza Mheshimiwa Rais. Jengo lililojengwa pale Mlimba lina hadhi ya kuwa Mahakama ya Wilaya, na limejengwa, na wakati huo lilianza na mzee wangu Mheshimiwa Prof. Kabudi, ndiyo alianzisha ujenzi wa ile Mahakama. Jengo hili ni la kisasa, lina hadhi ya Mahakama ya Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri ikimpendeza pamoja na kwamba Mlimba ni Halmashauri ya Wilaya, tunakwenda kutafuta hadhi ya Wilaya kamili, basi Mahakama itangulie. Ile Mahakama ya Mwanzo ya Mlimba pale ipate hadhi ya kuwa Wilaya, itoe huduma kwa wananchi wale wa Mlimba.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nitoe wito na niwakumbushe ndugu zetu wote ambao wamepata heshima kubwa katika taasisi au vyombo vya dola katika utoaji wa haki. Niwape rai moja, na hapa naomba ninukuu maneno ya Biblia, wakasome Zaburi ya 90:10 inasema maneno haya, "uhai wetu hapa duniani ni miaka 70, tukiwa ni wenye nguvu 80, kiburi chake ni taabu na mateso duniani." Maana yake nini? Duniani tunapita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukipewa jukumu la kutoa haki hebu toa haki vizuri kwa kuzingatia misingi ya sheria, kwa sababu duniani tunapita. Nimesema, na Biblia inasema ukizidi miaka 80 na kuendelea, kiburi chake ni taabu na mateso. Maana yake nini? Hata suti ya shilingi 1,000,000 ukiwa na miaka 90 huwezi kuvaa. Hata nyama huwezi kutafuna, ndiyo taabu na mateso duniani. Kwa hiyo, duniani maisha yetu ni *temporary. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, Waraka wa Mtume Paulo kwa Wakorinto anasema, "nikiitazama dunia ni ubatili mtupu." Kwa

hiyo, tunavyokwenda kutoa haki iwe katika *level* ya familia, iwe katika *level* ya taasisi za Serikali au Mahakama, tusimamie misingi ya haki tukijua kwamba hapa duniani tumekasimiwa haya majukumu kama neema; tumepewa kwa neema. Sasa hebu tutumie neema hii vizuri kuwatendea haki ambao kimsingi hawana hatia na wanataka kutendewa haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo yaliyopo duniani tuwe na mali, tuwe na fedha tutaziacha duniani na tutatangulia mbele za haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja, na itoshe tu kusema tumsaidie Mheshimiwa Waziri bajeti yake ipite kwa sababu nia njema ya Mheshimiwa Rais ni kuimarisha misingi ya haki nchini, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Kimei, ajiandae Mheshimiwa Neema Lugangira, na Mheshimiwa Gulamali, kama kutakuwa na muda.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Niseme hivi kwamba Mama yetu ametupatia elimu, ametupatia afya, ametupatia maji, ametupa bei ndogo za mahitaji yetu kwa ku-*maintain inflation* nchini, ametupatia umeme, ametupatia barabara, ametupatia *freedom of speech,* watu kuzungumza wanavyoweza kuzungumza, na anavumilia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mtu amekupa hayo yote, sasa anakuletea haki kwamba na upate na wewe haki yako pale ambapo kunakuwa na msuguano kati ya binadamu na binadamu, taasisi na taasisi, na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hiyo akapenda pia kwamba atupe safu nzuri kwenye Mhimili wa Mahakama na kwenye Wizara hii ambayo inasimamia masuala mazima ya Sheria na Katiba. Amepanga safu nzuri na ninaamini wote tunampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu, Jaji Mkuu na Mtendaji Mkuu wa Mahakama Mheshimiwa mpendwa

wetu Profesa Elisante Ole Gabriel na watendaji wengine pamoja Majaji na Mahakimu, tumepewa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake ni kwamba huyu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mheshimiwa Rais wetu ni mtu kweli anajali maisha ya binadamu *holistically,* kwa ujumla wake, tunataka kuishi namna gani? Ndiyo maana naamini kwamba anatekeleza kwa vitendo lile lengo la kwamba maendeleo ni maendeleo ya watu na sisi tunaona ya kwamba tunapata maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri tukiangalia, mimi nipo kwenye Kamati ya Bajeti. Kwa hiyo, tumepitisha kwa urahisi sana mapendekezo ya bajeti ya Mahakama. Tumepitisha kwa urahisi kwa sababu inaleta tija na unaona vitendo vikifanyika. Unaona wakitekeleza malengo yao kwa vitendo na kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme, ukiangalia dira yao kusema kweli watapunguza gharama za Mtanzania na mwananchi kufikia kupata haki yake. Pia, watapunguza gharama kwa wananchi kuanzia mdogo mpaka wa juu na taasisi pia kuweza kupata haki kwa gharama nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hiki kimefanyika zaidi kwa kuingiza mageuzi makubwa kwenye *delivery* ya *justice,* utaona kwamba na niseme ndiyo sababu nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na hususan Mtendaji Mkuu. Nampongeza sana kwa sababu mageuzi siyo kitu kinachokubalika kwa binadamu, hata kiumbe mwingine yoyote ambaye ana uhai, tuna *resist* mageuzi kwa sababu tunataka kukaa kwenye *comfort zone*. Sasa watu wanatutoa kwenye *comfort zone,* wewe bado unabaki upo *happy*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utaona kwamba kwenye Mahakama kumetokea mageuzi makubwa ambayo kwa kwa namna yoyote mimi nilifikiri kwa sababu Majaji wengi ni watu wazee kama mimi, (aah, mimi siyo mzee), wangekuwa wana-*resist* haya mageuzi, kwa sababu ni TEHAMA; wanaingiziwa TEHAMA, wanaingizwa kwa *speed* ambayo huwezi ku-*cope* kwa

sababu lazima upate mafunzo, utumie mbinu za kisasa za kuweza kujiingiza kwenye mageuzi yale na kutekeleza wajibu ambao unafanya. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwamba Mahakama wameweza, na niseme kwamba kwa namna ile wameweza kupunguza sasa gharama za kutoa haki, jukumu lao hilo na ni kitu ambacho kusema kweli kinafurahisha sana. Niseme kwamba pamoja na TEHAMA, utaona kwamba Mtendaji Mkuu wa Mahakama ambaye ndiye anafuatilia utekelezaji wa mambo mengine nje tu, siyo pale tu kwenye kutoa haki ameweza kubadilisha sana miundombinu kama tulivyoonesha kwenye ripoti yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, miundombinu ya Mahakama kuanzia Mahakama za Juu, kule juu ameshaweza sana mpaka kwenye Wilaya kwa kiasi, lakini sasa bado kidogo kwa sababu maendeleo ni hatua, bado kidogo kwenye Mahakama za Mwanzo hajaweza kukamilisha dira yake. Hata hivyo, kwenye bajeti ya mwaka huu ambayo tunapendekeza tupitishe, ameweka fedha za kuendeleza mchakato huu wa kuboresha majengo ya kutolea haki kwenye ngazi zote hizo za Wilaya pamoja na za Mwanzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, alikarabati Mahakama moja ya Mwanzo pale kwenye Jimbo langu kwenye Kata ya Kilema Kati ambayo haijakamilika, lakini natumaini atakamilisha. Pia, tuna Mahakama nyingine kwenye Kata ya Mamba Kusini ambayo imekwisha kabisa pamoja na hizo nyingine kwenye Kata nyingine za Mwika, Kata ya Marangu pamoja na Kata za Mkuyuni na kule Kirua Vunjo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kwamba ile pale Kisambu ina matatizo, inatakiwa iangaliwe kwa jicho la kipekee kwa sababu hata Hakimu hamna sasa hivi. Kwa hiyo, naomba kwamba katika changamoto tuliyoona mojawapo kwenye suala zima la utekelezaji wa majukumu ya Mahakama ni upungufu wa watumishi. Wanahitajika watumishi na waliomba kuajiri zaidi ya 1,000, lakini wamepata 600 tu kwa mwaka huu 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kwamba wakati huu unaofuata mamlaka itaweza kukubali waongeze ajira kwenye eneo hilo ambalo ni changamoto kubwa kwa Mahakama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mambo mengine ambayo yamefanyika na ambayo yanafurahisha sana ni uwezo wa Mahakama sasa hivi kutoa *proceedings* za mashauri pamoja na tafsiri zake kwa Kiswahili papo kwa hapo, baada tu ya kukamilika mawasilisho husika. Sasa hiyo wametumia akili mnemba na TEHAMA zinazohusika ili kuweza kufikia lengo hilo. Napongeza sana kusema kweli kwamba mashauri ya muda mrefu yamepungua, na ni kama yamekwisha. Wanasema, "*justice delayed is justice denied.*" Sasa naona hilo kweli wamezingatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri kulikuwa na mashauri ya muda mrefu yaliyozidi mwaka mmoja takribani 60,000 na sasa wameyapunguza mpaka 1,700. Wamepunguza kwa 97%, kwa hiyo, ni kitu ambacho nakipongeza sana na ni jambo ambalo limesaidiwa sana na matumizi njia hii mpya.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kimei, kengele ya pili hiyo.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kengele imelia?

**NAIBU SPIKA:** Ukizungumza vitu vizito muda unakwenda upesi sana.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, basi naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lugangira na tukiwahi Mheshimiwa Gulamali, atachangia.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata fursa ya kuchangia katika bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuanza kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuwa mtetezi wa haki za binadamu namba moja hapa nchini na kwa kuhakikisha kwamba Serikali inaimarisha mazingira ya haki jinai hapa Tanzania, na pia kuharakisha upatikanaji wa haki kwa kuja na hii *Samia Legal Aid Campaign* ambayo imeleta mageuzi makubwa katika kuharakisha upatikanaji wa haki ngazi ya jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tuweze kufikia maono haya ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika eneo hili mahususi la haki jinai, mimi napenda kujielekeza katika maeneo mawili yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la kwanza, ni katika eneo la matukio ya ukatili kwa maana ya ubakaji na ulawiti kwa watoto. Kwa mujibu wa taarifa ya Jukwaa la Haki Jinai Mkoani Kagera, kwa masikitiko makubwa ni kwamba Mkoa wa Kagera kwa mwaka 2024 umeongoza hapa nchini kwa matukio ya ukatili kwa maana ya ubakaji, ukatili na mauaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika, katika mwaka huu wa 2025 kati ya mwezi Januari hadi Machi, 2025, Mkoa wa Kagera tumekuwa na matukio ambayo yameshawasilishwa Mahakamani 67 ya ubakaji na ulawiti wa watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili siyo kwa Mkoa wa Kagera pekee yake, lakini kumekuwa na ongezeko kubwa la matukio ya ubakaji na ulawiti kwa watoto nchini kwetu hapa Tanzania. Kutokana na mianya ambayo ipo, kumekuwa kuna ucheleweshaji na wakati mwingine kutoweka kwa upatikanaji wa haki kwa wahanga wa watoto wa matukio ya ukatili, ubakaji na ulawiti. Kwa hiyo, ningependa kuishauri Serikali kwenye mambo yafutayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, watuhumiwa wa vitendo vya ukatili kwa watoto kwa maana ya ubakaji na ulawiti wasipate dhamana. Haya yaongezwe kwenye makosa ambayo hayapewi dhamana. Nasema hivi kwa sababu, pale ambapo mtuhumiwa wa ubakaji au ulawiti wa mtoto anaporudi katika jamii ile kwa sababu amepewa dhamana, moja ya vitu wanavyokwenda kufanya ni kwenda kuharibu ushahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa pili, yule mtoto kama bado yupo kwenye jamii au ile familia, tunakwenda kumwathiri zaidi kisaikolojia kwa kuendelea kuonana na huyu mtu ambaye ni mtuhumiwa. Tatu, inafifisha jitihada kubwa za Serikali za wananchi kuweza kujitokeza na kuwasilisha mashitaka haya. Kwa hiyo, nisisitize kwa Serikali, ione namna ya kuongeza makosa ya ubakaji na ulawiti kwa watoto kwenye orodha ya makosa ambayo hayapati dhamana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ni kwamba, pale ambapo kunakuwa na kesi za watoto kwenye masuala ya ubakaji na ulawiti zimefikishwa Mahakamani, kumekuwa na desturi ya kesi hizi kuchukua muda mrefu sana. Unakuta mawakili saa nyingine wanaowatetea wale watuhumiwa wanatumia mianya ya kuahirisha kesi mara kwa mara na matokeo yake zile kesi zinakuja ama kushindwa ama kujikuta hata wale ambao ni wahanga wamechoka katika ufuatiliaji wa kesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sana Serikali iweke kwamba inapotokea hizi kesi za ubakaji na ulawiti kwa watoto zisikilizwe ndani ya muda mfupi kwenye Mahakama na haki itendeke kwa maana ya maamuzi ya Mahakama yatolewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kesi itasikilizwa, isikilizwe mara moja au mara mbili, lakini haikubaliki kwamba kesi ya mtoto aliyebakwa ama amelawitiwa ichukue miezi mitatu, miezi sita au miezi saba na wakati mwingine mpaka mwaka jambo ambalo kusema kweli linafifisha jitihada kubwa za Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan za kuimarisha haki jinai na kuimarisha ulinzi wa watoto wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naiomba sana Serikali iweke ukomo wa muda ambao unapaswa utumike katika Mahakama zote hapa nchini kwenye kesi zinazohusu ubakaji na ulawiti kwa watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo langu la pili, ningependa kuchangia katika eneo hili la msaada wa kisheria. Kwanza kabisa napenda kuipongeza sana Serikali kwa namna ambavyo inashirikiana na mashirika ambayo siyo ya Kiserikali *(NGOs)* ambao ndio wanafanya kazi kubwa sana katika kutoa msaada wa kisheria ngazi ya kijamii kwa kushirikiana na wasaidizi wa kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama dhamira yetu ni kuhakikisha kwamba haya matokeo makubwa yaliyopatikana na mafanikio makubwa yaliyopatikana na *Samia Legal Aid Campaign* yawe endelevu, basi napenda kuishauri Serikali kwamba iende itekeleze takwa la kisheria katika maeneo mawili. Sheria inasema kwamba katika kila Kata kuwe kuna wasaidizi wa kisheria, jambo ambalo bado halijatekelezeka. Kwa hiyo, naomba sana Serikali iende ikatekeleze takwa hili la kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili, ni kwamba ili *Samia Legal Aid Campaign* iendelee, lazima kuwe kuna rasilimali fedha na sheria tayari ilishaliona hili, ndiyo maana ikaelekeza kwamba Serikali ianzishe *Legal Aid Fund*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa unyenyekevu mkubwa, naiomba sana Serikali iende kuweka mpango madhubuti wa kuja na *Legal Aid Fund* ili matokeo haya yaliyopatikana na *Samia Legal Aid Campaign* yawe ni endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuhitimisha, naomba nirejee, tena naiomba sana Serikali, watuhumiwa wa makosa ya ubakaji na ulawiti kwa watoto wasipate dhamana. Hali kadhalika, naiomba sana Serikali, muda wa kusikiliza hizi kesi za watoto ambao wamebakwa na kulawitiwa ndani ya Mahakama zitengewe muda mfupi (isikilizwe ama mara moja au mara mbili) na uamuzi wa Mahakama utolewe ili haki ipatikane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la tatu ni kwamba Serikali ihakikishe tuna wasaidizi wa kisheria kama ambavyo sheria inaelekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuhitimisha, Serikali ihakikishe inaanzisha *Legal Aid Fund* ili haya matokeo chanya makubwa tuliyoyapata kupitia *Samia Legal Aid Campaign* yaweze kuwa endelevu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru sana kwa fursa hii na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa naona muda wetu umekwisha. Jioni tutaanza na Waheshimiwa Wafuatao: Mheshimiwa Seif Gulamali, Mheshimiwa Joseph Tadayo, Mheshimiwa Noah Saputu, Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji, na Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo.

Baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 6.58 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirejea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBA WA BUNGE:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Majadiliano yanaendelea. Nilishamtaja Mhshimiwa Seif Khamis Gulamali, jiandae Mheshimiwa Tadayo, atafuatiwa na Mheshimiwa Saputu. Mheshimiwa Gulamali ameenda kusherehekea fainali ya mchongo nini!

Haya, Mheshimiwa Tadayo; na Mheshimiwa Saputu jiandae.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa Bahati ya kupata nafasi hii ya kuwa mchangiaji wa kwanza kwa mchana huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa jinsi ambavyo ameniongoza kuwatumikia wapigakura wangu wa Jimbo la Mwanga kwa kipindi changu hiki cha kwanza cha uongozi ambacho sasa kinaelekea mwishoni ili niweze kuanza cha pili. Namshukuru Mungu kwa ajili hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia namwomba Mwenyezi Mungu kwamba neema na rehema zake ziniongoze katika kipindi cha pili ambacho ninaamini atanijalia, zikuongoze na wewe pamoja na Wabunge wote wa Bunge hili la Kumi na Mbili katika awamu ya 2025 kwenda 2030.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nawashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Mwanga kwa jinsi ambavyo waliniamini na kunipa dhamana. Hiyo peke yake isingetosha, waliendelea kunipa ushirikiano kwa dua na sala ambazo zimeniwezesha kufanya kazi vizuri kwa kipindi chote cha miaka mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nakishukuru chama changu, Chama cha Mapinduzi na Serikali yangu kwa kuniunga mkono na kuniletea miradi mingi sana ambayo imeniwezesha kuwa na mafanikio makubwa ndani ya kipindi hiki. Hata hivi tunavyozungumza, tunaenda mwishoni lakini bado miradi inakuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi uliopita nilipata mradi wa umwagiliaji wa shilingi bilioni 16.874. Huu ni mradi mkubwa na unafanya kazi hii iweze kunoga. Kila nikiangalia bajeti inavyokwenda na mipango ya Serikali, naona kabisa kwamba huko mbele kunafurahisha zaidi. Kwa hiyo, ni vema sote turudi tuendelee kusimamia hizi kazi ambazo zinakuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri, rafiki yangu Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro pamoja na timu yake yote, pamoja na taasisi zinazomzunguka chini ya Mheshimiwa Jaji Mkuu, Mheshimiwa Mtendaji Mkuu wa Mahakama, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wakili Mkuu wa Serikali, Mkurugenzi wa Mashtaka pamoja na wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona kazi nzuri ambayo wamefanya, wamesimamia vizuri uwekezaji mkubwa wa Serikali katika sekta hii ya sheria na utoaji haki. Ujenzi wa miundombinu ya hali ya juu, mikakati katika masuala ya TEHAMA ambayo kwa kweli yameharakisha sana kumalizika kwa kesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sisi ambao tumefanya kazi na Mahakama hii toka miaka mingi kidogo, tunaona tofauti kubwa sana kwamba kwa mara ya kwanza nilipoangalia taarifa za mwaka 2024, idadi ya mahabusu ilikuwa ndogo kuliko wafungwa. Hii inaonesha ufanisi kwenye upande wa Idara ya Mahakama pamoja na wadau wengine wa eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, suala zima la hakijinai. Kwenye hili, kwa kweli Mheshimiwa Rais amefanya kazi ya maana sana, kwa sababu haki jinai ndilo eneo ambalo lina uwezo wa kuichafua sana nchi na kuichafua Serikali kuonekana kwamba watu wananyimwa haki, kwa sababu haki jinai inawagusa watu

wengi sana na watoto wadogo. lakini Tume ya Hakijinai imefanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeiona taarifa yake na nimeona kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwamba sasa inaandaliwa sera ya haki jinai. Nina hakika ikiandaliwa *inline* na ile taarifa, basi hali yetu inaenda kuwa nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, suala la kutafsiri sheria kwa Kiswahili pia litasaidia watu wengi kuzielewa na kwenda mbele. Ukiangalia haya maboresho kwa ujumla, yanasaidia sana lile eneo la haki moja ya msingi sana ya kuifikia haki *(access to justice)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ukitaka kujua vizuri dhana hii jinsi ambavyo ni kubwa ukisoma uamuzi wa Mahakama ya Rufaa kwenye ile kesi ya Julius Francis Ndyanabo maelezo ya Waheshimiwa Majaji wa Mahakama ya Rufaa yaliyotoka ni mazuri sana chini ya aliyekuwa Jaji Mkuu kuonesha jinsi ambavyo haki hii ni ya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila ya kuwa na miundombinu wezeshi yote ya kawaida, majengo na masuala haya ya TEHAMA na elimu, basi haki hiyo ni vigumu sana kuifikia. Pia ukiangalia maboresho haya yamegusa zaidi kwenye upande wa *vocabulary* kwa upande wa Kiswahili, kidogo inanisumbua, *public law*. *The Public Law* ni ile sheria ambayo inahusiana na mahusiano ya Serikali na mtu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa vipi Mamlaka ya Serikali na matendo yake yasimnyime mtu haki? Serikali imewekeza sana kwenye upande huu katika maana kwamba inajaribu kujidhibiti kwamba matendo yake yasiwanyime watu haki. Hili ni jambo la maana sana katika kusimamia utawala wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata kwenye *private law,* mambo ya mikataba yamefanyika, lakini naona kwenye upande wa *public law* ambao hasa ndiyo unagusa haki za msingi za watu, kazi kubwa sana imefanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamezungumziwa sana suala la ujenzi na kufunguliwa kwa jengo la kisasa sana la Mahakama, kwa kweli jambo hili ni kubwa sana na halipaswi kupitwa bila kutajwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jengo hili lenye mita za mraba 63,244 ni la kwanza Afrika kwa ukubwa na jengo la sita kwa dunia, lenye thamani ya shilingi bilioni 127.7, kwa kweli ni jambo ambalo ni la kujivunia sana kwa Tanzania. Linafungua milango kwamba sasa tunayo Mahakama Kuu, Mahakama ya Rufaa inayotarajiwa Makama ya Juu *(Supreme Court)* zikiwa mahali pamoja. Hiyo itarahisisha sana suala zima la uharakishwaji wa haki katika ngazi mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imewekeza fedha nyingi sana katika uboreshaji huu. Kazi inabaki sasa kwa watendaji kuhakikisha kwamba ukubwa huu wa namba moja Afrika usibakie kuwa wa jengo na miundombinu, ila uwe pia wa huduma ambazo zitatolewa pale, kwamba tuwe namba moja Afrika na namba sita Kidunia, uwe na thamani kubwa kama ile thamani ambayo imewekezwa pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ni changamoto kubwa lakini ni changamoto nzuri kwa sababu tukifikia hapo hiyo itakuwa inachochea pia maeneo mengine ya uchumi na maisha ya wananchi wetu kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahakama ina-*deal* na bidhaa isiyoonekana. Hakuna kuuza na kununua pale, ila ile bidhaa ya Mahakama au bidhaa ya sheria na haki kufanyika vizuri, hata hao wanaouza na kununua hawataweza kufanya vizuri. Kwa hiyo, hela yote ambayo imeingia pale kwa kweli inastahili, *it is worth it* lakini sasa tuitendee kazi ili isiwe hasara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mambo ambayo yanapaswa kuendana na uwekezaji huu mkubwa. Kwa mfano, hatutaona faida kubwa sana ya Mahakama ile katika ngazi ya juu kuwa ya thamani ile kama Mahakama za Mwanzo na Wilaya hazitafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimboni kwangu Mwanga nina Mahakama nzuri sana ya Wilaya, wanafanya kazi nzuri, lakini Mahakama za Mwanzo bado ni zile za mkoloni na hizo ndizo zinazohangaika na haki za watu za kila siku. Kwa hiyo, natoa wito tu kwamba uwekezaji pale uendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tarafa inayoitwa Jipendea kwenye Jimbo langu la Mwanga iko Mahakama ya Mwanzo ya kisasa ambayo inatarajiwa kujengwa Kata ya Kwakoa. Naomba sana kwamba tujitahidi, sasa tunakoelekea bajeti ya mwaka huu ile Mahakama sasa ijengwe ili huduma iende moja kwa moja kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, liko suala lingine ambalo ninalisema leo Bungeni, nafikiri ni kwa mara ya tatu toka nimeingia Bungeni. Mabaraza ya Ardhi kuwa chini ya Wizara ya Ardhi hili ni tatizo, kwa sababu kesi nyingi ni za ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza la Ardhi liko chini ya Wizara ya Ardhi wakati migogoro mingi wananchi wanailalamikia hiyo hiyo Wizara ya Ardhi na Watendaji wake, hati yangu imefanywa hivi, *double allocation* na kadhalika. Sasa pale ambapo waamuzi ni waajiriwa wa Wizara ya Ardhi kunakuwa na tatizo. Kwa hiyo, natoa wito kwamba, hilo tulitazame ama turudishe chini ya Mhimili wa Mahakama kwa sababu hata ikiwa chini ya Wizara ya Ardhi, bado rufaa na nafuu nyingine zinarudi tena chini ya Mahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Jaji Mkuu analazimika ku-*deal* na watu ambao hawako chini yake. Hili nadhani ni tatizo ambalo ni vizuri likashughulikiwa. Kwa hiyo, zirudi chini ya Mahakama au basi sheria irekebishwe mtu awe na hiari ya kwenda Baraza la Ardhi au kwenda Mahakama ya kawaida kama ilivyo kuanzia ngazi ya *High Court* kwenda juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo tunapaswa kulifanya ili tuweze kufurahia uwekezaji huu mkubwa ni kwa kadri itakavyowezekana turekebishe sheria zetu za mwenendo *(procedural laws),* na hili wananchi wengi hawatuelewi sisi

wanasheria. Hata *frustration* zinazotokea kwamba mbona kesi zinachelewa wakati mwingine? Ni kwa sababu ya sheria zetu za mwenendo, kidogo kutokuwa rafiki sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi siyo muumini wa kusema kwamba sijui makosa fulani tunyime dhamana mpaka sijui kufanya nini, hapana. Mimi ni muumini wa kusema kwamba haki itendeke kwa haraka, hizo kesi zisikilizwe haraka. Hakuna sababu ya kesi ya kubaka ya kawaida, hizi za watu wazima, *procedure* yake iwe sawasawa na hii *rape* ya watoto wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa sababu ile ya watoto wadogo kitu cha kwanza ni tendo limefanyika; kuna taarifa ya Daktari jambo la pili aliyefanya ni nani? Cha tatu, umri wa mtoto, cheti cha kuzaliwa, habari imeisha. Kwa hiyo, hakuna vita kubwa kama ile ya kusema je, alikubali? Alifikaje hapo? Aliingiaje kwa watu usiku? Na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nayasema hayo bila kusahau juhudi ambazo zimefanyika. Sote tumeona hii kesi ya juzi juzi hapa almaarufu ya afande jinsi ambavyo iliamuliwa kwa haraka. Lile ni jambo ambalo kwa kweli Mahakama na wadau wote wanastahili *credit* ya hali ya juu sana. Wanahitaji sifa na kupongezwa, kazi inafanyika vizuri, lakini bado tuweke mifumo ya kisheria. Tusitegemee lile ambalo lina kelele nyingi ili tuweze kumaliza haya mashauri kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *Mama Samia Legal Aid Campaign* limezungumzwa sana. Kwa nini limezungumzwa sana? Kila mtu anajua haki yake. Shamba hili ni la kwangu kila mtu anajua. Mke huyu ni wa kwangu kila mtu anajua, hata wanyama pia wanajua. Ukimpa mbwa wako chakula, kikishakua nyama ile ni ya kwake, ukijaribu kumnyang'anya, atapambana na wewe. Ninachotaka kusema ni kwamba, kila mtu anajua haki yake.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa kengele ya pili hiyo.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie.

**NAIBU SPIKA:** Haya, malizia.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo ni jinsi ya kupata ile haki, ndicho kitu ambacho huwa kinasumbua.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kampeni hii ya *Legal Aid* kama ya *Mama Samia Legal Aid Clinic,* hii inawafundisha watu jinsi ya kupata haki zao, kwa sababu watu wasipojua utaratibu wa kupata haki zao, maana yake ni kwamba watakimbilia kwenye vurugu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tumpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kuwa *champion* wa kampeni hii kama ambavyo amekuwa *champion* kwenye maeneo mengine makubwa. Tumpongeze sana kwenye hili, na pia nisisitize lile nililosema kwamba kuwe na mfuko ambao utawezesha kazi hiyo iweze kufanyika vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Gulamali karudi. Baada ya Mheshimiwa Gulamali, atakuja Mheshimiwa Saputu na baadaye Mheshimiwa Zahor Mohammed.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia na kuwa mtu wa pili baada ya mwenzangu Mheshimiwa Tadayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambazo amekuwa akizifanya ndani ya nchi yetu, pia amekuwa na utayari katika kutoa fedha ama kuruhusu Wizara mbalimbali kuongezewa fedha ikiwemo hii Wizara ya Katiba na Sheria. Nampongeza sana kwa mabadiliko makubwa ambayo ameyaleta katika sekta ya Mahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, nawapongeza Wizara kwa kusimamia sekta hii ya Wizara ya Katiba na Sheria vizuri. Vilevile, nampongeza Jaji Mkuu, Mtendaji Mkuu wa Mahakama na taasisi zote ambazo ziko chini ya Wizara ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda tu kusema, kwanza namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuja na hii *Mama Samia Legal Aids,* kwani imekuwa ni msaada mkubwa kwa jamii yetu na hasa katika mikoa mbalimbali ambayo nimeweza kutembea na kufika, imewasaidia wananchi ambao kwa namna moja ama nyingine hawana fedha za kuajiri mawakili au wanasheria kupeleka kesi zao Mahakamani au kusimamiwa katika vyombo vya haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia *Mama Samia Legal Aids* imekuwa na msaada mkubwa na bajeti ambayo wanayo ingependeza bajeti yao ya mwakani iongezeke zaidi ili kazi hii iweze kufanyika kwa ukubwa zaidi, iweze kushuka katika Wilaya zetu na iwepo kwa muda mrefu, kwani imekuwa na manufaa makubwa, na watu wengi wanahitaji kupata huduma. Kwa sababu ya ufinyu wa muda, nadhani kwa kuwa pia inazunguka mikoa yote nchi nzima, tukiiongezea bajeti kwa bajeti ya mwakani, itatusaidia kuongeza wigo mpana wa watu kupata haki zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuwa na utayari wa kuleta mabadiliko mbalimbali katika Mahakama zetu. Tumeona Mahakama zilivyobadilika, hasa Mahakama Kuu, katika ngazi ambayo leo kesi mbalimbali zinaendeshwa kwa teknolojia ya hali ya juu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwekezaji mkubwa umefanywa, fedha nyingi zimewekwa na tumeona majengo makubwa hata jengo kuu tuliona juzi Mheshimiwa Rais alizindua, kwa Afrika inawezekana ikawa namba moja na duniani ni namba sita, hongera sana. Huu ni utayari wa kutoa fedha katika uwekezaji, ninaamini fedha hizi katika uwekezaji huu utaenda katika *level* za mikoa, ninajua mikoani pia kuna Mahakama mbalimbali zimebadilishwa ikiwemo Tabora, kuna Mahakama kubwa inajengwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara, katika Wilaya yetu ya Igunga, tuna Mahakama ambayo ni ya Mwanzo, ndiyo imekuwa Mahakama ya Wilaya, nasi tunaomba Wilaya yetu ya Igunga ipate Mahakama yenye hadhi ya kuwa na jengo la Mahakama. Mwakani tuongeze fedha, tujenge Mahakama za Wilaya katika Wilaya mbalimbali nchini ambako hakuna Mahakama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia hata Mahakama za Mwanzo mtuongezee katika ngazi zetu za Vijiji na Kata tupate hizi Mahakama ambazo zitaweza kuwasaidia wananchi kuwapunguzia mzigo mkubwa wa kusafiri kutoka eneo moja kwenda eneo lingine kufuata haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wamekuwa wanasafiri kutoka kilometa zaidi ya 50, 60 mpaka 100 kwenda kusikiliza kesi. Wakati mwingine wanakata tamaa kwa sababu hawana hata fedha za kuwasafirisha kufika kwenye Mahakama hizi. Hii inawapelekea wengine kupoteza haki zao za msingi kwa sababu hawana nauli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Wizara ya Katiba na Sheria watenge fedha kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama za Mwanzo katika Wilaya mbalimbali. Lingine napenda tu kusema tumeona malalamiko, watu wanalalamika juu ya mabadiliko ya sheria mbalimbali za masuala mazima ya uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2024 ilikuwa mwezi wa Kwanza kwenda Bunge la mwezi wa Pili, Mheshimiwa Rais aliruhusu mabadiliko ya sheria za uchaguzi na tukakaa hapa, lakini pia ikatangazwa Tanzania nzima, na wakaitwa wadau, wengine wakaja hapa Bungeni katika Ukumbi wa Msekwa kutoa maoni juu ya namna gani tunaweza tukafanya chaguzi zetu na zikawa bora?

Mheshimiwa Naibu Spika, tumefanya mabadiliko ya sheria tatu za uchaguzi. Tumetengeneza Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi. Tumetengeneza Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani na tumetengeneza Sheria ya Vyama vya Siasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, malalamiko yalikuwepo, na hasa mengi yaliyotolewa yalikuwa yakihusu Wakurugenzi kusimamia uchaguzi, Wajumbe kuteuliwa na Rais, na jina la Tume. Bahati nzuri nami nikiwa mdau katika Kamati ile, wadau mbalimbali na vyama vyote vya kisiasa vilishiriki na wakatoa maoni yao katika kuboresha sheria hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona katika Sheria za Uchaguzi ambayo tulienda kubadilisha, tukabadilisha. Kwanza walisema jina la Tume tulibadilishe, tukabadilisha. Sasa hivi inaitwa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, ambapo walikuwa wanalilalamikia, wanasema hili jina halipo sahihi, tulifanye liwe hivi, tukakubali tukalibadilisha. Hili lilikuwa ni ombi lao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, wakasema Wakurugenzi nao wasiwe sehemu ya kusimamia uchaguzi, na yenyewe tumebadilisha. Sasa hivi tumeweka Maofisa Waandamizi kutoka Halmashauri, watakuwa Wasimamizi wa Uchaguzi, maana yake malalamiko yao yote yamefanyiwa maboresho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia juu ya wateule wanaosimamia uchaguzi katika ile Tume Huru ya Uchaguzi, katika malalamiko yao walisema wote walikuwa wanachaguliwa. Ni kweli, kwa utaratibu wa Sheria ya Uchaguzi, Wajumbe wote walikuwa wanateuliwa na Mheshimiwa Rais, lakini katika maboresho sasa Wajumbe karibu wote wanapitia kwenye usaili.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanapopitia kwenye usaili, ni nani anasimamia usaili wao? Wanaosimamia usaili wa kuwapitisha Wajumbe wa kwenda kusimamia uchaguzi wanasimamiwa na Jaji Mkuu wa Tanzania. Jaji Mkuu ndiye anayewasaili watu wanaotaka kwenda kusimamia kuingia kwenye Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Mjumbe mwingine ni Jaji Mkuu wa Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tuna Jaji Mkuu wa Tanzania, Jaji Mkuu wa Zanzibar na tuna Mwenyekiti wa Haki za Binadamu, naye ni mjumbe katika wale ambao wanakaa kuwasaili Wajumbe watakaokwenda kuwa katika Wajumbe wa

Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Kwa hiyo, unaweza ukaona watu hawa wana uzito na mjumbe mmoja anateuliwa na Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hawa watu wanne wanafanya usaili wa wajumbe kwenda kuingia kwenye Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi. Kwa hiyo, unaweza ukaona hawa wanaofanya usaili kwa nyadhifa zao ni Jaji Mkuu. Nani anamtilia mashaka Jaji Mkuu? Nani anamtilia mashaka Jaji Mkuu wa Zanzibar? Hawa ni watu ambao wana weledi mkubwa. Ni nani anamtilia mashaka Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu? Ni nani anamtilia mashaka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa ndio wanakaa, wanapitia, kuwafanyia usaili Wajumbe wote. Hata Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi wanapitia kwenye hii tume, wanapelekwa kwa Mheshimiwa Rais kuchagua katika wale waliopita kwenye hii Tume ya Usaili, ambayo yuko Jaji Mkuu wa Tanzania, yuko Jaji Mkuu wa Zanzibar, yuko Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa vyama vyote vimeshiriki. Leo kinaibuka chama, mtu amechaguliwa juzi tu kuwa Mwenyekiti, wanasema hatuendi kwenye uchaguzi. Hatuendi kwenye uchaguzi, tufanye nini? Tuvunje Katiba yetu? Katiba inasema nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, Katiba inasema, kila baada ya miaka mitano tufanye uchaguzi. Sasa miaka mitano imeisha, na hili Bunge ni la mwisho, na hapa zimebaki siku chache twende kwenye uchaguzi. Mtu anasema tubadilishe Katiba. Tubadilishe Katiba kwa Bunge gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu Wabunge tuliomo humu muda wetu umeshaisha. Ili tuweze kutengeneza Katiba inayotakiwa na Watanzania, maana yake ni twende kwenye uchaguzi mwaka 2025, tutakaporudi tunaweza sasa tukatengeneza au tukaanza kuunda Bunge la Katiba. Lile Bunge la Katiba ndiyo ambalo litaenda kujadili masuala yote ambayo tunahitaji mabadiliko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nawaomba ambao wanatembea huko, wanasema tusiende kwenye uchaguzi. Maana yake kwanza tunavunja Katiba yetu wenyewe, ambapo ni dhambi kubwa tunayotaka kuitenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Katiba inatuambia tufanye uchaguzi kila baada ya miaka mitano. Sasa, sisi hapa tunaenda ku-*expire* muda wowote. Sasa tunaendaje kutengeneza utaratibu mwingine ambao uko nje ya utaratibu wa Katiba?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nawaomba na Watanzania wafahamu kwamba, Wabunge ndio wana jukumu la kutengeneza hayo maoni. Kwa kuwa, sisi Wabunge muda wetu unaenda kwisha, tuombe Mwenyezi Mungu atujaalie tuweze kurudi. Tukirudi tena hapa tutengeneze utaratibu wa kuwa na Bunge la Katiba, maoni yakachukuliwe kwa Watanzania, yaje yachakatwe na baadaye yapitishwe, kama Watanzania wataridhia katika yale ambayo watu wanayahitaji. Kwa sasa hivi, mwaka huu ni wa uchaguzi na kwa sababu ni mwaka wa uchaguzi, tunaenda kwenye uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba Watanzania wote tujitokeze kwenda kupiga kura, kwenda kuchagua Wabunge na Madiwani na pia, kwenda kumchagua Rais ili sasa jukumu lingine la mabadiliko ambayo tunayahitaji ama wanayahitaji yataenda kupitia kwenye mchakato ambao ni rasmi. Tukisema tu tufanye sasa hivi, tunavunja Katiba yetu, lakini pia, ni nani anakubali kutenda dhambi hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiweza kutenda dhambi hii, tukaenda kienyeji, tukajiongezea muda pasipo kufuata utaratibu, Katiba imeshatuambia ukomo wetu ni miaka mitano. Tukaenda kujivunjia kwa sababu tunaamua tu wenyewe kwamba, tuongeze muda tujitengenezee mazingira, maana yake ni kwamba, tuna miaka mingine tujiongezee kama miwili hapa. Kimsingi itakuwa tunavunja Katiba, kwa hiyo, lazima tuchaguliwe kwanza, turudi, halafu ndiyo utaratibu mwingine uweze kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nawaomba, sana sana, wale wote ambao wanahitaji kutengeneza mabadiliko wanayoyataka ni lazima twende kwenye uchaguzi, ili tuweze kupata sasa yale mabadiliko mengine ambayo watu wanayahitaji. Tofauti na hapo, itakuwa ni jinai; tofauti na hapo ni uasi kwenye Katiba yetu na uvunjaji wa Katiba. Maana yake tukitenda kosa hili, kesho na kesho kutwa mtu anakuja kutokea tu anaamua akae kwenye madaraka hapa miaka 20 au miaka 100 kwa sababu, si tunaichezeachezea Katiba! Ni lazima tuiheshimu. Huu ndiyo Msahafu wetu sisi Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Msahafu huu ndiyo unaotuongoza. Tutafanyaje kazi zetu? Ajira zetu zitakuwaje? Tutafanyaje masuala ya uchaguzi na viongozi watapatikanaje kuanzia ngazi ya kitongoji, ngazi ya kijiji, ngazi ya kata mpaka *level* ya Ubunge pamoja na Rais? Kwa hiyo, huu utaratibu ni lazima tuuheshimu, na ni lazima kama kuna masuala, ambayo yanahitaji maboresho, maana yake sisi Watanzania tuna desturi zetu, tunakaa tunazungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais alivyoruhusu mabadiliko ya Sheria za Uchaguzi, kama ameweza kuongeza wajumbe ambao sasa hawateui yeye, katika wajumbe tisa, wajumbe saba hawateui yeye. Wajumbe wote wanapitia kwenye usaili wa Jaji Mkuu wa Tanzania, wanapitia kwa Jaji Mkuu Kiongozi, wanapitia kwa Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu. Unataka tuwatoe wapi hao wajumbe tofauti na hawa watu wakubwa; tofauti na hawa wabobezi wa Sheria?

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu zangu, na Watanzania kwa ujumla, kwa hiyo, nawaomba kwamba, tufuate utaratibu na tunaamini kwamba, jambo hili tutavuka salama. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuwa na utayari wa kuhakikisha kwamba, tutakwenda kwenye uchaguzi mwaka huu kwa sababu, hana tamaa hiyo. Amesema tutafanya uchaguzi mwaka huu, ili Watanzania wachague Rais wanayemtaka, wachague Mbunge wanayemtaka, wachague Madiwani wanaowataka, ili kazi iweze kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, nakupongeza wewe, na pia, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kutupatia mialiko kwenda kule Morocco. Huu mwaliko tunaujua, tumeupokea, japo fainali ya mchongo, lakini tunaupokea na tutashiriki. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Saputu. Jiandae Mheshimiwa Zahor na Mheshimiwa Salome Makamba, jiandae.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Bajeti hii ya Wizara ya Katiba na Sheria. Nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, yeye ambaye ametupa uzima kwa siku zote hizi kabla ya kuzaliwa kwetu na hata kufikia siku ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa jinsi ambavyo anaendelea kuendeleza Taifa letu na kutuhudumia kwa jinsi ambavyo Mungu anampa afya. Pia, nawapongeza Wizara ya Katiba na Sheria, kwa maana ya Waziri mwenyewe, wasaidizi wake, Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu, kwa jinsi ambavyo wanaendelea kuongoza Wizara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, naipongeza Mahakama yetu ya Tanzania kwa jinsi ambavyo inaendelea kutoa haki kwa wananchi wetu na kuendelea kufanya mhimili huo kuonekana kweli kwamba, ni mhimili unaotoa haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze tu kwa kuipongeza Mahakama ambavyo imejenga jengo ambalo limeshatajwa hapa, ni la sita aidha Barani Afrika au ulimwenguni. Ni jengo zuri na ambalo linaipatia sifa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, naipongeza Mahakama kwa jinsi ambavyo inaendelea kuboresha miundombinu ya Mahakama za Wilaya na za Mwanzo na kujenga Mahakama mpya. Hivyo, hii ni kazi nzuri na njema, ambayo inatekelezwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais anayependa haki kwa wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, ninaomba sasa Mahakama, kwa Maana ya Wizara, ikumbuke kukarabati Mahakama za Mwanzo ambazo zimetelekezwa tangu enzi za ukoloni. Majengo ya ukoloni ndiyo yapo mpaka leo hayajawahi kukarabatiwa, mengine yametelekezwa kabisa na hayo maeneo sasa yanaendelea kuwa hayatumiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kwenye Jimbo langu la Arumeru Magharibi, kuna Mahakama kama tano, kwa maana ya Mahakama ya Emaoi, inahitaji irekebishwe, ifanyiwe marekebisho mazuri ili iweze kutoa huduma, ambapo yenyewe inaendelea kutoa huduma mpaka sasa, lakini jengo hilo ni la zamani sana, la kikoloni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Mahakama ya Kisongo, ambayo imetelekezwa pia, haifanyi kazi kwa sasa. Pia, Mahakama ya Musa katika Kata ya Musa kwa sasa haifanyi kazi na jengo lipo, ni yale majengo ya kikoloni. Mahakama ya Nduruma, yenyewe inafanya kazi kwa sasa, lakini bado ni yale majengo ya zamani sana ya kikoloni. Mahakama ya Ngateu yenyewe sasa haifanyi kazi na ni yale yale majengo ya kikoloni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamaanisha kwamba, kwa kuwa, wakati ule wakoloni walipokuwa wamejenga hizo Mahakama watu walikuwa ni wachache. Kwa sasa watu ni wengi, wananchi wamekuwa wengi, migogoro ni mingi, kesi ni nyingi. Hizi Mahakama za Mwanzo zikifufuliwa zitatengenezea Mahakama yetu kutoa haki kwa haraka na kuifanya Mahakama Kuu na Mahakama nyingine za juu ziweze kuwa zinatoa haki kwa mujibu wa utaratibu zilizojiwekea na wananchi wanapata haki kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni suala la marekebisho ya Sheria. Kuwepo kwa sheria yoyote inatokana na kuhakikisha kwamba, wananchi wanapata haki, lakini pia, kuboresha uchumi wa nchi na kuleta usalama, umoja na mshikamano ndani ya nchi yetu. Jambo hilo limekuwa likifanyika katika nchi yetu mara kwa mara, kama ambavyo inaonekana na inaelezwa kwamba, sheria zinarekebishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kusema, mfano Sheria ya Ardhi. Sheria ya Ardhi inahitaji sasa kuangaliwa, kurekebishwa, kwa sababu, kwa mfano kwenye umiliki wa ardhi inakwambia kwamba, mgeni hamiliki ardhi, lakini ukienda kwa undani zaidi ni kama tu anamiliki ardhi, kwa sababu, mtu ambaye ana *title* ya miaka 99 ni miaka mingapi hiyo? Ni kama anamiliki na baada ya hapo ana uwezo wa kuuza hiyo ardhi kwa kiasi anachotaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ina maana hapo ni kujidanganya kwamba, wageni hawamiliki ardhi, lakini wanamiliki ardhi kwa upande mwingine. Kwa hiyo, hii sheria inatakiwa iangaliwe kwa sababu, bado ni changamoto katika utekelezaji wa umiliki wa ardhi, hasa katika uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Ardhi Na. 4 na Na. 5, kama nilivyosema, bado haitoi ule utaratibu wa umiliki wa ardhi. Inakwambia miaka 99, haiji chini kusema labda mtu amiliki kwa miaka, kwa maana ya wageni, wamiliki kwa miaka mitano, miwili, mitatu. Kwa sababu, huwezi kumwambia mtu leo anamiliki miaka 99 halafu unasema ni mwekezaji, bado hii siyo sawa. Iangaliwe hiyo sheria, hayo maeneo ya umiliki wa ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Sheria ya Uwekezaji *(Tanzania Investment Act),* ambayo ni ya Mwaka 1997 na yenyewe inatakiwa iangaliwe. Kwa mfano, kama kwenye madini tunachukua asilimia tatu, asilimia tatu kwenye madini bado naona ni kidogo, kwa sababu, kama ingewezekana tuongeze na tuangalie sera yetu ya madini, ili tuweze kufanya mabadiliko ya sheria hii, ili iweze kuwa na tija na kujenga uchumi wetu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, madini yamechangia sehemu kubwa sana kwenye uchumi wetu. Sasa hivi iko kwenye 10% ya kuchangia kwenye bajeti ya Taifa. Kwa hiyo, hii nayo iangaliwe, kwa sababu, tukiboresha sheria zetu hizi za kiuchumi tutajenge uchumi wetu wa ndani na kuwafanya wananchi waweze kufurahia rasilimali tuliyonayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakumbuka kwamba, suala la sheria ya utoaji wa haki, kwa maana ya Mabaraza ya Ardhi, kwa kweli yanatakiwa yahamishwe yaende kwenye mkondo wa Kimahakama, jinsi Mahakama ilivyo, kwa sababu, Mabaraza haya hayasimamiwi na mtu yeyote, yanasimamiwa na Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri ana muda mrefu kwenda kuangalia kwamba, hiyo Mahakama inafanya kazi namna gani? Hana muda kwa sababu, ana mambo mengi. Mabaraza haya ndiyo yanatoa haki ya ardhi. Ardhi ni mali ambayo ni muhimu sana kwa wananchi wetu wa Tanzania. Sasa ina maana kwamba, haki inacheleweshwa. Unakuta kwenye Baraza la Ardhi kesi inaweza ikapigwa tarehe miezi sita mbele bila kusikilizwa, mpaka mwaka bila kusikilizwa, lakini ukija kwenye Mahakama za kawaida zina muda wa kusikiliza mashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nadhani hebu muiangalie hii kwa sababu, kwa kweli inawatesa wananchi wengi. Madhumuni ya kuwepo kwa haki ni ili mtu apate haki mapema iwezekanavyo, kama ambavyo Katiba yetu inasema katika ile Ibara ya 107(A), ambapo ukisoma Kifungu cha Kwanza na cha Pili, naomba ninukuu Kifungu (b).

Mheshimiwa Naibu Spika, inasema, "*Not to delay dispensation of justice without reasonable ground.*" Kwa hiyo, Katiba inatusisitiza kwamba, haki lazima itolewe kwa wakati. Aidha, kama umekosa, hiyo ni haki pia; kama umepata, ni haki pia; lakini kuchelewesha haki kwa haya Mabaraza ya Ardhi, pia, naona kwamba, ni uvunjifu wa Katiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuchelewesha haki itakuwa ni kuwanyanyasa wananchi kwa sababu, hawajui pa kwenda zaidi

ya kwenye Mahakama. Kwa hiyo, tunatoa ushauri kwamba, haya Mabaraza sasa imefikia mahali yahamishwe yaende kwenye Mahakama ya kawaida, ili yasimamiwe na Jaji Mkuu na mfumo mzima wa Mahakama. Vinginevyo tutakuwa tunajidanganya zaidi pale ambapo tunasema tunawapa wananchi wetu haki, lakini bado hawapati kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana kuna msemo unasema "*Justice delayed is justice denied.*" Haki iliyochelewa ni sawa na haki iliyonyimwa. Kwa hiyo, naomba kusema, ushauri wetu au ushauri wangu, naomba sana Mabaraza haya yaweze kuangaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la msaada wa kisheria unaotolewa na Mheshimiwa Rais; nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa ubunifu wake na moyo wake huu wa utashi wa kujaribu kuwasaidia Watanzania, na hasa wale maskini ambao hawana uwezo wa kuweka mawakili binafsi, ili waweze kupata haki zao. Suala hili ni muhimu sana liendelee kutiliwa maanani na litengewe bajeti ambayo inatosheleza, ili wale wananchi maskini wapate haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba twende mbali zaidi katika kuanzisha taasisi ambayo inasimamia kusaidia watu maskini, kama ambayo Rais aliweza kuanzisha, kwa sababu, tukiacha hivi, baada ya muda inaweza ikaja ikapotea moja kwa moja, na ni jambo zuri ambalo limeanzishwa na Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sisi wote ambao ni Watanzania, na tunaamini katika kupata haki kwa kila mmoja wetu tunaomba sana sheria hizi, zikiwemo na sheria nyingine ambazo nimezitaja hapa, na sheria nyingine ambazo bado zinakuwa hazitoi haki mapema, lakini bado itakuwa haileti kuchochea uchumi wa Taifa kwa haraka, basi ziangaliwe ili ziweze kurekebishwa kwa haraka kwa sababu Bunge hili lipo kwa kazi hiyo. Pia, ninaamini hakuna kiongozi yeyote ambaye atakataa sheria zisirekebishwe, ambazo zinaleta manufaa kwenye Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zahor Mohamed. Jiandae Mheshimiwa Salome, jiandae Mheshimiwa Suma. *(Makofi)*

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kusimamia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini vilevile kwa kuimarisha vyombo vyetu vya utoaji haki na usimamizi wa haki kwa mujibu wa Katiba, naomba nimpongeze sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kulitekeleza hilo, naomba niungane na wenzangu waliozungumzia *issue* ya *Samia Legal Aid*. Kwa kweli, dhamira ya Mheshimiwa Rais ni nzuri sana, lakini ili tuweze kuiboresha, ninao ushauri kwenye maeneo mawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza ni kwamba, tuhakikishe kwamba, katika tarafa zetu, kwa sababu, kuna tarafa na kata sita mpaka 10, kwa bahati mbaya sana zote hizi zinategemea Mahakama moja ya Mwanzo, jambo ambalo linawafanya wananchi wanakimbia au wanatembea umbali mrefu, ili kutafuta haki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba sana wenzetu waliangalie hili, ili kuweza kutimiza azma ya Mama kuhakikisha kwamba, wananchi wanapata haki zao sawasawa. Kwa maana hiyohiyo, iko hoja ya Mahakimu wetu kuwa na kazi nyingi kwa sababu, Mahakimu ni wachache, kesi ni nyingi, uwezo wetu mdogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sana wataalamu wetu wale wa mambo wanaohusika na Mahakimu wahakikishe kwamba, wanaongeza idadi ya watumishi ambao wataweza kuhudumu, ili iweze kupunguza mlolongo na msongamano wa kesi kwa Mahakimu wetu. Kweli wana kazi kubwa sana na watu hawa ndiyo wanaanza kufuatilia mienendo

ya kesi mpaka waweze kutoa hukumu. Naomba sana Wizara iliangalie hili kwa macho mawili kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kusimamia Wizara hii vizuri, pamoja na taasisi zake zilizo nyingi. Pamoja na hilo, naomba pia kwenye hili Waheshimiwa Wabunge, ni juu yetu kwa sababu, kesi ni nyingi, wananchi wana malalamiko mengi, lakini bado hatujawezesha Wizara hii kupata fedha ya kutosha, ili kufanya Wataalamu wafanye kazi zao vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wenzetu wanaohusika na bajeti, pamoja na bajeti iliyotengwa hapa, ili tuweze kuondoa malalamiko yaliyopo na tuweze kupunguza yatakayokuja, naomba sana tuone ni namna gani tunaweza kuwasaidia kwa kuongeza bajeti kwa sababu, bajeti hii ni ndogo sana kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kwenye ukurasa wa 15 na 16 wa kishkwambi, kwenye bajeti hii, mchanganuo wa matumizi ya kawaida kwa mwaka 2024/2025, kwa mfano, utagundua Ofisi ya Mwanasheria Mkuu mpaka kufikia Februari imepata 49%. Kwenye fedha za maendeleo, hapo hapo tu, wala siendi pengine, imepata asilimia 5.3. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa akili zangu za haraka haraka zinaniambia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ndiyo tunayoitegemea kwenye mambo mengi sana. Kwa hiyo, unapokuwa unaiwezesha kwa staili hii, maana yake ndiyo yale yale aliyosema mtaalamu kwamba, tunachelewesha haki. Tunapochelewesha haki maana yake ni kwamba tumekataa. Kwa hiyo, ombi langu kwenye hili ni bado Serikali ama Wizara iangalie namna gani itaboresha taasisi hizi, ili kuhakikisha wanafanya kazi zao za kutoa haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwenye suala la wananchi kuelewa haki zao kwa sababu, mwaka 2021 Serikali ilianzisha *issue* ya Mahakama Mtandao. Naiomba sana Serikali tuone namna gani tutatoa elimu kwa sababu, inaonekana hata

wanasheria au baadhi ya wanasheria hawajui maana ya neno "Mahakama Mtandao." *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mimi sikusoma sheria, lakini sina hakika kama tumepewa nafasi ya kuamua wapi naweza kusikiliza kesi? Bunge hili na Serikali tumetunga sheria ili kuhakikisha kwamba tunatoa haki ya kila mwananchi kwa haraka iwezekanavyo. Ndiyo maana leo tumeweza kuweka mifumo ya kusikiliza kesi nchi nzima. Wapo watu leo wanadhani hili hawalitambui wakifikiri kwamba hii siyo sheria. hii ni sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu, wenzetu hawa pamoja na kuelewa sheria waendelee kuisoma vizuri sheria kwa sababu haki inatakiwa itolewe popote; uwe Mahakamani ama upo gerezani, iwe wewe ni mfungwa ama wewe ni mshitakiwa bado tunatakiwa tukupe haki yako kwa wakati. Kwa hiyo, Serikali ilipoanzisha Mahakama Mtandao, maana yake ni kwamba imesogeza huduma za Kimahakama kwenye maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana, na Serikali kwenye hili walichukue sana, wafanye kazi ya kutufundisha na kufundisha *public* ili waelewe madhumuni ya kuanzisha Mahakama Mtandao ili kuharakisha utaratibu wa kutoa haki kwa wananchi. Hajapewa mtu mamlaka ya kuamua wapi nataka nikasikilize kesi, hii hakuna. *Unless,* mtuambie kwamba ipo sheria imetungwa kwingine, lakini hapa hatujatunga sheria ya kwamba mimi nataka nisikilize kesi nikiwa nyumbani kwangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sana tuendelee kutoa elimu ili watu waelewe kwamba kwenye hili popote tulipowekewa kwa mujibu wa sheria, ndipo ambapo kesi itaweza kusikilizwa. Kwa maana hiyo hiyo, lengo la Serikali na kwa utaratibu wetu wa kisheria taasisi hii ndiyo inayosimamia haki zote, kwa sababu ina vyombo vingi ambavyo vinasimamia haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ombi langu, naomba sana, kwa sababu inaonekana tunao mlolongo wa kesi nyingi, inaonekana kama vile wananchi hawaelewi haki zao, inaonekana hakuna anayejua haki yangu nitaipata wapi, nikikosa haki?

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile inaonekana kwamba hata wale wanaosaidia kutoa taaluma ya sheria, bado ni wachache. Ombi langu kwa Serikali tutafute namna nzuri ya kuongeza wasaidizi hawa na kuongeza watu ambao wataendelea kutoa taaluma ili wananchi wa kawaida kabisa waweze kuelewa haki zao watazipata wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo, hiyo ajira ,zile za Mahakama ziongezwe ili tuweze kuongeza nafasi na tuweze kutatua matatizo ya haki ya kuwapa wananchi haki zao kwa muda unaostahiki. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Salome, wajiandae Mheshimiwa Suma na Mheshimiwa Neema Gelard.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, umenipa nafasi, nami nichangie Wizara hii muhimu ya Katiba na Sheria. Naomba nianze kwa kunukuu Ibara ya 74 (8) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayosema: *"74.- (8) Bunge laweza kutunga sheria kwa ajili ya kuweka masharti ya kuweka utaratibu wa kusimamia uchaguzi wa Wabunge wanaowakilisha majimbo ya uchaguzi."*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeanza na *quotation* hiyo kwa sababu uongo ukisemwa sana na usipotolewa ufafanuzi, unageuka kuwa kweli. Yapo maneno ambayo yanajaribu kupotosha kwamba kitendo cha Bunge na Tume ya Uchaguzi kuwalazimisha vyama vya siasa kusaini Kanuni za Maadili ni kinyume na Katiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 74(8) ya Katiba, baada ya kutoa mamlaka yao kwa Bunge, mwaka 2024 Bunge hili Tukufu nami nikiwa sehemu ya Wabunge tulitunga sheria mbili. Ieleweke

kwamba utungaji wa sheria hizi mbili ulipelekea kufutwa kwa sheria kubwa mbili. Sheria ya Tume ya Uchaguzi ya Mwaka 1985 na Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ya Mwaka 1979. Tukatunga sheria na kupitia sheria hiyo tukasema Tume ya Uchaguzi kwa kushauriana na Serikali na vyama vya siasa watatengeneza kanuni za namna bora ya uendeshaji wa uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Rais, Wabunge na Madiwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na masharti yote, mkataba huu ambao Tume ya Uchaguzi ilitakiwa kuutengeneza ulikuwa unavilazimisha vyama vya siasa na wagombea kwanza kujadiliana masharti yapi ya uchaguzi wanayataka, lakini pili wagombea na vyama vya siasa ni lazima wasaini masharti hayo ili kwanza tuweze kufanya uchaguzi wenye staha, uchaguzi wa kuheshimiana, uchaguzi wa kufuata sheria, kanuni, mienendo, taratibu na mila za Mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo ndugu zangu wa CHADEMA, wenyewe wanasema kwamba hawapo tayari kusaini Kanuni za Maadili za Uchaguzi. Kanuni hizi zimetoa adhabu kwa chama ambacho kitakataa kusaini masharti ya uchaguzi, na imewekwa *clear* kwamba watu hao hawatashiriki uchaguzi; na siyo Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 tu, na chaguzi zote ndogo zitakazofuata, mpaka pale watakapotunga masharti mapya 2030. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, chama changu hiki cha *CHADEMA* kinacho *room* ya kutoa sababu ya kwanini walishindwa kushiriki kusaini kanuni na wanaweza kushawishi Tume na Msajili wa Vyama vya Siasa ili waweze kusaini masharti haya kwa sababu nje ya hapo, itakuwa ni uvunjifu wa sheria, ni uvunjifu wa kanuni na uvunjifu wa Katiba yenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo maneno ya wasomi wanasema hakuna kanuni itakayokwenda kinyume na Katiba, *it is not true*. Kila haki ina wajibu, huwezi kuomba haki wakati hutaki kutekeleza wajibu. Ni kama tu ambavyo leo hii tunasema kwamba huwezi kwenda kupiga kura kama hujajiandikisha

kwenye Daftari la Kupiga Kura. Huo ni wajibu wako, kama hujajiandikisha kwenye daftari huwezi kupiga kura.

Mheshimiwa Naibu Spika, huwezi kulipwa mshahara kama hujafanya kazi. Ili ulipwe mshahara ambao ni haki yako ya msingi ni lazima ufanye kazi. Huwezi kushiriki uchaguzi kama hujakubaliana na wenzio kwamba yapo masharti ya kutunza staha za watu, yapo masharti ya kutunza heshima za watu, yapo masharti ya kuheshimu sheria za nchi ambayo tunakubaliana sisi Serikali, Tume ya Uchaguzi na vyama vya siasa kwamba tutayafuata kwenye chaguzi zote kuanzia 2025 mpaka 2030.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashauri CHADEMA, hakuna namna ya kusema kwamba watashiriki uchaguzi kama hawatakubaliana na Kanuni za Uchaguzi. Naomba nifafanue kidogo kuhusiana na hoja yao ya *no reform, no election*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2024 Bunge hili Tukufu kwa weledi lilipitia sheria namba moja na sheria namba mbili ya Tume Huru ya Uchaguzi na likapitia Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, taratibu za utunzi wa sheria zinataka wale wanaoleta mapendekezo, wakusanye maoni ya wadau; lakini ili kuondoa mashaka katika utungaji wa sheria hizi mbili *sensitive,* Bunge liliita wadau hapa Bungeni kwa ajili ya kutoa maoni.  Chama cha CHADEMA kiliwakilishwa na Katibu Mkuu wa Chama, John John Mnyika, wakaleta maoni hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, haikutosha,, wakaja Baraza la Vijana wakaleta maoni; haikutosha likaja Baraza la Wanawake wakaleta maoni; haikutosha, wakaleta hilo wanaloliita Bunge la Wananchi, chini ya mama yangu Suzan Lyimo, wakaleta maoni. Kwa taarifa tu, kwenye Bunge hili Tukufu, zaidi ya 95% ya maoni yalitolewa yakachukuliwa yakaingizwa na tukatunga sheria hizi mbili za uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wote tunajua ndani ya Bunge hili masharti kwamba ya ubadilishaji wa zile sheria yalikuwa ni

magumu sana, joto lilikuwa kubwa sana pale Msekwa. Hebu fikiria mazingira ambayo tunataka sisi Wabunge ambao kimsingi ndio tunaoshiriki uchaguzi tubadilishe sheria ambayo kimsingi ilikuwa inawa-*favor* Wabunge wengi ya kupita bila kupingwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa kuna kifungu kinasema ikitokea vyama vingine vimekosekana kushiriki uchaguzi, basi mgombea huyo atakuwa amepita bila kupingwa. Leo akibaki mgombea mmoja, sheria mpya inasema atapigiwa kura ya Ndiyo na Hapana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ni nani anaweza akakubali kitu cha namna hiyo? Joto la uchaguzi lilivyokuwa kali, lakini Bunge hili liliridhia mtu anapigiwa kura ya Ndiyo na Hapana, na yale yalikuwa ni maoni ya Vyama vya Upinzani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mazingira ya kawaida, Wakurugenzi wa Uchaguzi tulizoea, wana *machinery* zote za kusimamia uchaguzi, lakini maoni ya Serikali yalikuwa ni lazima wasimamie uchaguzi, na kesi zilipelekwa mpaka Mahakamani. Sisi kama Bunge tukaridhia, na Mheshimiwa Rais akasaini, kwamba sasa Wakurugenzi watakaa pembeni, atasimamia Mtumishi wa Serikali Mwandamizi na atasaidiwa na raia wa kawaida ambao watafanya maombi na watafanyiwa usaili, na watakapofanikiwa wale waliochaguliwa kusimamia uchaguzi kama wasimamizi wasaidizi watabandikwa kwenye Gazeti la Serikali, kila mtu ataona kwa uwazi ili tuweze kuwajibisha Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni nani anaweza akakubaliana na kifungu cha namna hiyo? Lakini Serikali hii chini ya Mheshimiwa Rais, ilikubali ili kuhakikisha kwamba uchaguzi unakuwa huru na haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wote tunafahamu hapa kwamba, kwenye Sheria ya Tume ya Uchaguzi, lengo la kila chama cha siasa ni kushika dola; na ili ushike dola unajua kwamba kuna mambo ambayo ni *privilege* utayapata.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais alikuwa na *privilege,* alikuwa na upendeleo wa kipekee wa kuchagua Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi, lakini leo ameamua kijivua madaraka yale, amekabidhi Kamati Maalum, ameweka Majaji, akaweka *element* ya Muungano, Sekretarieti ya Haki za Binadamu na mjumbe mmoja, na kusema wale ndio watampelekea majina matatu ambayo yata-*qualify* kuweza kupata Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi. Wanataka tufanye nini ili waweze kuelewa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapokea ushauri, lakini ni lazima tukubaliane, hapa tusipotoshe umma kutaka kutekeleza jambo ambalo tunajua kwamba hata wale wanaolipendekeza hawajatekeleza wajibu wao. Wote tunajua hapa wanasema *no reform, no election, well and good*.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa utunzi wa sheria unasema mtu binafsi Mbunge au Wizara yenye dhamana wanaweza kupeleka mapendekezo ya mabadiliko ya sheria au utunzi wa sheria Serikalini. Ukipeleka Serikalini mapendekezo yale yatapelekwa kwenye Baraza la Mawaziri, kwa maana ya Katibu Mkuu na Baraza la Mawaziri kwa ajili ya kuchakatwa yakitoka pale yataletwa Bungeni. Bungeni tutakuwa na *public opinion* kusikiliza, tukitoka hapo maoni yale yataingizwa Bungeni kwa ajili ya kujadiliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo Tundu Lissu, siyo *TLS,* siyo mwanasheria, siyo Mbunge; hakuna hata mtu mmoja aliyeanzisha mchakato wa mabadiliko ya sheria. Leo unasema *no reform, no election!* Utafanyaje *reform* kama mchakato wenyewe wa kubadilisha sheria haujafanyika?

Mheshimiwa Naibu Spika, utafanyaje *reform?* Hakuna mtu aliyejitokeza, hakuna Mbunge, sio wa upinzani wala wa chama tawala, hakuna Serikali ambayo ime-*move motion* ya mabadiliko ya sheria hiyo, *no reform* ni ya kwenye majukwaa! Hatuwezi kukubaliana na jambo hili, tusipotoshe umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimwambie Mheshimiwa *Attorney General,* ameishauri vizuri sana Serikali kwenye hili, kwa sababu ili tuweze kufanya mabadiliko ya sheria pengine linahitaji muda zaidi, lakini Bunge hili uhalali wake mwisho ni tarehe 27 mwezi wa Sita, likivuka hapo tunakiuka Katiba. Je, wanataka tufanye hivyo? Hatupo tayari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwanasheria Mkuu wa Serikali umeongoza vizuri jopo la mashauriano, nakupongeza. Waziri wa Katiba na Sheria umeongoza vizuri jopo la mashaurino, mimi nawapongeza. Hatuwezi kufanya mabadiliko ya sheria bila kufuata mifumo na utaratibu wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukubaliane hapa kwamba hakuna Serikali hapa duniani ambayo viongozi na wasimamizi wa uchaguzi wanatoka *from the vacuum,* haiwezekani. Iwe ni Kenya wanapopasifia, iwe ni Ulaya wanapopasifia, wote wale wanatokana na uteuzi wa Mheshimiwa Rais, wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu, na ndiyo maana ya uchaguzi wa mwaka 2015, tofauti ya kura ilikuwa ni ndogo sana kwa sababu mgombea wa upinzani aliweza kusimama akamshawishi msimamizi wa uchaguzi wa kwenye kata yangu kule Ibadakuli, akamshawishi msimamizi wa uchaguzi pale Shinyanga, akamshawishi Mheshimiwa *DC,* pengine akamshawishi Mkuu wa Mkoa, vyombo vya dola na ndiyo maana tofauti ya kura ikawa ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani *under the sun* wewe huwezi kushawishi vyombo vyote hivyo halafu unataka Tume ya Uchaguzi itoke kutoka kwenye roboti, haiwezekani! Ni lazima tuweke *candidate* wenye ushawishi ambao wanaweza kushawishi kuanzia ngazi ya Taifa mpaka ngazi ya kijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tofauti na hapo, ukiweka wanaharakati, ukaweka watu wanaopiga kelele majukwani; hata viongozi wa dini hawapendi viongozi wanaotukana matusi hadharani, hawapendi viongozi wanaodhalilisha watu, na hawependi viongozi hawaheshimu mifumo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mtu anataka kiongozi ambaye anaheshimu demokrasia na amani ya nchi. Kwa maana hiyo, mimi nawashauri ndugu zangu, sisi tunakwenda kwenye uchaguzi; *it is either* waende wakasaini fomu za maadili au wajitoe na hawatashiriki uchaguzi mpaka 2030. Huo ndiyo ukweli, na tusipotoshe jamii kwa kusema kwamba…

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Nani Taarifa?

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni mimi hapa.

**NAIBU SPIKA:** Wewe nani? Simama basi nikuone. Huonekani.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Stella Fiyao, kushoto.

**NAIBU SPIKA:** Haya. Mheshimiwa Stella.

**TAARIFA**

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nataka kumpa tu taarifa Mheshimiwa mzungumzaji kuwa hata maandiko matakatifu yanasema, iheshimuni sana mamlaka maana imetoka kwa Bwana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Salome, nimekuongezea muda kidogo.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea taarifa ya mdogo wangu Mheshimiwa Stella Fiyao. Ukweli ni kwamba hata wao wakifanikiwa kuingia madarakani, yaani wataona hii sheria kama Mheshimiwa Rais, Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan alikuwa ameilegeza sana. Wataona kama ilikuwa imelegezwa sana. Sidhani kama kwa utashi walionao wanaweza wakakubali eti washauriwe na kuletewa majina matatu ya Msimamizi wa Tume Huru ya Uchaguzi, sidhani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, kwa dakika moja, ipo *initiative* kubwa inafanywa na Wizara inayohusiana na utoaji wa msaada wa kisheria. Mimi nipo kwenye *legal field,* kama kuna jambo gumu linalowafika Watanzania, ni namna ya kufikia haki yao ya kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa watu wanafanya jambo kubwa sana, lakini changamoto kubwa ninayoiona ni muda wanaopata katika maeneo wanayokwenda kutoa msaada wa kisheria. Changamoto ya pili, ni uwezo wa kifedha kwenye mfuko wa *Samia Legal Aid Campaign.* Hii kampeni imebeba jina kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kada ya kisheria ni moja kati ya kada ambazo ni ngumu kidogo kwenye nchi hii. Nashauri kwamba ili kuleta ufanisi na tija kwenye nchi hii, mfuko huu upewe fedha maalum, na utengewe bajeti ya kutosha ili waweze kutekeleza majukumu yao, nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Salome. Waheshimiwa wageni wetu ambao mpo kwenye *gallery* pamoja na kutembelea Bunge, mafunzo ni sehemu; naomba mchukue mada hii aliyoisema Mheshimiwa Salome pamoja na Wabunge wengine muisaidie nchi kwa kusema ukweli.

Kwa dhamira ya Serikali hii ya Mama Samia, ni uchaguzi uwe huru na haki; na haki inapatikana kwa maelewano. Waje tujenge Taifa kwa pamoja, wasipotoshe watu kwa kuonesha picha mbalimbali ambazo wala siyo ukweli wa hali halisi ilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Suma, atafuatiwa na Mheshimiwa Neema, jiandae Mheshimiwa Kandege.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuchangia bajeti hii ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima na afya njema, amenipa kibali cha kuchangia mchango huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo alituletea msaada wa kisheria kule Mkoa wa Mbeya. Wananchi walio wengi sana hasa wanawake wa Mkoa wa Mbeya walikuwa wanashindwa sana kupata fedha kwa ajili ya kuendesha kesi Mahakamani ili wawalipe Wanasheria, lakini Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ametoa msaada wa kisheria ili kila mwananchi ambaye hana uwezo wa fedha kwa ajili ya kuendesha kesi zake, aweze kusaidiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo amewaona wananchi wa Tanzania na hasa wananchi wa Mkoa wa Mbeya. Tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitamani kushauri jambo muhimu kwa jinsi ambavyo Mheshimiwa Rais amejitoa kutoa msaada wa sheria. Pale kwetu Mbeya wananchi zaidi ya 200,000 wamepata msaada wa kisheria, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuishauri Wizara hii waandae makala maalum ambayo inaonesha namna ambavyo Mheshimiwa Rais amejitolea kusaidia msaada wa kisheria kwa wananchi mbalimbali. Kwenye Makala hiyo kiandikwe kichwa cha habari ambacho kinamsema Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, maana hili lisije likapita bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niingie kuishauri Serikali kwa upande wa *NIDA*. Wananchi walio wengi walijitokeza kujiandikisha ili waweze kupata vitambulisho vya *NIDA*. Naomba kushauri, kasi ya kutoa vitambulisho vya *NIDA* iongezeke, kwa maana kipindi wananchi wamejitokeza kwa wingi wapo wananchi ambao mpaka sasa hivi hawajapata vitambulisho vya *NIDA* ila wana namba za utambulisho kwamba wao ni raia wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana ndugu zangu ambao wanahusika na mambo ya *NIDA,* wafanye utaratibu wa

kutoa vitambulisho vimfikie kila mwananchi aliyejiandikisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina jambo lingine la kushauri hapa. Huko magerezani kuna wafungwa. Hao wafungwa ni binadamu kama binadamu wengine. Nashauri Serikali, kipindi cha uchaguzi, wafungwa hao nao wawe na haki ya kupiga kura kuwachagua viongozi ambao wanaona kwamba wanawafaa katika nchi yao ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, kuna wahalifu ambao wanahukumiwa miaka miwili, mitatu. Naomba niishauri Serikali, hao wananchi ambao wamefungwa kifungo hicho cha miaka miwili mpaka mitatu, basi wasikae bure gerezani. Wapewe kazi ya kufanya; walime mashamba, ili wakitoka huko wawe wamejifunza kitu kikubwa. Maana nchi yetu ni kubwa sana, ina mashamba maeneo mengi, hiyo itasaidia kuondoa uhalifu kwenye Taifa letu la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa pongezi ambazo Wabunge wamechangia hapa wakiongozwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa Majaliwa, kwa namna ambavyo wanatuasa wananchi wa Mkoa wa Mbeya kwamba tuhakikishe tunamrudisha Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jana Naibu Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko, aliongea hapa, kwamba, "wananchi wa Mbeya, ninawashauri sana msiache kumrudisha Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Bungeni." *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapokea shukrani nyingi sana, lakini pia tunawashukuru Waheshimiwa Wabunge. Wananchi wa Mbeya Jiji niliwapongeza na ninawapongeza sana kwamba mlimchagua Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, pia mlimpa baraka ambayo wananchi waliendelea kumwombea Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson. Alipofika hapa akagombea nafasi ya Uspika, nawashukuru sana Kamati Kuu walipendekeza jina la Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, na lilipofika Bungeni, Wabunge wote tulimpa

kura za kutosha akawa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru kipekee wananchi wa Mkoa wa Mbeya, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kumpa kibali Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, kwenda kugombea nafasi kubwa ya kuwa Rais wa Mabunge Duniani. Tunashukuru wa *support* hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Mbeya, kwa heshima waliyopewa na Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, na ushauri wa kila Mbunge mmoja mmoja aliyeshauri hapa, tumchague kwa heshima Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, ili arudi hapa. Tumeupokea na tunaufanyia kazi, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson ni mpakwa mafuta wa Mungu, Mwenyezi Mungu amemnyooshea mkono. Siamini kwamba kuna mtu atajitokeza kupingana naye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaheshimu mamlaka, Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, heshima kubwa aliyotupatia wananchi wa Mkoa wa Mbeya, tumeipokea kwa dhati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakushukuru sana kipekee hata wewe namna unavyoongoza Bunge hili Tukufu, Mwenyezi Mungu asikupungukie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kushauri upande mwingine kuhusu Mahakama. Kuna wakati fulani Mheshimiwa Hakimu ama Mheshimiwa Jaji anavyotoa hukumu, wale ambao walikuwa wana kesi pale, nakala za hukumu hawapewi kwa wakati. Hilo limekuwa ni changamoto kubwa sana kwa sababu wananchi wengi sana wanasumbuka kupata nakala za hukumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri sana kwa upande huu, pale ambapo Mheshimiwa Jaji au Mheshimiwa Hakimu anapotoa hukumu, si anasoma, basi pale pale ziwe zimeshaandaliwa nakala za hukumu ili wale ambao walikuwa wanahukumiana kesi wawe

wanakabidhiwa nakala zao pale pale kwa sababu hii imekuwa ni changamoto na kero kubwa sana. Wananchi wanasumbuka kufuatilia nakala za hukumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa kuendesha kesi, mfano kesi za mauaji, katika suala la namna ya upelelezi, wanasema ndani ya miaka 10 ndipo ambapo kesi zinakuwa zinaanza ama kuendeshwa. Wananchi walitamani sana angalau basi wafanye kwa miaka mitano ndipo mambo mengine yaendelee. Hilo lingekuwa jambo jema sana ambapo wananchi ingewapunguzia shida mbalimbali wanazozipata ndugu zao wanapokuwa magerezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kushauri kwamba Mahakama za Mwanzo zimesahaulika sana katika kufanyiwa ukarabati, hasa zile Mahakama kongwe. Naomba mtupie jicho hapo na Mheshimiwa Mtendaji Mkuu wa Mahakama yuko vizuri sana, namwelewa vizuri sana. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, kengele ya pili hiyo.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii, naunga mkono hoja. Ahsanteni kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, umenipongeza, nakushukuru, lakini hukuwaambiwa watu wa Ilala wanichague tena. Mheshimiwa Kandege, atafuatiwa na Mheshimiwa Tarimo, Mheshimiwa Mbunda jiandae. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Eeh, ni mimi!

**MBUNGE FULANI:** Hajakuita.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, samahani nina taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Naam!

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ulikuwa umeshaniita mimi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kandege unafuata baada ya Mheshimiwa Neema.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika Wizara yetu hii muhimu ya Katiba na Sheria. Kabla sijachangia mengine ambayo ninawiwa sana, niendelee tu kuipongeza Wizara kwa jitihada inayofanya kuhakikisha wananchi wanahudumiwa vizuri. Pia nampongeza Mwanasheria Mkuu wetu kwa sababu amekuwa akiendelea kufanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya tofauti kabisa, nampongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mama yetu kipenzi kwa namna ambavyo ameweza kuanzisha kampeni mbalimbali za utoaji wa huduma za haki kwa jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuanzia, nilitamani nami nianzie kwenye kipengele cha *Legal Aid Campaign* ambapo tumeona kabisa Serikali yetu Tukufu ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan wamekuja na kampeni ya utoaji wa msaada wa kisheria kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu kabisa kwamba wananchi wengi wana changamoto ya upataji wa haki. Wanakuwa hawajui mambo gani ni haki zao na pia ni wapi watapata hizo haki zao na ni akina nani wana wajibu wa kuwapatia hizo haki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa elimu hii ambayo inaendelea kutembea kwenye jamii yetu, sisi tunaishukuru Wizara, tunamshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan na tunampongeza kwa kweli kwa moyo huo wa kizalendo na kibinadamu na kama tunavyoona kaulimbiu ya CCM mwaka huu ni Kazi na Utu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa kitendo cha kuanzisha kampeni kama hizi, inadhihirisha kabisa kwamba Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, ana utu kwa kiwango gani, na anatamani kuona nchi yake inaongozwa kwa kuwa na upendo na utu kwa kiwango gani? Kuhusu hilo, naomba wanifikishie salamu zangu kwa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni mikoa karibu 25 ambayo wameshafika mpaka sasa hivi. Wanaenda wanatoa huduma, wanahama, wanaenda maeneo mengine wanatoa huduma, lakini kwa takwimu walizotuonesha hapa, inaonesha ni wananchi karibu 2,698,908 wameshawafikia. Hii idadi siyo ndogo, na siyo ya kuipuuza. Kwa hiyo, tunawapongeza sana kwa kuweza kuwafikia wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu katika hili, ni kwamba wakati wa utekelezaji wa zoezi hili, tumeona kuna baadhi ya changamoto ambazo zinajitokeza. Mfano, ushirikishaji kwa baadhi ya viongozi wa Serikali na vyama vya kisiasa ulikuwa mdogo. Sasa natamani wanapoendelea na zoezi hili, kwa sababu ninaamini wamepita na wataendelea kupita, wanapokuwa wanafanya mazoezi haya, viongozi wa kisiasa kama Wabunge, Madiwani wahamasishwe, wawe sehemu ya kushiriki hizo kampeni zinazokuwa zinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mungu, kwenye Mkoa wangu wa Songwe nadhani nilikuwa ni Mbunge pekee niliyeshiriki siku ile. Siyo kwamba barua hazikutolewa kwa Wabunge na huenda wakati mwingine hiki kitu kwa Wabunge unakuta hakifahamiki kwa uzuri, kwa hiyo, nayo inakuwa ni changamoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika zoezi lile sikuwaona Madiwani mkoa ule wakishirikishwa wote. Kwa hiyo, hili nalo niliona kuna *gap* la ushirikishwaji wa Madiwani kwenye utekelezaji wa zoezi hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani *may be* wanapoenda kwenye wilaya watawashirikisha wale Madiwani, lakini bado

nilivyofuatilia niligundua kwamba kwenye ngazi ya wilaya na zile kata walizoenda Madiwani hawakushiriki zoezi hili kikamilifu na tunajua Madiwani ndiyo watu wanaoishi na wananchi na ndiyo watu wanashinda na wananchi kila siku ambao wanaweza *at least* hata kuwafafanulia wananchi kwa habari ya mambo haya yanayofundishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, huwezi ukasema unamfundisha mwananchi habari ya haki wakati kiongozi wake anakuwa hafahamu hiyo haki inapatikanaje na inatolewa na nani? Wakati gani anaweza akaipata? Kwa hiyo, hilo nilitamani kuomba Wizara iweze kulichukua na wakati mwingine waweze kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina ombi lingine la ziada kwamba wanapokuwa wanatekeleza hizi kampeni, wajaribu kugatua, yaani itoke kwenye ngazi ya Kitaifa iende kwenye ngazi ya mikoa na wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, huwezi ukaniambia kwamba kampeni iwe inafanyika kwa *rotation* wakati hili ni zoezi endelevu. Upotevu wa haki za watu ni tendo endelevu. Mtu atakosa haki yake leo, lakini unakuta hata wanaopoteza haki wakati huo unakuta elimu hiyo ilikuwa inatolewa, wengine hawakuwa na *access* ya hiyo elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, natamani zoezi hili la elimu au hii *Legal Aid Campaign* ishushwe kwenye ngazi ya wilaya na tena itengewe bajeti ya kutosha ambayo itawawezesha wale watoa huduma hizo kwa wananchi waweze kupata haki zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu kabisa wahanga wa haki hizi ni wanawake na watoto na makundi maalum ambayo yako katika hali hatarishi ya kunyanyasika au kufanyiwa ndivyo sivyo. Tunafahamu kabisa wanawake wengi wanadhulumiwa mali, wanafanyiwa vitendo vya ukatili na hata sehemu ambayo wana haki na hilo jambo, wanafanyiwa vitendo vya ukatili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunafahamu watoto wetu wanafanyiwa matendo ya ukatili mengi, japo siku hizi kuna kampeni za kuibua kero za wanaume ambao nao wanafanyiwa ukatili. Hata hivyo, bado kesi zinaonekana wanawake wengi na watoto wengi na watu wenye mahitaji maalum ndiyo wanaofanyiwa ukatili mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa na ombi. Kwa kuwa wahitaji ni wengi, naomba huduma hizi washushe hadi ngazi ya wilaya ili tunavyoendelea mbele, basi ziendelee kushushwa hadi ngazi ya kata, kama ambavyo huduma nyingine za ugani zimeweza kushushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, kwenye habari ya mambo ya ukatili wa kijinsia, nina ombi moja. Mkoa wangu wa Songwe katika Wilaya yetu ya Momba Mji wa Tunduma ukatili umekuwa ukiongezeka siku hadi siku. Sisi kama viongozi wa eneo lile tunaumia, na tunaumia sana kwa sababu tunaona kama watu wetu wananyanyasika, na ufuatiliaji wa mashauri kwa wale watu wanaokuwa wanafanya vitendo hivyo vya ukatili tunaona kama hayachukuliwi kwa uzito huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali yangu, kwamba Mji wa Tunduma kulingana na wingi wa malori ambayo yako pale, vitendo vya ukatili vimeongezeka kwa kiasi kikubwa ikiwezekana waweke kambi maalum ya kuhakikisha wanafanya utatuzi wa changamoto zinazopatikana eneo lile. Pia, waje na mbinu mbadala za kuwasaidia wananchi wa eneo lile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kituo cha polisi cha pale hakina uwezo mzuri, ukiangalia Mahakama, hatuna majengo mazuri kwa Wilaya ya Momba. Hilo pia nilikuwa natamani Wizara kama Wizara, Mji wa Tunduma, Halmashauri ya Momba waitazame kwa jicho la tofauti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia baada ya kuongea hayo nilitamani niwaombe, suala la kuwapa dhamana watu wanaowabaka watoto wetu wadogo likose dhamana, kwa sababu haiwezekani mtu anabaka halafu mtu huyo huyo

anaenda kupewa dhamana. Hivi mtu anambaka mtoto, wewe huwezi ukaona kwamba hilo ni kama kosa la uuaji? Anawezaje kuthubutu? Kwa hiyo, nilitamani suala la kukatili watoto sheria yake itungwe na wakose dhamana. Tunaumia sana kwenye maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, natamani kuongea na Waziri, baba yetu Mheshimiwa Ndumbaro aweze kutusaidia. Aliniahidi Wilaya ya Ileje kutupatia Mahakama mbili. Jana nilimwuliza swali la msingi kuhusiana hatua za ujenzi wa Mahakama ya Wilaya ya Ileje inaendeleaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli ni kwamba Wilaya ya Ileje hata ujenzi haujaanza. Kwa hiyo, namwomba Waziri atakapokuwa anafanya *finalization* aje anipe kauli ya kwamba ni lini anapeleka fedha za kuanza ujenzi wa Mahakama ya Wilaya kwenye Wilaya ya Ileje?

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani Wilaya ya Ileje na ukongwe wake mpaka leo haina Mahakama hata moja. Huduma za Mahakama zinatolewa kwenye majengo ya upangishaji tena majengo ya CCM yaliyochoka. Kwa hiyo, namwomba Waziri atusaidie, Wilaya ya Ileje tunahitaji fedha kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama. Basi aanze hata na hizo wilaya nyingine, kwenye tarafa nyingine atafanya wakati mwingine kama ikishindikana kupata fedha zote. Ahadi ni deni, leo nimekuja kumdai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, natamani kuongelea kipengele cha haki za binadamu. Sisi wengine ni waumini wa haki, yaani ukitaka kukosana nami, onesha unamnyima mtu mwingine haki au unaninyima haki yangu. Hapo naweza nikavua viatu na nikakubali kupambana na wewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni mama wa wafungwa. Nilishajitolea kuwa msemaji wa wafungwa wasiokuwa na wasemaji. Humu ndani hatuna mwakilishi wa wafungwa hata mmoja. Wafungwa wanateseka. Sheria inatambua haki za binadamu, pamoja na mfungwa, kwani naye pia ni binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani mfungwa makazi yake yanakuwa ni sawasawa na eneo ambalo hata wewe ukisema tu ukasimame au ukae, huwezi. *Imagine* rumande mtu anakunya kwenye ndoo, wewe unawezaje? Kwa hiyo, niseme, maliwato ya wafungwa yaboreshwe. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, wafungwa wapewe na magodoro. Kama hawawezi, wawaruhusu wayalete, wenye uwezo na wana ndugu na jamaa wanaweza kuleta magodoro yao ya kulalia.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wageni waliopo Bungeni leo; tunao wageni 85 wa Mheshimiwa Spika, ambao ni Taasisi ya Mtetezi wa Mama, kutoka Mkoani Mbeya, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 80 wa Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde, Waziri wa Madini, ambao ni Mabalozi wa Mtaa wa Kikuyu kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 34 wa Mheshimiwa Santiel Kirumba, Taasisi ya Mtetezi wa Mama kutoka Mkoani Shinyanga, karibuni sana.

Tunao wageni 67 wa Mheshimiwa Nicodemas Maganga, Taasisi ya Mtetezi wa Mama kutoka Mkoani Geita, karibuni. *(Makofi)*

Tunaendelea na wachangiaji wetu. Mheshimiwa Kandege, atafuatiwa na Mheshimiwa Tarimo na Mheshimiwa Jonas Mbunda. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi nami niwe mchangiaji katika Wizara hii muhimu. Naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema kwa kunijaalia afya na kuweza kusimama leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, Mheshimiwa...

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, namwita Mwenyekiti kunipokea kwa dakika chache, endelea tu Mheshimiwa Kandege.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Mwenyekiti anakuja, hatua ya pili ilikuwa nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa na nzuri sana ambayo ameifanya katika maboresho na kuhakikisha kwamba haki inatolewa kwa wakati. Hili jambo linawezekana katika nchi chache Afrika na Tanzania tukiwa vinara. *(Makofi)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Joseph K. Mhagama) Alikalia Kiti*

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti. Nimepata fursa ya kuongea na Mtendaji Mkuu wa Mahakama, Mheshimiwa Waziri, na Naibu Waziri. Kwa hiyo, tulipata fursa ya kupata mengi juu ya maboresho makubwa ambayo yamefanyika kuhusiana na suala zima la utoaji haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipata historia moja nzuri sana ambayo Mtendaji Mkuu wa Mahakama alituambia sisi Wajumbe wa Kamati kwamba, kuna kipindi ambapo ilikuwa inatakiwa ushahidi utolewe na mtu ambaye yuko Marekani. Sasa akawa anaomba kwamba itabidi asubiriwe kipindi ambacho atapata likizo, maana anafanya kazi Marekani. Pia, ajikusanye atafute tiketi ili aje Tanzania, na suala lenyewe lilikuwa linahusu mambo ya sheria za ndoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa akaambiwa kwa *advancement* na kazi nzuri ambayo imefanywa Tanzania na

maboresho ambayo yamefanywa chini ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, huna sababu ya kupoteza muda wako kutafuta tiketi wala kutafuta likizo eti kuja kutoa ushahidi wako. Tanzania hii, akaambiwa tunachotaka kwako wewe utuambie muda wako, lini utakuwa uko tayari. Tunahitaji *hardly* saa mbili *maximum*, ukiwa Marekani huko huko sisi tutapata ushahidi wako. Hakuamini, lakini hicho ndicho kilitokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, akawa anatoa ushahidi na yeye mwenyewe anajiona, na akauliza maswali mpaka akaridhika. Alidhani kwamba labda haya yanawezekana Marekani, lakini hayo yanawezekana kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Hongera sana Mheshimiwa Rais katika kuhakikisha kwamba haki inapatikana kama nchi ambazo zimeendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi na maboresho makubwa ambayo yamefanyika, naomba niongelee ndani ya Wilaya ya Kalambo na Jimbo la Kalambo. Naomba niendelee kumshukuru Mheshimiwa Rais, Waziri, Naibu Waziri, na Mtendaji Mkuu wa Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji Mdogo wa Matai ni miongoni mwa miji ambayo imepangwa kisasa. Kwa hiyo, pale ambapo Serikali inaleta majengo, nataka yalingane na hadhi ya jinsi ambayo tunapanga mji wetu. Nashukuru, ujenzi wa Mahakama ya kisasa wa thamani ya shilingi bilioni 1.5 unaendelea na mkandarasi yuko *site*. Naishukuru sana Serikali kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya Kalambo tuna jumla ya tarafa tano, tuna jumla ya Mahakama za Mwanzo tano, lakini cha ajabu Tarafa ya Mambwenkoswe haina Mahakama ya Mwanzo hata moja, na hii ni tarafa ambayo iko mbali sana. Tafsiri yake ni kwamba, wananchi ambao wangependa haki yao ipatikane kwa wakati, wanakosa kupata haki yao ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juu ya utayari, tayari wameshatenga eneo kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama ya Mwanzo. Nami natamani Mahakama ya Mwanzo ingejengwa

jana. Kwa hiyo, naomba, na nilipata fursa ya kuteta na Mheshimiwa Waziri, akasema, kwa mujibu wa sera hii tarafa inastahili kujengewa Mahakama yake ya Mwanzo ili vijiji hivi 16 ambavyo wananchi wanataka kupata haki zao kwa muda muafaka, waweze kupata haki bila kutembea umbali mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, katika Mahakama zetu tano, Mahakama mbili zina hali nzuri ikiwemo Mahakama iliyopo Sopa na Mahakama iliyopo Msanzi. Mahakama inayojengwa Kasanga iko kwenye hatua nzuri, naipongeza Serikali. Kazi ambayo naiomba Serikali, pamoja na kuhakikisha kwamba tunaenda kujenga Mahakama ambayo haipo katika Tarafa Mwambenkoswe, lakini haipendezi pale ambapo ukienda kutazama Mahakama iliyopo Kijiji cha Mwimbi Tarafa ya Mwimbi ilijengwa kipindi cha mkoloni. Pia, Mahakama ya Mwanzo iliyoko Tarafa ya Mwashe na Kijiji cha Mwashe nayo ilijengwa kipindi hicho hicho cha mkoloni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wakati mwafaka sasa maboresho yafanyike. Pia, ikiwezekana, kwa sababu wakati mwingine ukarabati unakuwa ni gharama zaidi, ni bora ukaanzishwa ujenzi mpya ili tuendane na hali ya sasa ya majengo, kwani wananchi wa Kalambo wanapenda vitu vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo eneo lingine ambalo naomba nichangie. Nalo ni kazi nzuri ambayo inafanyika kuhakikisha kwamba haki inatolewa, lakini haki ikicheleweshwa au mtu akilazimika kutafuta haki kwa kutembea umbali mrefu, jambo hili halina afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kalambo hatuna Baraza la Ardhi la Wilaya. Kwa hiyo, mashauri yote ambayo yanahitajika yapate ufafanuzi na ufumbuzi kupitia Baraza la Ardhi yanaishia ngazi ya kata. Yakishaishia ngazi ya kata, pale ambapo rufaa inatakiwa ifuatwe kwa maana ya kwenda Wilayani, kwa sababu Kalambo hakuna Baraza la Ardhi la Wilaya, wananchi wa Kalambo wanalazimika kusafiri umbali mrefu kwenda kutafuta haki yao Sumbawanga Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafsiri yake ni nini? Mwananchi huyo lazima ajipange, maana huwezi ukahudhuria siku hiyo hiyo. Lazima atafute sehemu ya kufikia, lazima atumie nauli, lazima ajipange kwa chakula. Kwa hiyo, inafikia wakati mwingine mwananchi anaona kuliko kupata adha hii, wanaamua kumalizana kwa namna ambayo haki inakuwa haitendeki. Kwa malengo mazuri ya Wizara hii, sidhani kama mngependa jambo hili litokee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili limekuwa likiongelewa muda mrefu. Sijajua ni kwa nini hatupati ufumbuzi kuhakikisha kwamba Mabaraza ya Ardhi yanafanya kazi kama ambavyo Mahakama zinafanya kazi. Kuna kipindi mchakato ulionekana karibu unakamilika, lakini kuna habari ya kurudi nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, wakati hiyo michakato inaendelea, basi kama hakuna gharama kubwa sana mtutengenezee utaratibu ili wananchi wa Kalambo wakati wanasubiri utaratibu mwingine, Baraza la Ardhi la Wilaya lianzishwe, maana sisi ni Wilaya ambayo iko *fully fledged*. Hakuna sababu ya kwenda kulazimisha kukaa kwa ndugu ambaye sio ndugu yako eti kwa sababu umeenda kufuata haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishukuru sana, nimemwona Waziri anatikisa kichwa kwamba wananchi wa Tarafa ya Mwambenkoswe, watafikiriwa. Kwa hiyo, atakapokuja kuhitimisha atasema namna gani tunaanza kwenda kujenga Mahakama ya Mwanzo katika Tarafa ya Mwambenkoswe ambayo haina Mahakama hata moja ya Mwanzo. Vijiji 16, kata tatu tunasubiri kauli kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege. Namwita sasa Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, atafuatiwa na Mheshimiwa Jonas William Mbunda na Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, wajiandae.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii ya kuchangia katika bajeti hii ya Wizara ya Katiba na Sheria. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na timu nzima.

**MWENYEKITI:** Samahani Mheshimiwa Mchangiaji. Sekunde chache tafadhali.

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Endelea.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nilikuwa naendelea kutoa pongezi kwa timu nzima za Mahakama, Mabaraza ya Ardhi, pamoja na timu zote ambazo zinahusika katika mlolongo mzima wa kutoa haki. Tunaelewa kwamba wanafanya kazi kwenye mazingira magumu sana kutokana na uelewa wa watu na mazingira ambayo tunakabiliana nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kumpongeza kwanza, Mheshimiwa Rais kwa *Samia Legal Aid*, ilishafika Moshi Mjini na kwa kweli hata kwetu ilileta matumaini makubwa sana kwa watu, na watu walitamani ikae muda mrefu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kwamba, tuweze kuhakikisha tunapata fedha zaidi kwa ajili ya kuendesha zile kampeni ili ziweze kukaa kwa muda mrefu zaidi. Pia, tuzishushe chini zaidi zifike maeneo ya chini kwa wananchi mpaka kwenye ngazi za mtaa. Kwa hiyo, napongeza sana. Imefika mikoa 25, watu milioni mbili, na inaonyesha taswira halisi ya kiu ya watu ambao hawajapata haki kwa kupitia mifumo ya kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni jambo ambalo tunapenda ku-*encourage* liwepo kwa sababu limeweza kutoa haki kwa wale ambao wamekosa haki kwa mifumo ya kawaida kutokana na changamoto mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niangazie eneo la ardhi. Nadhani katika maeneo kwenye Mkoa wetu wa Kilimanjaro na hata pale Moshi ambapo tuna changamoto za kisheria, ni eneo la ardhi. Sasa, naomba sana tuangalie namna mbadala. Baraza la Ardhi limeleta mafanikio, lakini bado lina changamoto ambazo zinaikabili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri tungetafuta chombo ambacho kinaweza kuwa *mobile*, badala ya watu kufuata, kwa sababu ardhi siyo *mobile*, tuwe tuna chombo ambacho kinaweza kwenda kule kwenye kata, kwenye mitaa, na kwenye vijiji ili kishirikishe wale wananchi, haki ingeweza kupatikana kirahisi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata kama sijui tutafuta kitu gani, kitu ambacho kitajumuisha mamlaka zote zinazohusika na ardhi, lakini kiweze kwenda kule kwenye matatizo. Kwa sababu, hao watu wanaokuja huku saa nyingine mimi nafahamu hata kwenye taasisi hizi za kifedha, kuna sheria inasema, kama ni mwanafamilia unaweka labda hati kwa ajili ya *collateral*, lazima uende na mke. Sasa, hakuna *mechanism* sahihi ya kuonyesha kwamba huyu ni mke wa mhusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, unakuta watu kwenye familia mtu anachukua hati, anaenda kwenye taasisi za fedha, anaenda na mtu ambaye anasema ni mwenza, lakini siyo mwenza. Tukienda kule chini ambako wako pale na majirani wanajua, hii haki haswa kwenye ardhi inaweza ikapatikana kirahisi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo napenda kuliangazia ni eneo la wosia. Hakuna Mbunge ambaye katika matatizo yanayofika kwenye ofisi yake, matatizo ya mirathi hayapo. Sasa, mimi nadhani tumeona hapa kwamba talaka sasa zimefikia 16%; hilo ni tatizo; lakini hivi vitu vinaenda kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, 16% kwenye eneo la talaka maana yake tayari kuna tatizo kwenye hii taasisi ya ndoa. Najua, kuanzia kwenye ngazi za maendeleo ya jamii au ustawi wa jamii,

*focus* kubwa siyo kuachanisha watu, lakini ni kutatua changamoto ambazo wanazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa, kwa hizi asilimia tunazokwendanazo, moja, tunakwenda kutengeneza Taifa la watu ambao hasa wale watoto (tuache hawa ambao wameachana) ambao wanaachwa hapo Katikati, wanakuwa tayari wanapata shida kubwa sana ya malezi hasa kwenye malezi haya ya kawaida ya kifamilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa, tuangalie namna ambavyo katika mifumo yetu ni namna gani zaidi tunaweza kupata suluhisho badala ya kwenda kwenye kuachanisha hawa watu kwa maslahi makubwa ya wale watoto. Zaidi ya hayo, ikibidi lazima hao watu waachane, basi ni namna gani watashiriki kwa ulazima kuwalea wale watoto pamoja?

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu kwenye nchi zilizoendelea ni kawaida kabisa watu kuachana, lakini malezi ya watoto wana-*share*. Hapa kwetu watu wanaachana, lakini malezi ya watoto hata kama wana-*share,* lakini wanawachanganya wale watoto kwa sababu huyu anamwambia yule ni mbaya, akienda kwa huyu anamwambia yule ni mbaya, *psychologically* tunawaharibu wale watoto. Kwa hiyo, nadhani kuna haja ya kuliangalia hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudi hapo kwenye wosia. Watu wengi hasa kwenye jamii zetu wanaogopa kuandika wosia kwa sababu wanaona mara moja tu kwamba nikianza kuandika wosia najiandaa kufa, au ili niandike wosia mpaka niwe nimezeeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa, badala ya kwenda kwenye wosia moja kwa moja, mimi nadhani ni vizuri katika kila kitu ambacho watu wanamiliki kama inavyokuwa kwenye benki kuna *Next of Kin*, waandike. Kama ni kwenye ardhi awe ameandika pale. Hati ya ardhi, kama ni wazazi waende wakubaliane mume na mke kwamba *Next of Kin* wa hii ardhi yetu tukiwa hatupo ni nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama wana watoto, *automatically* haki ya watoto ilindwe, wale ambao ni chini ya miaka 18, lakini kama ni zaidi ya miaka 18 wawe na nafasi ya kuandika na wawe wana-*review* kama tunavyofanya kwenye kulipa *Land Rent*.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanapoenda kulipa *Land Rent* waandike *Next of Kin*, kwamba wakiwa hawapo ni nani aweze kuchukua hiyo kama ni *property*, kama ni *Bank Account*, kuyapunguza haya. Kwa sababu ingetokea hata wale ambao ni wasimamizi wa mirathi wamekuwa pia sio watu waaminifu, kitu kinachosababisha matatizo makubwa kwenye jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye eneo ambalo nimeona tunakazania sana kuwa na sheria ambazo zitawabana watu wa shisha na watu wa *betting*. Nadhani hapo kuna maeneo mawili ya kuongezea. Pamoja na shisha na *betting*, kuna pombe kali zisizokuwa na viwango vinavyotakiwa. Hii *trend* ya shisha, *actually* inaenda kwa watu wenye uwezo kidogo, wa kishua ambao ni wachache, lakini hizi pombe kali ambazo hazina viwango, zinakwenda kwa wale watu wa chini kabisa ambao ni wengi. Kwa hiyo, hizi sheria zi-*upgrade*. Hiyo shisha, *betting*, na pombe kali zisizokuwa na viwango, nayo tuangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande mwingine tunaangalia suala lingine ambalo kwetu linaweza kuwa na tija. Tunaangalia haya masuala matatu niliyoyataja kama masuala makubwa ambayo yana matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi nilisema, waendesha bodaboda na bajaji hawana leseni. Leseni ni chanzo cha mapato kwa Serikali. Wao hawa-*qualify* kwa sababu leseni ya kawaida ya daraja la chini nilisema tena ni karibu shilingi 340,000 kupata, kwa sababu unaanzia *driving school*, lakini wako barabarani hawana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini tusipitishe sheria ambayo wale ambao tayari wako barabarani, wana pikipiki na bajaji hawana leseni, tutoe *fee* ndogo kama ni shilingi 50,000 wafanyiwe *test* tu na Polisi? Anajua sheria za barabarani, anajua kuendesha,

apewe leseni. Badala ya kusema kwamba lazima twende *driving school* au twende huku na wanakufa bila kuwa na hii *driving license*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka kusema kwamba, kila sheria duniani ina *exception*. Sasa hatuwezi kuacha watu wanaendesha pikipiki na bajaji, wanakufa kwenye ajali hawawezi kupata *insurance,* hata ile ya *third party* kwa sababu hana leseni. Hiyo leseni ni chanzo cha mapato, halafu sisi hatuoni kwamba hilo ni tatizo. Kwa hiyo, naomba sana tuliangalie kama jambo ambalo tunaweza kulifanya kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mabadiliko ya sheria ambayo yanapigiwa kelele. Nafikiri ni vizuri na sisi tusimame na tuliangalie hili kwa upana. Kwa nini kikundi cha watu kinaweza kikasema hili ni tatizo wakati wanajamii wenyewe hawajaona kwamba ni tatizo? Wewe unasimama unasema bwana, sisi tunataka Katiba mpya. Kabla hujaipata hiyo Katiba mpya unasema tunataka *reform* za *election*; kabla hujaipata unaleta kitu kingine. *Basis* yao ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri tuwe na sheria ambazo ili mtu alete hoja, aibebe kama hoja ya Kitaifa, lazima iwe imesimamiwa na idadi ya watu kwenye kila kata, kwenye kila wilaya na kila mkoa, na wakishafika idadi fulani ndiyo inakuwa *National Agenda*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu anabeba ajenda yake anasema bwana sisi tatizo letu sasa ni Katiba mpya. Sisi tatizo letu sasa hivi sijui ni sheria za uchaguzi. Ni nani anamtuma? Ili iwe *National Agenda* iweze kupigiwa kelele ni lazima kuwe na idadi ya watu katika kila kata, mtaa na wilaya, wanao-*demand*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kuwa tuna watu ambao kwa sababu kuna *social media* watakuja waseme sasa hivi tatizo ni hili. Watarudi kesho waseme tatizo ni hili, halafu walete ajenda ambazo zinaichanganya nchi yetu. Kwa hiyo, naomba sana tutafute namna ya kuweka sheria ambayo italazimisha kuwe na

idadi ya watu ambao watasema hiki kitu ndiyo kiwe ni *National Agenda*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna uhalifu wa mitandao. Sina uhakika kama sheria zetu zina uwezo kiasi gani kupambana na uhalifu wa mitandao? Tuunde timu chini ya watu ambao watajaribu kufanya tathmini ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tarimo, ni kengele ya pili.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunda, wajiandae Mheshimiwa Issaay na Mheshimiwa Midimu.

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kukubali kufanya maboresho makubwa kwenye Wizara hii ya Nishati upande wa Mahakama, kwenye miundombinu na kwenye shughuli zote za utendaji kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro, Waziri wa Katiba na Sheria kwa kufanya kazi nzuri ya kuleta taarifa katika Bunge hili Tukufu, na pia kwa kufanya kazi nzuri sana ya kumsaidia Mheshimiwa Rais kutekeleza majukumu yake kwenye upande wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, ninachukua nafasi hii kumpongeza ndugu yangu Mheshimiwa Jumanne Sagini, Naibu Waziri. Pia nampongeza Eliakim Chacha Maswi, Katibu Mkuu, Dkt. Franklin Rwezimula, Naibu Katibu Mkuu, na bila kumsahau Profesa

Elisante Ole-Gabriel, Mtendaji Mkuu wa Mahakama, pamoja na wafanyakazi wote. Nawapongeza sana kwa sababu utendaji wa kazi wa Mahakama zetu sasa hivi ni tofauti kabisa na ile miaka ya nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika miaka ya nyuma kulikuwa na malalamiko makubwa sana ya upatikanaji wa haki kwa wananchi, lakini sasa hivi mambo yanakwenda vizuri. Kwa hiyo, lazima nichukue nafasi hii kuwapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza naipongeza Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kukubali kutoa fedha nyingi zaidi, sijapata *figure* kamili na sahihi, lakini ninajua ni fedha nyingi ambazo zimetumika kujenga jengo la Mahakama Kuu ambalo ni jengo la kisasa na limeweka mpaka akiba ya *Supreme Court* ambayo haipo kwenye Katiba yetu. Kwa hiyo, tunajua kama kutakuwa na mabadiliko, tayari nafasi hiyo itakuwa *accommodated* kwenye jengo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, naipongeza Wizara hii pamoja na Mheshimiwa Rais, kwa kutoa fedha kuanza kujenga Mahakama Jumuishi katika mikoa yetu. Kwa nafasi hii, naipongeza sana Wizara kwa sababu tayari kuna fedha nyingine zimetolewa kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama hiyo katika Mkoa wa Ruvuma na shughuli zimeanza kuendelea pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, niendelee kupongeza kwenye upande wa miundombinu, Serikali imetoa fedha nyingi kuendelea kujenga Mahakama za Wilaya na Mahakama za Mwanzo. Ni Mahakama za kisasa na ni nzuri ambazo zinajengwa sasa hivi, pia katika kuendelea kuboresha mifumo ya utoaji haki kwenye upande wa Mahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali, imeweka miundombinu ya kisasa ya TEHAMA, na kama alivyoongea Mheshimiwa Kandege kwa sababu nami nipo kwenye Kamati ya Bajeti, kwa taarifa iliyopo sasa hivi, Majaji wanapotoa hukumu wakimaliza neno la mwisho na hukumu inatolewa. Kwa hiyo, ni

mfumo mzuri na utasaidia sana katika utoaji haki kwa haraka kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuunda Tume ya kutayarisha Sera ya Haki Jinai na mikakati ya namna ya kutekeleza sera hiyo. Haya yote ni katika maboresho ambayo yamefanyika ili kuhakikisha kwamba haki inatolewa na wananchi wetu wanapata haki katika mazingira mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye upande wa utoaji haki Mheshimiwa Rais alianzisha msaada wa kisheria wa *Mama Samia Legal Aid*. Hiyo imesaidia sana kwa wananchi wetu kwa sababu watu wengi hasa wale wanaoishi vijiji hawajui sheria, hawajui namna gani ya kuendesha kesi. Kwa hiyo, hii inawasaidia sana wale ambao hawana uwezo wa kulipa gharama za kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha kwamba haki inatendeka, Serikali hii imetoa fedha nyingi kuhakikisha kwamba inatoa mafunzo ya Kikatiba kwenye Halmashauri zetu. Sasa hivi kulingana na taarifa ya Mheshimiwa Waziri takribani Halmashauri 50 …

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jonas, kengele ya pili hiyo.

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, takribani Halmashauri 50 tayari zimepata elimu kwa ajili ya huduma za kisheria.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jonas, ni kengele ya pili.

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Issaay, jiandae Mheshimiwa Midimu na Mheshimiwa Mgalu atafuata.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii ya Wizara ya Katiba na Sheria. Kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya Wabunge wenzangu na Watanzania kwa ujumla, nichukue nafasi hii kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi kubwa inayofanyika nchini kwa sekta mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee, kwa jinsi ambavyo sekta ya Mahakama imepata maboresho makubwa kama ambavyo huko nyuma tulivyotoka na hivi sasa kuna mambo mengi sana yamefanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kwa namna ya pekee kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro na Naibu Waziri pamoja na timu nzima ya Mahakama kwa kazi kubwa inayofanyika nchini, pia kwa jinsi ambavyo utendaji wa Mahakama umeimarika na sekta hii imetoa matumaini makubwa kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee, pia kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mbulu na Wilaya ya Mbulu kwa ujumla, naishukuru Serikali kwa ujenzi wa Mahakama hasa Waziri Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro, nimekwenda ofisini kwake mara kadhaa na hata ndani ya Bunge hili, na katika hoja mbalimbali za kudai ujenzi wa Mahakama mpya katika Wilaya ya Mbulu na hata alipoona ile picha ya Mahakama, alisema, "wala hatutakwenda Mbulu, wacha tutafute fedha tukajenge." *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi hiyo imeanza, sasa ina karibu mwaka japo inasuasua, ni kazi nzuri kwa sababu Mahakama ilikuwa barabarani na ilikuwa haina hata sehemu ya kutosha kwa wasikilizaji kwenda Mahakamani na kusikiliza kesi za wenza wao na jinsi ambavyo zinaendeshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba walau fedha zipatikane kwa ajili ya kuleta msukumo zaidi kwenye ujenzi wa ile Mahakama, na kama Mheshimiwa Waziri alivyoahidi hivi karibuni, alisema tutakwenda Mbulu kutembelea hiyo Mahakama, lakini nadhani kama hatutapata fedha, hata tukienda Mbulu haitasaidia. Zile fedha zitolewe, mkandarasi yule aendelee kujenga ile Mahakama, kazi ilishaanza, inaendelea vizuri, hapa katikati kidogo imesimama kwa muda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue pia nafasi hii kupongeza *Samia Legal Aid Campaign,* hii imetoa chachu kubwa kwa Watanzania kama Wabunge wenzangu walivyozungumza, lakini pia imetoa taswira ya kiu kubwa na ushauri wangu kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, sibishani na Wabunge wenzangu, naomba kama itawezekana pengine ipate mzunguko wa mara mbili kwa mwaka katika nusu mwaka walau na nusu nyingine ili iweze kufika kwa wananchi zaidi, lakini pia kuona yale yaliyofikiwa kama yanatekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli imekuwa kiu kubwa, kwani walipokuja Mbulu Mjini, hasa tulipozindua pale Manyara na baadaye ilipokuja Mbulu Mjini na Wilaya nzima ya Mbulu ilifanya kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali iangalie muundo wa mashtaka ama wa malalamiko yaliyo kwenye ule muundo yachujwe badala ya kwamba, wakija wale Maafisa kutoa ile huduma ya kuwasikiliza, basi walau kuwe na mchujo wa hoja zinazoenda pale kwa ajili ya kuwaelimisha wananchi. Kwa sababu nyingine zilikuwa zinaenda wala hazikuhitaji zile *level* ama kwa zile ngazi ambazo wamekwenda wale wananchi na ikawa ni kama vile muda hautoshi na idadi ya watu ni kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee, naomba pia Serikali itoe fedha. Nilipozungumza na Mheshimiwa Waziri kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama, ni kwamba kidogo ilikuwa inasuasua

kwa sababu ya upatikanaji wa fedha, na bajeti ya ujenzi kama tulivyosomewa na Waziri ilikuwa ni kiasi kidogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali ijitahidi ili hii miradi ambayo tulitarajia ikamilike kwa mwaka ule wa fedha uliotengwa, basi ikamilike kwa wakati na Wizara ipate fedha za miradi na fedha za uendeshaji, kwa sababu kadri ambavyo fedha za miradi zinakwama, ndivyo inaenda kufumua bajeti ya mwaka mwingine unaokuja; na kwa sababu hiyo, bajeti zetu zinaakisi mafanikio kidogo kwa ajili ya zile fedha za mwaka wa kwanza zinakuja kuvuruga bajeti ya mwaka unakuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, rai yangu kwa Serikali ni kwamba tujitahidi kuona namna ya kupata fedha hizi na namna ya utekelezaji wake na usimamizi ulio mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Mbulu ni Wilaya kongwe iliyoanzishwa na wakoloni. Kuna Tarafa zilikuwa na Mahakama za Mwanzo, sasa hivi kumebaki magofu, lakini pia huduma wananchi wanafuata pale Mjini na kwenye Tarafa kama za Haydom, Dongobesh na Tarafa ya Nambis ambayo ilikuwa na Mahakama mbili za wakoloni, ambazo hadi sasa ni magofu takribani miaka mingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kama inawezakana badala ya kujenga ngazi za kata, hebu Serikali itazame muundo wetu utoke kwenye ngazi ya mikoa, baadaye ngazi za wilaya, baadaye ngazi ya Mahakama za Mwanzo kwenye tarafa zetu nchini na hatimaye tunakwenda kwenye kata za kimkakati kulingana na jiografia ilivyo ili wananchi waweze kuhudumiwa katika huduma hii ya kupata haki za kisheria kwa karibu zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakumbuka tulipitisha utaratibu wa kuwa na wasaidizi wa kisheria na wakaajiriwa nadhani kwa sehemu kidogo kutokana na uwezo wa Serikali. Nilikuwa nashauri kwamba wasaidizi wale wa kisheria wangeajiriwa kwenye ngazi za Halmashauri ili kusaidia kesi nyingi zinazotokea baina ya wananchi kwenye vijiji vyao, kwa kata zao, kwa mali zao pamoja

na watu binafsi kusaidia maeneo hayo ambayo yatasaidia kwenye maeneo ya wananchi, lakini kwenye maeneo ya wale watu ambao...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Issaay, ni kengele ya pili. Ahsante kwa mchango mzuri.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Namwita sasa Mheshimiwa Midimu, atafuatiwa na Mheshimiwa Mgalu, jiandae Mheshimiwa Naibu Waziri.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi niweze kuchangia. Naomba nikupongeze kwa kazi nzuri unazozifanya. Umefanya kazi nzuri sana, na ninawaomba wananchi wa Ilala wakurudishe tena, kwani tunakupenda sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, nampongeza Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dkt. Tulia, amefanya kazi nzuri sana, na ninaendelea kusisitiza kuwaomba wananchi wa Mbeya waturudishie Mheshimiwa Dkt. Tulia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri wa Katiba na Sheria pamoja na Naibu, wamefanya kazi nzuri sana. Nampongeza Mheshimiwa Rais, kwa jengo zuri kubwa la Mahakama Kuu hapa Dodoma, ni jengo zuri sana la kwanza katika *East Africa* na Afrika ya Kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuanzisha kampeni ya msaada wa kisheria kwa wananchi. Kampeni hiyo imesaidia sana wananchi wetu hasa akina mama, walikuwa wanadhulumiwa ardhi, haki zao walikuwa hawajui wakimbilie wakazipate wapi? Mambo ya mirathi, sasa hivi

wananchi, hasa akina mama wanajua sehemu ya kwenda kupata haki. Kwa hiyo, kampeni hizi zimesaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, lakini kampeni hizi zinakomea Wilayani, kwa hiyo, naiomba Serikali kampeni hizi za msaada wa sheria zishuke kwenye kata. Pia naiomba Serikali kampeni hizi ziwe ni endelevu kwa vile zimesaidia wananchi sana, na wananchi wengi wanakimbilia kupata msaada. Hongera sana Mheshimiwa Rais kwa kuanzisha jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kusogeza Mahakama karibu na wananchi, imepunguza usumbufu. Wananchi wengi walikuwa wanapata taabu kwenda sehemu 'A' kwenda kupata haki zao. Naipongeza sana Serikali kwa Mkoa wetu wa Simiyu kwa kujengewa Mahakama katika Wilaya zote za Mkoa wa Simiyu nne. Kwa mfano, Wilaya ya Busega imejengwa Mahakama nzuri sana ya kisasa, Wilaya ya Bariadi imejengwa Mahakama nzuri sana ya kisasa, Wilaya ya Maswa imejengwa Mahakama nzuri sana ya kisasa na Wilaya ya Itilima imejengwa Mahakama nzuri ya kisasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninalo ombi kwa Wilaya ya Meatu. Mahakama ya Wilaya ya Meatu, majengo yamechakaa sana. Naomba Wilaya ya Meatu tujengewe Mahakama mpya. Maendeleo yana wivu, Wilaya ya Meatu wakiona Wilaya zote kwa Mkoa wa Simiyu; tuna Wilaya tano ambazo tumejengewa Mahakama mpya, wananchi wa Meatu wanakuwa na wivu kwa sababu majengo yao yamechakaa sana. Kwa hiyo, tunaomba kujengewa Mahakama mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Mahakama kwa kuweka mifumo ya kisasa ya uendeshaji wa Mahakama na kusaidia sana utoaji wa haki kwa wananchi. Nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri sana alizozifanya kwa miaka minne. Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya kazi nzuri sana, lazima apewe maua yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kura atakazozipata haijawahi kutokea, kwa vile

amefanya kazi nzuri sana. Nampongeza sana, na Mwenyezi Mungu ambariki Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mama yetu atembee kifua mbele, sisi watoto wake tupo, atashinda kwa kishindo. Tutatafuta kura kona kwa kona, uvungu kwa uvungu, kitanda kwa kitanda lazima kieleweke kwa Mheshimiwa Rais. Mtu mzima hatishiwi nyau, Mheshimiwa Rais hatatishwa na kitu chochote, ushindi lazima tushinde, lazima tuongoze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu gani kinachowafanya wapige kelele na kumtukana Mheshimiwa Rais? Hatutakubali, hatupo tayari kusikiliza matusi wanayomtukana na tukayavumilia. Lazima tutawajibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo yangu ya kuchangia ni hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Subira Mgalu, jiandae Naibu Waziri na Mheshimiwa *Attorney General* jiandae.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi kuwa mchangiaji wa mwisho wa upande wa Wabunge jioni ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro, Naibu Waziri, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Katibu Mkuu Ndugu Maswi kwa kazi nzuri wanayoifanya pamoja na watendaji wote pamoja na Prof. Elisante Ole Gabriel kwa kazi nzuri aliyofanya katika Mhimili wa Mahakama, lakini pia pamoja na Mhimili wote, Jaji Mkuu, kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama kuchangia bajeti hii, kwani kwa miaka mitano ya Bunge sijawahi kuichangia bajeti hii, lakini safari hii nimewiwa kuchangia bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kutokana na kazi nzuri iliyofanywa na Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuhakikisha Mhimili wa Mahakama unafanya kazi yake nzuri ya kuwa mamlaka ya mwisho ya utoaji haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Serikali ya Awamu ya Sita Kamati yetu ya Bajeti imeshuhudia Mfuko wa Mahakama ukitendewa haki na kupatiwa bajeti ya kutosha ambayo imeimarisha miundombinu ya Mahakama ikiwemo jengo la pekee ambalo limepatikana awamu hii baada ya miaka 104 pamoja na maboresho ya Mahakama mbalimbali katika mikoa na wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Rais kwa ujenzi wa Mahakama za Mwanzo zinazoendelea Mkoa wetu wa Pwani ikiwemo Mahakama ya Msata ambayo ipo Wilaya ya Bagamoyo, Mahakama ya Kimanzichana ambayo ipo Wilaya ya Mkuranga na Mahakama ya Bungu ambayo iko Wilaya ya Kibiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu Serikali iendelee kutenga fedha kwa sababu mahitaji ya ukarabati wa Mahakama za Mwanzo ni mkubwa, ikiwemo Mahakama zilizochakaa. Kwa mfano, Mahakama ya Kiwanga ipo Chalinze, Mahakama ya Mwambao, tuna Mahakama pia kule Miono, zote zinahitaji ukarabati mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, nimesimama kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Pwani kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna programu hii ya *Mama Samia Legal Aid* ilivyofanya vizuri, ilifika Mkoa wetu wa Pwani na wanawake wengi walijitokeza, lakini kipekee kwa namna ambavyo kampeni hii imefikia zaidi ya wananchi 2,600,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii pia imenzisha madawati katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 184 ambayo wananchi zaidi ya 6,000,000 wamefikiwa na huduma mbalimbali za kisheria, na tumeona migogoro ya ardhi ikitatuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wiki iliyopita UWT tulikuwa na semina, nimshukuru Waziri Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro, pamoja na Katibu Mkuu Ndugu Maswi kwa namna walivyotupitisha kwenye mafanikio makubwa, pia kwa namna ya kipekee wanavyoshirikiana na Umoja wa Wanawake wa Tanzania kwa

kuwa tumeunda Kamati ya Katiba na Sheria, nasi tunaunga mkono *Mama Samia Legal Aid* na tumeshafanya utoaji wa msaada wa kisheria katika Mkoa wa Dodoma na Tanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Naibu Waziri, Mwenyekiti wetu, Wakili Msomi Mheshimiwa Zainab Katimba, kwa kufanya vizuri. Hii UWT ndiyo ambayo kupitia uongozi wa hayati Mama Sofia Kawawa ndiyo ilianzisha Shirika la *SUWATA* ambalo lilikuwa linatoa huduma za sheria, lakini hili Shirika hata kuhamasisha Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971, pia ilishiriki katika kuhakikisha Sheria ya Kazi ya mwaka 1975 inaweka kipengele cha likizo ya uzazi kwa makundi yote ya wanawake bila kuzingatia hali ya ndoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kinachofanyika sasa Umoja wa Wanawake Tanzania chini ya Mama Chatanda ni mwendelezo wa UWT ya Marehemu Mama Sofia Kawawa na Mwenyezi Mungu ampumzishe kwa amani. Ndiyo maana tunaona kwa mara ya kwanza Serikali hii inapoongozwa na Mheshimiwa Rais wetu mwanamke, kwa kuzingatia kwamba wahanga wakubwa wa changamoto za upatikanaji wa sheria ni wanawake ameanzisha hii programu ya *Mama Samia Legal Aid,* tunampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, waliofikiwa na programu hii zaidi ya 9,000,000 kwa namna moja au nyingine, 2,600,000 wale wa madawati ya kisheria kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa zinamshukuru, na ni miongoni mwa watu ambao watampigia kura za kishindo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho, naipongeza Serikali kwa kuendelea kulinda Katiba yetu, kuendelea na maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025. Sisi tunasema tayari maboresho yamefanyika ya kuwezesha mazingira ya kufanyika kwa uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria tatu tulizopitisha hapa Bungeni ambapo watu wengi walishiriki ikiwemo taasisi zetu za kidini, ikiwemo wadau mbalimbali wa siasa, wameshiriki kuanzia

kutoa maoni wakati wa kikosi kazi pia walikuja hapa Bungeni wakati wa kusikiliza maoni yao kwenye Kamati. Kwa hiyo, tunaamini mazingira haya yaliyotengenezwa, yatauwezesha uchaguzi kufanyika kuwa huru na wa haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwapongeza Serikali na kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa maboresho haya, na niwatakie heri Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa maandalizi yanayoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja hii na kuwapongeza wote. Ahsante sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee naomba kuungana na Watanzania wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa kutimiza vyema miaka minne kwa kuongoza nchi yetu akiwa Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshuhudia mafanikio makubwa katika kuimarisha miundombinu hususan barabara, reli, viwanja vya ndege, bandari, huduma za kiuchumi na kijamii kama vile ujenzi wa madarasa, hospitali, zahanati na vituo vya afya, huduma za maji, utawala bora, pamoja na kuhamasisha uwekezaji na utalii. Pia naomba nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri iliyotukuka ya kumsaidia Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, kwa kuteuliwa kuwa Mgombea Mwenza wa nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa uzoefu na weledi wake, kama ilivyo kwa Watanzania walio wengi, nina imani kubwa kwa Mheshimiwa Nchimbi na kumtakia afya njema na kila la heri kwenye mchakato ujao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Mbunge, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa kutekeleza majukumu ya kumsaidia Waziri Mkuu, ikiwa na pamoja na jukumu la kuendelea kuisimamia ipasavyo sekta ya nishati.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi na Spika na pia uongozi wote wa Bunge kwa uongozi mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro, Mbunge na Waziri wa Katiba na Sheria kwa hotuba nzuri iliyojaa ubunifu mkubwa na imedhihirisha utayari wa Taifa letu katika ya ushindani wa Kimataifa *(National competitiveness)*. Bajeti hii ambayo ni ya mwisho, inaenda sambamba na Dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 ambayo ni Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi chake akiwa Waziri wa Katiba na Sheria, tathmini zinathibitisha mafanikio makubwa ya utekelezaji na usimamizi wa Mpango wa Kwanza na wa Pili na kupelekea Taifa letu la Tanzania kufanya vizuri mno katika mazingira ya kuboresha huduma ya kutoa haki kwa wananchi, na Tanzania inaongoza katika nyanja nyingi ukilinganisha na nchi nyingi duniani na hata Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Ofisi ya Mahakama imefanikiwa katika kuboresha mifumo ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) ikiwemo mfumo wa usimamizi wa mashauri na kupelekea kuongeza tija katika utatuzi wa mashauri, yakiwemo yaliyodumu kwa kipindi kirefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Mahakama imeendelea kutekeleza mpango wa ujenzi na ukarabati wa majengo ya mahakama katika ngazi mbalimbali nchini ikiwemo jengo la

Makao Makuu Dodoma ambalo ni la kwanza Afrika na la sita duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza Serikali iweke mkakati wa kuboresha ufanisi kwa taasisi zote zinazofanya kazi na Mahakama, zikiwemo Polisi, Mwendesha Mashtaka na hata Mawakili ili utoaji wa huduma uendane na ufanisi uliojengeka na Mahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa majukumu yake, Ofisi ya Mahakama inaendelea kukabiliwa na upungufu wa watumishi wa kada mbalimbali na uchakavu wa majengo ya Mahakama za ngazi zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyoshauriwa kwenye taarifa ya Kamati ya Bajeti, kuna haja kwa Ofisi ya Mahakama kuongeza watumishi katika Mahakama zote nchini ili kuongeza tija na ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napendekeza Serikali kuhakikisha inatenga fedha za kutosha za maendeleo ili kuendeleza ujenzi na ukarabati Mahakama za Mwanzo, Mahakama za Wilaya, Mahakama Kuu pamoja na nyumba za Majaji ili kuboresha na kusogeza huduma hii muhimu kwa wananchi. Mkazo wa elimu ulenge kujenga uwezo wa masuala ya mikataba ya Kimataifa na hasa *negotiations skills* za Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Mbeya bado ina changamoto za uhaba wa Mahakama za Mwanzo na inapelekea wananchi kusafiri umbali mrefu kupata huduma ya Mahakama ya Mwanzo. Mji Mdogo wa Mbalizi wenye idadi ya watu zaidi ya 100,000 ina Mahakama ya Mwanzo ambayo ni ndogo sana na chakavu ambayo ni hatarishi kwa usalama na afya ya watumishi na hata wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa Serikali kuanza ujenzi wa Mahakama ya Mwanzo katika eneo la Utengule Usongwe ambalo limetolewa na wananchi. Pia, naomba kuwepo

na kipaumbele cha ujenzi wa Mahakama za Mwanzo angalau mbili kwa kila Tarafa za Usongwe, Isangati na Tembela.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nampongeza sana Waziri wa Katiba na Sheria Dkt. Damas Ndumbaro, Mbunge na Naibu wake Mheshimiwa Jumanne Abdallah Sagini, Mbunge na wataalamu wa Wizara na taasisi zote zilizo chini ya Wizara hii kwa kazi nzuri wanazofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu utahusu umuhimu wa msaada wa huduma za kisheria kwa wananchi kupitia kwenye kampeni ya *Mama Samia Legal Aid.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu inaendeshwa kwa kuzingatia utawala wa sheria na misingi ya haki za binadamu. Vyombo vya sheria nchini vina jukumu la kusimamia utoaji haki, hifadhi ya Katiba, kutoa ushauri wa kisheria kwa Serikali na taasisi zake, kusimamia hifadhi za haki za binadamu na kuhakikisha sheria na taratibu za nchi zinafuatwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mhimili mkubwa wa utawala wa sheria ni Mahakama. Kazi kubwa ya Mahakama ni kuhakikisha usawa mbele ya sheria kwa watu wote. Katika kutoa haki, Mahakama hutumia mfumo wa wataalamu mbalimbali ambao hutafsiri sheria na kufikia mwafaka wa kutoa haki. Wataalamu hao ni pamoja na Waendesha Mashtaka, Mawakili/Wanasheria na Mahakimu au Majaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakili ni mtaalamu wa sheria anayepewa leseni ya kutoa ushauri wa kisheria na kuwakilisha wateja katika masuala mbalimbali ya kisheria. Wakili anaweza kuwa mtu ambaye amehitimu katika taaluma ya sheria, amefuzu mafunzo ya sheria na kisha kupokea leseni ya kufanya kazi ya uwakili. Kwa upande mwingine, mwanasheria ni mtu yeyote aliyesoma kozi ya sheria katika chuo kinachotambulika na kuhitimu na kufaulu na kupata Shahada ya Sheria *(LLB)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nchi yetu, Mawakili na Wanasheria huchukua jukumu kuu katika mfumo wa sheria kwa kuwa na uwezo wa kufafanua sheria, kutoa ushauri wa kisheria. Mawakili huwakilisha wateja Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mawakili wa Serikali ni watumishi wa Serikali na jukumu lao kubwa ni kutetea maslahi ya Serikali. Vilevile Wakili wa Serikali humsaidia mwananchi yeyote ambaye ana kesi kubwa kama ya mauaji au uhaini ambazo hukumu zake ni kifo. Kwenye hizi kesi kubwa, Serikali inamwekea mshtakiwa wakili wa kumtetea na analipwa na Serikali yenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mawakili binafsi, wamejiajiri na huduma wanayotoa hulipiwa na mteja. Kwa mantiki hii, wananchi wengi binafsi wanaohitaji huduma za kisheria wanapata huduma kutoka kwa mawakili binafsi kwa malipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mawakili binafsi wanalipwa, wananchi wanaohitaji huduma ya kisheria na wasioweza kumudu gharama za mawakili huishia kukosa huduma za kisheria. Kwa sasa hapa Tanzania, mwananchi wa kawaida akiwa na kesi inayohitaji wakili, huwa gharama za wakili ni kubwa sana na wengi hawazimudu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwa kuwa Wakili au Mwanasheria wa Serikali hawajibiki kusaidia wananchi mwenye tatizo binafsi la kisheria, basi kimbilio la wananchi lina mgogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, liwe liwalo, kupata wakili au mwanasheria ni hatua muhimu katika kuhakikisha kuwa haki za wananchi wasio na uwezo, zinalindwa na masuala ya kisheria yanashughulikiwa ipasavyo. Ni kwa mantiki hiyo nawiwa kuipongeza Wizara ya Katiba na Sheria kwa kuanzisha programu ya kutoa msaada wa huduma za kisheria kwa wananchi bure kupitia Kampeni ya *Mama Samia Legal Aid*. Katika miaka ya awali, kampeni hii itafanyika kwa miaka mitatu ambapo itahitimishwa mwezi Februari, 2026 katika mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar. Kampeni hii ni kielelezo kwamba *Rais Samia* anataka kumfikia kila Mtanzania anayehitaji huduma za kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, programu hii imekuwa ni ukombozi mkubwa, kwani huduma za kusaidiwa kisheria zimewafikia wananchi wasio na uwezo wa kulipia gharama za uwakili ili kupata huduma za kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia ni utekelezaji wa Rais Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha wananchi wanasaidiwa katika matatizo yote ya kisheria bila malipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla, zoezi la kutoa msaada wa kisheria katika mikoa tofauti limefanyika kwa mafanikio, kwani maelfu ya wananchi wameshafikiwa na huduma, wanaume na wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya Waziri, tumeambiwa kwamba tangu kuzinduliwa kwa kampeni hii, tarehe 27 Aprili, 2023, jumla ya mikoa 25 imefikiwa na Kampeni (Dodoma, Manyara, Shinyanga, Ruvuma, Simiyu, Singida, Iringa, Mara, Songwe, Morogoro, Njombe, Katavi, Tabora, Geita, Kigoma, Mtwara, Kilimanjaro, Mwanza, Mbeya, Lindi, Rukwa, Pwani, Arusha, Tanga na Kagera) na upande wa Tanzania Bara Mkoa uliobaki ni Dar es Salaam ambapo kampeni itatekelezwa ifikapo Juni, 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri ametueleza kwamba katika utekelezaji wa kampeni hiyo, wananchi wamepatiwa huduma mbalimbali ikiwemo elimu kuhusu masuala ya haki na wajibu; umiliki na utatuzi wa migogoro ya ardhi; matunzo ya watoto; utatuzi wa migogoro ya ajira na mahusiano kazini; ukatili wa kijinsia; wosia, mirathi, ndoa na familia; usajili wa matukio muhimu ya binadamu; na haki za binadamu. Aidha, kupitia mada zinazotolewa, wananchi wamepata fursa ya kuuliza maswali kuhusu masuala ya kisheria na kupatiwa majibu papo kwa hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumejulishwa kwamba kupitia kampeni hiyo, jumla ya halmashauri 180, kata 1,907 na vijiji/mitaa 5,702 zilifikiwa na jumla ya wananchi 2,698,908; wanaume

1,347,325 na wanawake 1,351,583 walifikiwa na kupata elimu ya huduma za kisheria kupitia mikutano ya ana kwa ana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeambiwa kwamba kupitia Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia, jumla ya migogoro 24,691 iliyodumu kwa muda mrefu ilipokelewa ambapo baadhi ilidumu kwa zaidi ya miaka kumi. Utatuzi wa migogoro hiyo umewezesha kuimarisha amani, utulivu na utengamano miongoni mwa wanajamii, kwani umeacha pande zilizokuwa na migogoro zimeelewana.

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro iliyoshughulikiwa ilihusisha masuala ya ardhi, ndoa za utotoni, matunzo ya watoto, madai, ndoa, jinai, ukatili wa kijinsia, ardhi, ajira na mengineyo. Aidha, jumla ya migogoro 5,704 ilitatuliwa na kuhitimishwa kwa njia mbadala kati ya migogoro 23,399 ya muda mrefu iliyopokelewa. Utatuzi wa migogoro 18,987 unaendelea katika ngazi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaishukuru sana Serikali, kwani kampeni ya *Mama Samia Legal Aid* imejikita katika kutoa elimu ya kisheria kwa wananchi hasa katika masuala ya ukatili wa kijinsia, migogoro ya ardhi, mirathi na usuluhishi wa migogoro kwa njia mbadala na masuala yanayohusiana na haki za binadamu kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo kuu la kampeni hiyo inayotekelezwa na Serikali kupitia Wizara ya Katiba na Sheria ni kulinda na kukuza upatikanaji wa haki kwa wote kupitia huduma ya msaada wa kisheria nchini huku ikitarajiwa kuleta mabadiliko chanya katika jamii na kuboresha upatikanaji wa haki kwa watu wote, bila kujali hali zao za kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufanikisha programu hii, utekelezaji wa kampeni umefanyika kwa kushirikiana na Wizara na Taasisi za Serikali, Asasi za Kiraia, Wanazuoni na wadau mbalimbali wa maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya muda mrefu wa kampeni hii ni kuchangia katika kuboresha upatikanaji wa haki kwa watu wasiojiweza, hususan wanawake, watoto na watu maskini walio katika mazingira magumu. Vilevile itachangia kuimarisha amani na utulivu hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, inategemewa kwamba jambo hili jema litaimarisha mfumo wa utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria katika ngazi za Serikali Kuu hadi Serikali za Mitaa na hatimaye itapunguza idadi ya migogoro na matukio yanayotokana na ukosefu wa uelewa wa sheria na kuimarisha uwajibikaji na uwezo wa taasisi za Serikali na zisizo za Kiserikali kwenye kutoa huduma za msaada wa kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maoni yangu, kampeni ya *Mama Samia Legal Aid* ni fursa pekee iliyotolewa kuwakomboa wanyonge wanaopitia dhuluma mbalimbali kwa kutoelewa sheria hapa nchini. Kwa kiwango kikubwa hili jambo linafanikishwa kupitia kwa wasomi wetu ambao ni Wanasheria na Mawakili wa Serikali na wale waliojiunga kwenye hili jambo jema na la heri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kampeni hizi zitatoa msaada wa kisheria kwa raia wa Tanzania wa kipato cha chini. Huduma hizi zitachangia kwenye kurudisha haki na utulivu kwa raia na familia maskini hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kazi iliyofanyika, nichukue nafasi hii kuwapongeza watekelezaji wa Programu ya *Mama Samia Legal Aid*. Mpaka sasa wamefanikiwa kutatua matatizo mengi kwenye maeneo waliyopita. Pia wameandaa ushahidi na kukabidhi kwa mamlaka zinazohusika katika kutoa haki ili waathirika waweze kusaidiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali kampeni hizi zisiishie mwezi Februari, 2026 bali ziwe ni kitu cha kudumu na endelevu. Kwa kufanya hivyo, Rais Samia atakuwa ameacha alama kubwa katika kipindi cha utawala wake, kwani programu hii imekuwa msaada mkubwa kwa wananchi kwa kutatua migogoro mbalimbali ya kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia kampeni hizo, Watanzania wamepata nafasi ya kusikilizwa na Mawakili waliobobea huku migogoro mingi ikipatiwa ufumbuzi wa papo hapo, na mingine ikipelekwa kwenye vyombo vya kutoa haki. Hivyo basi, inatakiwa kampeni hii iwe endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Katiba na Sheria, dakika kumi.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba nianze kutumia fursa hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuwa na afya njema iliyotuwezesha kukutana mchana huu kujadili hoja ya Mheshimiwa Waziri Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Waziri wa Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa imani yake kwangu na kunifanya niendelea kuwa msaidizi wake katika nafasi ya Naibu Waziri wa Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, ninashukuru taasisi zilizo chini ya Wizara na Mhimili wa Mahakama kwa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi, na pia kwa ushirikiano mkubwa wanaotupatia, Mheshimiwa Waziri pamoja na mimi kama Naibu Waziri. Nawashukuru viongozi wengine wa Kitaifa, akiwemo Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na Naibu Waziri Mkuu kwa miongozo yao inayotuwezesha kutimiza majukumu yetu kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na Wabunge, kama alivyozungumza Waziri wangu katika kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi nzuri anayoifanya, kuliongoza Bunge lako Tukufu. Aidha, nikupongeze wewe binafsi kwa mwongozo wako mzuri katika kumsaidia Spika kutekeleza majukumu yake. Nami

niungane na waliosema kuwaomba wananchi wa Majimbo haya mawili ya Mbeya Mjini pamoja na Ilala kuhakikisha wanawapa kura nyingi za kishindo na mweze kurejea na kuendelea kuliongoza Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyowashukuru Waziri wa Katiba na Sheria alipokuwa akiwasilisha bajeti yake, napenda kutumia fursa hii kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mbunge na Mwenyekiti wa Kamati, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Florent Kyombo na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti chini ya uongozi wa Mheshimiwa Oran Manase Njeza, kwa ushauri na miongozo yao iliyoiwezesha Sekta ya Katiba na Sheria kutimiza majukumu yao vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, naomba kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro, Waziri wa Katiba na Sheria, kwa namna anavyotuongoza sisi wasaidizi wake na *management* ya watumishi wengine wa Wizara katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria na taasisi zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, nawashukuru *Management* ya Wizara, Taasisi za Wizara pamoja na Mhimili wa Mahakama kwa kutupatia ushirikiano mkubwa, kutuwezesha kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba uridhie niwashukuru wananchi na wapigakura wa Jimbo la Butiama kwa ushirikiano wanaonipa mimi Mbunge wao, hasa ninapotekeleza majukumu mengine ya Kitaifa, hususan kwa nafasi ya Naibu Waziri wa Katiba na Sheria. Pia nawashukuru viongozi wa Chama Cha Mapinduzi ngazi ya wilaya na mkoa kwa uongozi wao ulioniwezesha kutimiza wajibu wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee, naishukuru familia yangu, hususan mke wangu kipenzi Bi. Mariam Sagini, watoto wangu ambao leo wamewakilishwa na Bi. Leila, Mama yangu Mzazi Zena Sagini kwa ushirikiano na dua

wanazoniombea ninapotekeleza majukumu ya Naibu Waziri wa Katiba na Sheria pamoja na Ubunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, naomba nitumie fursa hii kutoa maelezo kwa baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge, hususan kwenye sekta ya Mhimili wa Mahakama. Kwanza, niwashukuru Wabunge wote kwa pongezi kubwa walizozitoa kwa Mhimili wa Mahakama kwa mageuzi makubwa na uboreshaji wa miundombinu inayosaidia kutoa haki kwa wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, tunakiri, ni kweli, jengo lile lililojengwa ni kubwa, la kisasa na hakuna mfano wake Afrika na tumeambiwa ni jengo namba sita. Pongezi kwa Mtendaji Mkuu wa Mahakama, Jaji Mkuu na Mhimili wote wa Mahakama kwa ubunifu na kuja na jengo lililo bora sana. Nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa fedha zilizowezesha ujenzi huo kufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, yameelezwa mambo mbalimbali hapa, hususan upungufu wa watumishi katika Sekta ya Mahakama. Ni kweli kwamba, upungufu huo upo, lakini tunaishukuru Serikali ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kutoa vibali vya ajira kila mwaka, ili kuipunguzia Sekta ya Sheria upungufu wa wafanyakazi. Kwa mfano, mwaka uliopita, 2024 Mahakama ilipewa kibali cha kuajiri watumishi 522 na mwaka huu wameruhusiwa kuajiri watumishi 1,044. Kwa mwelekeo huo, tutaendelea kutatua tatizo la upungufu wa watumishi wa Sekta ya Mahakama hadi pale tutakapolimaliza kabisa, hususan kutegemea bajeti yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, limezungumzwa suala la uchakavu wa miundombinu ya Mahakama, hususan Mahakama za Mwanzo na baadhi ya Mahakama za Wilaya kwamba, zilijengwa wakati wa kipindi cha mkoloni.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua changamoto hii. Ni kwa msingi huo Mahakama iliweza kuandaa mpango wa maboresho ya Sekta ya Mahakama ikiwa ni pamoja na kujenga

miundombinu ya Mahakama Kuu, Mahakama ya Rufani, Mahakama za Hakimu Mkazi Ngazi ya Mkoa, Mahakama za Wilaya na Mahakama za Mwanzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, imeshauriwa hapo kwamba, kwa kuwa, kata zetu ni nyingi na tunazo tarafa ambazo zinakadiriwa kufikia karibu 1,000 ni muhimu tungewekeza kwenye ujenzi wa Mahakama ngazi ya tarafa badala ya kwenda kwenye kata ambazo hatujafika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wizara, tunachukua ushauri huo kwa madhumuni ya kuhakikisha kwamba, tarafa zetu zote zinafikiwa na Mhakama, halafu baada ya hapo ndiyo twende kwenye ngazi ya kata.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme mpango tunaoendeleanao sasa hivi, ni kuimarisha Mahakama ngazi ya Mahakama Kuu, Mahakama Jumuishi Ngazi ya Mkoa, na tunakwenda kwenye Mahakama za Wilaya na tunaendelea na hizi Mahakama 72 tulizoanzanazo katika awamu hii tunayoendelea nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahakama itaendelea kutekeleza mpango wake wa ujenzi na ukarabati wa majengo ya Mahakama, kama ilivyoombwa na Wabunge wa majimbo mbalimbali. Tunafahamu Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mbeya ameongea juu ya Mahakama ya Ileje. Nimhakikishie Mbunge kwamba, mpango wa kuijenga Mahakama ya Wilaya ya Ileje upo na utendelea kutekelezwa na Mahakama kadiri ya upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, tumepata maoni ya maandishi kutoka kwa Mheshimiwa Mbunge wa Kiteto, Mahakama yake ya Wilaya ya Kiteto pia ipo kwenye mpango huo, itatekelezwa sanjari na mpango mwingine wa ujenzi na ukarabati wa Mahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ombi la kuanzisha Mahakama, Ngazi ya Wilaya ya Mlimba, ni kweli, Mahakama inao

mfumo unaozingatia utawala wa Serikali Kuu. Kwa hiyo, kwa vile hakujaanzishwa Wilaya ya Mlimba, inakuwa vigumu sana kwa Mahakama kuanzisha Wilaya katika Jimbo la Mlimba, lakini tunamhakikishia, pale itakapofika Mlimba kuwa na sifa za kuanzisha Wilaya kwa taratibu za TAMISEMI, Mahakama pia itajipanga kupeleka Mahakama ya Wilaya katika ngazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, umetolewa ushauri mwingi kuhusu uimarishaji wa utoaji wa haki kwenye Mahakama zetu, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, ushauri wote utachukuliwa na kufanyiwa kazi kwa sababu, ni dhamira ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kuhakikisha kwamba wananchi wanapata haki, na ndiyo maana mtaona Mheshimiwa Waziri atazungumzia habari ya utoaji wa msaada wa kisheria wa *Mama Samia Legal Aid Campaign.* Ni dhamira yake kuona kwamba, Watanzania wanapata haki, hivyo, Mahakama itaendelea kuimarishwa ili kuona haki hiyo inawafikia wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo ninaunga mkono hoja, nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mwanasheria Mkuu wa Serikali, dakika kumi, na mtoa hoja jiandae.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hotuba ya bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria. Nitumie nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kuniteua kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Vilevile, nichukue nafasi hii kumpongeza kwa uongozi wake mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, nichukue nafasi hii kumpongeza Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na kumshukuru Mheshimiwa Jaji Mkuu, Spika wa Bunge, na wewe mwenyewe; Mawaziri, Waziri wa Katiba na Sheria, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na uongozi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kazi nzuri wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuchangia kwa baadhi ya Wabunge ambao walitoa maoni yao. Nianze na Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, ambaye alizungumzia suala la majadiliano ya mikataba kuchukua muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwa yakini kabisa, kwa asilimia kubwa ya mikataba, ambayo Taifa hili tunajadili inachukua muda ambao ni muafaka na wa kawaida ndani ya misingi ile ya majadiliano. Ni kweli, ipo mikataba michache ambayo imechukua muda mrefu kama alivyotaja, lakini niseme kwamba, mikataba mikubwa na ya kimkakati kwa kawaida inachukua muda mrefu kwa sababu mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ile *complexity* ya *regime* ya mambo ambayo mnayajadili; unazungumzia *technical issues, business case* yenyewe, *legal regime, investment regime, tax regime, liability regime, security regime* na mambo mengine, *including pecuniary issues.* Kwa hiyo basi, ni kawaida sana majadiliano ya mikataba mikubwa kama hii kuchukua muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe mifano ya mikataba ambayo pia imechukua muda mrefu duniani. Kwanza ni *Gabčíkovo-Nagymaros Project;* huu ni Mradi wa Kujenga Bwawa la Umeme ambapo majadiliano kati ya Hungary na Czechoslovakia yalichukua miaka 20 kwa sababu ya *complexity* ya maeneo hayo ambayo nimeyataja. Ilikuwa ni kuanzia mwaka 1950 mpaka 1977 walipomaliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, majadiliano kati ya Marekani na Canada juu ya ujenzi wa bwawa la umeme katika Mto Columbia yalichukua miaka 49. Kwa nini? Kwa sababu ya *complexity* ya *issue* na kila upande unataka kuvutia kwenye maslahi yake kuangalia maeneo yote yale ambayo nimeyataja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi za Ulaya, majadiliano ya matumizi ya *River Rhine,* kule Ulaya, *round* ya kwanza yalitumia miaka 17 mpaka walipokuja ku-*conclude*. Kwa hiyo, niwatoe wasiwasi, ni kawaida, hasa katika miradi mikubwamikubwa kama

hii yenye *complexities of regime,* ambapo kila upande unataka kuhakikisha kwamba, wakimaliza wanatoka na mkataba mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mkataba wa *LNG* halikadhalika na Mkataba wa Liganga na Mchuchuma ina-*involve complexities of regime*. Tunataka kuangalia mambo mengi. Tunataka itakapokamilika iwe mikataba ambayo ina maslahi kwa Taifa hili, lakini kwa upande mwingine nao wanataka uwe na maslahi kwao. Ni kawaida sana kwa mikataba hii kuchukua muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la usikilizwaji wa mashauri kwa njia ya mtandao, na hapa nasikitika sana, hasa ninaposikia kauli za baadhi ya wanasheria wengine wakisema kwamba, suala hili ni uvunjwaji wa Katiba na Sheria, inasikitisha sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wito wangu ni kwamba, tuache kufanya hivyo kwa sababu, sisi katika Sekta ya Sheria tulisema Taifa hili linasonga mbele na ku-*support* ukuaji wa uchumi. Tuliamua kwa makusudi kama Taifa, tu-*embrace technology* na sisi katika Sekta ya Sheria tutafanya hivyo, tuta-*embrace* TEHAMA. Kwa hiyo, ku-*embrace* TEHAMA, ni jambo la muhimu na ni la msingi kwa maendeleo ya Taifa lolote. Hata katika Sekta ya Sheria, tulisema hatutakaa nyuma katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo basi, katika Sheria ya Usimamizi wa Haki na Matumizi ya Sheria *(Judicature and Application of Laws Act,* Sura ya 358) ukipitia Kifungu cha Nne tuliamua kwa makusudi kabisa, kama Taifa, kutengeneza kanuni za usikilizwaji wa mashauri kielektroniki nje ya Mahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni suala la Kisheria na asitokee mtu akasema kwamba, suala hili siyo la kisheria, huo ni uongo na upotoshaji. Ni suala la kisheria; na kwa nini tulifanya hivyo? Kwa sababu yapo mazingira mbalimbali ambayo, kama Taifa, tuliyabaini na tuliona kwamba, tunapokwenda huko mbele, lazima tuje na utaratibu ambao tunaweza ku-*embrace* TEHAMA

katika utoaji wa haki katika usimamizi wa haki na matumizi ya Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, katika kanuni zile za mwaka 2021 nilizozisema, Kanuni za Usikilizwaji wa Mashauri Kielektroniki nje ya Mahakama *(Judicature and Application of Laws Remote Proceedings and Electronic Recordings)*, Kifungu cha Nne, nitakisoma na nitajaribu kukitafsiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunasema kwamba, "*The court may on its own motion or an application by a party allow proceedings to be conducted remotely on its own motion.*" Maana yake ni kwamba, Mahakama ita-*assess* mazingira yaliyopo siku hiyo na kuona kwamba, tulisikilizeje shauri hili, hasa kama kuna mazingira katika mitandao na *social medias* zinarushwa habari za ajabuajabu na nyingine ni za kutisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahakama jukumu lake siyo tu mashauri, lakini kuhakikisha na huko wananchi wengine waendelee na shughuli zao; shughuli za kiuchumi ziendelee. Siyo shauri linasikilizwa na kila kitu kimefungwa, barabara zimefungwa, haiwezekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mahakama iki-*assess* mazingira, inaweza ikaamua na ni kwa mujibu wa sheria na kifungu kile kimeweka utaratibu na *methods* za namna ya kusikiliza shauri kwa njia ya mtandao nje ya Mahakama na Kifungu cha Tano sasa kinaweka zile *procedures.*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukifuatilia kilichotokea tarehe 24, *procedures* zile zilikuwa *properly followed.* Sasa huyu mtu anayetokea anasema kwamba, kuna uvunjifu wa sheria. Sheria zipi? Sheria si ndiyo hii!

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ndiyo Sheria na mimi ninayezungumza hapa ndiye Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kwa hiyo, watu waache upotoshaji. Unaweza kuwa na malengo yako, lakini siyo kwa kupotosha na kusema kwamba sheria za nchi zinavunjwa, hapana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilisema nitumie fursa hii kulizungumzia hili jambo kwamba, suala hili ni kwa mujibu wa Sheria na hata siku nyingine yoyote Mahakama ita-*assess* tu mazingira na kuona isikilize wazi au isikilize kwa njia ya kimtandao nje ya Mahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawasihi sana wananchi na wanasheria wenzangu wanaojaribu kupotosha, waache kufanya hivyo kwa sababu, kufanya hivyo kunasababisha taharuki na kuwafanya wananchi waone kwamba, Serikali yao inaendesha mambo nje ya sheria, jambo ambalo siyo kweli. Mahakama haiwezi ikaamka tu asubuhi ikasema wanasikiliza kwa njia ya mtandao, hapana. Ni kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, nichukue nafasi hii kumpongeza mchangiaji, Mheshimiwa Salome Makamba, kwa uchangiaji mzuri na wa kiufundi na amechangia ndani ya sheria. Amechambua vizuri kuanzia Katiba, Sheria na mpaka ilivyoteremka kwenye Kanuni za Maadili. Kwa hiyo, nampongeza sana; Wanasheria wa namna hii tunawapongeza sana wanapokuwa wanachangia vitu ndani ya sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji, tunakushukuru kwa michango yako. Niseme tu kwamba, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali siyo tu kusubiri bajeti, kuna vitu vingi tunaweza kuvifanya kwa mazingira tuliyonayo na tutaendelea kutoa ushauri wa kisheria. Kwa mfano tu, kwa mwaka huu tunaomaliza tumetenga kiasi cha kutosha sana katika mafunzo, lakini kuna mafunzo mengine tunayafanya wenyewe bila kuhitaji fedha na jambo hilo tutaendelea kulifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nichukue nafasi hii tena kumpongeza Waziri wetu kwa uongozi wake mzuri pamoja na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na viongozi wote katika Sekta ya Sheria. Namshukuru Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mwandishi Mkuu wa Sheria kwa kazi nzuri wanayoifanya na wanavyonisaidia. Naishukuru sana Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria na Wabunge wote ambao tumekuwa tukifanya kazi pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru Wabunge wote ambao wamechangia leo kwa michango yao mizuri ambayo inalenga kuboresha sekta ya sheria kwa ujumla. Niwaombe Wabunge watuunge mkono kupitisha bajeti hii ili tuweze kwenda kuyatekeleza yale yote yaliyoelezwa na Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria katika hotuba yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima na taadhima, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ahsante kwa maelezo sahihi na mazuri. Mheshimiwa Mtoa hoja, dakika 20. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuifanya siku ya leo iende vizuri mpaka tunafikia hatua hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Rais, Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu kwa namna ambavyo wanatuongoza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru tena wewe na Mheshimiwa Spika kwa kuliongoza Bunge letu vizuri kabisa. Tunamwombea Mheshimiwa Spika na tunakuombea Mheshimiwa Naibu Spika mpate mitano tena kule Mbeya na mitano tena pale Ilala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba, na Sheria, Mheshimiwa Dkt. Mhagama pamoja na Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, ndugu yangu Mheshimiwa Njeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru wapigakura wa Songea Mjini kwa namna ambavyo wananiunga mkono, na kwa namna ambavyo tunashirikiana nao. Tunaamini kwa umoja wetu 2025 tutafanikiwa kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru familia yangu ikiongozwa na mke wangu kipenzi Bi. Flora pamoja na watoto kwa kuendelea kuniunga mkono wakati natekeleza majukumu ya Kiserikali. Namshukuru sana Mwanasheria Mkuu wa Seriali kwa ushirikiano ambao anatupatia Wizara ya Katiba na Sheria, na kwa maelezo yake mazuri ambayo ameyatoa hivi punde. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Naibu Waziri, Mheshimiwa Jumanne Sagini, Mbunge wa Butiama, naye namwombea kila la heri katika mwaka huu wa 2025. Namshukuru Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote kwa kufanikisha mambo mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge 21, ambapo 19 wametoa michango yao kwa njia ya kuongea na wawili wametoa michango yao kwa njia ya maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru Mhimili wa Mahakama kwa ushirikiano ambao wanatupatia, na leo hapa umewakilishwa vema na Mheshimiwa Profesa Elisante Ole Gabriel pamoja na Mheshimiwa Eva Nkya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Naibu Spika, ushauri wote ambao umetolewa na Waheshimiwa Wabunge kwa njia ya kuongea na kwa njia ya mdom,o tumeupokea. Tuahidi, Wizara hii ni Wizara sikivu, tutaenda kuufanyia kazi. Tutawapa majibu mengine kwa maandishi, lakini wataona utekelezaji wa mambo hayo kwa kadiri ambavyo siku zinakwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niruhusu niongee mambo makubwa matatu. Jambo la kwanza ni kuhusu Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia *(Mama Samia Legal Aid Campaign)*. Kila Mheshimiwa Mbunge aliyesimama na kuchangia kwa maandishi amepongeza kwa dhati kampeni hii na umuhimu wake katika jamii katika kuleta haki, usawa, amani, na maendeleo. Tunazipokea pongezi hizo kwa niaba ya Mheshimiwa Rais, na tutamfikishia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kampeni hii ina misingi yake. Msingi wa kwanza ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hususan Ibara ya 13(1), ambayo inasema kuwa kila mtu ni sawa mbele ya sheria. Hivyo, kampeni hii inalenga kuwafanya Watanzania wote wanapokuwa mbele ya sheria wawe sawa, na ndicho ambacho tunakitekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kampeni hii inatokana na Sheria ya Bunge, Sheria Na.1 ya mwaka 2017, Sheria ya Utoaji wa Msaada wa Kisheria, sheria ambayo Bunge hili Tukufu liliitunga ili iwasaidie Watanzania. Utekelezaji wa kampeni hii ni utekelezaji sheria hiyo ya Bunge. Hivyo, Bunge hili nalo linastahili pongezi kwa kutunga sheria ambayo inawasaidia Watanzania hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kampeni hii ni utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi hususan Ibara ya 120(b). Wakati Ilani hii inaandikwa, Mheshimiwa Dkt. Bashiru alikuwa ndiye Katibu Mkuu. Ibara ile ambayo uliiandika kipindi kile ndiyo tunaitekeleza sasa katika kuhakikisha kwamba tunawapa wananchi haki yao stahiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa mpango huu ni maelekezo mahsusi ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. Januari, 2023 Waziri wa Katiba na Sheria aliniita, akaniambia tunataka tutekeleze ilani, tunataka tutekeleze Katiba, tunataka tutekeleze sheria ili tuwafikie Watanzania wengi waweze kupata haki. Wizara ikatekeleza na leo ndiyo matunda haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeyasema haya kwa sababu ni lazima tujue kwamba kampeni hii ina misingi thabiti kabisa. Kwa misingi hiyo, kampeni hii haiwezi kufa kwa sababu imejikita kwenye misingi ambayo ipo na ni endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Wizara tumeweka mkakati. Mkakati wa kwanza, tayari kuna Maafisa Dawati katika halmashauri zote 184, ambao kazi yao ni kuendeleza utoaji wa msaada wa kisheria kipindi kile cha kampeni cha siku 10

zinapokuwa zimekwisha. Maafisa Dawati hawa wanafanya kazi nzuri kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, tumeingia makubaliano na Chama cha Mawakili Tanzania, asasi za kiraia ambazo zinatoa msaada wa kisheria, vyuo vikuu, na wadau wengine mbalimbali ili kuufanya mpango huu kuwa endelevu, na utakuwa endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Juni mwaka huu wakati tunafanya kwa Mkoa wa Dar es Salaam, tutafanya mambo makubwa mawili. Moja, ni kuhitimisha *round* ya kwanza. *Round* ya pili ni kufungua awamu ya pili ambayo itaanza mara baada ya kuhitimisha Mkoa wa Dar es Salaam, itafanya uendelevu wa mkoa huu. Tutapita tena kila sehemu kuhakikisha kwamba tunatekeleza hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya Waheshimiwa Wabunge ya kwamba tuwe na Mfuko wa Msaada wa Kisheria *(Lega Aid Fund)* tumeipokea, tutakwenda kuichakata kama Serikali, na kwa kuwa tuko kwenye mpango wa kukamilisha Sera ya Msaada wa Kisheria, hilo nalo tutalipa uzito kupitia jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo ningependa kulisema, Waheshimiwa Wabunge wamechangia sana kuhusiana na umuhimu wa kuzingatia Katiba, umuhimu wa kufanya uchaguzi, na kujibu hoja ambazo zimetolewa, zinazosema, *no reform no election*.

Mheshimiwa Naibu Spika, niruhusu niseme kidogo kuhusiana na *Reforms*. Mwaka 1958 na 1959 nchi yetu ilifanya Uchaguzi Mkuu ambao ulijikita kwenye ubaguzi wa rangi. Vyama vya siasa vilitakiwa vichague mgombea mmoja Mwafrika, mgombea mwingine Muasia au Mhindi na mgombea mwingine Mzungu kutoka Ulaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1962 tulifanya *reforms* tukayaondoa haya, tukaleta uchaguzi ambao hauzingatii ubaguzi wa rangi. Tukaendelea na uchaguzi huo chini ya mfumo wa chama Kimoja, tukiwa na Rais mmoja mgombea.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipofika mwaka 1995 – 2024 tumefanya mabadiliko. Tunafahamu, baada ya vyama vingi tuliondoa habari ya chama kimoja tukaleta vyama vingi. Tukaondoa mgombea mmoja kwenye nafasi ya Urais tukaleta wagombea wengi. Huko nyuma tulikuwa na wagombea wawili tu kwenye Ubunge, sasa tuna wagombea wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara ya mwisho mimi Songea Mjini tumegombea, ndani ya chama tu tulikuwa 31. Haya ni mabadiliko ambayo yamefanyika ndani ya mfumo wetu wa kisheria na wa Kikatiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, niruhusu niseme, kati ya mwaka 1995 mpaka mwaka 2004 tulikuwa na sheria mbili za uchaguzi; Sheria ya Taifa ya Uchaguzi ya mwaka 1985 na Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ya mwaka 1979. Tunavyoongea leo sheria hizo hazipo tena kwa sababu tumefanya mabadiliko, kuanzia mwaka 2004 kuja sasa tumefanya mabadiliko.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge, tumefanya mabadiliko makubwa 15 ambayo napenda sana tuyasikilize tuweze kuyaongea vizuri, ili ambao wanataka kutuvuruga waache kutuvuruga. Badiliko la kwanza, tumefuta Sheria ya Uchaguzi ya Taifa ya Mwaka 1985 na kazi hiyo ya kufuta ilifanywa na Bunge hili Tukufu, linastahili pongezi zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumefuta Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ya mwaka 1979. Kazi hiyo nzuri imefanywa na Bunge hili Tukufu. Bunge hili linastahili maua yake. Mabadiliko mengine ni kutunga sheria mpya ya uchaguzi wa Rais, Wabunge, na Madiwani. Siyo kufanya mabadiliko, tumetunga sheria mpya, na mnafahamu sheria hii tuliitunga mwaka jana; Februari 2024 katika Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mjadala mrefu na kushirikisha pande zote, tukapata sheria yenye vifungu 168, ikielezea kila jambo linalohusu uchaguzi, kila mchakato, na watu

wote walishirikishwa. Kama *reforms* kubwa tumezifanya Februari, 2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tujiulize, kutoka Februari, 2024 mpaka leo tunataka *reform* gani tena? Sheria hii ni mpya, haijawahi hata kutumika. Kwa hiyo, mabadiliko haya yamefanywa na chombo chenye mamlaka, ni Bunge hili Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, tumetunga sheria kwa mara ya kwanza, Sheria ya Tume Huru ya Uchaguzi ya Mwaka 2024. Tume ya Uchaguzi ilitajwa kwenye Ibara ya 74 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ilikuwa haijatajwa na sheria mahsusi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara ya kwanza tumefanya *reforms* hizi kubwa Februari, 2024. Sasa Tume iko vizuri, ina sheria yake. Uhuru ambao umetamkwa kwenye Katiba, umefafanuliwa vizuri sana kwenye sheria hii. Ukitaka kuusoma uhuru wa Tume, siyo kwa jina tu, kwa kila kipengele; nenda kasome sheria hii utaielewa na utaitilia maanani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, tumetunga Kanuni za Maadili ya Uchaguzi wa Rais na Madiwani za Mwaka 2025. Vyama vyote vimesaini kanuni hizo, isipokuwa Chama cha CHADEMA. CHADEMA waliamua kutokusaini kwa utashi wao; wala hawakuzuiwa na mtu yeyote, na huwezi kumlazimisha mtu kusaini. Hizi ndizo *reforms* ambazo tumeziweka sasa. Kanuni za Uchaguzi za Mwaka 2025 ni *reforms* kubwa ambazo ziko hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Sheria ya Uchaguzi ambayo tuliitunga, kuna mambo ya msingi ambayo napenda pia kuyaongea. Moja, suala la kupita bila kupingwa limeondolewa kabisa. Hili ndilo lililokuwa lalamiko kubwa sana, mpaka watu walikwenda Mahakamani, Mahakama ikatoa hukumu. Hukumu ya Mahakama ile imetekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii tunajifunza hapa kwamba, kumbe tukitaka mabadiliko, twende Bungeni ama twende

Mahakamani, siyo kulazimisha watu kuingia mtaani na barabarani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na malalamiko kuhusu Wakurugenzi kusimamia uchaguzi. Suala hili limeshapatiwa tiba. Sasa hivi uchaguzi utasimamiwa na Maafisa Waandamizi ambao watateuliwa na Tume na kwa njia ya ushindani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeanzisha Kamati ya Usaili ya kupata viongozi wa juu wa Tume ili kupata umoja. Kamati hii inaongozwa na Majaji Wakuu wa Tanzania na wa Zanzibar. Pia, inaongozwa na Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, pamoja na mtu mwingine ambaye atateuliwa kutengeneza *column* ya watu watano**.**

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme hapa, duniani kote namna ya kufanya uteuzi katika nafasi nyeti kama hizi ni ama ateuliwe na Rais ama ateuliwe na Bunge, halafu Rais aidhinishe, au ateuliwe na chombo huru na Rais aweze kuidhinisha. Sasa Tume hii ya Uchaguzi tungeileta humu Bungeni tuiteue sisi, haki isingetendeka, kwa sababu sisi tungekuwa tunaandaa Majaji wa kuamua shughuli yetu wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, chombo hicho ndicho mwafaka, ndicho chombo huru kabisa na kimezingatia viwango vya Kimataifa vya kuhakikisha kwamba Tume ya Uchaguzi inakuwa huru kama jina lake ambavyo limesema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uteuzi wa Mwenyekiti na Mkurugenzi pamoja na viongozi wengine wa juu utatangazwa. Watu wataomba, na watashindanishwa kwenye usaili. Wale watakaofuzu ndio watakaopendekezwa kwa Mheshimiwa Rais kwa ajili ya uteuzi. Jambo hili halijawahi kufanyika toka nchi hii imepata Uhuru. *Reforms* hizi tunazozifanya sisi hapa, sasa tuwaulize ndugu zetu, wanataka *reforms* gani zaidi ya hizi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *reforms* zimekwenda mpaka Magereza. Sasa wafungwa nao wanaruhusiwa kupiga kura. Hii

inakwenda sambamba Kifungu cha 10 pamoja na Jedwali la Tatu linalotupa maelezo haya. Pia, kura ya Rais inaweza ikapigwa popote pale, siyo katika kituo ambacho umejiandikisha. Haya ni mageuzi makubwa sana ambayo yamefanyika. Makosa ya unyanyasaji wa kijinsia yameingizwa na yamepewa msimamo mkubwa ili uchaguzi wetu siyo tu uwe huru, bali pia utende haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatujaishia hapo, suala la pingamizi limefafanuliwa vizuri. Wale wasioweza kulielewa wakasome Kifungu cha 26 pamoja na Kifungu cha 53, vinaelezea kuhusu pingamizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kama Waziri mwenye dhamana ya Katiba na Sheria niseme kwamba tumefanya *reforms* nyingi kuanzia mwaka 1961 mpaka leo. Tumekuwa na sheria nane, na tumekuwa na kanuni sita. Tumeshafuta sheria mbili na tumefanya mabadiliko *(amendments)* ya sheria sita. Hizo ni *reforms* kubwa kuliko zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, natamka hapa kama Waziri mwenye dhamana ya Katiba na Sheria; dhamana ya kusema kuna uchaguzi au hakuna uchaguzi kwa mujibu wa Ibara ya 74 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano, kwa mujibu wa Sheria Na. 1 na Na. 2 za mwaka 2024, ni Tume ya Uchaguzi ya Taifa na siyo mtu mwingine yeyote yule. Mtu mwingine atakayesema hivyo anajivisha joho ambalo sio lake. Tuwaombe Watanzania wampuuze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu ambalo ningependa kulisema ni umuhimu wa bajeti hii ambayo tumeipitisha safari hii. Bajeti hii sisi tunaita bajeti ya haki, kwa sababu ni bajeti ambayo inatampa haki Mtanzania, bajeti ambayo itatoa shibe kwa Watanzania wenye njaa na kiu ya haki; watapata haki katika kila eneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni bajeti ambayo italeta mwanga na inaondoa giza la dhuluma ya haki kwa Watanzania wanyonge katika kona zote za Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania; bajeti ambayo itafuta chozi la mnyonge aliyekosa haki kwa muda mrefu sana; na bajeti ambayo ni mtetezi wa wananchi wanyonge, hasa wenye migogoro sugu na ya muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni rai yetu Waheshimiwa Wabunge waweze kutuunga mkono ili kupitia bajeti hii tupeleke haki kwa Watanzania wanyonge ambao wanahitaji zaidi wapate haki hiyo, ambayo itawapa usawa, ambayo itawapa amani na hatimaye itawapa maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru tena sana wewe kwa namna ambavyo umetuongoza kwa siku ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD - KATIBU WA BUNGE:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD - KATIBU WA BUNGE:**

**KITABU CHA PILI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 12 – Tume ya Utumishi wa Mahakama**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*……………..Sh.2,910,465,000
Kifungu 1002 – Finance *and Accounts Unit*……………Sh.244,790,000
Kifungu 1003 – *Procurement Management*

*Unit*.........................................................Sh.148,810,000
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*…….......................Sh.133,518,000
Kifungu 1005 – *Recruitment, Appointment and Confirmation Unit* ………………………..Sh.885,000,000
Kifungu 1006 – *Ethics and Discipline Section*…………..Sh.890,400,000
Kifungu 1007 – *Planning, Monitoring and Evaluation* ……………………….……Sh.490,000,000
Kifungu 1008 – *Information and Communication Technology Unit*……………………..........Sh.826,534,000
Kifungu 1009 – *Legal Service Unit*……………………..……Sh.137,450,000
Kifungu 1011 – *Government Communication Unit*…..Sh.300,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Kutokana na muda, tunakwenda kwenye *Guillotine*.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD - KATIBU WA BUNGE:**

**Fungu 16 – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali**

**MWENYEKITI:** Katibu, rudia tena.

**NDG. BARAKA I. LEONARD- KATIBU WA BUNGE:**

**Fungu 16 – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*....................................Sh. 9,155,785,280
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*………...Sh. 1,901,859,000
Kifungu 1003 – *Planning Division*…............................Sh. 2,767,389,800
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*……........................Sh. 792,809,100
Kifungu 1005 – *Government Communication Unit*….Sh. 781,105,000
Kifungu 1007 – *Procurement Management Unit*…….Sh. 905,177,000
Kifungu 1008 – *Research and Library Service Unit*…..Sh. 436,854,660
Kifungu 1009 – *Information and Communication*

*Technology Unit*……………………….Sh. 2,388,472,000
Kifungu 2001 – *Coordination and Advisory Service*……………………………….…Sh. 9,081,370,860
Kifungu 2003 – *Legislative Drafting*……………………..Sh. 0
Kifungu 3002 – *Treaties and Contracts Division*…….Sh. 8,705,584,110
Kifungu 5001 – *Regional Attorney General's Office-* Dar es Salaam……………………………Sh. 458,934,690
Kifungu 5002 – *Regional Attorney General's Office* Arusha……………………………………Sh. 337,637,000
Kifungu 5003 – *Regional Attorney General's Office* – Mbeya…………………….......Sh. 337,585,000
Kifungu 5004 – *Regional Attorney General's Office* – Kilimanjaro……………………Sh. 330,468,000
Kifungu 5005 – *Regional Attorney General's Office* – Mtwara………..………………Sh. 335,415,000
Kifungu 5006 – *Regional Attorney General's Office* – Mwanza………..………………Sh. 445,921,500
Kifungu 5007 – *Regional Attorney General's Office* – Kagera…………………………Sh. 323,415,000
Kifungu 5008 – *Regional Attorney General's Office* – Tabora…………………………Sh. 332,925,000
Kifungu 5009 – *Regional Attorney General's Office* – Tanga…………………………Sh. 334,542,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 19 – Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*…………………………Sh.15,721,996,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*…………..Sh. 641,461,000
Kifungu 1003 – *Planning Division*…..........................Sh. 993,844,000
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*……......................Sh. 450,849,000
Kifungu 1005 – *Procurement Management Unit*…….Sh. 543,912,000
Kifungu 1006 – *Information and Communication Technology Unit*………………………..Sh. 827,610,000
Kifungu 1007 – *Government Communication Unit*… Sh. 490,724,000
Kifungu 1008 – *Library Service and Research Unit*…..Sh. 466,345,000

Kifungu 1009 – *Legal Registry Unit*……….…………...Sh. 1,239,212,000
Kifungu 2001 – *Case Management and Quality Assurance*………………………………Sh. 2,197,755,000
Kifungu 2002 – *Arbitration Division*……………………Sh. 6,523,080,000
Kifungu 2003 – *Litigation Division*...............................Sh. 8,400,966,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 35 – Ofisi ya Taifa ya Mashtaka**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*…………………………Sh.69,231,924,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*…..……..Sh.1,566,827,000
Kifungu 1003 – *Planning Division*...............................Sh.1,382,469,000
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*……..........................Sh.567,057,000
Kifungu 1005 – *Procurement Management Unit*…....Sh.622,875,000
Kifungu 1006 – *ICT and Information Unit*…...................Sh.604,328,000
Kifungu 1007 – *Government Communication Unit*…..Sh.380,475,000
Kifungu 1008 – *Research and Library Services Unit*….Sh. 321,875,000
Kifungu 1009 – *Legal Registry Unit*……….…............Sh.1,887,144,000
Kifungu 2002 – *Civilization and Prosecutions*………..Sh.3,668,955,000
Kifungu 2004 – *Regional Office Arusha*………………Sh.1,242,800,000
Kifungu 2005 – *Regional Office Dodoma*……………Sh.3,951,988,000
Kifungu 2006 – *Regional Office Dar es Salaam*…….Sh.1,694,400,000
Kifungu 2007 – *Regional Office Iringa*…………………..Sh.879,965,000
Kifungu 2008 – *Regional Office Moshi*………………..Sh.1,314,800,000
Kifungu 2009 – *Regional Office Kagera*……………...Sh.1,773,200,000
Kifungu 2010 – *Regional Office Mbeya*………………Sh.1,311,200,000
Kifungu 2011 – *Regional Office Mtwara*…………….Sh. 1,030,000,000
Kifungu 2012 – *Regional Office Mwanza*…………….Sh.1,583,800,000
Kifungu 2013 – *Regional Office Ruvuma*…………….Sh.1,212,000,000
Kifungu 2014 – *Regional Office Sumbawanga*……….Sh.807,200,000
Kifungu 2015 – *Regional Office Tabora*………………Sh.1,497,600,000
Kifungu 2016 – *Regional Office Tanga*……………..…Sh.1,483,600,000
Kifungu 2017 – *Regional Office Shinyanga*……………Sh.930,400,000
Kifungu 2018 – *Regional Office Singida*……………..…Sh.855,200,000
Kifungu 2019 – *Regional Office Lindi*………………….Sh.1,179,630,000
Kifungu 2020 – *Regional Office Mara*………………..…Sh.881,100,000

Kifungu 2021 – *Regional Office Manyara*…………….…Sh.999,590,000
Kifungu 2022 – *Regional Office Kigoma*……………..Sh.1,372,000,000
Kifungu 2023 – *Regional Office Pwani*……………….Sh.1,543,100,000
Kifungu 2024 – *Regional Office Njombe*……………….Sh.742,400,000
Kifungu 2025 – *Regional Office Morogoro*…………..Sh.1,559,160,000
Kifungu 2026 – *Regional Office Geita*………………..Sh.1,274,800,000
Kifungu 2027 – *Regional Office Simiyu*……………….Sh.1,077,200,000
Kifungu 2028 – *Regional Office Katavi*………………….Sh.687,200,000
Kifungu 2029 – *Regional Office Songwe*……………….Sh.772,200,000
Kifungu 2030 – *Regional Office Ilala*…………………….Sh.514,400,000
Kifungu 2031 – *Regional Office Kinondoni*…………….Sh.789,600,000
Kifungu 2032 – *Regional Office Temeke*………………Sh.749,600,000
Kifungu 2033 – *Regional Office Tarime*…………………Sh.570,000,000
Kifungu 3001 – *Fraud, Money Laundering and Corruption*………………………………...Sh.3,209,240,000
Kifungu 3002 – *Assets Forfeiture Transnational & Specialized Crime*…………………….Sh.3,274,500,000
Kifungu 3003 – *Case Management, Coordination of Criminal Cases*…………………………Sh.7,108,145,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 40 – Mfuko wa Mahakama**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*.................................Sh.133,694,112,123
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*……………Sh. 612,861,000
Kifungu 1003 – *Planning and Monitoring Division*…Sh.16,668,535,755
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*…….........................Sh.401,048,600
Kifungu 1005 – *Information, Communication and Technology Unit*...............................Sh.5,105,413,492
Kifungu 1006 – *Information, Education and Communication Unit*...........................Sh.528,500,000
Kifungu 1007 – *Procurement Management Unit* ……Sh. 588,615,000
Kifungu 1008 – *Estates Management Unit*……………Sh.1,106,673,700
Kifungu 1009 – *Records Management unit*……………Sh.457,185,000
Kifungu 1010 – *Library Services Unit*…………...........Sh.353,559,900
Kifungu 1011 – *Legal Services Unit*…………………....Sh.115,942,400

Kifungu 1012 – *Transport Management Unit*……......Sh.1,766,018,900
Kifungu 1013 – *Monitoring and Evaluation Unit*……….Sh.774,138,845
Kifungu 2001 – *High Court Main Registry* ……………Sh.9,663,721,300
Kifungu 2002 – *Court of Appeal*..............................Sh.15,658,857,336
Kifungu 2004 – *High Court Divisions*………..………..Sh.275,000,000
Kifungu 2299 – *Commercial Court*……………………Sh.1,338,808,000
Kifungu 2300 – *Land Court*……………….............Sh.1,304,961,000
Kifungu 2301 – *Labour Court*………………………......Sh.1,162,318,440
Kifungu 2302 – *Case Management Division*…………Sh. 810,331,508
Kifungu 2303 – *Complaints Management and Inspectorate*…………………………….Sh. 607,953,900
Kifungu 2310 – *Mediation Centre*………………………..Sh.554,563,900
Kifungu 2326 – *Corruption and Economic Court*……..Sh.871,205,200
Kifungu 2327 – *Judiciary Delivery Unit*…….…………….Sh.471,940,000
Kifungu 2347 – *IJC Temeke*.......................................Sh.1,211,730,000
Kifungu 3001 – Arusha *Zone*………………..............Sh.1,566,780,300
Kifungu 3002 – Coast *Zone*………………………..........Sh.782,155,800
Kifungu 3003 – Dar es Salaam *Zone*…….…………….Sh.4,097,531,103
Kifungu 3004 – Dodoma *Zone*…………………………Sh.1,646,074,000
Kifungu 3005 – Iringa *Zone*……………………………….Sh.956,445,600
Kifungu 3006 – Simiyu *Zone*………………………………Sh.658,232,100
Kifungu 3007 – Kigoma *Zone*………………………….Sh.1,231,660,515
Kifungu 3008 – Moshi *Zone*…………………….........Sh.1,253,264,000
Kifungu 3009 – Lindi *Zone*…………………………….….Sh.591,133,000
Kifungu 3010 – Mara *Zone*…………………………….Sh.1,301,687,900
Kifungu 3011 – Mbeya *Zone*…………………….........Sh.1,421,304,000
Kifungu 3012 – Morogoro *Zone*……………….……….Sh.1,474,101,300
Kifungu 3013 – Mtwara *Zone*…………………………..Sh.1,033,058,800
Kifungu 3014 – Mwanza *Zone*………………………….Sh.1,903,315,100
Kifungu 3015 – Songea *Zone*…………………………….Sh.978,475,400
Kifungu 3016 – Sumbawanga *Zone*……………………Sh.968,466,500
Kifungu 3017 – Manyara *Zone*…………..…………Sh.1,088,375,900
Kifungu 3018 – Bukoba *Zone*………………………….Sh.1,577,369,900
Kifungu 3019 – Singida *Zone*……………………..……Sh.587,377,902
Kifungu 3020 – Shinyanga *Zone*………………………Sh.1,209,437,900
Kifungu 3021 – Tabora *Zone*……….…………..….…Sh.1,284,817,680
Kifungu 3022 – Tanga *Zone*…………………………….Sh.1,487,875,101
Kifungu 3023 – Songwe *Zone*……………………………Sh.570,403,400
Kifungu 3024 – Katavi *Zone*………………………………Sh.550,607,300

Kifungu 3025 – Njombe *Zone*……………………………Sh.578,536,100
Kifungu 3026 – Geita *Zone*……………….……………Sh.1,128,548,100

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 41 – Wizara ya Katiba na Sheria**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management Division*...........................Sh.13,924,944,800
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*……..…....Sh. 710,112,000
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Division*…..........Sh.1,290,068,000
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*……..........................Sh.533,712,000
Kifungu 1005 – *Government Communication Unit*…...Sh.560,820,000
Kifungu 1006 – *Procurement Management Unit* …......Sh.461,496,000
Kifungu 1007 – *Information and Communication Technology Unit*…………………………Sh.699,388,400
Kifungu 1008 – *Monitoring and Evaluation Unit*……....Sh.613,780,000
Kifungu 2001 – *Human Right Division*…..…………..…Sh.1,937,356,000
Kifungu 2002 – *Legal Aid Service Unit*……………...Sh.12,277,604,000
Kifungu 2004 – *Public Legal Services Division*……….Sh.4,597,180,000
Kifungu 2005 – *Natural Wealth and Resource Observatory Unit*………………………Sh.1,088,784,000
Kifungu 4001 – *Constitutional and Justice Monitoring Division*............................Sh.6,480,049,800

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 55 – Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*...................................Sh.4,917,522,566
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*……………Sh.344,663,126
Kifungu 1003 – *Internal Audit Unit* ….............................Sh.204,951,959
Kifungu 1004 – *Legal Services Unit*…….........................Sh.668,307,779
Kifungu 1005 – *Procurement Management Unit*……..Sh.172,685,567
Kifungu 1006 – *Management Information System Unit*…………………….………….…..Sh.340,892,773

Kifungu 1007 – *Planning, Monitoring and Evaluation Unit* ………………………..……..………..Sh.375,363,525
Kifungu 2001 – *Complaints and Investigation Division* ..………………………………...Sh.1,412,218,860
Kifungu 2003 – *Public Education, Communication Research and Documentation*……….Sh.792,573,360
Kifungu 3001 – *Zanzibar Office* …………………………Sh. 592,348,331
Kifungu 3002 – *Mwanza Office*……….…………………Sh. 301,990,331
Kifungu 3003 – *Mtwara Office*………………..………Sh. 244,129,546
Kifungu 3004 – *Pemba Branch*…………………..………Sh. 191,286,514
Kifungu 3005 – *Dar es Salaam Office*…………..……...Sh.1,185,030,763

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 59 – Tume ya Kurekebisha Sheria**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*…………………….…..Sh.1,964,433,401
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*…………...Sh.518,974,208
Kifungu 1003 – *Planning and Coordination Unit*……..…Sh.560,63,951
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*……...........................Sh.301,547,089
Kifungu 1005 – *Procurement Management Unit*…..…..Sh.321,544,555
Kifungu1006 – *Legal Education and Awareness Unit*………………………………………Sh. 862,969,808
Kifungu *1007 – Law Review Unit*……………..……...Sh.1,190,995,000
Kifungu *1008 – Law Research Unit*…..………………....Sh.1,141,554,000
Kifungu 1009 – *Legal Services Unit*…………………..….Sh.167,027,443
Kifungu 1010 – *Information and Communication Technology Unit*………….……………Sh.173,111,896
Kifungu 1011 – *Monitoring and Evaluation Unit*……….Sh.53,795,717
Kifungu 1012 – *Government Communication Unit*…..Sh.145,712,932

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 101 – Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resource Management Unit*……………………Sh.4,972,138,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*………..…Sh.498,366,000
Kifungu 1003 – *Planning and Budgeting Unit*………...Sh.565,522,000
Kifungu 1004 – *Procurement Management Unit*…….Sh.388,392,000
Kifungu 1005 – *Information and Communication Technology Unit*……………………...…Sh.666,396,000
Kifungu1006 – *Internal Audit Unit*…………………..…..Sh.306,896,000
Kifungu1007 – *Monitoring and Evaluation Unit*……….Sh.301,844,000
Kifungu 1008 – *Quality Assurance Unit*………………….Sh.797,910,000
Kifungu 1009 – *Government Communication Unit*…...Sh.335,194,000
Kifungu 2001 – *Legislative Drafting Division*…………Sh.2,251,415,000
Kifungu 2002 – *Legal Translation Division*…………….Sh.2,480,562,000
Kifungu 2003 – *Laws Revision, Research and Training Division*……………….……...Sh.3,818,329,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. BARAKA I. LEONARD- KATIBU WA BUNGE:**

**KITABU CHA NNE**

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 16 – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*……………..….........Sh. 788,704,000
Kifungu 1003 – *Planning Division* …...............................................Sh.0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 35 – Ofisi ya Taifa ya Mashtaka**

Kifungu 1001 – *Administration and Hunan Resources*

*Management*...................................Sh.15,866,110,000
Kifungu 2002 – *Civilization and Prosecutions*…...........................Sh. 0
Kifungu 3001 – *Fraud, Money Laundering and Corruption Offence*..........................................Sh. 0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 40 – Mfuko wa Mahakama**

Kifungu 1003 – *Planning and Monitoring Division*…………………………………Sh.93,025,200,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 41 – Wizara ya Katiba na Sheria**

Kifungu 1003 – *Policy and Planning Division*……....Sh. 52,558,773,000

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 55 – Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora**

Kifungu 1007 – *Planning Monitoring and Evaluation Unit*……….Sh. 0

*(Kifungu Kililotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.
Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD - KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Mtoa hoja.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 123(3)(a) na (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kutoa taarifa kuwa Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi, limekamilisha kazi zake. Naomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Sasa nitawahoji kwamba Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Wote wameafiki. Nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri wewe na timu yako Mheshimiwa *AG* kwa michango mizuri.

Waheshimiwa Wabunge, bajeti hii sasa imepita, tunakwenda sasa kupeleka maendeleo na haki kwa Watanzania. Nawaomba taarifa kama hizi za kueleza umma ukweli na kufuta upotoshaji, Serikali lazima muwe mstari wa mbele. *(Makofi)*

Katibu Mkuu umepongezwa sana leo. Naomba hivi vipengele vilivyosomwa hapa na Waziri, *AG,* Mheshimiwa Salome na wengine, mvi-*highlight,* mviweke kwenye *social media,* wala hamhitaji bajeti.

Unasema kabisa, Tume haitachaguliwa na Rais, Rais kajivua madaraka kwa kupenda Taifa lake, mna-*quote* maendeleo mnaweka orodha ya majina ya watu waliohudhuria kwenye michakato, vyama vyao na viongozi wao waliokubaliana na hivi vitu, umma ujue. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mwaka 2015 kama mnakumbuka kwenye Uchaguzi wa 2015, Tume haikuwa na ubora kama Tume hii, lakini humu ndani Wapinzani waliingia 112 kwa Tume ambayo ilikuwa haina ubora wowote. Nani anajua? Mheshimiwa Prof. Kitila, ulikuwepo huko. *(Makofi/Kicheko)*

Wabunge waliokuwepo wa upinzani; CHADEMA 69, *CUF* 41, *ACT* mmoja na *NCCR* Mageuzi mmoja, jumla 112 na Tume ambayo haikuwa na ubora kama hii ambayo Rais amejivua Madaraka, ameachia usaili, ameachia watu wamletee majina matatu. Wananchi sikilizeni ukweli. *(Makofi/Kicheko)*

Mimi juzi nilikuwa kwenye nchi sitaki kuitaja jina, hiyo nchi ni kubwa, *ruling party* wako 120, *opposition* wako 90. Njooni kwenye uchaguzi tujenge Taifa letu, marekebisho yatafanywa humu ndani, siyo mitaani. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri, chukueni nafasi ya kuelimisha umma kwenye *social media.* Wao wanatumia mitandao na ninyi tumieni mitandao. Ni muhimu sana wananchi wakajua ukweli ili waache kusikiliza mambo ya upotoshaji. Watu wengine wanaamini hivi vitu, niwaombe sana Serikali tumieni muda mwingi kuelimisha wananchi. *(Makofi)*

Baada ya maneno haya niwapongeze tena Waheshimiwa Wabunge, Serikali kwa kazi nzuri iliyofanya, twendeni tukaelimishe wananchi.

Ninaahirisha shughuli za Bunge mpaka tarehe 2 Mei, 2025, Ijumaa saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.49 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 2 Mei, 2025 Saa Tatu Asubuhi)*